Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini – Tarehe 12 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**DUA**

*Spika (Mheshimiwa Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunajitahidi sana kupunguza haya matangazo na kwa kweli itabidi iwe ni kwa sababu maalum tu ndio tutatangaza wageni. Vinginevyo, itakuwa ni wageni rasmi watakaokaa *Speakers Gallery* ndio watatangazwa. Wengine wengi ni wananchi yaani Watanzania wenzetu ambao ni haki yao kuwa humu, kuhudhuria Bunge. Ila leo tunao wanafunzi 56 na walimu wao watano (5) kutoka Shule ya Msingi Kondoa.

Natangaza hili kwa sababu tu Shule hii ndiyo aliyosoma Mheshimiwa Zabein Mhaji Mhita, ambaye ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii. Vijana mnaweza kusimama na walimu. Wale pale mkono wa kulia. Karibuni sana. Ahsante. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:**

Maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha Uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 186

**Kituo cha Afya Tandahimba**

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA (K.n.y. MHE. JUMA A. NJWAYO)** Aliuliza:-

Kwa kuwa Kituo cha Afya cha Tandahimba kilipewa kibali na Wizara ya Afya kubadilishwa kuwa Hospitali ya Wilaya ya Tandahimba mwaka 2004 na kwa kuwa hadi sasa Hospitali hiyo haina vifaa kama *X-Ray*, mashine ya *Ultra-Sound* wala gari la wagonjwa kama ilivyo kwa Hospitali nyingine za Wilaya nchini licha ya kukamilika kwa jengo la *X-Ray*:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaa vyote nilivyotaja kwenye Hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata kibali cha kubadilisha Kituo cha Afya Tandahimba kuwa Hospitali ya Wilaya 2004, Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba imefanya mambo yafuatayo:-

- Kuajiri watumishi wa muda na kuwalipa mishahara kutokana na vyanzo vyake vya mapato.
- Ujenzi wa majengo muhimu ya kutolea huduma.
- Kununua vifaa na dawa kwa fedha za uchangiaji.
- Kujenga wodi 3 zenye uwezo wa kulaza wagonjwa 24 kila moja.
- Kununua vifaa kama vile vitanda 78, shuka 312, magodoro 78 na mablanketi 120.

- Kujenga jengo la *X-Ray*, jengo la huduma za macho na jengo la huduma za meno, nyumba ya Mganga Mkuu wa Wilaya na wodi 2 ambazo ujenzi wake unaendelea.

- Pia, Wahisani wa *District Health Improvement Project (DHIP)* wamejenga jengo la upasuaji ambalo ni *two in one*, jengo la maabara na kuweka vifaa vyake, nyumba 4 za madaktari, uzio kuzunguka eneo la Hospitali na kurekebisha mfumo wa maji safi na maji taka hapo hospitalini.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi hizo, maeneo yaliyopewa kipaumbele ni yale yenye huduma muhimu ambazo kukosekana kwake kulikuwa kunasababisha kuongezeka kwa vifo kwa wagonjwa, Matumizi makubwa ya mafuta ya magari katika kusafirisha wagonjwa wanaohitaji huduma hizo kwenda Hospitali ya Wilaya iliyo jirani ya Newala. Maeneo hayo ni pamoja na huduma ya upasuaji, *X-Ray*, macho na meno.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeishaliona tatizo la magari ya kubebea wagonjwa katika Vituo vya Afya na Hospitali mbali mbali katika nchi nzima. Kama nilivyokwisha liarifu Bunge lako Tukufu wakati wa Kikao Cha Tatu nikijibu swali Na. 17 la Mheshimiwa Damas P. Nakei la tarehe 29/3/2006 na katika Kikao hiki tarehe 4/7/2006 wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Juma Nkumba. Hivyo Hospitali ya Wilaya ya Tandahimba inaweza kupata gari hilo kama itakidhi vigezo.

Mheshimiwa Spika, gharama ya mashine moja ya *X-Ray* kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ni *USD* 65,000 na mashine ya *Ultra-Sound* ni *USD* 12,000, kifaa cha kusafisha na kukausha picha za *X-Ray* ni *USD* 13,000 na mashine ya Mabara ni *USD* 7,000.

Kwa jumla zinahitajika takriban Sh.121,250,000/= kwa ajili ya kununulia vifaa hivyo vya Hospitali ya Wilaya. Hivyo, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba itaangalia uwezekano wa kupata fedha za kununulia vifaa hivyo.

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, na pili nipongeze wapiga kura wa Jimbo la Tandahimba kwa jinsi walivyojenga Hospitali yao kwa njia ya kujenga taifa. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Moja, hoja hapa ya msingi ni kwamba Tandahimba hawana huduma hizi zilizoulizwa kwenye swali. Inabidi wazifuate Wilaya jirani ya Newala. Sasa, Tandahimba hawazipati wala gari la kuwapeleka Newala hawana. Hivyo, katika hali hiyo Mheshimiwa Waziri anategemea wananchi hawa wa Tandahimba wakimbilie wapi? Tandahimba huduma hazipo lakini pia hawana usafiri wa kuwapeleka wale walio taaban wanaohitaji huduma kwenda hospitali ya jirani.

Swali la pili, kwa kuwa hata huko Newala wanakoenda, hakuna Madaktari. Wilaya nzima ya Newala haina *Medical Officer*! Wako *Assistant Medical Officers.*

Hivyo watu hawa wa Tandahimba na Newala, Mheshimiwa Waziri na akizingatia kwamba hata Kanda yenyewe ya Kusini haina Hospitali ya Rufaa. Hivi, Wizara inawaonaje watu hawa? Mnawasaidiaje watu wa Tandahimba na Newala?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswli mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George H. Mkuchika kama kama ifuatvyo:-

Nafahamu fika kwamba vifaa hivyo muhimu ni wajibu wa Serikali kuvinunua na kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, tutahakikisha kwamba vifaa hivyo vitapatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukosefu wa watumishi. Ukosefu wa Watumishi kwa Kusini inafahamika na sasa hivi Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, tunawapeleka watumishi moja kwa moja kutoka Vyuoni kwenda katika Wialaya husika. Nina uhakika kwamba Kanda ya Kusini itapata kipaumbele zaidi ikilinganishwa na Kanda zingine kulingana na tatizo kubwa la uhaba wa watumishi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ningeomba nimshukuru Naibu Waziri Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Ningependa kuongeza maelezo ya nyongeza kwa niaba ya Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ni kweli hivyo vifaa vilivyotajwa ni muhimu na ni azma ya Serikali kwamba kila Hospitali ya Mkoa na Hospitali ya Wilaya ipate mashine ya *Ultra-Sound* na *X-Ray*. Miaka michache iliyopita tuliingia kwenye mradi unaitwa *OLET* pamoja na Waholanzi ambao tuliweza kusambaza vifaa hivyo katika Hospitali zote. Sasa, kuna Hospitali mpya za Wilaya ambazo zinaibuka na tuna mpango maalum wa kuwapa kipaumbele ili na wenyewe wapatiwe.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni kwamba Mheshimiwa George H. Mkuchika, amezungumzia habari za Hospitali ya Rufaa katika Kanda ya Kusini. Hiyo taarifa tunayo tunayo na toka mwaka jana tumekuwa tukitenga pesa. Mwaka jana tulitenga pesa shilingi milioni 300 na mahali penyewe ambapo wananchi wa Mtwara wamepachagua nilikwenda kukagulia. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Serikali inawajali tofauti na anavyofikiria na tuna imani kwamba hiyo Hospitali itajengwa. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES M. WANYANCHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Vifaa vinavyotakiwa hapa katika Wilaya ya Tandahimba ni muhimu sana. Sasa, kweli Serikali ya Tanzania haina Dola 110 kuwasaidia hawa watu ambayo ni sawa sawa na bei ya kununua *VX* moja. Hatuna hela kweli mpaka watu waendelee kufa!

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ningependa kumjibu Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha kwamba Serikali ya Tanzania inazo hizo dola. Lakini mahitaji ni mengi, kwa hiyo inakuwa kupanga ni kuchagua. Hapo tutakapofikia Hospitali ya Tandahimba tutawasaidia hilo na kuna Hospitali nyingi sana ambazo kama nilivyosema zimeibuka sasa hivi kama Hospitali za Wilaya na hizi tunazifanyia mpango ili kila moja ipate ikiwa ni pamoja na Tandahimba. *(Makofi)*

Na. 187

**Barabara Kati ya Simanjiro na Babati**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA** Aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali nimekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya barabara inayounganisha Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro na Mkoa:-

(a) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekwishatumika kwa matengenezo ya barabara hiyo?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimekisiwa kukamilisha ujenzi huo?

(c) Je, ni lini barabara hiyo itakamilika ili kuwezesha wananchi wa Simanjiro kufika Mkoani kwa urahisi.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE. DR. MILTON M. MAHANGA)** Alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabra kati ya Simanjiro na Babati unatokana na agizo la Mheshimiwa Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa alilotoa baada ya kuanzishwa Mkoa Mpya wa Manyara ambao kijiografia umegawanyika katika pande mbili za Magharibi na Mashariki zisizo na mawasiliano ya moja kwa moja.

Barabara hii ni ya Mkoa na inashughulikiwa chini ya Wizara ya Miundombinu kupitia *TANROADS* na inajengwa kwa kiwango cha udongo na changarawe kwa maeneo korofi. Barabara hiyo itaunganisha Makao Makuu ya Wilaya za Simanjiro na Kiteto na Makao Makuu ya Mkoa, Babati, ambapo kwa sasa wasafiri wa sehemu hizo hulazimika kupitia Arusha na Kondoa. Barabara hiyo itakapokamilika itapunguza gharama za utawala na kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii Mkoani Manyara.

Mheshimiwa Spika, barabara hii yenye urefu wakilomita 245 imegawanyika katika sehemu nne kama ifuatavyo:-

- Gendi – Gedamar (km.17.5)
- Gedamar – Kimotorok (km. 62.9)
- Kimotorok – Mbuyuni (km. 64.5)
- Kimotorok – Sukuro (km. 100.1)

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mbunge wa Simanjiro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mpaka hivi sasa sehemu ya kwanza ya barabara hiyo, (Gendi – Gedamar) yenye urefu wa kilometa 17.5 imekamilika mwezi Oktoba 2005 kwa gharama ya jumla ya shilingi milioni 830.05. Sehemu ya pili, Gedamar – Kimotorok yenye urefu wa kilometa 69.2 imeanza kujengwa ambapo kilometa 5 zimekamilika mwezi Machi 2006 kwa jumla ya shilingi 336.9 milioni. Aidha, kiasi cha shilingi 250 milioni kimekwishalipwa kwa Mkandarasi na Mhandisi Mshauri kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006. Hivyo, jumla ya shilingi bilioni 1,416.95 zimetumika kwa ujenzi wa sehemu zote mbili.

(b) Ili kukamilisha ujenzi wa barabra hiyo yote, jumla ya shilingi zipatazo bilioni 18 zitahitajika kwa sehemu zilizobaki ikiwa ni pamoja na gharama za Mhandisi Mshauri na fidia kwa wananchi ambao mali zao zitaathirika na mradi huu.

(c) Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa barabara hiyo kutategemea upatikanaji wa fedha za ujenzi kama nilivyokwisha sema unakadiriwa kufikia kiasi cha bilioni 18. Kwa kuwa gharama za ujenzi wa barabra hii ni kubwa sana Wizara yangu itaendelea kutenga fedha katika Bajeti za kila mwaka ili kujenga barabara hiyo muhimu. Katika mwaka huu wa Fedha jumla ya shilingi 1.35 bilioni zimetengwa kuendeleza sehemu ya pili kati ya Gadamar – Kimotorok. Tunategemea kwamba uwezo wa fedha ukiongezeka, Serikali itatenga mafungu makubwa zaidi kuanzia Bajeti ijayo 2007/2008 na zinaziofuata ili kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo mapema zaidi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa kuwa hadi sasa wananchi wa Wilaya za Simanjiro na Kiteto wanalazimika kupita Mikoa kati ya miwili au mitatu ili kufika Makao Makuu ya Mkoa; Na kwa kuwa kwa mahesabu haya ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza, itachukua zaidi ya mika 20 kuweza kuunganisha Wilaya ya Simanjiro na Makao Makuu ya Mkoa, na Makao Makuu ya Wilaya ya Kiteto na Makao Makuu ya Mkoa, hii ni kutokana na ripoti ya watu wa *TANROADS*. Je, Waziri haoni sasa kwamba kiasi kinachotengwa cha fedha cha shilingi bilioni 1.3 zilizotengwa mwaka huu, kama Serikali itaendelea kuetenga fedha kiasi hicho na miaka 20 ikahitajika kuwaunganisha wananchi hawa na Makao Makuu ya Mikoa yao, Serikali haioni sasa ipo haja ya kutafuta fedha zingine kutoka vyanzo vingine ili kuondoa adha hii kwa watu wa Simanjiro? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili ni kwamba, Waziri atakubaliana nami kwamba kwa kuwa alipokuwa akitangaza barabara itakakopitia ametamka kijiji cha Skura ambacho mwanzoni kilikuwa kimekwepwa na hili lilikuwa ni ombi la Wabunge wa Mkoa wa Manyara; na kwa kuwa Wizara imekubali kupitisha barabara hiyo kutoka Kimotorok- Libosiret- Narakawo- Sukuro na Berera, Waziri sasa atakubaliana na kupokea pongezi za Wananchi wa Simanjiro kwa uamuzi huo kwa kusikia kilio cha wananchi kupitia kwa Wabunge wa Manyara, na mimi ni Mbunge wao? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Naibu Waziri wa Miundombinu, sijui majina hayo utayaweza maanake… *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswli ya nyongeza ya Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, ni imani yangu kwamba uwezo wa kifedha wa Serikali ukiongezeka kuanzia mwaka ujao wa Fedha yaani 2007/2008, Serikali itaanza kutenga mafungu makubwa zaidi ili barabara hii ikamilike mapema zaidi na wala si kufika miaka 20. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba tuko pamoja na wananchi wa Mkoa wa Manyara kuhakikisha kwamba barabara hii inafunguka mapema iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali lake a pili kwamba Serikali imekubali sasa barabara hiyo iende sasa kupitia Sukuro, nataka nimthibitishie kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba Wizara imekubali na ombi hilo na sasa barabara hiyo itapita kuelekea Sukuro na niko tayari kupokea pongezi za wananchi wa Manyara. *(Makofi)*

Na. 188

**Mipaka ya Baharini**

**MHE. FETEH SAAD MGENI** Aliuliza:-

Kwa kuwa mara nyingi mipaka yetu ya Baharini inatupa matatizo ya Ki-ulinzi; na kwa kuwa mara nyingi wavuvi wa nchi jiarani na hata meli za nchi zilizoendelea huvua samaki kwenye maeneo yetu ya bahari, samaki ambao ni sehemu kubwa ya uchumi wetu:-

(a) Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati muafaka wa kuimarisha ulinzi wa uchumi wetu wa bahari na katika Maziwa Makuu?

(b) Je, Serikali haioni kuwa iko haja kubwa ya kuweka kwa uwazi *Beacons* kwenye mipaka ya bahari yetu, kutayarisha *Navigation Charts*, *Landmarks* na *Navy Boyars* hasa katika Ziwa Victoria na Tanganyika?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

(a) Serikali nimeendeleza jitihada zake za kuboresha ulinzi wa rasilimali ya uvuvi katika maeneo ya uvuvi nchini. Katika maboresho hayo, Serikali imeweka na kutekeleza mikakati mbali mbali kama ifuatavyo:-

- Kuanzisha vituo vya doria vya Kanda. Vituo hivyo vimeanzishwa Ziwa Victoria katika Mikoa ya Mwanza, Kagera na Musoma; Ziwa Tanganyiaka, Kigoma, Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi, Mbegani na Tanga. Aidha Serikali inatarajia kuanzisha kituo cha doria Ziwa Nyasa pale Kyela na Ziwa Tanganyika upande wa Mkoa wa Rukwa katika Mwaka wa Fedha 2007/2008.

Ili vituo hivyo viweze kutekeleza majukumu yake yaliyokusudiwa, vimepewa vitendea kazi muhimu ikiwemo maboti yaendayo kasi, watumishi wenye taaluma zinazotakiwa pamoja na redio kwa ajili ya mawasiliano.

Pamoja na kuanzishwa kwa vituo hivyo, Serikali inao utaratibu wa kufanya doria za mara kwa mara nchi kavu na majini kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu kwenye maeneo ya uvuvi na biashara ya magendo ya mazao ya uvuvi. Vile vile kwa upande wa baharini, dori za kutumia meli na ndege zimefanyika, ambapo katika kipindi cha tangu Agosti 2005 hadi Februari 2006 jumla ya doria 69 za kutumia meli na 6 za angani zilifanyika.

- Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Baharini, Serikali imeendeleza jitihada za kudhibiti uvuvi kwa kufunga mtandao wa kutumia kompyuta wa kudhibiti mienendo ya meli za uvuvi.

- Ili kuwa na udhibiti endelevu, Serikali inao utaratibu baina yake na nchi jirani wa kupeana taarifa kuhusu meli zinazohisiwa kupora mazao ya uvuvi baharini.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa nchi kuwa na mipaka rasmi katika suala zima la ulinzi wa rasilimali zake majini na nchi kavu. Kwa upande wa Baharini, Serikali ilifanya makubaliano na nchi za Kenya, Msumbiji na Visiwa vya Shelisheli.

Uwekaji mipaka nchi kavu tunategemea alama zinazoonekana kwa macho kama alama za upimaji ardhi. Mipaka ya majini, huwa ni ya kimahesabu ambayo huchorwa juu ya ramani na kuainishwa kwa orodha ya vipimo vya Longitudo na Latitudo.

Kwa mujibu ya makubaliano ya kimataifa, waendeshaji wa vyombo vya majini ni lazima wawe na vifaa vya kusoma longitudo na latitudo ili kila wakati wafahamu wako wapi katika bahari ama katika ziwa.

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimefurahi sana na nimeridhika na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini, nitamwomba swali moja tu la nyongeza akubali niliulize.

Mheshimiwa Spika, tunaamini kwamba na naamini Waziri anaamini kwamba kwa sasa Tanzania Mgodi wetu wa pili ni Bahari na Maziwa yetu. Katika *Lake Tanganyika* ambalo ni Ziwa Mwenyezi Mungu katupa zuri, lina bahati katika Ulimwengu likiwa ni la pili katika Dunia lenye kina kirefu.

Mheshimiwa Spika, lakini, mpaka leo halijapata hasa sifa zinazofaa ili likavutia kwa wawekezaji. Kwa mfano, Ziwa lile halina *Beacons*, halina Gati ya kufikia wala alama za kusaidia usafiri.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri anijibu kwamba Je, mambo haya lini yatashughulikiwa ili livutie wawekezaji waweze kuwa na moyo wa kuja?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, kama ifuatavyo:-

Kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi, alama za mipaka katika maji huwa ni alama za kimahesabu na si alama za *Beacons*. *Beacons* ni alama zinazoonekana kwa macho. *Beacons* huwa zinawekwa nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, lakini, kuhusu gati, tutaangalia, tuone uwezekano wa kulitengeneza kutegemea na uwezo wa fedha wa kiserikali ili liweze kuvutia na wawekezaji wengi waweze kufika na kuwekeza katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

**MHE. MANJU M. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Katika majibu yake ya msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri ametueleza kwamba katika Maziwa zipo boti ziendazo kasi zinazosaidia doria.

Lakini, majuzi hapa Waziri wa Usalama wa Raia alipokuwa anajibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, alilihakikishia Bunge hili kwamba boti liendalo kasi katika Ziwa Tanganyika ni bovu kwa zaidi ya miaka minne na wavuvi katika Ziwa Tanganyika, doria wanafanya wnyewe kwa kutumia mitumbwi inayotumia makasia. Hivi boti liendalo kasi ambalo Mheshimiwa Naibu Waziri amelieleza limepatikana lini na usalama wa wavuvi katika Ziwa Tanganyika ukoje? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kama alivyosema wananchi wavuvi wa Ziwa Tanganyika wanatumia wakati mwingine boti zao

katika doria, kwanza ningeomba kwanza niwapongeze sana wavuvi wa Ziwa Tanganyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nimefika mpaka katika Jimbo la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, nimekutana na wavuvi, wavuvi wale wamesema kwa kuwa boti liendalo kasi ambalo limepelekwa pale huwa lina matatizo na kweli huwa lina matatizo na huwa linatengenezwa mara kwa mara. Lakini hata hivyo walinieleza kwamba hawatakaa tu kusubiri wanatumia boti zao wanaweka mafuta na wanafanya doria ni kitendo cha kupongezwa sana. Naomba niwapongeze. (*Makofi*)

Na. 189

**Eneo la Kumbukumbu ya Solomon Mahlangu**

**MHE. OMARI ALI MZEE** aliuliza:-

Kwa kuwa Chuo Kikuu cha Sokoine (*SUA*) kina eneo la kumbukumbu ya Solomon Mahlangu ambalo ni eneo zuri sana kuwa kivutio kwa Watalii kama vile majengo, viwanda, mashamba na makaburi ya Wapigania Uhuru kutoka Afrika ya Kusini, ambapo utalii unaweza kuimarishwa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuliboresha na kulitangaza eneo hilo ili kuvutia watalii na kuiingizia mapato Chuo hicho?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Omari Ali Mzee, Mbunge wa Kiwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatambua kuwepo kwa Kampasi ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambacho awali kilitumika kama kituo cha Wapigania uhuru na ubaguzi wa rangi wa Afrika ya Kusini kilichoanzishwa kama kambi mwaka 1978. Baada ya Afrika Kusini, kuondoa utawala wa ubaguzi wa rangi, kituo hicho kilikabidhiwa kwa Serikali na baadaye mwaka 2000 kukabidhiwa kwa Chuo Kikuu cha Sokoine. *(Makofi)*

Aidha miili ya wapigania uhuru imezikwa kwenye makaburi yaliyopo eneo hilo. Vile vile kuna hospitali, kiwanda cha samani, shamba na eneo kwa ajili ya kufugia wanyama ambavyo ni sehemu ya historia ya eneo hilo. Kwenye kuta bado zipo picha zilizochorwa na wapigania uhuru zinazoashiria hisia za wapigania uhuru hao na historia ya mapambano yao.

Kila mwaka Ubalozi wa Afrika ya Kusini, hufanya kumbukumbu katika eneo hilo. Taarifa tulizo nazo ni kuwa katika kipindi hicho, wananchi wengi wa Afrika Kusini, huja kwa lengo la kuweka mashada ya maua katika makaburi au kutembelea tena mahali walipoishi wakati wa kupigania uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna juhudi mbalimbali zinazofanywa na Serikali, taasisi na mashirika mbalimbali. Kati ya juhudi hizo ni pamoja na mipango inayofanywa na Idara ya Mambo ya Kale kupitia Mradi wa Kujenga Uwezo wa Idara, kutambua na kuweka kumbukumbu za makaburi, makambi, makazi na maeneo yaliyotumiwa na wapigania uhuru na baadaye yaweze kutambulika na kulindwa kisheria.

Juhudi nyingine ni ile inayofanywa na Ofisi ya *UNESCO* Dar es Salaam kwa kutumia wataalamu wa Idara ya Mambo ya Kale na Jeshi la Wananchi wa Tanzania, kuyatambua na kuweka kumbukumbu za maeneo ambayo yalitumika wakati wa Ukombozi. Chini ya mradi huu kwa kutambua mchango mkubwa wa Tanzania katika kuleta uhuru Kusini mwa Afrika na kuwaenzi mashujaa wa mapambano hayo maeneo hayo yatafanyiwa kazi ili yawe kivutio kizuri cha utalii wa kihistoria na Utamaduni.

Na. 190

**Umeme – Ubinafsishaji wa Uongozi wa *TANESCO***

**MHE. LUCAS L. SELELII** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliwakaribisha wawekezaji kwa kubinafsisha uongozi wa *TANESCO* na kwa kuwa *Net Group* wameonekana kuwa hawana mpango wa kuendeleza Nishati nchini na hivyo kuonekana kuwa wamekuja kuvuna bila kupanda.

(a) Je, Serikali ipo tayari kusitisha na kuangalia upya mkataba baina yao?

(b) Je, ni faida gani zilizopatikana kutoka *Net Group*?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii, Mbunge wa Nzega, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeshatoa notisi kwa *Net Group* na haina nia ya kuingia mkataba mpya na kampuni hiyo wakati mkataba wa sasa utakapoisha mwishoni mwa mwaka 2006. Faida zilizopatikana kutoka *Net Group* ni zifuatazo:-

- Kuongeza kwa nidhamu ya ulipaji wa bili za umeme;

- Kuongeza kwa makusanyo kutoka wastani wa shilingi bilioni 11 kwa mwezi mwaka 2002 wakati *Net Group* ilipoingia madarakani hadi wastani wa shilingi bilioni 20 kwa mwezi kwa sasa; na

- Ili kuleta ufanisi wa upatikanaji wa umeme, uongozi wa *Net Group* umetumia kiasi kikubwa cha mapato ya shirika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vipya na matengenezo ya mifumo ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *Net Group Solution* ilikuja zaidi kukusanya mapato badala ya kuwekeza na katika majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ameeleza jinsi ambavyo *Net Group Solution* wamefanya na nidhamu ya kukusanya mapato zaidi.

(a) Je, kuna maeneo gani mapya ambayo *Net Group Solution* wameongeza kuwekeza hasa yale ya vijijini?
(b) Kwa kuwa *Net Group Solution* walikuja na mkabata ambao Serikali ilifanya nao na kwa kuwa imeonekana *net group* hawana faida ndio maana Serikali inajiondoa. Je, Serikali iko tayari kuwachukulia hatua wale walioingia nao mkataba kwa sababu ni kama walifanya uhujumu kuhujumu nchi yetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi *Net Group* katika kipindi chake cha mkataba imetumia kiasi kikubwa cha mapato ya shirika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vipya katika maeneo mengi nchini ikiwemo Mkoa wa Mtwara katika kununua *generator* mpya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kipindi hiki haijasema kama ilivyosema Mheshimiwa Mbunge, kwamba hakukuwa na faida kwa kuingia mkataba na *Net Group* hayo ni maneno yake.

Ningependa kumfahamisha kwamba kila mkataba huwa una muda na muda wa mkataba wa *Net Group* ndio umefika kikomo chake. Kutokana na kufika mwisho na kutokana na sharti lingine ambalo lilikuwepo kwenye mkataba kwamba waandae menejimenti ya kizalendo kuweza kuendesha kampuni ya *TANESCO* katika kipindi hiki Serikali imeamua kwamba haitaendelea na mkataba. (*Makofi*)

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali dogo kutokana na jibu la msingi kwamba *Net Group solution* wametumia kiasi kikubwa cha mapato kununua vifaa vipya. Sasa nilitaka kujua Serikali ina mpango gani wa kuvigawa vifaa vipya kwani katika Wilaya ya Kahama, tuna tatizo kubwa sana zaidi ya wateja 3,000 kwenye Mji wa Kahama na Kagongwa hawana mita wala vikombe. Serikali ina mpango gani wa kuvigawa vifaa hivi ambavyo *Net Group Solution* imetumia kiasi kikubwa cha fedha kuvinunua? (*Makofi*)

**SPIKA:** Hilo ni swali jipya kwa hiyo, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo.

Na. 191

**Fedha kwa Mradi wa Chumvi**

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ya Tanzania ilikopeshwa fedha na Serikali ya Ufaransa, ili kujenga mradi wa kutoa chumvi kwa kutumia nishati ya jua badala ya kuni kama ilivyokuwa hapo mwanzo na kwa kuwa, chumvi hiyo ina soko kubwa kwenye Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (*DRC*) Burundi na Rwanda:-

(a) Je, Serikali inaweza kuliambia Bunge fedha hizo zilikuwa kiasi gani?

(b) Je, mradi huo ulikamilishwa na kama jibu ni ndiyo umetoa chumvi kiasi gani?

(c) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuongeza wazalishaji wa chumvi hiyo kwa kuwa yapo masoko ya uhakika?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanne Ismaily Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mnamo mwaka 1973, Serikali ya Ufaransa ilitoa mkopo wa shilingi milioni 21 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kutengeneza chumvi kwa kutumia nishati ya jua huko Uvinza.

Mradi huo ulikuwa unaendeshwa na Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) na ulitarajiwa kuongeza uzalishaji chumvi kutoka wastani wa tani 12,000 kwa mwaka hadi kufikia wastani wa tani 60,000 kwa mwaka na kuisafirisha nje ya nchi. Mradi huo baada ya kukamilika uliendelea na uzalishaji kwa mwaka mmoja tu kabla ya mitambo kuhitaji matengenezo makubwa. *STAMICO* haikuweza kugharamia matengenezo *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiasi cha chumvi kilichozalishwa na mradi huo ni karibu tani 60,000 kwa kuwa kiwanda hicho kilifanya kazi mwaka mmoja.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba ni muhimu kuongeza uzalishaji chumvi na kwamba soko la chumvi lipo hapa nchini na nje ya nchi kama vile Rwanda, Burundi, Zaire, Malawi. Wizara yangu itaendelea kuhimiza uzalishaji chumvi ili tuweze kunufaika zaidi na soko lililopo.

Takwimu zilizopo zinaonyesha kuwa mahitaji ya chumvi hapa nchini ni wastani wa tani 120,000 kwa mwaka na kiasi cha chumvi kinachozalishwa na wazalishaji chumvi wote ni wastani wa tani 87,000 kwa mwaka. Mgodi wa chumvi wa Uvinza kwa sasa unauza nje ya nchi wastani wa tani 25,000 za chumvi na kiwango hiki kinategemea kuongezeka kufuatia juhudi za mmiliki wa mgodi huo kuboresha vifaa vilivyopo vya kukaushia chumvi.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa sasa hivi hilo soko kubwa hapa nchini na kuna wafanyabiashara ambao huwa wanapeleka bidhaa hizo nje kama *export*. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuondoa kodi ya bidhaa hiyo ili hao wafanyabiashara waweze kupeleka katika masoko makubwa ya nje bila usumbufu wowote? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kabla hujajibu, idara ya ufundi leo wameachia mitambo haizimi simu kabisa, simu zinaita wakati wote. Tafadhari mrekebishe.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ombi lake tumelisikia tutaliangalia na ikiwezekana tutalifanyia kazi. (*Makofi*)

**MHE. MANJU S. O. MSAMBYA:** Mheshimiwa Spika, katika swali la msingi hoja ilikuwa ni kutengeneza chumvi kwa kutumia nishati ya jua na Mheshimiwa Naibu Waziri, amesema mtambo uliharibika sasa sijui ni mtambo gani uliharibika ni jua liliharibika au vipi? (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kumthibitishia kuwa halikuharibika. Tulichoeleza katika jibu la msingi ni kwamba mtambo ule wa kwanza ndio uliharibika kwa hivi sasa mitambo inafanya kazi. (*Makofi*)

Na. 192

**Sherehe za Kutimiza Miaka 100 ya Vita vya Maji Maji**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI (K.n.y. MHE. DR. SAMSON F. MPANDA)** aliuliza:-

Kwa kuwa tarehe 27/2/2006 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alihudhuria shereza za kuhitimisha miaka 100 ya Vita vya Maji Maji vilivyoanza Songea mwaka 1905 na kwa kuwa, maelezo hayo ni potofu kwani ukweli ni kwamba vita hivyo vilianzia Kilwa kwa Wamatumbi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kusahihisha upotofu huo wa habari na kusema iliyo kweli ili tusiendelee kupotosha historia ya nchi kwa vizazi vijavyo?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Samson Mpanda, Mbunge wa Kilwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa tarehe 27/2/2006 zilifanyika kumbukizia za awali za miaka 100 ya Vita vya Maji Maji. Akisoma risala kwa niaba ya walioandaa sherehe hizo na wananchi wa Mkoa wa Ruvuma kwa Rais, Profesa Amandina Lihamba wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alisema nanukuu: "Vita vya Maji Maji ni mojawapo ya vita kadhaa vilivyopiganiwa nchini mwetu kwa madhumuni ya kuondoa ukoloni. Vita hivi vilidumu kwa muda wa miaka miwili na mwezi mmoja, yaani toka Julai 1905 hadi Agosti 1907. Vilianzia katika Kijiji cha Nandete ambacho leo kiko katika Wilaya ya Kilwa, Mkoa wa Lindi. Lakini baada ya muda mfupi jamii karibu zote za Kusini mwa Tanganyika wakati huo zilijiunga bila kujali tofauti zilizokuwepo miongoni mwao kabla ya ujio wa Mjerumani. Makabila hayo ni pamoja na Wamatumbi ambao ndio waanzilishi, Wazaramo, Wamwera, Wangindo, Wapogoro, Wabena, Wahehe, Wapangwa, Wandendeule na Wangoni" mwisho wa kunukuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo ni dhahiri kuwa historia haikupotoshwa bali iliendelea kukumbukizwa na mchango wa Wamatumbi na Mji wa Kilwa uliwekwa bayana kama chimbuko la mapambano hayo dhidi ya Mjerumani. Hata hivyo ni ukweli usiosutika kuwa Wamatumbi waliungwa mkono na makabila mengine dhidi ya mkoloni wa Kijerumani. *(Makofi)*

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali sasa inatambua kwamba vita vya Maji Maji vilikuwa ni vita vya kupigania uhuru wa nchi hii tofauti na Wakoloni walivyokuwa wanadai ya kwamba ilikuwa ni *Maji Maji Rebellion.* Sasa inajulikana kama *Maji Maji Resistance.* Ili kurekebisha vizuri historia ili isome vizuri kwa vizazi vijazo. Je, Serikali haioni ya kwamba ingekuwa vema kurekebisha vitabu vya historia ili isisemekane ya kwamba Tanzania haijawahi kumwaga damu katika kutafuta uhuru wake na pia hata bendera yetu iongezwe rangi nyekundu kudhibitisha hilo? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika**,** la kwanza katika historia ya nchi yetu imewekwa bayana kwamba vita ya Maji Maji ni sehemu kamili ya historia ya Ukombozi wa nchi yetu. Lakini tunapoamua kama tulimwaga damu katika kupigania uhuru au hatukumwaga damu tunaangalia mtawala wetu wa mwisho alikuwa nani. Mtawala wetu wa mwisho alikuwa Mwingereza, tumepata uhuru kwa majadiliano baada ya kujenga hoja zilizoelewaka. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kabla sijauliza swali langu, nataka

niwapongeze wananchi wa Ruvuma kwa jinsi ambavyo wamejenga minara sehemu zile za historia ya vita vya Maji Maji. Lakini je, kulikoni kulikoanzia vita Kilwa na mwanzilishi Kinjekitile Ngwale. Je, kwa vile kule Kilwa mpaka sasa hivi pale ilipoanzia vita hakuna kumbukumbu yoyote. Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kujenga angalau mnara kwa kutunza historia yetu na heshima ya Kinjekitile Ngwale, mwanzilishi wa Vita vya Maji Maji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, la kwanza tunakubali kama Serikali umuhimu wa kupeleka mnara sehemu ile na tunapokea kwa unyenyekevu na furaha na pongezi hizo kwa niaba ya watu wa Mkoa wa Ruvuma hususan Songea. Swali hili litazingatiwa na kufanyiwa kazi tutashirikiana na Mheshimiwa Mkuchika. Ahsante. (*Makofi*)

**MHE. MWANAWETU S. ZARAFI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hii historia ilipotoshwa hapo ilipokuwa inatakiwa Ruvuma ifanye sherehe hii kwa mara ya kwanza, lakini kihistoria naona kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nimeelewa kwamba ilikuwa kweli ni upotevu kwamba vita ile ilianzia pale na kwa kuwa sherehe hii ilifanyika Ruvuma na kihistoria inaonyesha kwamba hii vita ilianzia Kilwa sehemu ya Kibata na mwanzilishi akiwa Kinjekitile. Je, Waziri anaonaje pia hii sherehe pia ifanyike katika Mkoa wa Lindi kwa kuwa hii vita ilianzia Kilwa? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO - (MHE. EMMANUEL J. NCHIMBI):** Mheshimiwa Spika, la kwanza Serikali imesema wazi kwamba historia haikupotoshwa, iliwekwa vizuri zile zilikuwa sherehe za awali. Waandalizi wa sherehe zile wameandaa Agosti mwakani ziwe sherehe kamili sasa kwa ajili ya kumbukumbu ya vita vya Maji Maji ya miaka 100. Kwa hiyo, zitafanyika katika Kijiji cha Nandete Wilaya ya Kilwa. (*Makofi*)

Na. 293

**Ujenzi wa Vyuo vya Ualimu na Ufundi**

**MHE. ERNEST G. MABINA (k.n.y. MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA)** aliuliza:-

Kwa kuwa, Wilaya ya Geita ni kati ya Wilaya zinazoongoza kuwa na idadi ya wanafunzi wengi nchini na kwa kuwa Wilaya hiyo pia ina tatizo la upungufu wa walimu na kwa kuwa Jimbo la Busanda tuko tayari kutoa eneo bure la kujenga Chuo cha Ualimu na Chuo cha Ufundi:-

(a) Je, Serikali iko tayari kusaidiana na wananchi kutekeleza miradi hiyo katika Jimbo la Busanda?

(b) Kwa kuwa wananchi wa maeneo hayo wako tayari. Je, ni lini Serikali nayo itakuwa tayari kuanza mradi huo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mbunge wa Busanda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, kuna vyuo vya ualimu 52 vilivyosajiliwa, vyuo 32 ni vya Serikali na vyuo 20 visivyo vya Serikali. Aidha kuna vyuo vya ufundi 21 katika Mikoa 18 nchini. Vyuo vya Ualimu ni vya Kitaifa, hupokea wanachuo kutoka Mikoa na Wilaya zote. Wahitimu wa vyuo hivyo hupangwa katika Mikoa na wilaya zote pia. Kutokuwepo chuo cha Ualimu Wilaya ya Geita, hakusababishi wanaohitimu Elimu ya Sekondari kutoka Wilaya hiyo kukosa nafasi za mafunzo ya ualimu katika vyuo vingine vilivyopo nchini na walimu wanaohitimu hupangwa katika Wilaya hiyo.

Kwa sasa Serikali haina mpango wa kujenga Chuo cha Ualimu katika Wilaya ya Geita. Endapo kutahitajika ujenzi wa Chuo kipya cha Ualimu au Chuo cha Ufundi kipaumbele kitakuwa katika Mikoa ambayo haina Vyuo vya Ualimu au Vyuo vya Ufundi.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Geita kwa kuwa tayari kuanza ujenzi wa Chuo cha Ufundi. Nawaomba waendelee na juhudi hizo. Serikali iko tayari kushirikiana na wananchi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwemo ya ujenzi wa Vyuo vya Ufundi Stadi. Hata hivyo ni wajibu wa Wilaya kuandaa mchanganuo wa ujenzi wa chuo hicho.

Mchanganuo huo uonyeshe majukumu ya kila upande yakiwemo yale ya Serikali kupitia *VETA* na upelekwe kwa Mkurugenzi wa *VETA* Kanda ya Ziwa kwa ajili ya tathmini na kuona utekelezaji wake Utakuwa vipi. Kwa sasa sera ya *VETA* ni kusaidia wananchi katika ujenzi na wa Vyuo vya Ufundi na jukumu la uendeshaji wa vyuo hivyo ni la wananchi wenyewe.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imesema kwamba haitakuwa na nafasi ya kujenga Chuo cha Ualimu Wilayani Geita na tatizo kubwa tulilonalo Wilayani Geita ni walimu. Geita haina walimu na wanafunzi ni wengi na shule ni nyingi sana za msingi pamoja na za Sekondari tuna shule 35 za Sekondari. Je, Serikali inaonaje kutoa kipaumbele kuleta walimu wengi wa shule za msingi pamoja wa Sekondari katika Wilaya yetu ya Geita? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Wilaya ina wanafunzi wengi na shule nyingi lakini walimu tunawapanga Kimkoa kama hivi karibuni ambavyo mikoa yote tumewapelekea walimu wa kutosha.

Lakini Mkoa wa Mwanza una vyuo viwili, Chuo cha Butimba ambacho ni chuo kikubwa sana kinatoa walimu wengi na Chuo cha Murutunguru. Sasa vyuo hivi

vinapotoa walimu pamoja na vyuo vingine katika Mikoa mingine nchi nzima wanapangwa nchi nzima na Wilaya ya Geita inapata walimu kwa mtindo huu.

Suala ni Wilaya ya Geita wajipange vizuri ili wale walimu wanaopangwa katika Wilaya ile wawapokee vizuri ili waweze kuwapanga katika shule zao na wale walimu wengine wasiweze kuacha kwenda katika Wilaya hiyo. *(Makofi)*

Na. 194

**Sheria ya *Community Service***

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA** alijibu**:-**

Kwa kuwa, Bunge lilipitisha Sheria ya *Community Service* ili pamoja na mambo mengine kupunguza wafungwa magerezani:-

(a) Je, tangu sheria hiyo ianze kutumika ni wafungwa wangapi wamehusika/wamenufaika?

(b) Je, ni miradi ipi imenufaika?

(c) Je, hali ikoje sasa katika magereza?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu a, b, na c kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Huduma kwa Jamii (*The Community Service Act, No* 6/2002) ilizinduliwa rasmi tarehe 9 Februari, 2005 na wafungwa kuanza kutumikia adhabu zao chini ya Sheria hii, mwezi Julai, 2005. Kwa hivi sasa, Sheria hii inatekelezwa katika Mikoa sita ya majaribio, ambayo ni Dar es Salaam, Mbeya Mtwara, Kilimanjaro, Dodoma na Mwanza.

Nia ya Serikali ni kuhakikisha kuwa Sheria hii inatekelezwa katika Mikoa yote ya Tanzania Bara, ifikapo mwaka wa fedha 2007/2008. Kwa mujibu wa sheria hii, wafungwa wenye makosa madogo madogo ambao vifungo vyao havizidi miaka mitatu, wanapewa adhabu ya vifungo vya nje, badala ya kufungwa magerezani. Wakiwa nje wanatakiwa wafanye kazi za kutumikia jamii bila malipo yoyote hadi muda wa kifungo unapomalizika. Hadi kufikia Mei, 15 2006, idadi ya wafungwa walionufaika na utaratibu huu ni 273

(b) Mheshimiwa Spika, miradi iliyonufaika na utaratibu huu ni pamoja na uzibuaji wa mifereji ya barabara, usafi wa mazingira ya hospitali, zahanati, vituo vya afya na ofisi za Serikali. Miradi mingine ni ujenzi wa madarasa, upandaji wa miti, ukarabati mdogo wa barabara pamoja na utunzaji wa bustani za Halmashauri za Miji na Wilaya.

(c) Mheshimiwa Spika, hali ya msongamano magerezani bado si ya kuridhisha kwa kuwa idadi ya wafungwa wanaotumikia adhabu kupitia sheria hii ni ndogo na sheria hii bado inatekelezwa kwenye mikoa sita kama nilivyosema, wakati idadi ya wafungwa na mahabusu magerezani, inaongezeka siku hadi siku.

Aidha mwaka ujao wa fedha (2007/2008) mikoa mingine sita (6) itaingizwa katika programu hii; Mikoa ya Arusha, Kagera, Mara, Iringa, Shinyanga na Tanga.Hatua hii itaongeza idadi ya wafungwa wa vifungo vya nje na kupunguza msongamano magerezani kwa kiasi fulani. Program hii itakapoenezwa katika Mikoa yote, tunategemea itatupunguza msongamano magerezani. (*Makofi*)

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kunipa nafasi ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza, pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa maelezo yake.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza kwamba sheria hii haijaweza kutekelezwa katika mikoa yote. Hivi ni tatizo gani hasa la msingi linalofanya sheria hii isitekelezwe katika mikoa yote hasa ikizingatiwa kwamba kazi hizi wanazofanya ni kwa manufaa ya jamii. Lakini pia inapunguza msongamano wa wafungwa magerezani. Pia inapunguza gharama kwa Serikali kwa ajili ya kuwatunza wafungwa wakiwa magerezani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, yapo matatizo ya msingi mawili. Tatizo la kwanza ni gharama za *probation officers* Maafisa ambao watatakiwa kupata *training* na kusambazwa kote nchini ili waweze ku-*monitor* na kuangalia shughuli za hao wafungwa wa vifungo vya nje. Ni fedha nyingi na ni gharama kubwa na ndiyo maana mpaka sasa Serikali imeshindwa kutekeleza mradi huu katika mikoa yote ya Tanzania. Lakini lipo tatizo la pili, ni kwamba utaratibu wenyewe wa *Community Service* unahitaji kibali ya Serikali ya Kijiji na wale watu waliofanyiwa makosa kwenye vijiji. Sasa inatokea kwamba katika sehemu nyingine wananchi wanakataa kuwapokea wafungwa hawa wa vifungo vya nje na tunapata matatizo hayo, mpaka hapo itakapofanyiwa marekebisho na uma kuhamasishwa tunadhani mambo yatakwenda vizuri.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge saa ya maswali imekwisha. Ninayo matangazo hapa. Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge wa CCM kutoka Zanzibar anawatangazia Wajumbe wote wa umoja huo kuwa kutakuwa na kikao leo mchana mara baada ya kikao hiki cha asubuhi. Yaani baada ya saa 7. Ukumbi Na. 428 gorofa ya nne jengo la Utawala. Waheshimiwa Wabunge wote wa Zanzibar wa Chama cha Mapinduzi (CCM) wakutane baada ya saa 7.00 mchana Chumba Na. 428. Wajumbe wote Kamati Ndogo ya Ulinzi na Usalama wanatangaziwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Kanali Feteh Saad Mgeni kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo siku ya Jumanne tarehe 12 katika Ukumbi Na. 133, gorofa ya kwanza, jingo la Utawala saa 5 kamili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge kwenye ratiba ya kuwasilisha Makadirio ya Wizara mbalimbali mtaona kwamba kwenye ratiba ilikuwa inaonyesha kwamba kesho ingekuwa ni Wizara ya Maliasili na Utalii halafu ingefuatiwa na Wizara ya Utumishi.

Lakini nimearifiwa na *Chief Whip* na ninatangaza kwa ajili ya maandalizi kwa sababu wengine mngependa kuchangia. Sasa kinachotangulia ni kuwasilishwa kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi kesho tarehe 13 Julai, 2006. Kesho kutwa ndiyo Wizara ya Maliasili na Utalii, wamebadilishana, kwa hiyo siku moja. Naomba mzingatie hilo ili mnapoleta maombi ya kuchangia mjue kwamba kesho ni Ofisi ya Rais, Utumishi, kesho kutwa ndiyo Maliasili na Utalii.Baada ya hayo namwita Katibu kwa shughuli zinazofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007
### Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)

**WAZRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2006/07.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kuwa hapa sote kutekeleza jukumu kubwa la kikatiba. Nampongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Amani Abeid Karume, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa ushindi wao mkubwa na wa kishindo walioupata katika uchaguzi huo.

Napenda pia kuchukua fursa hii kuungana na wenzangu kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa kwa kuteuliwa kushika wadhifu huu muhimu katika uongozi wa taifa letu aidha, hotuba yake ambayo imetoa malengo yatakayowezesha usimamizi thabiti katika kutekeleza shughuli mbalimbali za Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007. *(Makofi)*

Aidha, napenda kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kuchaguliwa kushika nyadhifa hizo. Nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri, Naibu Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushindi uliowawezesha kuja kuwawakilisha na kuwahudumia wananchi katika kipindi hiki cha miaka mitano. Nampongeza tena Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na hatimaye kuchaguliwa katika nafasi za Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwashukuru Waziri wa Mipango, Uchumi, na Uwezeshaji, Mheshimiwa Dr. Juma Alifa Ngasongwa; na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Zakhia Hamdani Meghji. Hotuba zao zimefafanua sera za jumla za uchumi na fedha na kuweka mwelekeo wa hatua ambazo Serikali inachukua kuimarisha uchumi pamoja na kupambana na umaskini na utoaji wa huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, kutokana na uchaguzi wa Chama cha Mapinduzi uliofanyika hivi karibuni, napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Lt. Yusufu Makamba kuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Capt. Jaka Mwambi kuwa Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, kuwa Katibu Mwenezi, Mheshimiwa Rostam Azizi kuwa Mweka Hazina, Mheshimiwa Asha Rose Migiro, kuwa Katibu wa Ushirikiano wa Kimataifa na Mheshimiwa Kidawa Saleh, kuwa Katibu wa Mipango na Oganaizesheni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Job Ndugai. Kamati ya Kudumu ya Sheria, Katiba na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa George Lubeleje

Kamati ya Maliasili na Mazingira ilifanya uchambuzi wa kina wa sekta ya Mazingira na Kamati ya Kudumu ya Sheria, Katiba na Utawala ilifanya uchambuzi wa masuala muhimu ya Muungano. Maoni na maagizo ya Kamati hizi yamezingatiwa katika kukamilisha makadirio haya. Maoni na maelekezo hayo yataisadia Serikali katika utekelezaji wa mipango yake katika kipindi cha mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2005/2006 na matarajio katika kipindi cha mwaka 2006/2007. Makamu wa Rais ana majukumu mahsusi ya kitaifa ya kumsaidia na kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala yote ya nchi kwa ujumla. Ofisi ya Makamu wa Rais pia inaratibu shughuli za Mazingira na Muungano kama ifuatavyo:-

Kutoa ushauri juu ya masuala ya mazingira kisera na kitaalamu;

Kuratibu kwa mapana programu za mazingira,

Kuratibu mipango na miradi ya sekta hii mtambuka iliyo nje ya uwezo wa sekta moja moja;

Kuendeleza mchakato wa uratibu ili kuhakikisha kwamba sera, mikakati ya maendeleo na shughuli zinazogusa mazingira zinatekelezwa,

Kushirikisha umma na kupokea ushauri wa kisayansi ili maamuzi yenye manufaa yafikiwe,

Kukuza ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya mazingira kwa manufaa ya taifa,

Kulinda, kuendeleza na kuratibu masuala ya Muungano na yasiyokuwa ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi kilichopita cha mwaka 2005/2006, nchi yetu ilikabiliwa na shughuli muhimu za Uchaguzi Mkuu. Katika kipindi hicho kati ya mwezi Agosti na Desemba 2005, Mheshimiwa Makamu wa Rais alifanya ziara nchi nzima, Tanzania Bara na Zanzibar, kuwatembelea na kuzungumza na wananchi kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo, ikiwa ni pamoja na Uchaguzi Mkuu.

Katika ziara zake, Mheshimiwa Makamu wa Rais alitumia fursa hiyo kuwahamasisha na kuwahimiza, wananchi kushiriki kikamilifu katika uchaguzi huo na kutumia haki yao kikatiba ya kuwachagua viongozi wanaowafaa kusimamia maendeleo yao na kuendeleza demokrasia hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira ya Nchi yetu, Mheshimiwa Makamu wa Rais alitoa tamko rasmi la Serikali kuhusu suala la hifadhi ya mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji. Alieleza hatua za haraka za kuinusuru nchi yetu kupatwa na janga ikiwa uharibifu na uchafuzi wa rasilimali hiyo muhimu utazidi kuendelea. Tamko la Mheshimiwa Makamu wa Rais limeleta msukumo mpya na matumaini mazuri katika suala la hifadhi ya mazingira.

Katika kipindi hiki Mheshimiwa Makamu wa Rais alitembelea maeneo mbali mbali yaliyoathiriwa na mafuriko kujionea uharibifu uliotokea na kuwafariji wananchi waliopatwa na maafa.

Aidha, Mheshimiwa Makamu wa Rais alitumia fursa ya ziara zake za mikoani kuwashukuru wananchi kwa kuweza kuichagua na kuiweka madarakani Serikali ya Awamu ya Nne chini ya Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Spika, mapema mwezi Mei, mwaka huu, Mheshimiwa Makamu wa Rais alimwakilisha Mheshimiwa Rais katika kikao Maalum cha Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika kilichofanyika mjini Abuja, Nigeria. Kikao hicho muhimu kiliitishwa kujadili mafanikio, na mikakati mipya ya utekelezaji wa Azimio la Abuja kuhusu mapambano dhidi ya Ukimwi, Kifua kikuu na Malaria katika nchi za Afrika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makamu wa Rais alifungua mkutano wa Waziri Mkuu wa Serikali ya Muungano wa Tanzania na Waziri Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulioitishwa kufuatia agizo la Mheshimiwa Rais Kikwete kukaa pamoja na kuzungumzia matatizo ya Muungano. Alisema, dhamira ya dhati, mashirikiano na maelewano katika kushughulikia kero za Muungano ndiyo njia sahihi ya kuyapatia ufumbuzi matatizo hayo. Alisisitiza haja ya vikao husika vya masuala ya Muungano kufanyika kila mara na maamuzi yake kutekelezwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makamu wa Rais alihudhuria Mkutano wa Tatu wa Dunia kuhusu Makazi Mijini *(Third World Urban Forum)* uliofanyika Vancouver, Canada, tarehe 19 hadi 23 Juni, 2006. Mkutano huo uliitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi ya Binadamu, *UN-HABITAT* ambapo alihutubia mkutano huo wakati wa ufunguzi akitoa mtazamo wa nchi zinazoendelea na mada ya mkutano ikiwa ni Mstakabali Wetu. Miji Endelevu-kutekeleza Dhana katika Kitendo *Our Future: Suistainable Cities-Turning Ideas Into Action.* Katika hotuba yake, Mheshimiwa Makamu wa Rais alitoa wito kwa Jumuiya ya kimataifa kuyaimarisha kifedha na kiutendaji mashirika ya kimataifa yaliyoundwa kushughulikia maendeleo endelevu ya miji duniani ili yaweze kuzisaidia nchi, hasa zile zinazoendelea, zifanikishe lengo la maendeleo ya milenia la kuwapatia makazi bora, ifikapo 2020, watu milioni 100 wanaoishi katika makazi duni mijini. Tarehe tarehe 29 Juni 2006, alifanya ziara mjini Ndola Zambia, kwa lengo la kuhudhuria Maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara. Katika hotuba yake Mheshimiwa Makamu wa Rais aliwahimiza wafanyabiashara kutumia kikamilifu fursa zinazotolewa na Maonyesho hayo ili kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kati ya Tanzania na Zambia. Tarehe 1 Julai 2006, Mheshimiwa Makamu wa Rais pia alifanya ziara nchini Burundi katika maadhimisho ya sikukuu ya uhuru wa nchi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 47(1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu wa Rais amepewa jukumu la kumsaidia Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano kwa jumla hususan, kufuatilia utekelezaji wa siku hadi siku wa Mambo ya Muungano. Aidha, Serikali ilitunga Sheria Na. 34 ya mwaka 1994 iliyoanzisha Ofisi ya Makamu wa Rais ikiwa na majukumu ya kuratibu mambo ya Muungano na kuwa kiunganishi kati ya Serikali zetu mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuongeza ushirikiano kwa mambo yote ambayo si ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2005/2006 iliendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji katika sekta mbalimbali kama ifuatavyo; Sekta ya fedha imeandaa mkakati wa pamoja wa misaada, yaani *Joint Assistance Strategy (JAS)* ambao maandalizi yake yameshirikisha pande zote za Muungano na wafadhili. Mkakati huu utasimamia ushirikiano wa Tanzania na wafadhili watakaokubali kuingia katika makubaliano ya kutoa misaada hiyo. *(Makofi)*

Upatikanaji na ugawaji wa misaada na mikopo toka nje umeendelea ambapo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kupata gawio la asilimia 4.5. Utaratibu wa kudumu wa mgao kwa Zanzibar unafanyiwa kazi na Tume ya Pamoja ya Fedha, ambapo mstadi aliyepewa kazi hii ameshakamilisha kazi. Kwa hivi sasa Tume inachambua taarifa hiyo ili kuwasilisha mapendekezo kwa Serikali zetu mbili za Muungano.

Mheshimiwa Spika, Tanzania imeendelea kufaidika na msamaha wa madeni toka kwa wafadhili *(Multilateral Debt Relief Initiative).* Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetengewa asilimia 4.5 kutokana na msamaha huo kwa ajili ya kugharimia uagizaji bidhaa kutoka nje. Aidha misamaha ya Benki ya Dunia na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(Africa Development Bank-ADB)* itafuata mgao uliokubalika.

Mheshimiwa Spika, umewekwa utaratibu wa kukopa nje, ambao unaishirikisha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Waziri wa Fedha wa Serikali ya Muungano wa Tanzania ndiye mwenye mamlaka ya kukopa baada ya kuwasiliana na Kamati ya Kudhibiti Madeni. Kamati hii inajumuisha wajumbe kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar akiwemo Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Maombi ya mikopo ya Zanzibar yanazingatiwa ipasavyo. Aidha, utaratibu utaanzishwa ambao utaiwezesha Zanzibar kukopa katika soko la ndani bila dhamana ya Serikali ya Muungano wa Tanzania ili Serikali ya Muungano wa Tanzania isilazimike kulipa madeni hayo iwapo Zanzibar itashindwa kulipa.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya tathmini ya mapato halisi kutokana na vyanzo mbalimbali vya Muungano na gharama halisi za kuendesha Mambo ya Muungano. Katika kutimiza jukumu hili, Tume ya Pamoja ya Fedha imefanya kazi ya kubainisha Wizara, Asasi na Idara zinazohusiana na Mambo ya Muungano, na kuchanganua gharama za kuendesha mambo ya Muungano katika kipindi cha kuanzia mwaka 1993 hadi 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya kazi hii imechangia katika kazi ya kubainisha vyanzo vya mapato vya Muungano na vigezo vya kugawana mapato na kuchangia gharama za Muungano. Mstadi aliajiriwa ili kupendekeza utaratibu wa kugawana mapato ya Muungano na kuchangia gharama za Muungano. Taarifa ya Mstadi huo imekamilika na Tume inafuatilia uchambuzi yakinifu ili kuleta maoni kwa Serikali zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki Kuu ya Tanzania ni Asasi ya Muungano na mtaji wake ulitolewa na Hazina ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na muafaka wa mwaka 1994 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inapokea mgao wa asilimia 4.5 unaotokana na faida za benki hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mambo ya Nchi za Nje yameendelea kuratibiwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania. Watumishi katika Wizara na Balozi za Tanzania nje ya nchi wanatoka katika sehemu zote za Muungano ambapo kwa upande wa Zanzibar kuna Naibu Waziri mmoja, mabalozi watatu na watumishi 26. *(Makofi)*

Aidha, uwakilishi wa kimataifa umendelea kuratibiwa na Serikali ya Muungano wa Tanzania, kwa sababu Jumuiya za Kimataifa zinaitambua Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tu. Hivyo Tanzania inaposimama mbele ya mataifa mengine ni vyema ikaonyesha sura ya Muungano kwa kuwa na mchanganyiko wa watu toka pande zote mbili za Muungano. Utaratibu unaandaliwa ili kabla ya kwenda kwenye mikutano ya Kimataifa wahusika wakutane na baada ya vikao hivyo, taarifa za pamoja ziandaliwe na utekelezaji wa maamuzi uzingatiwe.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Mei 2006, ulifanyika mkutano kati ya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ambao ulijadili Masuala ya Muungano, ambayo ni :-

Uvuvi katika ukanda wa Bahari Kuu.

Utekelezaji wa Sheria kuhusu Haki za Binadamu.

Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi.

Ugawaji wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nchi za nje, Faida ya Benki Kuu na mikopo.

Katika kikao hicho mambo yafuatayo yalifikiwa muafaka:-

Wizara ya Mali Asili na Utalii itayarishe Muswada wa kuunda Mmamlaka ya Uvuvi katika Bahari Kuu na upelekwe Bungeni mapema iwezekanavyo. Aidha serikali ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikubaliana kimsingi

Kuhusu mapato yatokanayo na uvuvi ambapo, asilimia hamsini (50%) itatumika kugharimia shughuli za Mamlaka ya Uvuvi na itakayobakia itagawanywa kwa uwiano wa asilimia sitini (60%) kwa Serikali ya Muungano wa Tanzania na asilimia arobaini (40%) kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Sheria kuhusu Haki za Binadamu, ni suala la kikatiba na ni la Muungano kama inavyoonekana katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipengele cha kwanza. Hata hivyo Sheria hii haikuweza kutumika Tanzania Zanzibar kwa kuwa haikumtaja Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora ambaye anawajibika kupeleka ripoti za Tume kwenye Baraza la Wawakilishi. Hivyo ilikubalika katika Sheria hii, yafanywe marekebisho yatakayomtaja Waziri mwenye dhamana ya Utawala Bora Zanzibar ili awe na uwezo wa Kisheria kufikisha ripoti za Tume katika Baraza la Wawakilishi. Baada ya marekebisho hayo ya Sheria, Tume itaweza kufanya kazi zake Zanzibar bila kikwazo chochote.

Kuhusu Utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia, ilikubalika kuwa Wizara ya Nishati na Madini itafute Mshauri Muelekezi ambaye atazishauri Serikali zote mbili juu ya mgawanyo wa fedha zitakazopatikana kutokana na mafuta na gesi asilia. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ilitaka madini yote yaongezwe katika orodha ya mambo ya Muungano. Kikao kiliamua kupeleka suala hili kwa wakuu wa Nchi ili watoe maelekezo yao.

Suala la ugawaji wa mapato yatokanayo na misaada kutoka nchi za nje, Faida ya Benki Kuu na mikopo lilijadiliwa. Ilivyo hivi sasa Zanzibar inapata mgawo wa asilimia 4.5. Katika kikao hiki ilikubaliwa kuwa ni vema ikasubiriwa taarifa kutoka Tume ya Pamoja ya Fedha ambayo inaendelea na mchakato wa jinsi gani mapato hayo yatagawanywa. Tume hiyo inategemewa kumaliza kazi hiyo mwaka huu na kuwasilisha Taarifa kwa Serikali zote mbili za Muungano.

Aidha, Kikao kilijadiri kero kuhusu utozaji wa mapato katika pande zote mbili za Muungano. Ilikubalika kuwa iundwe Kamati itakayojumuisha wajumbe kutoka Wizara za

Fedha wa pande zote mbili za Muungano, itakayokuwa na jukumu la kupitia maeneo yote yenye kasoro na kuleta mapendekezo yao ya utatuzi wa kasoro hizo katika kikao kijacho.

Mheshimiwa Spika, Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba, miradi ya pamoja inaandaliwa na kutekelezwa katika pande zote mbili za Muungano, hii ikiwa ni pamoja na mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*Tanzania Social Action Fund-TASAF),* ambapo jumla ya miradi 76 ilitekelezwa Zanzibar mpaka sasa, ambayo kwa upande wa Unguja ni miradi 43 na Pemba miradi 33. Kati ya miradi hiyo 70 imekamilika na miradi sita inaendelea. Aidha, mradi wa kutoa mikopo kwa ajili ya miradi midogo midogo ; *Small Entrepreneur Loan Facility (SELF)* ulitekelezwa ambapo jumla ya shilingi Milioni 190.5 zilitolewa kwa vikundi na Mashirika yasiyo ya kiserikali 6 ya Zanzibar. Mchanganuo wa mikopo hii ni kama ifuatavyo ; Changamoto shilingi milioni 54, *Pride Tanzania* shilingi milioni 94, Karafuu ni Uhai shilingi milioni 12.5, *ZATTAG SACCOs* shilingi milioni 15, Akiba Haiozi shilingi milioni 10 na Utalii *SACCOs* shilingi milioni 5. Mafunzo na semina mbalimbali kuhusu miradi midogo midogo yalifanyika kwa watu 3,000 toka Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya habari imeweza kuandaa taarifa na makala mbalimbali zinazohusu masuala ya Muungano na kuvirusha hewani kwa nia ya kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kuimarisha na kuendeleza Muungano wetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ili Muungano wetu uweze kuimarika na kuendelea, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2006/07 inatarajia kuanzisha mfumo wa mawasiliano ambao utatumika katika tafiti mbalimbali zitakazohusu Mambo ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali zetu mbili kwa lengo la kuondoa matatizo mbalimbali ya Muungano yaliyopo na yatakayojitokeza. Ili kufikia lengo hili Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya vikao na wadau wote wa Mambo ili kuweza kukusanya maoni mbalimbali ya namna ya kuboresha ushughulikiaji wa masuala haya na kisha kuandaa taarifa na kuzisambaza kwa wadau. Aidha, taarifa pamoja na kumbukumbu mbalimbali za Muungano zitahifadhiwa katika Maktaba ya kielektroniki *(Electrononic Library)* ambapo wadau wa Muungano watakuwa na haki ya kupata taarifa sahihi za Muungano wetu. Vifaa mbalimbali vimeshapatikana kwa ajili ya maktaba hiyo, na kwa hivi sasa juhudi za kukusanya nyaraka mbalimbali zinaendelea ili kuweza kuzihifadhi katika mfumo wa kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ili kuwa na uwezo wa kutosha wa kushughulikia Muungano wetu, mafunzo kwa watumishi sita wa Ofisi ya Makamu wa Rais yatatolewa katika stadi ya habari mawasiliano na uperembaji. Muungano wetu unakua na umepitia hatua mbalimbali hivyo imejitokeza haja ya kuongeza maeneo mengine katika orodha ya mambo ya Muungano. Ili uratibu wa Mambo ya Muungano ufanyike kwa ufanisi zaidi kila Wizara, Idara na Asasi za Muungano na zile ambazo si za Muungano katika Serikali zetu mbili zitafanya angalau vikao viwili kwa mwaka kuanzia Julai, 2006 na taarifa za maamuzi ya vikao hivi zitawasilishwa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa uratibu na kufuatilia utekelezaji wake. Katika kufikia lengo hili Ofisi ya Makamu wa Rais itaandaa

na kushiriki katika vikao vyote na kupitia taarifa za vikao hivyo na kuandaa mapendekezo yake kwa Serikali zetu mbili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itachukua hatua za makusudi kuelimisha jamii kuhusu Mambo mbalimbali ya Muungano wetu. Katika kutekeleza jukumu hili Idara itafanya yafuatayo:-

Kuandaa makala nne za Jarida la Muungano na kuzisambaza kwa wadau.

Kuandaa vipindi 24 vya radio vinavyohusu masuala ya Muungano na kuvirusha hewani.

Kuandaa vipindi 24 vya Televisheni juu ya Mambo ya Muungano na kuvirusha hewani.

Aidha, utaanzishwa ukurasa wa Mambo ya Muungano na kuunganisha katika tovuti ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, tarehe 26, Aprili kila mwaka ni siku ya kuadhimisha kuanzishwa kwa Muungano wetu. Shughuli mbalimbali zinafanyika katika kuuenzi na kuundeleza Muungano wetu ikiwa ni pamoja na kuwaenzi waasisi wa Muungano wetu ambao ni Hayati Mwalimu J.K. Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Aman Karume.

Ofisi ya Makamu wa Rais itashiriki kikamilifu katika maandalizi na kuhudhuria Sherehe za Muungano ikiwa ni pamoja na kufuatilia matukio mbalimbali yatokanayo na sherehe hizo.

Aidha, utaandaliwa utaratibu wa kukusanya maoni toka kwa wadau wa Muungano, kuyafanyia upembuzi na kutoa mapendekezo kwa Serikali zote mbili. Ofisi ya Makamu wa Rais itafanya uperembaji na tathimini katika utekelezaji wa mambo mbalimbali ya Muungano na kutoa mapendekezo kwa Serikali zetu mbili. Tathmini itafanyika kila baada ya robo mwaka kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Idara na kuandaa taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais itaandaa vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi angalau vitatu kwa mwaka wa fedha 2006/2007, ambavyo vitatanguliwa na vikao vya Wataalamu na Mawaziri wa Sekta husika. Vikao hivi ni muhimu sana katika kuboresha na kuondoa kero za Muungano.

Mheshimiwa Spika, juhudi za kuondoa umaskini na kuleta maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii haziwezi kufanikiwa katika mazingira yaliyoharibika na uzalishaji ulio duni. Katika mazingira ya aina hii, ni vigumu kujikwamua na umaskini kwa sababu juhudi za maendeleo na ustawi wa jamii hurudishwa nyuma na matatizo yanayotokana na uharibifu wa mazingira tunayoyategemea.

Umaskini hauwezi kuondolewa pasipo juhudi za dhati na mafanikio katika kuhifadhi mazingira ya nchi yetu. Kwa kutambua haya, Serikali ya Awamu ya nne imetoa msukumo maalum kwa hifadhi ya mazingira ili kushughulikia changamoto mbalimbali ambazo zinalikabili Taifa letu. Sambamba na maelekezo ya Ilani ya uchaguzi ya CCM 2005, kwa kuanzia Serikali imepitisha Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji ambapo hatua mbalimbali zinachukuliwa ili kukabiliana na changamoto 12. Changamoto hizo ni:-

Uharibifu wa mazingira utokanao na uvamizi wa wafugaji kwenye maeneo ya vyanzo vya maji;

Uharibifu wa mazingira kutokana na uvamizi wa shughuli za kilimo kwenye miteremko ya milima, mabonde na vyanzo vya maji;

Uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji miti kwa ajili ya kuni na mkaa na ujenzi wa nyumba mijini;

Umwagiliaji usiokuwa endelevu unaosababisha kutoweka kwa bioanuai na upungufu wa maji ya kuendeshea mitambo ya kuzalisha umeme;

Ukosefu wa kumbukumbu, takwimu sahihi na za kutosha kuhusiana na vyanzo vya maji na kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi na maendeleo katika ngazi ya wilaya.Changamoto nyingine ni:-

Uharibifu wa mazingira na wa vyanzo vya maji utokanao na moto. Kukauka kwa vyanzo vya maji kutokana na aina ya miti inayotumia maji mengi;

Kuenea kwa hali ya jangwa na ukame katika maeneo mengi nchini;

Uelewa na ushiriki mdogo wa wananchi katika hifadhi ya mazingira;

Migongano katika matumizi ya ardhi baina ya wadau mbalimbali na uharibifu wa mazingira unaotokana na migongano hii; na

Uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za uchimbaji madini na Uchafuzi wa mazingira utokanao na taka za plastiki.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006 hatua mbalimbali za kutekeleza Mkakati zimechukuliwa. Hatua hizo ni pamoja na:-

Kuondoa wavamizi katika vyanzo vya maji hasa katika bonde la Usangu. Kuhamasisha jamii juu ya mkakati katika ngazi zote;

Kuimarisha udhibiti wa ukataji holela wa miti kwa ajili ya mkaa na kuni; na

Kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kuhifadhi mazingira na upandaji miti nchini.

Pamoja na mkakati huu, katika kipindi cha 2005/2006 shughuli mbalimbali za hifadhi ya mazingira zilitekelezwa. Shughuli zilizotekelezwa zililenga katika:- utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004; kutekeleza programu na miradi mbalimbali ya hifadhi ya mazingira; kutekeleza mikataba na itifaki za kimataifa zinazohusu mazingira; utoaji wa tuzo ya Rais ya uongozi na ubora wa hifadhi ya mazingira katika uchimbaji wa madini; na hatua mbalimbali za ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu mwezi Novemba mwaka 2004, ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 2005.

Kanuni zinazohusu Tathmini ya Athari kwa Mazingira, Ukaguzi wa Uharibifu wa Mazingira, pamoja na Kanuni za Usajili wa Wataalamu wa Mazingira ziliandaliwa. Aidha Sheria hii imetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili iweze kuwafikia na kueleweka na wananchi wengi zaidi. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria hii, ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni, miongozo, viwango vya mazingira na taratibu zilizobaki ili kuiwezesha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kutekelezwa kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kukuza weledi wa wananchi juu ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais inakamilisha maandalizi ya Programu ya Kujenga Uwezo wa Wadau kuielewa na kuitekeleza Sheria hii kikamilifu. Programu hii itakamilishwa katika kipindi cha mwaka 2006/2007. Aidha, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira inaelekeza kuteuliwa kwa Waratibu wa Mazingira katika Wizara, kuteuliwa kwa Wataalamu wa Usimamizi wa Mazingira katika Mikoa, pamoja na Maafisa Mazingira katika ngazi zote za Serikali za Mitaa. Katika kipindi cha 2005/2006, Ofisi ya Makamu wa Rais imewasiliana na Sekta husika pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu uteuzi huu. Tayari baadhi ya Wizara zimeunda Sehemu za Mazingira pamoja na kuwateua Waratibu wa Mazingira katika sekta zao. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kushirikiana na Wizara mbalimbali pamoja na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kukamilisha zoezi la uteuzi wa Waratibu wa Mazingira wa Sekta zilizobaki na Maafisa wa Mazingira katika ngazi mbalimbali za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Jumla ya mbawakavu milioni 36 walizalishwa katika vituo 13 na kusambazwa katika maeneo kando kando ya ziwa na mto Kagera. Juhudi za kuondoa magugu kwa kutumia zana nyepesi ziliendelea, hususan katika mialo na sehemu za kuvutia maji, ambapo magugu maji yamethibitiwa kwa karibu asilimia 90. Kwa kushirikiana na vikundi vya doria dhidi ya uvuvi haramu ulinzi umezidi kuimarika. Zaidi ya zana haramu za uvuvi 1,144 zilikamatwa na wahalifu 217 walikamatwa. Jumla ya vifaranga 1000 vilisambazwa kwa wakulima wa Igunga, Tabora. Mwongozo wa ufugaji bora uliandaliwa kwa ajili ya kusambazwa. Wataalamu walitoa ushauri wa ufugaji bora kwa wafugaji wa mikoa ya Mwanza, Mara na Kagera.

Aidha, utafiti umeendelea kufanyika, hususan kwenye maeneo 18 yaliyoathirika kutokana na shughuli mbalimbali, yaliyoko Bukoba 6, Mwanza 6, na Musoma 6. Utafiti wa maji machafu yaingiayo ziwani uliendelea kwenye mto wa Kagera na mto wa Mara. Kituo cha uzalishaji bora viwandani *(Cleaner Production Centre)* kinafuatilia kwa karibu viwanda vinavyo husika katika utekelezaji wa programu ya hifadhi ya mazingira ya ziwa Victoria. Viwanda 12 vilivyoko katika mikoa ya Mwanza, Kagera na Mara vinavyotekeleza mbinu za kupunguza taka kwa dhana ya uzalishaji bora vilifanyiwa tathmini na taarifa iliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Elimu na uhamasishaji wa wananchi umeendelea. Mkazo umewekwa zaidi katika kuhifadhi misitu ya asili na kutoa mafunzo ya uhifadhi wa udongo. Jumla ya wanavijiji 378 wa maeneo ya Mayega, Lamadi na Nyitundu wameelimishwa kuhusu hifadhi ya udongo na matumizi sahihi ya madawa ya kilimo. Miti milioni 3.1 ilipandwa, kati ya hiyo milioni 2.4 ilipona, ambayo ni sawa na asilimia 79.

Semina na warsha zilizowahusisha wanavijiji kuhusu hifadhi ya maeneo oevu zilifanyika. Aidha, mipango ya kukarabati na kusimamia maeneo oevu iliandaliwa kwa ajili ya utekelezaji. Miradi 4 ya ujenzi wa madarasa ya shule; ujenzi wa visima vifupi vya maji 3; zahanati 4 na miradi ya kuvuna maji ya mvua katika shule 3 imekamilika. Mwanafunzi 1 anaendelea na mafunzo ya Udaktari wa Falsafa na mwanafunzi mwingine anaendelea na mafunzo ya Uzamili kwa ufadhili wa programu hii. Wadau wote wameendelea kuelimishwa na kuhamasishwa kwa njia ya redio, luninga, warsha, magazeti, vijarida na vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/06, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikamilisha taratibu zote za kuanza utekelezaji wa programu ya Hifadhi ya Mazingira ya Bonde la ziwa Tanganyika. Akaunti ya mradi ilifunguliwa mjini Kigoma/Ujiji; taratibu za ajira za watumishi wa utekelezaji wa programu zilikamilika; na ofisi ya utekelezaji wa programu ilipatikana na kuandaliwa. Napenda kuchukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa mkoa wa Kigoma kwa kutoa na kuandaa ofisi kwa shughuli za programu hii.

Mheshimiwa spika, Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, miradi 3 ya utekelezaji wa programu hii itaanza kutekelezwa. Miradi hii ni; mradi wa hifadhi ya mazingira ya bonde la ziwa *(Catchment),* kwa gharama ya shilingi bilioni 2.2, ikiwa ni msaada kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(Global Environment Facility (GEF)* kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(United Nations Development Programme (UNDP);* mradi wa usimamizi na udhibiti wa Majitaka katika manispaa ya Kigoma/Ujiji utakaogharimu shilingi bilioni 6 ikiwa ni mkopo kutoka *Nordic Development Fund,* na msaada wa shilingi milioni 300 kutoka *GEF* kupitia *UNDP;* na mradi wa uvuvi endelevu na hifadhi ya mazingira, utakaogharimu shilingi bilioni 7.4, ikiwa ni mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB).*

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza Mradi wa Ushirikishwaji wa Wananchi katika Kuhifadhi Maliasili na Usimamizi wa Mazingira ambao unafadhiliwa na Serikali ya Marekani. Katika kipindi hiki shughuli zifuatazo zilifanyika: kuanzishwa kwa Hifadhi ya Jamii *(WMA)* ya Kijiji cha Burungi Wilayani Babati; kukamilisha Ujenzi wa Shule ya Msingi Katika Ranchi ya Manyara iliyopo chini ya *Tanzania Land Conservation Trust (TLCT);* ununuzi wa Madume 10 ya ng'ombe kwa ajili ya kuboresha mifugo ya *Ranch* ya Manyara; kuendesha warsha ya ushirikishwaji kwa ajili ya kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi kwa vijiji 6 katika Wilaya ya Simanjiro; na kukamilisha matengenezo ya barabara katika Hifadhi za Taifa za Tarangire na Manyara.

Aidha, wakulima 20 kutoka wilaya za Mpanda, Sikonge, Uyui na Urambo wamepata mafunzo ya kilimo cha mseto. Jumla ya hekta 169, 198 zimetengwa kama maeneo ya hifadhi ya vijiji vinavyozunguka hifadhi ya akiba ya Ugalla. Eneo la hifadhi ya msitu wa Mpanda Kaskazini Mashariki *(Mpanda North-East)* pamoja na makazi ya wakimbizi ya Katumba yaliyomo ndani ya hifadhi hiyo limepimwa na kuandaliwa ramani. Mradi huu pia umegharimia maandalizi ya Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa Sheria ya usimamizi wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kuwa pamoja na kwamba mradi huu umekamilika katika kipindi cha mwaka jana, Serikali imekubaliana na Serikali ya Marekani kuendelea kutekeleza shughuli zilizoanzishwa chini ya mradi.

Katika makubaliano hayo, Programu ya Usimamizi wa hifadhi ya Mazingira na Maliasili *(Environment and Natural Resources Programme)* itatekelezwa. Programu hii ni ya miaka kumi, kuanzia Oktoba 2005 hadi Septemba 2014. Programu itatekeleza Sera na Sheria za Sekta mbalimbali zinazohusika na Hifadhi ya Mazingira na Maliasili, na Maendeleo, ikiwa ni pamoja na kuhuisha masuala ya mazingira katika sera, sheria na mikakati ya kisekta na katika MKUKUTA. Programu itasaidia pia ushirikishwaji wa wananchi katika kupanga, kusimamia na kutekeleza shughuli mbalimbali zinazohusu mazingira na matumizi ya maliasili. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na mambo mengine katika kutekeleza Programu ya Usimamizi wa Mazingira na Maliasili itaendesha warsha za mafunzo kwa wataalamu wa Sekta mbalimbali, Mahakama na Serikali za Mitaa kuhusu Sera na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Programmu hii itagharimu shilingi milioni 20 za sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba katika kikao cha bajeti cha bunge lako tukufu mwaka 2004/2005 Ofisi ya Makamu wa Rais ilitoa taarifa kuhusu kukamilika kwa maandalizi ya programu ya hifadhi ya mazingira ya Bonde la Ziwa Nyasa, kwa ushirikiano na nchi za Malawi na Msumbiji. Kwa sababu ya ukosefu wa fedha, programu hiyo haikutekelezwa kama ilivyokusudiwa. Bonde la Ziwa Nyasa linakabiliwa na matatizo ya uharibifu wa mazingira kutokana na kilimo kisicho endelevu katika Bonde; ukataji wa miti hovyo; na uvuvi usioendelevu. Hali hii imesababisha kuongezeka kwa virutubisho ndani ya Ziwa na upungufu mkubwa wa samaki na viumbe wengine katika ziwa. Matarajio ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha 2006/2007 ni kufanya maboresho ya programu hii na maandalizi ya utekelezaji kwa kutumia fedha zetu na za wafadhili, zitakapopatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu, kitaifa, Programu ya hifadhi ya mazingira ya Bonde la mto Nile, inayotekelezwa pia na nchi tisa zilizo katika bonde hili. Nchi hizo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC),* Burundi, Rwanda, Uganda, Kenya, Sudan, Ethiopia na *Egypt.* Programu hii ilizinduliwa mnamo mwezi Mei 2004, na ni ya miaka mitano. Ofisi ya kanda ya uratibu ya uendeshaji wa programu iko mjini Khartoum, Sudan, na kila nchi husika inayo ofisi ya uratibu, kitaifa. Lengo kuu la programu hii ni kuandaa mkakati wa usimamizi wa mazingira ya bonde na maji ya mto Nile. Programu hii inalenga katika kujenga uwezo na mfumo wa ushirikiano katika kusimamia kuhifadhi na kulinda mazingira ya bonde la mto Nile kufuatana na matarajio ya dira ya pamoja. Programu ina vipengere muhimu vifuatavyo: ushirikishaji jamii kwenye hifadhi ya ardhi, misitu na maji kwa ajili ya kugharamia miradi midogo midogo ya wananchi; kutoa elimu ya mazingira kwa umma; hifadhi ya ardhi oevu na bioanuai; na uperembaji wa hali ya ubora wa maji katika bonde la mto Nile. Ofisi ya mratibu wa kitaifa wa miradi midogo midogo *(micrograns)* iko Jijini Mwanza. Programu inafadhiliwa na Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(GEF)* kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Benki ya Dunia, na Shirika la Maendeleo la Canada *(CIDA).* Programu itagharimu dola za Marekani milioni 3.6.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 kazi zifuatazo zilifanyika: kuendesha mafunzo juu ya utayarishaji wa vitini vya kufundishia elimu ya mazingira kwa walimu wa vyuo vya ualimu katika kanda ya ziwa, ambapo walimu 18 kutoka vyuo 8 walishiriki; kuendesha warsha ya maafisa wa rasilimali za maji na maabara za maji kuhusu usimamizi wa hali ya ubora wa maji katika bonde la mto Nile. Kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, shule kumi za Sekondari zilishirikishwa, ambazo ni Seminari ya Makoko (Musoma), Shule ya Sekondari ya Nansimo (Bunda), Shule ya Sekondari ya Wasichana Maswa (Maswa), Taasisi ya Biashara Shinyanga (Shinyanga), Lake Secondari (Mwanza), Shule ya Sekondari ya Wasichana Bwiru (Mwanza), Shule ya Sekondari ya Wasichana Nganza (Mwanza), Shule ya Sekondari Karagwe (Karagwe), Shule ya Sekondari Bukoba (Bukoba), na Shule ya Sekondari Rugambwa (Bukoba). *(Makofi)*

Pamoja na mambo mengine shule hizi zimeanza kubuni miradi ya mazingira itakayotekelezwa. Vile vile kulifanyika mashindano ya insha, uchoraji na upigaji picha kwa vijana wa shule za sekondari. Mashindano yalikuwa wazi kwa shule zote za sekondari za mikoa ya Kagera, Mara, Mwanza na Shinyanga. Ninafuraha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Mshindi wa kwanza wa Insha kitaifa aliyetoka Seminari ya Makoko pia aliongoza na kuwa mshindi wa kwanza kikanda kwa nchi zote tisa za bonde la mto Nile. Aidha, mtandao wa kanda wa wanahabari pia ulianzishwa. Miradi midogo midogo ya mazingira imeanza kutekelezwa ambapo miradi tisa (9) yenye thamani ya dola za Marekani 192,000 imekubaliwa na hadi sasa dola za Marekani 88,657 zimekwishawafikia walengwa. Miradi hiyo iko katika wilaya za Bukoba Vijijini, Muleba, Misungwi, Magu, Ukerewe, Bunda, Musoma Vijijini na Tarime.

Katika kipindi cha 2006/2007 shughuli zifuatazo zitatekelezwa: kuendesha warsha itakayojadili athari za sera za maendeleo kwa mazingira; warsha ya mafunzo kwa

walimu wa shule kumi za sekondari katika mikoa ya kanda ya ziwa kuhusu teknolojia ya habari na mawasiliano kwenye elimu ya mazingira; warsha ya wabunge kuhusu programu pamoja na changamoto za mazingira zinazolikabili bonde la mto Nile. Miradi zaidi itabuniwa kutoka tisa (9) ya sasa hadi 22. Kiasi cha dola za Marekani 350,000 zimetengwa kutumika kwa miradi hii. Aidha, miradi 10 ya shule za sekondari itatekelezwa yenye thamani ya jumla ya dola za Marekani 20,000. Mashindano ya insha, uchoraji na upigaji picha yatafanyika tena; na mafunzo na mikutano ya wadau mbalimbali iataendelea.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Mkataba wa Hifadhi ya Bioanuai *(Convention on Biological Diversity (CBD)* na Itifaki ya Cartagena. Itifaki ya Cartagena ilikamilishwa mjini Montreal, Canada mwezi Januari 2000 na kuanza kufanya kazi tarehe 11 Septemba 2003 baada ya kuridhiwa na nchi 50 duniani. Aidha, Bunge lako tukufu lilipitisha na hatimaye Tanzania kuridhia Itifaki ya Cartagena tarehe 16 Machi 2003. Madhumuni ya Itifaki hii ni kuhakikisha usalama kwa mazingira, afya ya binadamu na viumbe vingine kutokana na bidhaa, mazao na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki, hasa katika matumizi yake, uingizaji wake nchini na usafirishaji nje ya nchi na ufungaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Ofisi ya Makamu wa Rais ilikamilisha maandalizi ya muundo na mwongozo kuhusu usimamizi wa bidhaa, mazao na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki *(National Biosafety Framework (NBF)* na *Guidelines).*

Aidha, maandalizi ya awamu ya pili kuhusu mradi wa kujenga uwezo wa taasisi zetu; upatikanaji wa vifaa vya kuimarisha tathmini na udhibiti wa athari za matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa; utambuzi wa bidhaa, mazao au viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na uperembaji wa tekinolojia hii nchini yalikamilika. Sekretariati ya Mkataba wa Bioanuai imekubali kufadhili mradi huu ambao utagharimu shilingi milioni 800 na utekelezaji wake unategemewa kuchukua miaka minne. Vilevile, maandalizi ya mradi wa ubadilishanaji taarifa ndani na nje ya nchi kuhusu vinasaba vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki yalikamilika. Mradi huu utagharimia mafunzo kwa wataalamu na elimu kwa umma, ubadilishanaji taarifa na upatikanaji wa vitendea kazi kwa sekta muhimu. Randama *(Memorandum of Understanding)* kuhusu utekelezaji wa Mradi huu imeshasainiwa na kutumwa kwenye Sekretariati ya Mkataba wa Bioanuai. Mradi utagharimu shilingi milioni 50 na utekelezaji wake utachukua miezi 18.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 Ofisi ya Makamu wa Rais itatekeleza awamu ya pili ya mradi kuhusu matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa. Mafunzo yatatolewa kwa sekta mbalimbali na upatikanaji wa vifaa vya maabara kwa ajili ya utafiti na kutambua bidhaa, mazao na viumbe vilivyofanyiwa mabadiliko ya kijenetiki na athari zinazoweza kusababishwa na matumizi ya biotekinolojia ya kisasa, utafuatiliwa. Aidha, kanuni kuhusu matumizi salama ya biotekinolojia ya kisasa zitaandaliwa. Ofisi ya Makamu wa Rais, itasimamia na itaendelea kutoa elimu, kukuza weledi kwa sekta mbalimbali na umma kuhusu Muundo na miongozo na kuratibu utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyolieleza Bunge lako tukufu mwaka jana, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Kituo cha Uzalishaji Bora na Hifadhi ya Mazingira Tanzania *(CPCT)* inasimamia mradi wa usafi wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu ya viwanda ambao ulianza mwezi Desemba 1999. Mradi huu una madhumuni ya kujenga uwezo wa viwanda na wadau wengine nchini katika tekinolojia na mbinu za uzalishaji bora zenye lengo la kupunguza au kuzuia uchafuzi wa mazingira utokanao na shughuli za viwanda.

Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Kituo kiliandaa warsha ya kitaifa kwa lengo la kujadili na kuboresha mkakati wa kupenyeza tekinolojia endelevu *(National Cleaner Technology Strategy)* katika sekta muhimu za kiuchumi zilizobainishwa katika tafiti zilizofanyika awali (*Diagnostic Study of Opportunities and Capacities for the Creation of National Cleaner Technology Strategy -2004/05)*. Tafiti zilizofanyika mwaka jana (2004/2005) zilibainisha sekta sita za uchumi kuwa na uwezekano mkubwa wa kufaidika na utumiaji wa tekinolojia endelevu. Sekta hizo ni bidhaa za vyakula, madini, utalii, viwanda vidogo vya uzalishaji sukari, kilimo cha mboga na maua, na bidhaa za mbao. Warsha hiyo ya kitaifa ilifanyika mwezi Januari mwaka huu na kuhudhuriwa na washiriki zaidi ya sitini kutoka wadau mbali mbali zikiwemo idara za serikali, taasisi za serikali na zisizo za kiserikali, vyuo vikuu na vyombo vya habari.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine muhimu iliyotekelezwa na Kituo katika kipindi cha mwaka 2005/06 ni kuanza ukarabati wa jengo ambalo Kituo kimepewa na serikali kwa ajili ya ofisi. Mkandarasi amekwisha chaguliwa na ameanza kazi. Ukarabati wa jengo unatarajiwa kukamilika mwezi Agosti, 2006. Vile vile katika kipindi hicho, Kituo kilitekeleza shughuli nyingine zifuatazo: kuratibu shughuli za Sekretariati ya *African Roundtable on Sustainable Consumption and Production;* kufanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati *(Cleaner Production Assessment)* katika kiwanda cha nguo cha Karibu *Textile Mills kilichopo Dar es salaam*; kufanya tathmini ya uendelezaji wa tekinolojia endelevu kibiashara *(Evaluation of CP Business Proposals)* kwa viwanda vya *Sandari Wood Industries* na *Tanga Fresh* vya mjini Tanga; kuendesha semina nne (4) za kukuza ufahamu wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu kwa washiriki mbalimbali zaidi ya mia moja kutoka Manispaa za Moshi, Tanga na Dodoma. Semina zilishirikisha watendaji wakuu wa serikali za mitaa; wenye viwanda, wafanyabiashara na wataalam toka Manispaa husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Kituo kinatarajia kutekeleza shughuli muhimu zifuatazo: kukamilisha ukarabati wa jengo la Ofisi; kuandaa na kuendesha semina ya kitaifa juu ya mafanikio ya utekelezaji wa mbinu za uzalishaji bora; kufanya tathmini ya uzalishaji bora na matumizi bora ya nishati kwenye viwanda mbalimbali vinavyohitaji huduma hiyo; kuendesha semina na warsha za kukuza ufahamu wa dhana ya uzalishaji bora na matumizi endelevu kwa wadau mbalimbali; na kuandaa mkutano wa kimataifa kuhusu uzalishaji wa matumizi endelevu, utakaofanyika Arusha, Desemba 2006.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kuratibu utekelezaji wa Itifaki ya Montreal kuhusu kudhibiti matumizi ya

madawa yanayomong'onyoa ukanda wa hewa ya Ozoni angani. Tanzania iliandaa na kuendesha Mkutano wa 9 wa pamoja kwa nchi za Afrika zinazozungumza Kiingereza na Kifaransa Jijini Arusha na uliohudhuriwa na nchi zote wanachama wa Itifaki ya Montreal katika ukanda wa Afrika. Madhumuni ya mkutano huo yalikuwa ni kuimarisha ushirikiano na kuendeleza jitihada za pamoja za kutokomeza kemikali zinazochangia kuharibu ukanda wa hewa ya Ozoni. Aidha, mkutano huo ulitoa fursa kwa maofisa wasimamizi wa utekelezaji wa Itifaki kupata habari za kitaalamu juu ya upatikanaji wa kemikali mbadala na tekinolojia ambazo hazina madhara kwa ukanda wa hewa ya Ozoni.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa na kuendesha warsha kuhusu uhalifu wa kimataifa wa mazingira Jijini Arusha mwezi Novemba 2005 ambapo nchi za Ethiopia, Kenya, Rwanda, na Uganda zilishiriki. Warsha ilihudhuriwa na wasimamizi wa mikataba ya kimataifa ya mazingira, maofisa forodha na wanahabari. Madhumuni ya warsha yalikuwa ni kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya mazingira kwa kujenga uwezo ili waweze kutambua uhalifu unapotokea katika maeneo yao ya kazi na mbinu zinazotumika katika uhalifu wa aina hiyo. Warsha hii pia ilikuza weledi wa umma kupitia vyombo vya habari, kuhusu tatizo la uhalifu wa kimataifa wa mazingira. Kituo cha Uzalishaji bora na Hifadhi ya Mazingira Tanzania kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais kiliendesha mafunzo kwa wadau juu ya mbinu za kisasa za kuzima moto zisizotegemea *CFCs* aina ya *halons* na namna ya kutumia *halons* kwenye maeneo nyeti *(essential uses)* kama vile kwenye ndege (*aviation*) na magari maalum ya kijeshi (*Military Tactical Vehicles*).

Mheshimiwa Spika, maadhimisho ya siku ya Ozoni Duniani hufanyika tarehe 16 Septemba kila mwaka. Katika kuadhimisha siku hiyo, mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais iliendesha maonesho katika Jiji la Dar es Salaam. Maonesho yalilienga kuelimisha umma kuhusu bidhaa zenye kemikali zinazochangia kuharibu ukanda wa hewa ya Ozoni, pamoja na bidhaa zisizo na kemikali hizo kwa lengo la kukuza weledi kwa wadau na umma kwa ujumla ili waweze kuzitofautisha. Vilevile maonesho hayo yalielimisha umma umuhimu wa kutunza ukanda wa Ozoni na hivyo kuwahamasisha kuingiza kwa wingi bidhaa ambazo ni salama na kupunguza utumiaji wa bidhaa zenye kemikali zenye madhara.

Aidha, maonesho hayo yalitumika kukuza weledi kwa mafundi mchundo wanaohudumia viyoyozi na majokofu kuhusu gesi mbadala na namna ya kuhudumia vifaa vyenye kemikali zinazoharibu ukanda wa Ozoni kwa usalama. Pia mafunzo yalitolewa kwa vitendo jinsi ya kunasa na kurejesha gesi kwenye vifaa hivyo ili ujuzi huo utumike katika shughuli zao za kila siku kwa lengo la kulinda ukanda wa hewa ya Ozoni. Jumla ya makampuni 8 yanayoshughulika na uuzaji na uhudumiaji wa majokofu na viyoyozi, utengenezaji na uuzaji wa madawa ya kupulizia na manukato na uuzaji na utoaji wa huduma ya kuzima moto yalishiriki. Uelimishaji umma juu ya umuhimu wa ukanda wa hewa ya Ozoni ulifanyika pia, kupitia vyombo vya habari (redio, Luninga na magazeti), majadiliano na makala *(Press Releases).* Aidha, vipeperushi 200 vyenye ujumbe mbalimbali wa ukanda wa Ozoni kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza vilisambazwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 kazi ya kukuza weledi wa umma kuhusu ukanda wa Ozoni na mbinu za kudhibiti madhara yake itaendelea kwa kuhusisha vyombo mbalimbali vya habari ikiwa ni pamoja na redio, luninga na magazeti. Aidha, mafunzo kwa mafundi mchundo wa majokofu na viyoyozi kuhusu aina ya gesi mbadala zinazoweza kutumika nchini na njia bora za kuhudumia viyoyozi na majokofu yataendelea. Pia maofisa forodha wataendelea kupewa mafunzo kuhusu mbinu za kutambua gesi zinazoingizwa nchini kwa ajili ya matumizi ya majokofu na viyoyozi na udhibiti wa uingizaji wa gesi zinazoharibu ukanda wa hewa ya Ozoni. Vilevile kanuni za kusimamia uingizaji na matumizi ya gesi zinazoharibu ukanda wa hewa ya Ozoni zitakamilishwa. Hatua hizi zitasaidia nchi kutekeleza majukumu yake chini ya Itifaki ya Montreal hususan kupunguza matumizi ya *CFCs* kwa asilimia 85 ifikapo tarehe 1 Januari 2007.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Stockholm unaohusu udhibiti wa kemikali zinazochukua muda mrefu sana kuoza katika mazingira *(Persistent Organic Pollutants (POPs).* Madhumuni ya Mkataba huu ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara ya kemikali za aina hii. Katika kipindi hiki, Mpango wa Taifa wa Kutekeleza Mkataba wa Stockholm ulikamilishwa na kuwasilishwa Sekretariati ya Mkataba.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira iliendesha warsha kwa nchi za *SADC* Jijini Arusha mwezi Novemba 2005, ili kujadili matokeo ya uchunguzi wa mafuta ya mitambo ya kusambaza umeme inayoashiria kuwa na kemikali aina ya *PCB* na kuweka mikakati na mipango ya kikanda kuhusu usimamizi wa kemikali na mitambo yenye kemikali hizi. Mikakati inahusu upatikanaji wa kemikali na tekinolojia mbadala, mafunzo kwa mafundi umeme, kujenga uwezo wa uchunguzi wa kemikali hizi na kuboresha sheria na kanuni za kudhibiti matumizi ya kemikali hizi. Matokeo ya uchunguzi wa kemikali aina ya *PCB* katika mafuta ya mitambo ya umeme yamesambazwa kwa wamiliki wa mitambo hiyo pamoja na ushauri wa kitaalamu ili waweze kuchukua hatua za kudhibiti madhara kwa binadamu na mazingira. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 miradi mbalimbali itaandaliwa kuhusu maeneo ya kipaumbele ya usimamizi wa kemikali hizi na kutafuta wafadhili.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Basel unaohusu udhibiti wa taka za sumu baina ya nchi na nchi na utupaji wake, na pia ni mwanachama wa Mkataba wa Bamako ambao unazuia uingizaji wa taka za sumu barani Afrika. Mkataba wa Basel umeweka taratibu za kimataifa za kudhibiti usafirishaji na utupaji wa taka za hatari baina ya nchi zinazozalisha taka za aina hii na zile zinazopokea kwa madhumuni ya kurejeleza au kuziharibu. Mkutano wa tatu wa Nchi wanachama wa Mkataba huu uliofanyika Geneva, Septemba 1995 uliamua kuanzishwa kwa vituo vya kikanda kwa ajili ya kutoa mafunzo na kusambaza tekinolojia mbalimbali. Katika bara la Afrika, nchi ya Senegal ilipendekezwa ianzishe kituo kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kifaransa, Misri kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kiarabu, na Afrika Kusini kwa ajili ya nchi zinazozungumza Kiingereza. Nigeria ilipendekezwa iwe na kituo cha kuratibu vituo vyote hivyo vitatu vilivyopo katika bara la Afrika. Hadi sasa jumla ya vituo 13

vimeanzishwa katika kanda mbalimbali duniani na vimeanza kazi iliyokusudiwa kabla ya kusajiliwa rasmi.

Madhumuni ya kuanzisha vituo hivi vya kanda ni kuimarisha uwezo wa nchi wanachama, kitaaluma, kisheria na kitaasisi, katika kusimamia usafirishaji na utupaji wa taka zenye sumu kama ilivyobainishwa kwenye Mkataba wa Basel. Kituo kwa ajili ya nchi za Afrika zinazozungumza Kiingereza kipo Pretoria, Afrika ya Kusini. Nchi zinazohudumiwa na kituo hiki ni 21, nazo ni Afrika ya Kusini; Botswana, Eritrea, Ethiopia, Gambia, Ghana, Liberia, Kenya, Lesotho, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Rwanda, Namibia, Nigeria, Sychelles, Swaziland, Uganda, Zambia, Zimbabwe na Tanzania. Kituo hiki bado kusajiliwa rasmi, nchi 11 zimesaini mkataba wa kuunda kituo hiki na zipo katika hatua tofauti za kuuridhia. Mauritius iliridhia mkataba wa kuunda Kituo hiki mwaka huu, na Namibia na Botswana zipo katika hatua ya mwisho ya kuridhia mkataba wa kuanzisha kituo hiki.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taratibu za kuridhia mkataba wa kuundwa kwa kituo cha Afrika cha Usimamizi wa Taka za sumu na Nyinginezo zinaendelea. Katika maandalizi haya, Ofisi ya Makamu wa Rais imefanya mawasiliano na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na wizara na taasisi mbalimbali za serikali na wamekubaliana na umuhimu wa kuundwa kwa kituo hiki ili nchi iweze kudhibiti taka zenye sumu na kuepuka uchafuzi wa mazingira. Katika kipindi cha 2005/2006 kazi zilizofanywa kuhusiana na Kituo cha Pretoria ni pamoja na kuandaa programu ya mafunzo kwa wadau mbalimbali juu ya usimamizi wa taka zenye sumu katika sekta za Afya, Viwanda na Usafirishaji; kuandaa mkakati kuhusu upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za kituo, kuandaa mapendekezo ya miradi na kuyatafutia wafadhili; kuendesha mafunzo juu ya kuimarisha ushirikiano na mikataba ya kemikali na programu za kimataifa na za kanda zinazotekelezwa chini ya mikataba hiyo; kuendesha warsha ya mafunzo kuhusu usimamizi wa taka zenye sumu kwa maafisa wa Idara na Taasisi za Serikali; na kutoa mafunzo kuhusu usimamizi wa taka za hospitali na jinsi ya kuandaa miradi inayoweza kuvutia uwekezaji katika tekinolojia zenye kudhibiti athari za taka zenye sumu.

. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, shughuli zitakazofanywa na Kituo ni pamoja na kuwezesha nchi zinazohudumiwa na kituo kuridhia mkataba wa kuundwa kwa kituo hiki; kuwezesha nchi wanachama kuandaa mkakati wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa taka, kuandaa mapendekezo ya miradi mbalimbali na kuiwasilisha kwa wahisani; kuendesha warsha ya mafunzo kuhusu usimamizi wa taka zenye sumu kwa maofisa wa Idara na Taasisi za Serikali; na kuendesha semina ya kuhamasisha viongozi wa ngazi za juu serikalini kuhusiana na majukumu yao katika usimamizi wa taka zenye sumu.

Mheshimiwa Spika, Usimamizi wa taka za plastiki (mifuko na chupa) hasa katika maeneo ya mijini ni changamoto na tatizo linalokua siku hadi siku hasa kutokana na utupaji ovyo wa taka hizi. Utenganishaji wa taka mahali zinapozalishwa haufanyiki. Wananchi walio wengi mijini na vijijini hawana tabia ya kukusanya taka na kuzitenganisha ili kurahisisha urejelezaji kwenye viwanda husika. Aidha, Halmashauri za

miji hazijaweka miundombinu ya kurejereza taka, hivyo asilimia kubwa ya taka zinazokusanywa mijini hutupwa katika madampo ambayo hayajaandaliwa kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Kwa mfano, katika jiji la Dar es Salaam kiasi cha asilimia 4 tu za taka za plastiki hurejelezwa kwa siku ambazo ni sawa na tani 124. Hiki ni kiwango kidogo sana, hivyo juhudi za kuelimisha jamii na kuhamasisha ili ishiriki katika shughuli za ukusanyaji na urejelezaji wa taka zitaendelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maliasili na Mazingira katika kikao chake cha kujadili bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais cha tarehe 27 Mei 2004 ilishauri serikali ichukue hatua mara moja ya kupiga marufuku utumiaji wa mifuko ya plastiki inayosababisha kero ya uchafuzi wa mazingira. Napenda kuliarifu bunge lako tukufu kuwa mwezi Aprili 2006 Serikali ilitoa tamko kuwa utengenezaji, uagizaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki laini yenye unene wa chini ya *microns* 30 (au milimita 0.03) na ile ya kufungia maji na maji ya matunda, ya unene wa *microns* 65 (au milimita 0.065) unapigwa marufuku ifikapo mwezi Oktoba 2006. Pia, kodi kwenye mifuko ya plastiki ya aina nyingine ya rambo yenye unene wa *microns* 30 (milimita 0.03) na zaidi, iongezwe kwa zaidi ya asilimia mia moja ili kuhamasisha uingizaji wa mifuko mbadala kama vile vikapu vya asili na mifuko ya nguo na karatasi. Serikali imetoa muda ili wahusika waweze kujiandaa ipasavyo. Halmashauri za wilaya, miji, manispaa na jiji zimeelekezwa kuweka mifumo madhubuti ya ukusanyaji taka. Katika kufanya hivyo ziweke mifumo na vyombo maalum vya kukusanya na kutenganisha taka, kuanzisha vituo na maghala ya kukusanya taka na kuhamasisha uwekezaji katika kurejereza taka, hivyo kupunguza uchafuzi wa mazingira, kuongeza ajira na kutumia rasilimali ya taka. Aidha, Serikali imeagiza halmashauri hizo kuondosha taka za plastiki zilizozagaa kwenye mazingira kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Ofisi ya Makamu wa Rais imekamilisha maandalizi ya Mpango wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi *(NAPA)*. Maandalizi ya Mpango huu yamefadhiliwa na Mfuko wa Mazingira Duniani *(GEF)* kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP)*. Mpango huu unaainisha maeneo ya kipaumbele yanayohitaji kushugulikiwa ili kuhimili madhara yatokanayo na athari za mabadiliko ya tabianchi. Kutokana na Programu hii, miradi ya kipaumbele yenye lengo la kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi itaandaliwa na kuwasilishwa *GEF* kwa ufadhili. Katika majadiliano na *GEF* wakati wa mkutano kuhusu athari za Mabadiliko ya Tabianchi, huko Ujerumani, mwezi Mei mwaka huu, *GEF* wamekubali kutoa Dola 300,000 (laki tatu) kwa kila nchi iliyoandaa *NAPA* ili kutekeleza miradi ya kipaumbele iliyoainishwa kwa mwaka huu 2006/07. Aidha katika kipindi hiki Ofisi ya Makamu wa Rais iliandaa mradi kwa ajili ya kufanya tathmini ya kina kuhusu madhara yatokanayo na athari za mabadiliko ya Tabianchi katika sekta za Kilimo, Afya na Maji. Mradi huu unafadhiliwa na Serikali ya Kifalme ya Denmark kupitia shirika lake la maendeleo la *DANIDA*. Pia katika kipindi hiki Ofisi imeanza maandalizi ya ripoti ya Pili ya Kitaifa kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Second National Communication)*. Maandalizi ya ripoti hii yanafanywa kwa kushirikiana na *UNEP* na itaainisha pia mikakati ya nchi katika kutekeleza changa moto za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki warsha ya mafunzo kwa wadau kuhusu uandaaji wa miradi ya *Clean Development Mechanism (CDM)* ilifanyika. Miradi hii inatekelezwa kulingana na Itifaki ya Kyoto ya Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Lengo kuu la warsha hii ni kukuza uelewa juu ya miradi ya *CDM* na kuonyesha fursa zilizopo ili kunufaika na miradi hiyo. Warsha hii ilijumuisha washiriki toka Sekta za Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs),* vyombo vya habari na sekta binafsi. Tayari Jiji la Dar es Salaam kwa kushirikiana na kampuni ya *Consorzio Stabili Globus* ya Italia limeandaa mradi wa kukusanya gesi ya *methane* itokanayo na taka kwa ajili ya kuzalisha umeme chini ya mpango wa *CDM.*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali itatekeleza Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Serikali katika Kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame nchini. Mradi huu wa miaka miwili, ulianza mwaka jana 2005 na unategemewa kukamilika mwaka huu 2006. Katika kipindi hiki mafunzo juu ya kuhuisha Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame *(NAP)* katika mipango ya maendeleo ya wilaya yalitolewa kwa Maafisa Mipango pamoja na Maafisa mazingira wa wilaya tisa (9). Wilaya ambazo zilifaidika na mafunzo haya ni Singida, Manyoni na Iramba (Mkoani Singida); Magu, Kwimba na Misungwi (Mkoani Mwanza); na Shinyanga, Kishapu na Meatu (Mkoani Shinyanga). Mafunzo haya pia yalishirikisha baadhi ya Vikundi vya Jamii na Mashirika Yasiyokuwa ya Kiserikali *(NGOs & CBOs)* kutoka katika maeneo haya. Aidha Maafisa wa Wilaya wanaoshughulikia Mazingira walipewa mafunzo juu ya ukusanyaji, uchambuzi, utunzaji na usambazaji wa taarifa zinazohusiana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame katika maeneo yao. Ofisi ya Makamu wa Rais pia iliipatia kila wilaya iliyoshiriki pamoja na Chama cha Waandishi wa Habari za Mazingira *(JET)* kompyuta moja ili kuwezesha uratibu wa utunzaji wa taarifa/kumbukumbu hizo katika wilaya. Katika kipindi cha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na mambo mengine itakamilisha utekelezaji wa Mradi wa Kuimarisha Uwezo wa Serikali katika Kupambana na kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame nchini kwa kuendesha mafunzo kwa wadau mbali mbali kwa kushirikisha *JET.*

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nililiarifu Bunge lako Tukufu kwamba katika kipindi cha mwaka 2005/06, Serikali itatekeleza Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kupambana na Umaskini kupitia Utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa ya Mazingira *(Multilateral Environmental Agreements (MEAs),* unaofadhiliwa na Serikali za Norway na Ubeligiji kupitia *UNEP.* Katika kipindi hiki Ofisi ya Makamu wa Rais imeunda Kamati ya Kitaifa ya Kuratibu Utekelezaji wa Mradi huu. Kamati hii inayojumuisha Sekta mbalimbali, pamoja na mambo mengine inalo jukumu la kupitisha miradi midogo midogo inayoomba ufadhili kutoka kwenye mradi huu na kufuatilia utekelezaji wake. Tayari mradi huu umeanza kufadhili miradi midogo midogo ya mazingira na kupambana na umaskini inayotekelezwa na Vikundi vya Jamii. Vikundi ambavyo vimeshafadhiliwa mpaka sasa ni kutoka: Kibaha, Pwani; Muleba, Kagera; Dar Es Salaam; Mwanza; Masasi, Mtwara; Shinyanga; na Arusha. Katika kipindi cha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kutekeleza mradi huu ikiwa ni pamoja na kusaidia miradi midogo midogo ya vikundi vya jamii inayolenga kuhifadhi mazingira na kupambana na umaskini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2005/06 imeendelea kuratibu shughuli za Mfuko wa Mazingira Duniani hapa nchini. Katika kipindi hiki miradi mikubwa miwili ya kikanda imeandaliwa kwa msaada wa *GEF* na kuwasilishwa *GEF* kwa ufadhili. Miradi hii ni Mradi wa Kupunguza Athari zitokanazo na Utalii wa Pwani unaohusisha nchi za Tanzania, Kenya, Msumbiji, Seychelles, Nigeria, Senegal, Gambia Ghana na Cameroon na Mradi wa Kuhifadhi mazingira ya Bonde la Mto Kagera utakaotekelezwa katika nchi za Tanzania, Uganda na Rwanda. Miradi hii itatekelezwa pindi fedha zitakapotolewa na *GEF*. Aidha katika kipindi hiki, Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kupokea, kuchambua na kupitisha miradi mbali mbali ya vikundi vya kijamii inayolenga katika kuhifadhi mazingira na kupambana na umaskini. Miradi hii imekuwa ikifadhiliwa na programu ya miradi midogo midogo ya GEF *(Small Grants Programme)*. Katika kipindi cha mwaka 2005/06 Jumla ya vikundi 15 vya kijamii vimefadhiliwa kupitia mfuko huu kwa kiasi cha dola za kimarekani zipatazo Laki tatu na elfu sabini, sawa na Shilingi milioni mia nne sitini (460,000,000.00). Vikundi vilivyofaidika ni kutoka mikoa ya Iringa, Morogoro, Dar es Salaam, Kigoma, Mara, Mwanza na Kilimanjaro. Maeneo ya kipaumbele katika miradi hii midogo midogo ni upandaji miti, upatikanaji wa nishati mbadala, kilimo cha umwagiliaji, hifadhi ya viumbe adimu duniani na hifadhi ya misitu na ardhi. Aidha katika kipindi cha mwaka 2006/07, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kufuatilia upatikanaji wa fedha kutoka *GEF* kwa ajili ya kufadhili miradi iliyokwisha wasilishwa na mipya itakayoandaliwa, na kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za mfuko nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita nililiarifu Bunge lako Tukufu kuhusu juhudi zinazofanywa katika kufikia malengo ya Milenia *(Millenium Development Goals)* ikiwa ni pamoja na kujumuisha masuala ya mazingira katika Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini (MKUKUTA) ili kuwezesha masuala ya hifadhi ya mazingira kuzingatiwa na wadau wote wanaotekeleza mkakati huu. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 Ofisi ya Makamu wa Rais iliendelea kutekeleza Programu ya Kujumuisha Masuala ya Mazingira katika Mchakato wa Kupunguza Umaskini. Programu hii inayofadhiliwa na *UNDP* pamoja na *DANIDA* imesaidia mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo ya kuhuisha masuala ya mazingira katika MKUKUTA na katika mipango ya maendeleo ya sekta mbalimbali na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuandaa Programu ya Kujenga Uwezo wa Wadau wa Mazingira kwa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira kikamilifu; na kufadhili miradi midogo midogo ya vikundi vya jamii inayolenga kuhifadhi mazingira na kupambana na umaskini. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu utekelezaji wa masuala ya Mazingira katika MKUKUTA pamoja na Programu ya Kujenga Uwezo wa Wadau wa Mazingira, kutekeleza Sheria ya Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge watakumbuka kuwa Tuzo hii ilianza kutolewa mwaka 2002 chini ya uratibu wa Ofisi ya Makamu wa Rais. Katika kipindi cha mwaka 2005/2006 jumla ya makampuni makubwa manne na kampuni moja ya kati ya uchimbaji madini yaliingia katika mashindano hayo. Mshindi wa Tuzo hiyo kwa mwaka huu ni Kampuni ya Geita Gold Mine Limited ya Geita, Mwanza. Katika kipindi cha

mwaka 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuratibu mashindano haya sambamba na yale ya Tuzo ya Upandaji Miti na Kuhifadhi Vyanzo vya Maji Nchini. Rais ameridhia kuanzishwa kwa Tuzo ya Rais ya Upandaji Miti na Kuhifadhi Vyanzo vya Maji. Ofisi ya Makamu wa Rais inaratibu tuzo hii ambayo itatolewa kwa mara ya kwanza mwaka 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Bunge lako Tukufu linavyofahamu upana wa suala la mazingira, ambalo ni suala mtambuka. Sekta nyingi ikiwa ni pamoja na vikundi mbalimbali, taasisi, makampuni na Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wananchi kwa ujumla wanaguswa na umuhimu wa mazingira bora. Kutokana na juhudi za serikali za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa hifadhi ya mazingira baadhi ya wananchi wameanza kuelewa umuhimu huo. Kwa sasa juhudi za wananchi katika hifadhi ya mazingira zinatia moyo. Katika kipindi cha mwaka jana wananchi kutoka mikoa yote ya Tanzania bara waliendelea na wito wa azimio la Dodoma la Kampeni ya Upandaji Miti ambapo jumla ya miti 78,943,332 ilipandwa msimu wa 2004/2005 na kati ya hiyo, miti 69,254,900 ilipona. Kutokana na hali ukame kwa msimu uliopita, kiwango cha upandaji miti kilikuwa hafifu ikilinganishwa na msimu wa 2003/2004 ambapo idadi ya miti ipatayo 94,338,614 iliyopandwa, na kati ya hiyo, miti 75,732,445 ilipona. Aidha vikundi mbalimbali vinavyohusika na hifadhi ya mazingira vilipatiwa huduma ya ushauri ili kuboresha uhifadhi na utunzaji mazingira. Katika kipindi cha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais itaendelea kuelimisha wananchi, kwa umuhimu wa Kampeni ya upandaji miti inayokidhi mahitaji ya wananchi katika maeneo mbalimbali.

Aidha, kwa mujibu wa hatua mbalimbali za utekelezaji wa Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji, kila Wilaya inatakiwa ipande na kutunza miti isiyopungua milioni 1 na laki 5 kwa mwaka. Kama nilivyoeleza katika aya ya 27, Mkakati una changamoto 12, hatua mbalimbali za utekelezaji na unahusisha watekelezaji wengi. Kwa ufafanuzi zaidi, Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 9.4 katika bajeti ya mwaka huu wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Mkakati huu. Fedha hizi zimeombwa kupitia bajeti za Wizara husika kama ifuatavyo:- Ofisi wa Waziri Mkuu (TAMISEMI), Shilingi milioni 100; Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Shilingi milioni 100; Maliasili na Utalii, Shilingi milioni 100; Maji, Shilingi bilioni 1; Maendeleo ya Mifugo, Shilingi milioni 300; Viwanda, Biashara na Masoko, Shilingi milioni 300; Miundombinu, Shilingi bilioni 1; Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi bilioni 2; Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Shilingi bilioni 4; na Nishati na Madini, Shilingi milioni 500. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyofanyika miaka iliyopita, tarehe 5 Juni kila mwaka Tanzania huungana na nchi nyingine duniani kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Hali kadhalika, mwaka huu maadhimisho yalifanyika kwa shughuli mbalimbali, nchi nzima kwa kipindi cha wiki moja, hadi siku ya kilele. Shughuli hizo ni pamoja na :- upandaji na palizi ya miti, mafunzo mbalimbali kuhusu mazingira, warsha na mashindano ya nyimbo na ngonjera ili kukuza weledi juu ya umuhimu wa hifadhi na usafi wa mazingira. Maadhimisho ya kitaifa yalifanyika mkoani Singida. Napenda kuwashukuru wananchi na viongozi wa Mkoa wa Singida kwa kuchukua dhamana ya kufanya maadhimisho kitaifa mkoani mwao, na kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2005/2006, Baraza liliendelea kutekeleza mradi wa Tathmini ya Uchafuzi wa Hewa Jijini Dar es Salaam, unaofadhiliwa kwa pamoja na Serikali, Wakala wa Mazingira wa Serikali ya Marekani *(US-EPA)* na Shirika la Mazingira Duniani *(UNEP)* ambapo katika kipindi hicho, upelembaji wa hali ya hewa katika jiji la Dar es salaam ulifanyika. Katika kipindi cha 2006/2007, Baraza litaendelea na uperembaji wa hali ya hewa katika jiji la Dar es salaam kwa kufanya utafiti wa kina na kwa kushirikisha wadau wengine wakiwemo Wizara ya Afya na Chuo Kikuu cha Dar es salaam.

Katika kipindi cha 2005/2006, maandalizi ya mradi wa kuteketeza madawa chakavu ya kilimo nchini, kwa ushirikiano na Shirika la Chakula la Umoja wa Mataifa *(FAO)* yalikamilika. Katika Kipindi cha 2006/2007, utekelezaji wa mradi huu kwa mikoa yote ya Tanzania Bara utaendelea, baada ya kutia saini mkataba wa utekelezaji kati ya wafadhili Benki ya Dunia na Serikali.

Katika kipindi cha 2005/2006, Baraza lilikamilisha rasimu ya Mpango wa Taifa wa Utafiti wa Masuala ya Mazingira *(National Environmental Research Agenda).* Mpango umelenga kufanya tafiti katika mikataba ya mazingira, ambayo serikali imeridhia na matatizo sugu ya mazingira nchini. Mpango utatumika kama dira ya utafiti wa mazingira hapa nchini. Katika Kipindi cha 2006/2007 uboreshaji wa mpango huu utafanyika kwa kupata maoni ya wadau katika ngazi ya wilaya na vijiji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, utafiti wa haraka *(Rapid Assessment)* ili kutathmini hali ya mazingira ya milima nchini ulifanyika. Wataalamu walitembelea milima ya Nguru (Tao la Mashariki), Chenene (Dodoma), Rugwe (Mbeya), Heru juu (Kasulu) na Monduli (Arusha) na kufanya utafiti wa kina. Katika kipindi cha 2006/2007 utafiti wa kina wa ikolojia utafanyika katika safu za mlima ya Livingstone, mkoa wa Mbeya, Iringa na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Baraza lilifanya mapitio ya taarifa 38 za Tathmini ya Athari kwa Mazingira *(TAM)* na kutoa ushauri. Jumla ya hati 12 zenye masharti ya kuboresha mazingira zilitolewa kwa miradi mbalimbali. Vile vile taarifa za ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit Reports)* 3 zilipitiwa na kutolea ushauri wa namna ya kuboresha masuala ya mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo.

Mapitio ya fomu za usajili wa miradi, taarifa za awali na hadidu za rejea *(Registration, Preliminary Impact Assessment reports and Terms of Reference)* 14 na taarifa za mipango ya Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Jamii *(Environmental and Social Management Plans)* 5 yalifanyika. Kwa ushirikiano na Wizara ya Maji, Baraza lilifanya uchambuzi wa masuala ya kuzingatiwa ili kuboresha mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi midogo midogo 408 ya kusambaza maji katika vijiji 617 mkoani Mara na Mwanza.

Baraza liliendelea, kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwenye Mazingira *(TAM)* hususan katika kuandaa miongozo na kuelimisha wadau juu ya umuhimu wa *(TAM)*. Mafunzo yalitolewa katika Wilaya sita zikiwemo (Rufiji, Kilombero, Bagamoyo, Muheza, Mufindi na Kilolo), Manispaa za Ilala na Arusha. Miradi iliyofanyiwa *(TAM)* ni ya uchimbaji madini, viwanda vya minofu ya samaki, nishati, utafutaji wa mafuta, ujenzi wa barabara na madaraja, ujenzi wa hoteli na vivutio vya kitalii na ujenzi wa viwanja vya Ndege.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Baraza linatarajia kufanya mapitio ya taarifa 55 za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kutoa ushauri. Vile vile litapitia taarifa za ukaguzi wa mazingira *(Environmental Audit Reports)* na kutoa ushauri wa kuboresha mazingira wakati wa utekelezaji wa miradi. Mapitio ya fomu za usajili wa miradi, taarifa za awali na hadidu za rejea *(Registration, Preliminary Impact Assessment reports and Terms of Reference)* na taarifa za mipango ya usimamizi wa Mazingira na masuala ya jamii *(Environmental and Social Management Plans*) yataendelea kufanyika kwa lengo la kudhibiti uharibifu wa Mazingira. Kwa kushirikiana na sekta mbalimabli na Serikali za Mitaa, Baraza litaandaa miongozo ya *(TAM)* ya kisekta na ile ya kutumika wakati wa kufanya uchambuzi wa masuala ya kuzingatiwa wakati wa kutekeleza miradi ya jamii.

Katika kipindi cha 2005/2006, wilaya zinazozunguka ziwa Victoria ziliwezeshwa ili kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuhifadhi maeneo ya ardhi oevu katika vijiji vitano vinavyozunguka maingilio ya mto Simiyu wilaya ya Magu. Aidha, uhamasishaji wa kutengeneza mikakati ya aina hiyo katika Wilaya za Musoma, Geita, Bunda, Bukoba, Misungwi na Geita uliendelea. Katika kupambana na kasi ya umaskini, Baraza lilitoa mafunzo kwa wanakijiji 46 wanaozunguka ziwa Victoria wa kijiji cha Ilungu wilayani Magu ya ususi bora unaotokana na mazao ya ardhi oevu. Katika kipindi cha 2006/2007 wilaya za Magu, Musoma, Geita na Bunda zitaendelea na utekelezaji wa mikakati hiyo. Aidha juhudi za kuhamasisha wilaya zingine zitaendelea.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/06, Baraza kupitia mradi wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ya Pwani na Bahari *(Tanzania Coastal Management Partnership (TCMP)* liliendelea kutekeleza Mkakati wa Uwiano wa Kuhifadhi na Kusimamia Maeneo ya Pwani na Bahari pamoja na wa Kupambana na Umaskini. Utekelezaji huu ulianza na Wilaya za Bagamoyo, Pangani na Mkuranga. Katika kipindi hicho utekelezaji wa mpango wa Tuzo ya Hifadhi ya Mazingira ya Pwani *(Coastal Environmental Award Scheme)* katika Wilaya zinazopakana na Bahari ya Hindi umeendelea. Katika kipindi cha 2006/2007, utekelezaji wa mkakati utaendelea kwa kushirikiana na wananchi wa wilaya za Kilwa, Lindi, Mtwara na Tanga katika kuandaa na kutekeleza mipango ya uwiano wa kuhifadhi maeneo ya pwani katika wilaya zao. Aidha, mpango wa tuzo mbalimbali za Hifadhi ya Mazingira na ushiriki katika maandalizi ya maadhimisho ya siku ya mazingira duniani utaendelea.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2005/2006 Mchakato wa kutengeneza miongozo itakayotumika katika kutambua maeneo tete (special or critical sites), kwa lengo la kuyahifadhi na kuyaongoa (restoration) ulianza. Katika kipindi cha 2006/2007,

Baraza litaendelea kukusanya taarifa za awali kwa lengo la kuandaa viashiria kwa ajili ya uperembaji. Katika kipindi cha 2005/2006, utekelezaji wa shughuli za utunzaji wa mazingira katika bonde la Kihansi, kwa kushirikiana na jamii, na Serikali za Mitaa, uliendelea. Katika kipindi cha 2006/1007, taratibu za kukamilisha mradi ifikapo Desemba, 2006 zitaendelea, ambapo taarifa mbalimbali kuhusu mradi zitaandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha 2005/2006, Baraza liliendelea kufanya ukaguzi wa miji na viwanda kwa lengo la kudhibiti uchafuzi wa mazingira. Aidha, ushauri ulitolewa kwa viwanda katika miji ya Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Arusha na Mwanza hususan vile vinavyozalisha nondo, mafuta ya kupikia na nguo. Katika kipindi cha 2006/2007 ukaguzi wa aina nyingine za viwanda utaendelea katika miji mingine, ili kujua hali ya viwanda vyetu nchini. Katika kipindi cha 2005/06, Utafiti wa njia bora za kudhibiti taka ngumu ulianza, ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa maafisa wa Baraza na taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2005/2006, Baraza liliandaa kongamano la Kitaifa la Kisayansi, juu ya Madhara ya mabadiliko ya Tabia Nchi kwa lengo la kuhakikisha taarifa za kisayansi zinawafikia wananchi na kuelimisha wananchi athari zake. Aidha, Baraza liliandaa warsha huko Tanga kuhusu mifumo ya ikolojia hapa nchini na jinsi wananchi wanavyoitegemea kuondoa umaskini. Napenda kuwashukuru *UNEP* and *UNDP* kwa msaada wa fedha waliotoa kufanikisha kongamano hilo. , katika kipindi cha 2005/2006, utekelezaji wa mkakati wa Kitaifa wa Kuhifadhi ardhi na vyanzo vya maji uliendelea. Baraza liliendelea kuandaa programu ya Kitaifa ya kuhamasisha Umma juu ya Umuhimu wa Kuhifadhi Mazingira na Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Mazingira kwa kutoa taarifa za mazingira kwa wadau kupitia maktaba na kuandaa makala katika vyombo vya habari, warsha, mtandao wa tovuti, vipeperushi, majarida makongamano na mikutano. katika kipindi hicho, utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Elimu ya Mazingira na Mawasiliano ulianza. *(Makofi)*

Lengo ni kukuza weledi wa wanahabari, watekelezaji wa elimu ya Mazingira na kukuza uwezo wa kufanya maamuzi juu ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Aidha, miongozo, makala za ushauri na kuelimisha jamii imeandaliwa kwa kushirikiana na wadau. Katika kipindi cha 2006/2007, Baraza litaendelea kushirikiana na wadau husika katika kuandaa miongozo ya namna ya kuendeleza elimu ya mazingira kwenye taasisi za elimu na wanahabari, kwa kuimarisha huduma ya mawasiliano, maktaba na tovuti, ikiwa ni pamoja na kuendesha warsha, semina, kushindanisha shule na vikundi mbalimbali, kuchapisha makala, vipeperushi, majarida na kalenda ili kukuza uelewa juu ya hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2006/2007, Baraza limeelekeza nguvu zake katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya 2004 hususan katika kujenga uwezo, kupanua ajira ili kuweza kukabiliana na majukumu ya utekelezaji wa Sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhakikisha kuwa Sheria Na. 8 ya Ajira ya mwaka 2002 inatekelezwa ipasavyo imeweza kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, na Tume ya Utumishi wa Umma kuandaa

warsha kwa watumishi wote ili kuwaelimisha watumishi juu ya Sheria hiyo. Kwa mwaka wa Fedha 2005/06 watumishi 8 wameajiriwa kwa njia ya ushindani ili kujaza nafasi zilizokuwa wazi. Watumishi wa 14 wa kada tofauti wamepandishwa vyeo kwa njia ya ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kulinda, kudumisha na kuendeleza haki za wafanyakazi iliandaa Baraza la Wafanyakazi mwezi Novemba 2005, mjini Moshi, Mkoani Kilimanjaro. Katika kikao hicho cha Baraza la wafanyakazi masuala ya Ajira, Maslahi ya Watumishi, Kanuni za Manunuzi na Fedha za mwaka 2001. *(Public Procurement Act and Pubilc Finance Act of 2001)* yalijadiliwa kwa pamoja na watumishi wote na kuyaelewa. Pia katika kikao hicho watumishi waliweza kupata fursa ya kujadili masuala mbalimbali ya utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Rais. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na wawakilishi kutoka TUGHE Mkoa wa Dar es salaam imeweza kuandaa vikao mbalimbali vya kuchagua wawakilishi wa Baraza la Wafanyakazi na Viongozi wa TUGHE katika Ofisi ya Makamu wa Rais mwezi Juni 2006. Wajumbe wapya wamechaguliwa baada ya muda wa wakilishi wa zamani kufikia ukomo.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2005 mapambano dhidi ya janga la UKIMWI yameendelea kuimarishwa. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania *(TACAIDS)* iliandaa warsha kwa watumishi wake. Warsha hizo zililenga kuwakumbusha, kuwaelimisha na kuwashirikisha katika mapambano dhidi ya UKIMWI sehemu za kazi. Ofisi imechagua wawakilishi toka kila Idara ambao kwa pamoja wanaunda kamati ya kuratibu masuala ya UKIMWI *(Technical Aids Committee Secretariet)*. Ili kuweza kuongeza wigo wa ufahamu katika kupambana na janga hili la UKIMWI Ofisi ilituma mwakilishi kuhudhuria warsha iliyofanyika mwezi April 2006 nchini Afrika Kusini ili kubadilishana uzoefu na mbinu mbalimbali katika kupambana na janga la UKIMWI. Warsha hiyo ilijumuisha mataifa yaliyo Kusini mwa Afrika.Ofisi ya Makamu wa Rais haikubaki nyuma katika mapambano dhidi ya Rushwa na kuendeleza Utawala Bora. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na kitengo cha Utawala, Uratibu wa Utawala Bora, Ofisi ya Rais, mwezi Aprili na Mei 2006 iliandaa warsha mbili kuhusu Rushwa na Utawala Bora. Katika warsha hizo watumishi waliweza kukumbushwa mambo muhimu yahusuyo Utawala na Utawala Bora, Misingi ya Utawala Bora na kuhuisha Utawala Bora na Utumishi wa Umma.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mapambano dhidi ya kuondoa Umasikini yamezingatiwa. Ofisi ya Makamu wa Rais iko katika hatua za awali za uanzishaji wa Chama cha Kuweka na Kukopa *(SACCOs)* ili kuweza kuinua maisha ya watumishi kwa kupata Mikopo nafuu na endelevu. Vikao mbalimbali vya kujadili jinsi ya kuendesha *SACCOs* ya Ofisi ya Makamu wa Rais vimekaa, Rasimu ya Katiba imeandaliwa, na viongozi wa muda wamechaguliwa. Ofisi ya Makamu wa Rais katika kuhakikisha watumishi wake wanakuwa na ujuzi unaostahili ili kwenda sambamba na karne ya 21 ya Sayansi na Tekinolojia imeweza kugharamia mafunzo kwa watumishi 35 ndani na nje ya nchi katika kipindi cha mwaka wa Fedha 2005/2006. Watumishi 23 wamehudhuria mafunzo ya muda mfupi na watumishi 12 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu yakiwemo

mafunzo ya shahada ya uzamili na shahada ya kwanza katika fani mbalimbali. Mafunzo hayo ni yale ya fani za utawala, habari, uendeshaji miradi, utunzaji wa kumbukumbu, kilimo, udereva, uhasibu, ugavi, biashara na na uendeshaji ofisi. Mafunzo haya yameongeza ufanisi katika utendaji kazi wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kwamba watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wanakuwa na afya bora,ushirikiano mzuri kati yao na Wizara nyingi imefanikiwa kuanzisha klabu ya michezo ambayo hushiriki katika michezo inayo andaliwa na Shirikisho la Michezo ya Wizara (SHIMIWI). Mwaka wa Fedha 2005/2006 Ofisi ya Makamu wa Rais ilikuwa kati ya Wizara zilizoshiriki mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara Mkoani Morogoro. Ushiriki katika michezo umeongeza ari ya ushirikano katika utendaji kazi udugu, urafiki na ukaribu kati ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara nyingine za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mkakati wa kuhakikisha kwamba Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na watumishi wake wanapata Ofisi ya kufanyia kazi yenye ubora unaostahili imeweza kusimamia ujenzi wa jengo lililopo katika mtaa wa *Luthuli Plot No.10, Dar es Salaam*. Jengo linatarajia kukamilika mwezi Septemba ,2006. Kukamilika kwa jengo hilo kutapelekea asilimia 80 ya watumishi wa Ofisi hii kuwa katika jengo moja. Aidha, itarahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Ofisi, na kupunguza gharama za kukodisha majengo kwa matumizi ya Ofisi. Vifaa mbalimbali vya kumuwezesha mtumishi kufanya kazi vimenunuliwa . Vifaa hivyo ni kama:- kompyuta, viti, meza pamoja na vifaa vyote vya Ofisini. Ujenzi wa jengo la makazi ya Makamu wa Rais unatarajia kuanza huko Tunguu, Zanzibar mara tu baada ya kupata Hati ya Kumiliki eneo toka Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ofisi imekwishalipa gharama za fidia Shilingi 5,000,000 na gharama za upimaji Shilingi 264,000.

Mheshimiwa Spika, katika masuala yahusuyo fedha kwa mwaka 2005/2006 tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutoa taarifa za kifedha zilizo sahihi na kwa wakati. Taarifa hizo zilionesha mlingano halisi wa Bajeti na mwenendo wa matumizi kulingana na malengo yaliyowekwa katika kila muhula kwa kutumia mfumo wa Intergrated Financial Management System *(IFMS).* Mahesabu ya mwaka yameandaliwa kwa kutumia viwango vya Kimataifa vya Uhasibu *(International Public Sector Accounting Standard (IPSAs)* ili kuwezesha wawekezaji wa nje kusoma taarifa za mahesabu yetu kwa urahisi na kufanya maamuzi yaliyosahihi katika kuwekeza. Kutokana na umakini na ufanisi wa kazi Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2005/2006 imepata Hati ya Usahihi *(Clean Certificate)* kwa fungu 26 na 31. Ili kuimarisha zaidi utendaji kazi na usimamizi mzuri wa matumizi ya rasilimali za Serikali, Ofisi ya Makamu wa Rais imeanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani pamoja na Kamati ya Ukaguzi *(Audit Committee).* Kitengo hiki kitaongeza ufanisi katika kuhakikisha utunzaji mzuri wa rasilimali na nyaraka za Serikali, na kuhakikisha malengo yaliyopangwa na Ofisi katika vipindi vya mwaka yanazingatiwa.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 itaendelea Kuratibu, Kusimamia na Kushughulikia masuala yote ya watumishi yahusuyo

ajira, maslahi ya watumishi, nidhamu, kupandishwa vyeo kwa wale wanaostahili, kushughulikia haki za wafanyakazi, zikiwemo likizo, kuongeza taaluma na ujuzi na kuhakikisha kuwa watumishi wanapata vitendea kazi vya kutosha ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wao. Mapambano dhidi ya ugonjwa hatari wa UKIMWI pamoja na vita dhidi ya rushwa ni kati ya shughuli zitakazotekelezwa katika Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha Makadirio ya Matumizi ya fedha kwa mwaka 2006/2007, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake thabiti na maelekezo yake yaliyowezesha Ofisi yetu kutekeleza vizuri majukumu yake. Namshukuru Mheshimiwa Samwel Sitta, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania na Mheshimiwa Anna Makinda, Naibu Spika kwa kuongoza Bunge hili Tukufu. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu Bwana Abubakar Rajab, Naibu Katibu Mkuu, Bwana Sazi Salula, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wafanyakazi wote na wadau mbalimbali kwa kushirikiana na Ofisi yangu katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani za pekee kwa Wahisani mbalimbali ambao wamekubali kugharamia fedha za maendeleo kwa ajili ya miradi inayotekelezwa katika maeneo muhimu niliyoyataja. Wahisani hao ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*), Benki ya Dunia (*WB*), Shirika la Maendeleo la Marekani (*USAID*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuendeleza Viwanda (*UNIDO*), Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (*UNEP*), Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Mfuko wa Maendeleo wa Nchi za Nordic (*NDF*), Mfuko wa Mazingira wa Dunia (*GEF*), Mashirika yasiyo ya Kiserikali na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, anawashukuru wananchi wa Kwahani kwa imani kubwa waliyompa kumchagua kuwa Mbunge wao kwa kipindi cha 2005/2010. Anawashukuru pia wananchi wa Mkuranga kwa kumkubali kuwa Mbunge wao mwaka 2000/2005. Prof. Mark Mwandosya, anawashukuru kwa dhati kabisa wananchi wa Rungwe Mashariki, kwa kumchagua bila kupingwa, kwa vipindi viwili mfululizo kuwa Mbunge wao. Anaahidi kuilipa dhamana hiyo kwa kuwatumikia kwa nguvu zake zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2006/2007, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 26 - Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha 2006/2007 naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Sh.1,989,528,000/= kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida ya Makamu wa Rais. Kati ya fedha hizo Sh. 384,728,000/= ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi na Sh. 1,604,800,000/= ni kwa ajili ya matumizi mengine.

Mheshimiwa Spika, Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, katika mwaka wa fedha 2006/2007, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makadirio ya Matumizi ya Sh. 32,734,990,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Kati ya fedha hizo, kiasi cha Sh. 678,895,000/= ni mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Sh. 462,515,000/= ni ruzuku ya mishahara ya Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC).* Sh. 21,196,080,000/= ni kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar, Sh. 9,147,500,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Sh. 1,250,000,000 ni ruzuku ya matumizi ya mengineyo ya *NEMC*. Kiasi cha Sh. 8,556,794,000/= kinaombwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo, za ndani ni Sh. 1,076,994,000/= na fedha za nje ni Sh. 7,479,800,000/=.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Waziri na hasa kwa kuzingatia muda na taarifa nzuri. Hotuba ni nzuri. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano.

**MHE. HASSAN R. KHATIB - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kifungu Na. 81(1) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2004, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006 na Makadirio ya Mapato ya Matumizi ya Fungu 26 - Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira ambao ndio waliochambua Bajeti hii nao ni Mheshimiwa Job Ndugai - Mwenyekiti, Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Bahati Abeid, Mheshimiwa Halima Mamuya, Mheshimiwa Prof. Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Riziki O. Juma, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa James Lembeli, Mheshimiwa Emanuel Luhahula na Mheshimiwa Lucy Mayenga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo,
Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Abdukarim Shah, Mheshimiwa Salim Khamis Salim, Mheshimiwa Mohamed Soud, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mhe. Ernest Mabina,

Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Juma Nh'unga, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Ali Khamis Seif na Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata maelezo ya kina toka kwa Mheshimiwa Waziri, alielezea dira, mwelekeo na majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, utekelezaji wa maagizo/maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa 2005/2006. Pia, alielezea kuhusu mapato na matumizi kwa kipindi cha fedha 2005/2006, mafanikio na matatizo ya Utekelezaji katika kipindi kilichopita. Aidha, Kamati ilipata maelezo ya kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2006/2007 na maombi ya fedha za matumizi kwa kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha 2006/2007 yalifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa ushauri na maagizo ya Kamati kwa mwaka 2005/2006, katika mwaka wa fedha uliopita, Kamati yangu ilitoa ushauri na maagizo katika maeneo mbalimbali hasa yanayohusu Mazingira, nafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kiasi kikubwa imeyafanyia kazi maeneo husika na hatua za utekelezaji zimeonekana. Hata hivyo, katika maeneo ambayo, Kamati imeona juhudi zaidi zinahitajika, imeshauri na kutoa maagizo ipasavyo.

Mheshimiwa Spika**,** katika mapitio ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka wa fedha 2005/2006, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipangiwa kukusanya jumla ya Sh. 540,000/= hadi kufikia Aprili 2006 kiasi cha Sh. 4,141,032/= kimekusanywa. Kiasi hiki ni sawa na mara nane zaidi ya makusanyo ya mwaka yaliyokadiriwa. Katika mwaka wa fedha 2005/2006, Ofisi ya Makamu wa Rais ilitengewa jumla ya Sh. 29, 933,555,500/=. Hadi kufikia tarehe 31/05/2006, Ofisi hiyo ilikuwa imepewa kiasi cha Sh. 23,325,367,715/= ambayo ni asilimia 80 ya fedha iliyotengwa.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na matatizo katika utekelezaji wa Bajeti 2005/2006. Baadhi ya mafanikio hayo ni pamoja na kuratibu shughuli za utekelezaji wa Sera ya Mazingira ambapo mkakati wa kuhifadhi mazingira, ardhi na vyanzo vya maji umeandaliwa, umepitishwa na umeanza kutekelezwa. Kwa mfano, kuondolewa kwa wafugaji waliovamia bonde la Ihefu katika wilaya ya Mbarali, kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki; Kampeni ya Taifa ya Upandaji Miti ilifanyika; Utaratibu wa utoaji wa tuzo ya Rais ya Uhifadhi ya Mazingira katika shughuli za uchimbaji madini umetekelezwa.

Pili, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) imeratibu utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa ya Mazingira ambayo Tanzania ni Mwanachama ikiwemo programu ya kitaifa ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi, *(National Adoptation Programme of Action-MAPA);* Mpango wa Taifa wa kutekeleza Mkataba wa *Stockholm* unaohusu udhibiti wa Kemikali zinazochukua muda mrefu kuoza katika Mazingira (*persistent Organic Pollutant –POPS);* Ripoti ya tatu kuhusu Mkataba wa Bioanuwai.

Tatu, utekelezaji wa Programu za Hifadhi ya Mazingira mfano uzalishaji endelevu viwandani, Hifadhi za Taifa, Mapori ya akiba na hifadhi ya Mazingira ya Ziwa Tanganyika .

Nne, utekelezaji wa Sheria ya Mazingira hasa Kanuni kuhusu tathmini ya athari kwa Mazingira, ukaguzi na kanuni za usajili wa wataalamu wa kutathimini athari za mazingira.

Tano, taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Wizara Bungeni, iliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* lilifanya baadhi ya mambo yafuatayo:-

(a) Tathmini ya haraka *(Rapid assessment)* ya hali ya milima nchini, utekelezaji wa mkakati wa uhifadhi wa mazingira ya maeneo ya Pwani na kufanikisha Kongamano la Pili la Kisayansi na Kitaifa la Mazingira kuhusu mabadiliko ya hali ya hewa *(climatechange).*

(b) Katika kuzuia uchafuzi wa Mazingira, Baraza limekagua viwanda mbalimbali vikiwemo vinavyozalisha nondo, mafuta ya kupakaa, nguo na kutoa mafunzo kwa Maafisa wa *NEMC* na Taasisi mbalimbali ili kuwaandaa kwa ajili ya kusimamia Sheria mpya ya Mazingira.

(c) Baraza limepitia Ripoti 35 za tathmini ya athari kwa Mazingira *(EIA)* na kutoa ushauri, limetoa hati za Mazingira *(Environmental Certificate)* kwa miradi 12 na limetoa mafunzo ya tathmini ya athari za miradi katika mazingira *(TAM)* kwa Madiwani, Makatibu Tarafa na Wataalamu katika Halmashauri nane.

(d) Baraza limehamasisha Umma katika utunzaji wa Mazingira kwa kusambaza taarifa mbalimbali za Mazingira kwa njia ya mikutano, vitabu, vijarida, miongozo, vipeperushi, fulana na kalenda.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu, pamoja na mafanikio hayo, Kamati iliainisha matatizo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Uhaba wa watumishi, vitendea kazi na kutokuwa na Ofisi moja kwa wafanyakazi wote;

(ii) Ukosefu wa fedha za kutosha;

(iii) Utekelezaji wa mradi wa utafiti na udhibiti wa Bonde la Mto Msimbazi haukutekelezwa kwa sababu fedha za Wahisani hazikutolewa.

Mheshimiwa Spika, kazi zitakazotekelezwa katika kipindi cha mwaka wa fedha 2006/2007, Ofisi ya Makamu wa Rais, itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuwaendeleza watumishi kitaaluma na mapambano dhidi ya UKIMWI;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam na Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar;

(iii) Kwa upande wa Idara ya Mazingira, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira;

(iv) Baraza la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira litaendelea kukagua viwanda, kufanya mapitio ya ripoti ya tathmini ya athari kwa Mazingira *(EIA)* za miradi mbalimbali inayoanzishwa nchini, litaendelea kutekeleza programu mbalimbali zinazohusu Mazingira, kuandaa mipango ya usimamizi wa maeneo oevu *(Wetlands)*, pia litaendelea kuishauri Serikali katika masuala mbali mbali ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mkakati wa kulinda Mazingira nchini ili kuweka msingi endelevu wa shughuli zetu za maendeleo. Katika kutekeleza azma hiyo, Kamati yangu inaishukuru Wizara ya Fedha, katika Bajeti yake ya mwaka 2006/2007 imetenga kiasi cha Shilingi bilioni 9.4 kwa ajili ya utekelezaji wa mkakati wa kutunza mazingira nchini.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa Kamati ni kwamba, kwa kuwa nchi yetu inakabiliwa na uharibifu mkubwa wa mazingira, hususan uharibifu wa ardhi na vyanzo vya maji, uharibifu huu ndio kiini kinachosababisha hali ya jangwa, ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji nchini.

Kamati yangu inaliunga mkono tamko la Serikali lililotolewa tarehe 01 Aprili, 2006, kuhusu hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji nchini.

Aidha, Kamati yangu inaishauri Serikali itafute maeneo kwa ajili ya wafugaji wanaohamishwa kutoka kwenye maeneo ambayo ni vyanzo vya maji. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa Umma.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu imekumbwa na tatizo la uharibifu wa mazingira unaotokana na uvamizi wa makazi na shughuli za Kilimo kwenye miteremko ya milima, mabonde na vyanzo vya maji hasa katika maeneo ya Milima ya Uluguru, Udzungwa, Kilimanjaro, *Livingstone*, Usambara na Pare. Kamati imeishauri Ofisi ya Makamu wa Rais itekeleze mkakati ulioandaliwa wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imeishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), iwe inaihusisha Kamati hii katika kupitia Ripoti za tathmini ya athari kwa Mazingira ya miradi mikubwa ya maendeleo kabla ya utekelezaji wa miradi hiyo ili Kamati iweze kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa kuna Sheria ya Mazingira hapa nchini, Kamati inalishauri Baraza litekeleze wajibu wake kama inavyotegemewa.

Mheshimiwa Spika, suala la kuelimisha wananchi kuhusu utunzaji wa mazingira ni muhimu sana. Kamati inaishauri Serikali, katika mwaka wa fedha ujao itenge fedha za kutosha kwa ajili ya elimu ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuna uchimbaji holela wa madini katika maeneo mengi hapa nchini ambao kwa namna moja au nyingine unaharibu mazingira. Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kuhakikisha shughuli hizi za uchimbaji madini zinakomeshwa kama ilivyoainishwa kwenye mkakati wake wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, maombi ya fedha kwa mwaka 2006/2007, Makadirio ya Mwaka wa Fedha 2006/2007 ya Ofisi ya Makamu wa Rais, yameandaliwa kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele yanayotarajiwa kufikiwa katika utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA). Baada ya uchambuzi wa kina, Kamati inakubaliana na Makadirio ya Bajeti ya Makamu wa Rais - Fungu 26, jumla ya Sh. 1,989,528,000/= na Ofisi ya Makamu wa Rais - Fungu 31, jumla ya Sh. 41,291,784,000/= kati ya hizo, Sh. 32,734,990,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh. 8,556,794,000/= ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Hivyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha fedha zinazoombwa.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Wanakamati wenzangu, ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Katibu Mkuu wake Abubakar Rajabu, Naibu Katibu Mkuu wake Sazi Salula na Watumishi wote wa Ofisi hii na Taasisi ama Mashirika yaliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa ushirikiano mkubwa walioipatia Kamati katika kipindi chote ambacho tumefanya nao kazi. Tumepata elimu wakati wa Semina mbalimbali na tulipotembelea shughuli zao. Kamati inawashukuru sana na kuwatakiwa mafanikio makubwa zaidi katika kazi za ujenzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwashukuru Wajumbe wenzangu kwa ushauri na busara zao zilizoniwezesha kuiongoza Kamati hii. Michango yao kwa wakati wote ilitolewa kwa uwazi na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Damian Foka na Makatibu wake Wasaidizi wa Kamati hii Ndugu Lawrence Makigi na Michael Kadebe kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuratibu shughuli zote za Kamati. Pia, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuihudumia Kamati ipasavyo katika hatua zote za maandalizi ya taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. RAMADHAN A. MANENO (K.n.y. MHE. GEORGE M. LUBELEJE (MWENYEKITI WA KATIBA, SHERIA NA UTAWALA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Katiba, Sheria na Utawala, naomba kuwasilisha kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano kwa mwaka 2005/2006 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kabla sijawasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, kuhusu Makadirio ya Mapato ya Matumizi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), naomba nieleze kwa kifupi hatua iliyotangulia kabla ya kuishughulikia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, wakati wa Serikali ya Awamu Nne ilipoingia madarakani yalifanyika mabadiliko makubwa ya Wizara na baadhi yake zikapewa majina na majukumu mapya. Kufuatia mabadiliko hayo, hata mfumo wa Kamati ya Bunge wa kushughulikia Bajeti ya Wizara wakati wa Vikao vya Kamati kwa ajili ya kuchambua Bajeti ya Wizara mwezi Mei na Juni, ilibidi urekebishwe kwa muda ili kukidhi mabadiliko hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia madaraka yako uliyopewa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, mbali na kuiletea Kamati yangu kazi ya kuchambua Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Rais na Wizara ya Katiba, Sheria na Utawala, pia ulileta kazi ya kujadili Makadirio ya Ofisi ya Rais (Muungano) na kuipelekea Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, kazi ya kuchambua Makadirio ya Ofisi hiyo sehemu ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa mujibu wa kanuni Na. 81(1), sasa naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Rais (Muungano) kwa mwaka wa fedha 2006/2007 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema kwamba Kamati yangu ilikamilisha kazi hii Dar es Salaam tarehe 29 Mei, 2006 kwa kupokea maelezo ya Serikali yaliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano).

Mheshimiwa Spika, kama ilivyokuwa kwa Wizara nyingine, Kamati ilipokea maelezo kuhusu dira ya Ofisi hii kuwa ni kuendeleza na kudumisha Muungano. Kwa kuongeza ushirikiano na kutafuta ufumbuzi wa kero za muungano, aidha, Kamati ilijulishwa kuhusu mwelekeo wa Ofisi ya Makamu wa Rais katika masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusaidia Serikali na kusimamia shughuli za Muungano. Pia, Kamati ilifahamishwa juu ya majukumu mbalimbali yaliyopo katika Ofisi hii, mojawapo ikiwa ni jukumu la kulinda, kudumisha na kuendeleza Muungano.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine lilihusu utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati ya Bunge ya Maliasili na Mazingira, wakati wa kujadili Bajeti ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2005/2006. Miongoni mwa ushauri uliotolewa, ulihusu mambo ya Muungano, ambao Ofisi ya Makamu wa Rais iliyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, ilipokea taarifa ya utekelezaji wa ahadi za Serikali zilizotolewa Bungeni wakati Vikao vya Bunge vya Bajeti ya mwaka 2005/2006. Ahadi hizo zilihusu jinsi Serikali ilivyoshughulikia masuala ya Muungano kulingana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na kutafuta ufumbuzi kero mbalimbali za muungano kama zilivyoahinishwa katika Kamati ya Shellukindo. Napenda kuipongeza Serikali kwa kuainisha utekelezaji wa ahadi hizo kipengele kwa kipengele.

Mheshimiwa Spika, mbali na hayo, Kamati ilijulishwa kiasi cha fedha zilizopangwa kukusanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais kutoka katika vyanzo mbalimbali hadi kufikia Aprili, 2006. Aidha, Kamati ilipata maelezo juu ya muhtasari wa matumizi ya kawaida hadi kufikia tarehe 31 Me, 2006, na kiasi cha fedha kilichotolewa kuchangia janga la njaa. Pia, Kamati ilielezwa juu ya mafanikio na matatizo yaliyojitokeza katika kipindi hicho, katika utekelezaji wa majukumu katika maeneo ya Muungano, Utawala, Utumishi na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka fedha cha mwaka 2006/2007 Kamati ilijulishwa juu ya kazi mbalimbali zilizopangwa kutekelezwa katika maeneo mbalimbali ikiwemo mikakati na mipango iliyokusudiwa kuboresha masuala ya Muungano.

Mwisho, Kamati iliomba kupitisha Makadirio ya Fngu Na.31 ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea muhtasari wa Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano, Kamati ilikuwa na maoni na mapendekezo katika maeneo kadhaa. Aidha, katika maeneo mengine, ilihitaji ufafanuzi wa Serikali na Serikali ilifanya hivyo. Nitaanza na yale ya jumla.

Kwanza, Kamati inaipongeza Ofisi hii na Serikali zote mbili kwa kazi nzuri na jitihada kubwa zilizofanywa na kuimarisha Muungano wetu na kufikia hatua tuliyonayo leo hii.

Pili , dosari zilizopo ambazo ni za kawaida katika nchi zilizoungana kama alivyozungumzia Mheshimiwa Waziri Mkuu, wakati anahitimisha mjadala wa matumizi wa Ofisi yake Bungeni, tarehe 30 Juni, 2006, Kamati inaamini kuwa wananchi wengi wa Tanzania wanaopenda Muungano na wanapenda kuona kero zilizopo zinatatuliwa kwa hekima na busara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tarehe 23 hadi 26 Mei, 2006, Kamati ndogo ya Katiba, Sheria na Utawala ilibahatika kutembelea visiwa vya Unguja na Pemba kukagua miradi ya

mfuko wa maendeleo wa jamii *TASAF*, unaosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Rais. Kamati hiyo ilikuwa na Wajumbe sita kama wafuatavyo:-

Mheshimiwa Tatu Ntimizi Mbunge - Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wa msafara alikuwa Mheshimiwa Dr. Slaa, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Salim Mohamed, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Ramadhan Maneno na Katibu wa Kamati hiyo, Ndugu Charles Mloka, pamoja na Viongozi wa *TASAF* kutoka Makao Makuu.

Jambo la kufurahisha ambalo Kamati hii imelishuhudia ni jinsi wananchi wa visiwa hivyo walivyoelewa umuhimu wa miradi ya *TASAF* na walivyoitikia na kuonyesha mshikamamo mkubwa katika miradi inayohusu maendeleo yao bila kujali tofauti zao za kisiasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kupitia Bunge hili Tukufu, napenda nichukue fursa hii kuipongeza Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mfuko wa Maendeleo wa Jamii, yaani *TASAF* kwa kusimamia kikamilifu miradi hii tangu awamu ya kwanza na wamu ya pili iliyoendeleza hivi sasa.

Aidha, napenda niwashukuru na kuwapongeza wananchi wote tulikutana nao katika sehemu mbalimbali tulipokagua miradi hiyo Pemba na Unguja kwa kutupatia ushirikiano wa kutosha na kuonyesha mshikamano na uzalendo wa hali ya juu.

Baadhi ya wanachi walidiriki kusema kuwa ziara yetu ilikuwa ya kihistoria, kwani walidai kuwa hawajawahi kuiona Kamati ya Bunge ya Jamhuri ya Muungano kuwatembelea kwa madhumuni ya kukagua miradi ya maendeleo. Hii imewatia faraja kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati ilipafanya ziara hiyo, tuliwadhihirishia wananchi kuwa, Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunapokuwa katika masuala yanayohusu maendeleo ya wananchi huwa hatuonyeshi tofauti zetu za kisiasa na tulisema wazi kuwa tofauti zetu zipo kwenye majukwaa ya kisiasa, tunapokuwa kwenye Vyama vyetu, lakini tukishachaguliwa na kutambulika kama Wabunge wa Jamhuri ya Muungano, basi itikadi zetu zinaishia milango mikuu ya kuingilia Bungeni na tunapoingia Ukumbini, lugha zetu na kauli zetu zina dhamira moja ya kumkomboa na kumwendeleza Mtanzania. *(Makofi)*

Jambo ambalo tumeridhihirisha katika maeneo mbalimbali tuliyopita, ni pale ambapo wananchi walishindwa kugundua tofauti zetu za kisiasa hadi pale tulipowaeleza mwisho mwa hotuba zetu kuwa tulikuwa tunatoka Vyama tofauti na tuliwaomba waige mfano wetu na kuonyesha mshikamano. Nina hakika mshikamano tuliouonyesha uliitikiwa kikamilifu na wananchi hao. Napenda nichukue nafasi hii kusema kuwa hali halisi ya kisiasa tuliyojionea Pemba na Unguja, kwa kipindi tulichokaa ni tofauti na vile tulivyokuwa tukisikia ama kutoka kwa watu binafsi au kwa baadhi ya vyombo vya habari. *(Makofi)*

Kwa kweli kama kuna tofauti, tunadhani ni ndogo na tunafikiria njia mojawapo ya kuondoa tofauti za namna hiyo, ni kwa viongozi na Taasisi zetu kama Bunge, kuwatembelea na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kushikamana.

Mheshimiwa Spika, ukiacha ziara hiyo, pia kwa kujadili Makadirio, Kamati ilitaka kupata maelezo kuhusu jitihada mbalimbali za Serikali zinazofanyika kuhusu kuimarisha na kutatua kero za Muungano. Moja ya kero hii ni kuhusu Tume ya Haki za Binadamu ambayo Kamati ilibaini kuwa hadi sasa haijaanza kufanya kazi Zanzibar. Nafurahi kuwa, Serikali imeijulisha Kamati kuwa suala hili inalifanyia kazi.

Eneo lingine lilihusu mgao wa fedha za msamaha wa madeni kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pamoja na kazi nzuri iliyofanywa katika kutatua kero mbalimbali za Muungano, Kamati inaona kuwa, eneo hilo linahitaji kufanyiwa kazi ya ziada ili kupunguza malalamiko yanayoweza kujitokeza baina ya Serikali hizi. Kwa ajili hiyo, Kamati inashauri kuwa Serikali ya Muungano iweke wazi utaratibu wa mgao wa fedha za msamaha wa madeni kwa Serikali zote mbili.

Mheshimiwa Spika, haya ni maeneo machache ambayo Kamati yangu ilihitaji ufafanuzi kutoka Serikalini na kutoa ushauri kwa madhumuni ya kuyaboresha Bajeti ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kwa mara nyingine kuwasilisha taarifa ya Kamati na vilevile napenda nimshukuru Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, Katibu Mkuu, Wakuu wa Idara na Vitengo kwa kushirikiana vyema na Kamati wakati wote tulipochambua makadirio ya Ofisi hii.

Mwisho kabisa, napenda niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya na kukamilisha taarifa ya Kamati mapema ilivyowezekana. Naomba niwatambue kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa George Malima Lubeleje - Mwenyekiti, Mheshimiwa Tatu Musa Ntimizi - Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wafuatao: Mheshimiwa Hazara Pindi Chana, Mheshimiwa Steven Galinoma, Mheshimiwa Athuman Janguo, Mheshimiwa Rajab Juma, Mheshimiwa Shoka Juma, Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimwia Salum Mohamed, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Fatma Maghimbi, Mheshimiwa Ramadhan Maneno, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. *(Makofi)*

Pia, niwashukuru Makatibu wa Kamati hii, Charles Mloka na Ernest Zulu, kwa kutayarisha taarifa ya Kamati hii kwa kuihudumia Kamati katika hatua mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee taarifa hii na kukubali kuidhinisha jumla ya Sh.

41,291,784,000/= kwa Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, naiunga mkono hoja hii na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa, kama ulivyoona Mheshimiwa Maneno sio Makamu wa Mwenyekiti, kumbe yeye leo alikuwa anakaimu tu. Sasa upande wa Kambi ya Upinzani, kwa mpangilio ule ule wa robo saa ili kutimiza ile nusu saa yao nawaita Waheshimiwa mmoja baada ya mwingine kwa mpangilio walioupanga wa Mazingira na Muungano.

**MHE. SAID AMOUR ARFI (k.n.y. MHE. ALI KHAMIS SEIF - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani Bungeni, napenda kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007, kama inavyoelekezwa na Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004, Ibara ya 43 (5) (b) (c) na 81 (1).

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani Bungeni. Aidha, ninamshukuru na kumpongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Anne Makinda kwa nafasi hiyo muhimu sana katika historia ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Vile vile nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya kwa kuongoza Wizara hii muhimu sana hapa nchini. *(Makofi)*

Vile vile, napenda kuchukua fursa hii kupongeza hatua za Serikali za kulinda mazingira kama zilivyozinduliwa na Makamu wa Rais mapema Aprili Mwaka huu. Ni matarajio yetu kwamba yote yaliyoahidiwa yatatekelezwa kikamilifu kwa kuzingatia hali halisi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ni nyeti kwelikweli na ni ajenda ya kidunia. Mikutano ya kiulimwengu kama ule wa kule Rio de Janeiro, Brazil mwaka 1992 na ule wa Johannesburg, Afrika ya Kusini mwaka 2002, yote ikiwa imeandaliwa na Umoja wa Mataifa, ni uthibitisho tosha wa namna hoja nzima ya mazingira ilivyo nzito duniani.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mazingira ndiyo uhai wenyewe, maendeleo ya kijamii na kiuchumi yaliyo makini hayaelezeki nje ya Menejimenti makini ya mazingira. Ni jambo la busara zaidi kwa Taifa letu kuwekeza zaidi katika Menejimenti Makini ya Mazingira. Bajeti ya Serikali ni lazima ionekane kuutambua ukweli huu. Imekwisha dhihirika kwamba shoka na panga vinavyotumika kukata miti, vinaweza kuwa hatari zaidi kuliko bunduki na mabomu. Fedha za matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha

wa 2006/2007 ni Sh. 5,675,971,000/= na fedha za maendeleo ni Sh. 8,556,794,000/=. Jumla ya Bajeti ya Wizara ni kama Shilingi bilioni 14 tu.

Mheshimiwa Spika, kutunza mazingira ni suala la kufa na kupona na upo wakati linachukua sura ya vita. Hata haya matatizo ya kijamii kama ujambazi, vibaka, uchangudoa na matumizi ya madawa ya kulevya, yana uhusiano wa karibu na kuharibika kwa mazingira na hasa kukosekana kwa ardhi yenye rutuba na tija na ukame usio na mwisho.

Tunaweza sana kupunguza gharama za Polisi kufukuzana na vibaka na pia zile za kupanua Magereza kwa kusimamia kiumakini matumizi bora ya mazingira. Kama kilimo kinalipa kutokana na ardhi yenye rutuba na mvua safi, kishawishi kwa kijana kuwa kibaka kitatoka wapi? Uchovu wa ardhi na ukame, vinachochea hata ongezeko la maambukizi ya UKIMWI. Ardhi yote haina rutuba kutokana na mmomonyoko wa udongo na mbolea za chumvichumvi hazikamatiki kwa bei. Matokeo yake, watu hawakai Vijijini. Kila mtu anataka aje Mjini kubangaiza na Miji ni fedha. Vishawishi vya matumizi ya madawa ya kulevya na maovu kadha wa kadha mzizi wake mkuu ni umaskini.

Mheshimiwa Spika, umaskini uliokithiri unapaliliwa na uwekezaji mdogo sana wa Serikali kwenye jambo nyeti na zito kama Menejimenti bora ya mazingira. Hizi sio zama za kununua zaidi mabomu, vifaru na ndege za kivita. Hizi ni nyakati za kuwekeza zaidi katika raslimali-watu, kwa maana ya afya, elimu, maji na Menejimenti nzima ya Mazingira.

Mheshimiwa Spika, wananchi wengi Vijijini wanajikimu kupitia kilimo cha kiangazi na hasa mabondeni. Wananchi hao hawana namna nyingine mbadala ya kujipatia mkate wao wa kila siku isipokuwa kilimo cha aina hiyo. Ukulima wa vinyungu katika Wilaya kadhaa za Mkoa wa Iringa, ni shughuli muhimu ya kiuchumi Mkoani humo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na nia njema ya kulinda vyanzo vya maji, sio busara pia kuwavuruga wakulima huko Vijijini bila ya kuwaonyesha mbadala wowote ule wa maana. Kuwahamisha wakulima na kuanza kuwaswaga kupitia maagizo kadhaa ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kunapalilia njaa na umaskini wa wananchi. Uamuzi mzima wa Serikali kuhusu hifadhi bora ya vyanzo vya maji ufanywe kwa kutulia na sio kukurupuka na mikakati ya kiopereshení. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkakati wa kusambaza umeme Vijijini, ni kejeli kubwa kuwaambia watu wa Vijijini waache kulima mabondeni na maeneo yaliyo jirani na mito eti kwa sababu watu wa Mijini na hasa Dar es Salaam watakosa umeme! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maisha ya kisasa ni haki ya kila Mtanzania. Watu wa Vijijini nao wanastahili umeme. Umeme ukifikishwa Vijijini utaokoa misitu na utapunguza sana umaskini kwa kuchochea shughuli za kiuchumi kama viwanda vidogo vidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watumiaji umeme ni asilimia sita mpaka nane tu ya Watanzania. Asilimia 90 ya Watanzania wanatumia nishati inayotokana na miti. Ni vyema sasa Serikali ikaelekeza nishati mbadala kwa Watanzania hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado upo mtazamo katika nchi yetu unaomwona mkulima wa jembe la mkono kama ni chanzo kikubwa cha uharibifu wa mazingira na hasa ukataji miti Vijijini. Mkulima wa chai kule Tukuyu, mkulima wa tumbaku kule Urambo na Kidamali, Mkulima wa Kahawa kule Mbinga na Machame na hata mkulima wa pamba wa Kwimba na yule wa karafuu kule Mgogoni, hao wote wanalazimika kuzalisha kila kinachohitajika na mfumo wa Kimataifa wa ubepari kupitia Soko la Dunia. Anayehitaji na kuhimiza mazao kama Tumbaku, Chai, Kahawa, Pamba na Pareto yalimwe na wakulima wetu kwa manufaa yake. Huyo ndiye wa kumwajibisha kwa kuhusika na umalizaji misitu ya asili badala ya kuwarundikia lawama wakulima ambao wao ni matokeo tu ya tatizo na kamwe sio chanzo cha tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC)* lipo tangu mwaka 1983 na ndilo lililosimamia utayarishwaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 1997. Sheria Na.20 ya mwaka 2004 ya Usimamizi wa Mazingira ambayo ilianza kutumika tarehe 01 Julai, 2005 pia inasimamiwa kwa karibu na Baraza hili.

Baraza la Taifa la Mazingira bado halijaonekana kuwa na uwezo unaostahili wa kupambana na rafu mbalimbali katika suala zima la Menejimenti Makini ya Mazingira. Pamoja na *NEMC* kutayarisha Miongozo ya Kanuni zinazotawala tathmini ya athari za kimazingira *(EIA)* za shughuli mbalimbali, bado Baraza linakosa uwezo wa kuparua na hata kuuma meno pale inapostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya sera za kiuchumi na kisiasa za soko huria, huwa upo uwezekano mkubwa kwa wawekezaji na wafanyabiashara kwa jumla, kushawishika kujitafutia faida hata kwa gharama ya kuchafua na kuyaweka rehani mazingira. Chombo cha kusimamia utekelezaji wa Sheria na sera katika eneo la mazingira kama *NEMC*, ni lazima kiwe na uhakika usiotia shaka kwamba kinao uwezo wa kuusimamia kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na manufaa ya uwekezaji kutoka nje, ni jambo la msingi kwa Taifa letu kujiridhisha kwamba uwekezaji huo hauhatarishi maisha ya Watanzania kwa kuharibu mazingira. Zipo taarifa za uwekezaji katika Sekta ya Madini kuandamana na uchafuzi mkubwa wa mazingira katika Tanzania. Uchimbaji wa dhahabu kule Geita, Mwanza unaofanywa na *Ashanti Goldfields (Tanzania) Limited* unazalisha takataka za aina tofauti *(waste rock and low-grade ore)* zitakazofikia mpaka tani milioni 74. Mradi huo pia unaendelea kutumia kemikali hatari ya *Sodium Cyanide* ambayo ina athari kubwa kwa afya za watu ikijipenyeza hadi kwenye vyanzo vya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kushangaza kuona kemikali kama *Sodium Cyanide,* ambayo hata nchi kama Canada ilikwishapigwa marufuku, inaendelea kutumiwa na wawekezaji katika Sekta ya Madini na hasa uchimbaji wa dhahabu hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina hakika kama ni kutokana na uzembe, hujuma, au ni shinikizo la rushwa kwa wataalam wetu na wanaotoa maamuzi kwenye eneo zima la madini, lakini hoja ni kwamba mazingira yanaharibiwa na maisha ya Watanzania wa leo na kesho yamo hatarini. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itupatie ufafanuzi kuhusu jambo hili.

Mheshimiwa Spika, vyombo vyetu mbalimbali vya kuwasimamia na kuwaamulika wawekezaji na hasa katika eneo la athari zao katika mazingira na hasa *TIC* na *NEMC*, ni lazima vijitazame upya na vijipange upya. Vyombo hivyo vimebeba dhamana ya maisha ya Watanzania wa leo na kesho visiruhusu mchezo wa Kamari kwenye uhai wa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira na vita dhidi ya mazingira ni yetu wote, kila mmoja awajibike pale alipo.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI OFISI YA MAKAMU WA RAIS MAMBO YA MUUNGANO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa maoni ya Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais kuhusu masuala ya Muungano kwa mwaka wa fedha 2006/2007, kama ninavyoelekezwa na Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2004, Ibara ya 43 (5) (b) (c) na 81 (1).

Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwani yeye ndiye aliyetupa uwezo na kutufikisha hapa Bungeni hii leo, tukiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *Inshaalah* atujalie uadilifu mkubwa katika kuwatumikia Watanzania wote. Amina. *(Makofi)*

Aidha, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kutoa salaam za rambirambi kwa familia ya Prof. Sethi Chachage, kilichotokea hivi majuzi akiwa kwenye harakati ya kutafuta ufumbuzi wa matatizo ya Muungano wetu. Mwenyezi Mungu aipumzishe mahala pema Peponi roho ya Marehemu, shujaa na mtetezi mahiri wa Haki za Binadamu. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aipe familia ya Marehemu moyo wa ujasiri na ustahimilivu, jamii nzima ya Watanzania ipo pamoja nao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi. Aidha, ninamshukuru na kumpongeza Naibu wako, Mheshimiwa Anne Makinda kwa mfano aliotuonyesha sisi akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa uongozi mzima wa Chama changu cha Wananchi *(The Civic United Front-CUF)* kwa kuwa na imani na mimi na kuniteua kuwakilisha Viti Maalum. Ninaahidi kuwa nitafanya kila niwezalo kutimiza kazi zangu zote na kutunza imani yenu mliyonayo kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nampongeza Waziri Mheshimiwa Dr. Hussein Mwinyi kwa kupewa nafasi hiyo, lakini ninampa pole kwani anayo kazi kubwa katika kutatua matatizo na mpasuko uliopo ndani ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona na kuweka wazi mpasuko uliopo katika Muungano wetu. Ijapokuwa yeye binafsi anadhani mpasuko huo ni wa kiutendaji, lakini kwa ujumla mpasuko huo ni wa kimfumo na muundo tofauti na alivyo nukuliwa Mheshimiwa Rais akinena katika hotuba zake mbalimbali na kupelekea kuagiza mikutano ya Watendaji Wakuu katika Serikali zilizopo sasa, kwani hii inatokana na kukumbatia Katiba ambayo imejengeka katika mfumo wa Chama kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja kati ya mambo yanayoleta manung'uniko toka kwa wananchi wa Bara ni kwanini Zanzibar ina Baraza lake la Mawaziri na Wabunge wake na vile vile wa Muungano? Kwa hali ya kawaida utakuta kuwa Zanzibar kila Jimbo linakuwa na Wabunge wawili wa kuchaguliwa na wananchi, yaani Mwakilishi na Mbunge na kama ikitokea Viti Maalum kwa Bunge na Baraza la Wawakilishi unaweza kukuta kila Jimbo lina Wabunge wanne.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wa upande wa Bara wanataka kujua ni kwanini wao wakoseshwe haki hiyo? Dai hili halali kabisa linathibitishwa na ukweli kwa kuangalia hali halisi ya mazingira na ukubwa wa Majimbo ya Bara. Ni wazi wao pia wana haki sawa na wenzao wa visiwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya yote yanahitaji marekebisho ya Katiba ambapo wananchi wa pande zote za Muungano waamue ni aina ipi ya Muungano na Serikali ngapi ziwepo. Kwa njia hii, tuna uhakika kabisa Muungano wetu utakuwa ni wa kuigwa na majirani zetu wanaotaka kujiunga na Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna faida kubwa ambayo kwa udugu wetu tuliokuwa nao na tulio nao kama tutakuwa na mamlaka tatu tofauti na mamlaka hizo zikaingia katika Jumuiya nyingine za Kimataifa, basi tutakuwa na uwezo mkubwa kimaamuzi katika masuala yanayohusiana na kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume mbili tofauti zilizowahi kuundwa kuhusiana na Katiba ya nchi na mfumo wa siasa, Tume ya Jaji Nyalali ya mwaka 1992 na Tume ya Jaji Kisanga ya mwaka 1998 na Tume zote hizi zilitoa mapendekezo.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Jaji Nyalali pamoja na mambo mengine ilipendekeza mabadiliko ya muundo wa Muungano kuwa wa Serikali tatu kwa kuanzisha Serikali ya Tanganyika, ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ambayo tayari ipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, chini ya mapendekezo hayo, ilikusudiwa kwamba Serikali za Tanganyika na Zanzibar ziendeshe mambo yote yasiyo ya Muungano na yale ya Muungano yashughulikiwe na Serikali ya Muungano pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tume ya pili ya Jaji Kisanga, iliundwa kufuatia Waraka wa Serikali *(White Paper)* Na.1, 1998, katika kuangalia mchakato mzima wa demokrasia nchini na kuwawezesha wananchi kuamua wanataka Katiba ya aina gani.

Mheshimiwa Spika, inasemwa kuwa asilimia 96.5 ya wananchi waliohojiwa Zanzibar walitaka muundo wa Serikali mbili na asilimia 84.97 ya wananchi waliohojiwa Tanzania Bara walitaka muundo wa Serikali mbili.

Hata hivyo, pamoja na utafiti huo, Tume iliibuka na pendekezo la Serikali tatu kama ilivyofanya Tume ya Jaji Nyalali kwa kuzingatia ilichokiita maslahi ya Taifa wakati uliopo na siku za usoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, Serikali za Awamu zilizopita zimekuwa na kawaida ya kukataa taarifa za Tume zinazoziunda zenyewe. Hazijawahi kukiri au kukubali taarifa za Tume zake. Serikali hutumia fedha nyingi kuunda Tume hizo, fedha za walipa kodi na baadaye taarifa hizo kutofanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Rais wa Zanzibar kufanywa Mjumbe wa Baraza la Mawaziri la Serikali ya Muungano. Katiba, ibara ya 54(i), je nini wajibu, nafasi na majukumu ya Rais huyu katika Baraza la Mawaziri? Mbona hatumwoni akija humu Bungeni kujibu maswali kama Mawaziri wengine? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni kama kuna tatizo kuwa na Makamu wa Rais wa Muungano ambaye hana uhusiano wowote wa kikazi na Serikali ya Zanzibar? Je, Serikali imejaribu kufikiria madhara ya baadaye ya kutokea kupata Rais na Makamu wote wa Bara? Kwani Katiba inatamka tu kuwa mgombea mwenza atatoka upande wa pili wa Muungano na wala sio sharti awe ni Mzanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni mambo mengi sana hata kama yakitajwa hapa, sio mageni, ila kitu kikubwa kitakachofanya Muungano wetu kuwa imara na madhubuti na kuwafanya majirani zetu kujiunga na Muungano, ni kutungwa kwa Katiba mpya itakayoridhiwa na Watanzania wote na kueleza ni aina ipi au mfumo upi wa Muungano na Serikali ngapi zinazotakiwa kuwepo katika Muungano.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapenda kupata majibu ya kina kuhusu masuala haya yote na sio majibu ya kisiasa tu. Haya ni masuala ya kikatiba. Wote tumeapa kuilinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano, basi pale panapokuwa na masuala mazito yenye kuhitaji majibu sahihi, Serikali isiwe na utamaduni wa kuyapuuza na kuyafumbia macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala hayo, Kambi ya Upinzani inapenda Serikali itoe majibu ya kina kuhusu masuala yafuatayo kama njia ya kuyapatia ufumbuzi matatizo na migogoro ya Muungano:-

(i) Ni lini Serikali inafikiria kuleta angalau kwa njia ya Semina Hati za Muungano *(Articles of Union)* Bungeni kwa nia ya kutazama upya Hati hizo na kuangalia ni kwa njia ipi Bunge hili kama Mwakilishi wa Watanzania wote wa Bara na Visiwani, linaweza kuondoa kero mbalimbali zilizojitokeza katika Muungano wetu?

(ii) Serikali ieleze kwa kina: Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano ndiyo pia Serikali inayoshughulikia masuala ya Tanzania Bara? Ikiwa hivyo ndivyo: Je, Serikali inaeleza vipi suala la kuwa katika hali halisi ya mfumo wa Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?

(iii) Muungano ni sawa na ndoa. Wanandoa wanapotaka kuzungumzia matatizo na migogoro kati yao, huzungumza wao wenyewe ili waweze kuyatatua. Sasa tujiulize, ni aina gani ya Muungano hasa tunaoutaka?

(iv) Mheshimiwa Spika, kuna mifano mingi ya nchi zilizoungana au kuwahi kuungana Duniani. Ni vyema tukajifunza kutokana na nchi hizo ili tuweze kuwa na Muungano bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa, nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaongelea suala la Jamhuri ya Shirikisho la Afrika Mashariki. Hivi tumeshawahi kujiuliza ni nini nafasi ya Zanzibar katika Shirikisho hili tarajiwa? Je, Tanganyika itaingia kama nchi moja na hivyo kutimiza lengo la Serikali moja na kuua *identity* ya Zanzibar?!

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu ni wa kipekee katika Bara la Afrika, lakini sio wa kipekee Duniani. Nchi ya *Greenland* na Visiwa vya Faroe ni sehemu ya nchi ya Denmark. Lakini nchi hizi zina uhuru kwenye mambo yake mengi tu. Kwa mujibu wa Kitabu cha *Zanzibar and The Union Question* ambacho kimehaririwa na *Professor* Haroub Othman na *Professor* Chris Peter Maina, Faroe Island wana uhuru hata katika masuala kadhaa ya Kimataifa. Kwa mfano, wakati Danmark ni nchi mwanachama wa Jumuiya ya Ulaya, *Greenland* sio mwanachama na hivyo masuala yote yanayoamuliwa huko Brussels hayaihusu. Je, Serikali inashindwa hata kutambua uanachama shiriki wa Zanzibar katika Jumuiya ya Afrika Mashariki *(Associate Membership)? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Afrika Mashariki inafanya maamuzi yanayoiathiri Zanzibar. Mfano dhahiri ni kuhusu Kodi ya Forodha ambayo sio ya Muungano, lakini Serikali ya Muungano ikajadiliana na Kenya na Uganda kuhusu Umoja wa Ushuru wa Forodha bila kujali kuwa Zanzibar inapaswa kuwa mshiriki mkuu. Je, haya tunayafanya kwa faida ya nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani Bungeni, inapendekeza yafuatayo ili kuboresha Muungano wa Tanzania:-

(1) Suala la Muungano lisiwe suala la sera ya Chama fulani cha siasa. Suala hili liwe ni suala la Kitaifa na lizungumzwe Kitaifa. Kulifanya suala hili kuwa ni sera ya Chama ni hatari kwa Muungano pindi Chama kingine cha siasa kikiingia madarakani. *(Makofi)*

(2) Utatuzi wa kero za Muungano ufanywe kama sehemu ya mapitio ya Katiba ya Tanzania. Tunashauri Serikali izindue mjadala wa Kitaifa kuhusu Katiba na katika mjadala huu, tuwe na mjadala wa wazi na unaohusisha wananchi wote kwa ujumla kuhusu Muungano na suala zima la mpasuko wa kisiasa Zanzibar. *(Makofi)*

(3) Uboreshaji wa Muungano wetu uzingatie hali ya baadaye ya Tanzania katika ushirikiano wa Kimataifa kama Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, sote tunautakia mema Muugano wetu. Muungano usihodhiwe na Chama fulani. Muungano ni wa Watanzania na ni Watanzania watakaoulinda na kuutetea. Tujadili Muungano wetu kwa uwazi ili kuuimarisha.

Mheshimiwa Spika, nawashukuru kwa kunisikiliza na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninayo orodha ya wachangiaji 12 hadi sasa. Sijui kama itawezekana kuchangia wote kwa sababu tutafunga mjadala saa 11.30 ili kuruhusu saa 11.45 Waheshimiwa Mawaziri nusu saa kila mmoja kuweza kujibu hoja na tuingie kwenye Kamati saa 12.45 ili tupate saa moja ya Kamati. Kwa hesabu zangu hapa

inaelekea watakaoweza kuchangia ni kumi, lakini tujaribu tuone maana yake tumeokoa muda kidogo pengine itawezekana. Naomba niwataje ili wajiandae. Ambao hawajachangia kabisa ni Mheshimiwa Riziki Said Lulida na Mheshimiwa Abubakar Khamis Abubakar. Hawa hawajachangia, kwa hiyo, wana kipaumbele. Waliochangia mara moja ni Mheshimiwa Masilingi, Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Prof. Mwalyosi, Mheshimiwa Haroub, Said Masoud, Mheshimiwa Faida Bakar, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Sameer Ismail Lotto, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahiri na Mheshimiwa Mariam Mfaki. Aliyechangia mara mbili ni Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

Sasa nilisema nitawapa kipaumbele wale wawili ambao hawajachangia, wataongea tu, ila naomba nitoe nafasi maalum leo kwa mwenzetu Mheshimiwa Wilson Mutagaywa Masilingi, ni sikukuu yake ya kuzaliwa anatimiza miaka 50. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wataniwia radhi Waheshimiwa Abubukar na Mheshimiwa Riziki ili Mheshimiwa Masilingi atangulie halafu sasa ndio atafuata Mheshimiwa Riziki na baadaye Mheshimiwa Abubakar.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi kwa upendeleo maalum kama zawadi ya siku yangu ya kuzaliwa ambapo nimetimiza miaka 50. Nakushukuru sana na namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuifikisha miaka hii 50, nilikuwa naisubiri kwa hamu kweli. Wengi niliozaliwa nao wametangulia mbele ya haki na wanaozaliwa hivi karibuni. Kwa hiyo, ni jambo la kipekee kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu. Najua kuna kaka zangu wengi humu ndani ya Bunge na wadogo zangu pia. Wale wadogo zangu nawaombea kila la kheri na wao wafikishe miaka 50. *(Makofi)*

Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nawashukuru wazazi wangu, Marehemu mama na baba walionilea na kunitunza na kunijengea mazingira mazuri ya kufikisha miaka 50. Namshukuru mke wangu pia, ananitunza vizuri. Nasema haya kwa sababu sitafanya sherehe ya kuzaliwa kwangu kwa sababu kuna watoto wengi chini ya miaka mitano Jimboni kwangu hawakufikisha miaka 5. *(Makofi)*

Lakini namshukuru na Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere na Waasisi wa Taifa letu kwa kututafutia uhuru, nasheherekea miaka 50 kwenye nchi huru na amani. Pia nawashukuru kwa kunipatia elimu, maana bila mipangilio mizuri ya Waasisi wa Taifa letu nisingekwenda Shule na nisingekwenda shule nisingeijua Dodoma na kuwa Mbunge. Kwa hiyo, nawashukuru sana sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema maneno hayo machache ya utangulizi, ya furaha ya sherehe ya kuzaliwa, sasa naingia kwenye hoja.

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Serikali nzima ya Awamu ya Nne kwa sababu maalum. Mazingira, lengo lake ni kuhifadhi watu. Mazingira, ina maana pana, ni suala mtambuka. Mheshimiwa Waziri Mkuu baada ya mchango wangu wa awali katika hotuba yake katika dakika nane baada ya kukaa nilipomaliza kuchangia, alichukua hatua za haraka sana. Waziri wa Afya akaagizwa aende Jimboni na mimi nikashirikishwa na Serikali kwa uwazi na ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zaidi ya hapo, Serikali imechukua hatua za haraka kweli kweli. Wananchi Jimboni Muleba Kusini na hususani hospitalini Lubya pale watu wanauguza watoto kwa matumaini makubwa sana. Dawa zimekwenda na misaada mingi kutoka Serikalini imekwenda.

Mheshimiwa Spika, kupitia kwa Waziri Mkuu, namshukuru Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Tulikutana naye Mwanza nikiwa na Waziri wa Afya. Akataarifiwa na Mheshimiwa Waziri wa Afya, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Rais wa Awamu ya Nne, aliipokea taarifa hizo kwa masikitiko lakini akampongeza Waziri Mkuu wake kwa hatua hizo alizochukua na akamwambia Waziri wa Afya, "fuatilia kwa haraka sana na mtatue tatizo haraka," akatutakia kila la kheri na baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la kusifu. Kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Muleba Kusini, naishukuru Serikali hii na namshukuru kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *speed* hii yaku-*respond* kwa maelezo ya Waheshimiwa Wabunge. Sio Mbunge, anazungumza maneno, mtu anasema iundwe Tume ya kuchunguza kama Mbunge anazungumza ukweli.

Mheshimiwa Spika, huwezi ukawa Mbunge ukaingia Bungeni kusema uongo, labda uwe una matatizo fulani na hayo yanadhibitiwa kwa mujibu wa kanuni unapotakiwa kuthibitisha kwenye Meza ya Spika kwa unayoyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siku moja kujadili Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira na Muungano, kwa kweli haitoshi. Nashauri wakati ujao wapewe siku mbili. Mambo ya mazingira na muungano ni muhimu sana na kwa kweli katika mfumo wa uendeshaji wa shughuli za nchi yetu tuhakikishe tunayapa uzito unaostahili.

Kwa hiyo, wachangiaji wakiwa wachache, Taifa halitapata maoni ya Wabunge kuhusu masuala mengi ya mazingira na muungano ambayo ni nyeti na yangepaswa kupata ushauri wa Wabunge walio wengi kwa kauli ingawaje najua wengine watachangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nianze na eneo la Muungano. Naunga mkono hoja kama ilivyowasilishwa na Mawaziri Wawili, Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Muungano na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Wamezungumza, wameweka mambo mazuri sana. Nawapongeza sana na watumishi au Watendaji katika Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kazi wanazozifanya katika kuboresha mazingira yetu na kuimarisha Muungano.

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi kwa jitihada ambazo wameanza kuzifanya kuzungumzia matatizo yanayotokana na utekelezaji chini ya Muungano. Mimi sitaseme mengi juu ya Muungano kwa sababu nilishachangia maoni yangu juu ya Muungano. Naamini itatosheleza tu, kunukuu Katiba, Ibara ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nitanukuu na Ibara ya tatu fasili ya kwanza ya Katiba hiyo. Ibara ya Kwanza yenye mstari mmoja inasema: "Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano." Mwisho wa kunukuu Ibara ya kwanza ya Katiba. Tanzania ni nchi moja na ni Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, Katiba inasema ni nchi moja. Ibara ya Tatu inazungumza fasili

ya kwanza: “Jamhuri ya Muungano ni nchi ya Kidemokrasia na ya kijamaa isiyokuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, nimenukuu haya kwa makusudi ili niweze kunukuu aliyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Muungano. Katika hitimisho na maneno mengi aliyoyazungumza katika kutekeleza wajibu wake kama Msemaji wa Kambi ya Upinzani ambayo ndiyo sehemu ya utekelezaji wa Sera yetu itokanayona Katiba ya Demokrasia katika Muungano wetu, anasema hivi, namnukuu: “Sote tunautakia mema Muungano wetu, Muungano usihodhiwe na Chama fulani, Muungano ni wa Watanzania na ni Watanzania watakaoulinda na kuutetea. Tuujadili Muungano wetu kwa uwazi ili kuuimarisha.” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni siku yangu ya kuzaliwa, sitaki kukorofishana na mtu. Unajua siku ya *birthday* hupaswi kukorofishana na watu. Kwa hiyo, niliona ninukuu hilo na kusema yale aliyoyasema mwanzoni sitayabadili ili kuimarisha Muungano kwa sababu demokrasia inahitaji kila mtu azungumzie Muungano.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi, wameanza kuzungumzia matatizo yatokanayo na utekelezaji. Mimi siamini kabisa kwamba kuna kero za Muungano katika imani yangu. Mimi naamini Muungano ni faraja, isipokuwa katika Muungano kuna matatizo ya utekelezaji. Sasa inawezekana ni matatizo ya Kiswahili, lakini ukisema kero za Muungano unamaanisha Muungano unakera. Hii sio sahihi. Lakini mimi nikiangalia orodha ya mambo ya Muungano katika Katiba ukurasa wa 128 yapo mambo 22, haya, hayatoshi kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi katika kukutana kwao, katika agenda zao, wote naamini wana agenda ya kuimarisha Muungano kweli kweli. Naomba wafikirie kuongeza orodha ya mambo ya Muungano. Hii orodha haitoshi. Kwa mfano mtu unazungumza uraia, lakini huingizi afya za raia hao. Afya pia iwe ni jambo la Muungano, kwa maoni yangu. Mfano mwingine, katika Katiba unaweka Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania na mambo yote yanayohusika na kazi ya Baraza hilo halafu unasema mambo ya Muungano yabaki ni Elimu ya Juu tu! Elimu ya Msingi iingizwe kwenye orodha ya mambo ya Muungano. Tunauimarishaje Muungano kama hatuimarishi hata vipengele vinavyoimarisha Muungano kama afya za watu wetu na elimu?

Mimi ningependekeza Elimu ianzia Shule za Msingi, *Kindergarten* mpaka Elimu ya Juu iwe ni suala la Muungano. Kwani inadhuru nini katika maslahi ya Muungano? Elimu italenga kuimarisha Watanzania watakaoujenga Muungano. Mimi najua Watanzania kadri miaka inavyokwenda na mimi namwomba Mwenyezi Mungu aniongezee miaka mingine 50 niwepo, kuna mijadala mingine ndani ya Bunge hili itakwisha kabisa hasa tukiboresha Elimu, tukapambana na umaskini. Kwa hiyo, masuala ya kugawana madaraka, nani anamiliki kipi, yatakosa nafasi ili maslahi ya Taifa na hivyo ya Muungano wetu yatashika nafasi ya pekee. Nimeyasema hayo kama mchango kwenye Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye mambo ya Mazingira ninataka kuchangia kwenye ukurasa wa 64 wa hotuba. Kwenye hotuba, ninanukuu kwa sababu sitasema mengi. Wanasema, namnukuu Mheshimiwa Waziri: "Katika kipindi cha mwaka 2006/2007 Baraza limeelekeza nguvu zake katika utekelezaji wa Sheria ya Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 hususan katika kujenga uwezo, kupanua ajira ili kuweza kukabiliana na majukumu ya utekelezaji wa sheria hiyo." Mwisho wa kunukuu. Hayo ni majukumu ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, lakini ningeshauri hivi, kwa vile tunayo Sheria hiyo Na. 20 ya mwaka 2004 Serikali iweke mkakati wenye fedha za kutosha kwa sababu ukiangalia kwenye Bajeti ya Maendeleo, fedha za ndani tumetenga Sh. 854,294,000/=. Fedha nyingi ni za kigeni, Sh. 7,239,800,000/=.

Kwa hiyo, katika kutekeleza mkakati huu wa Hifadhi ya Mazingira tumetenga fedha kidogo sana katika Bajeti hii ya kuhifadhi mazingira. Kwa hiyo, Bajeti inayokuja, tutenge fedha za kutosha kutekeleza Sheria Na. 20 ya mwaka 2004. Hii itawezesha kupeleka Hifadhi ya Mazingira hadi Vijijini na Mitaani, kwa sababu tulivyo sasa hivi, Hifadhi ya Mazingira inaendeshwa kwa *operation,* "Ondoa Mifugo Hapa," "Ondoa Watu Hapa," "Shika Kiwanda Hiki." Lakini kwa lengo la Sheria, inapaswa iwe ni shughuli ya kudumu na wataalam wa Mazingira katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Hifadhi ya Mazingira, wawe na majukumu ya kweli kwa kuongeza Watendaji.

Mheshimiwa Spika, kuna vijana wengi wametoka Vyuo Vikuu na Vyuo vya Juu, wanatafuta ajira, watalaam wa misitu, wataalam wa Hifadhi ya Mazingira hawana ajira na wakiajiriwa watakwenda mpaka Wilayani na Hifadhi itakwenda Vijijini ili tuweze kujenga mazingira yetu kwa ajili ya watoto wetu na wajukuu wetu.

Mheshimiwa Spika, mimi naamini huwezi ukazungumzia mazingira bila kuzungumza umaskini. Mimi mwenyewe Mbunge, kwenye familia yangu tunatumia mkaa. Hakika! Nyumbani Jimboni, natumia kuni. Kwa hiyo, tutaendelea kukata miti. Hakika! Sasa tukiendelea hivi na haiepukiki, tutaharibu mazingira na nishati mbadala huwezi ukasema igharamiwe na Serikali. Tutakachotakiwa kufanya ni kuhakikisha kwamba iende sambamba na kuwawezesha wananchi kiuchumi ili hata ukisema tutumie gesi, waweze kuinunua, waweze kuulipia umeme. Mataifa ya nje kama tulivyokubaliana katika Mikataba ya Kimataifa, pesa wanazotoa Shilingi bilioni saba, kwa kweli siyo pesa za kutosha kuchangia hifadhi ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali idai zaidi. Tanzania tumeji-*sacrify* sana. Tumetenga nchi yetu kwa kiwango kikubwa zaidi ya asilimia 25 ya nchi yetu kwa ajili ya hifadhi, urithi wa dunia. Wanakuja wanaangalia misitu yetu, mbuga za wanyama na milima, lakini michango Dola za Kimarekani milioni saba. Huu sio mchango wa kutosha kusaidia kuhifadhi mazingira ya Tanzania ambayo ndiyo milki ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI L. SAID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ambayo kwangu nimefarijika sana.

Awali ya yote, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa CCM kwa kishindo kikubwa. *(Makofi)*

Pili, napenda kutoa salamu zangu na pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya aliyoionyesha kwa kutembelea Mkoa wa Lindi na kujionea mazingira na mandhari ya Lindi. Napenda upokee hizo pongezi.

Tatu, napenda kutoa pongezi kwa Sekretarieti nzima ya CCM iliyochaguliwa. Mwisho, napenda kumpongeza Waziri wa Mazingira Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandosya kwa kupewa hii Wizara ya Mazingira na yeye mwenyewe akiwa mwanamazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hasa katika Wizara ya mazingira.

Mheshimiwa Spika, mazingira ni uhai na uhai ni mazingira. Sitakuwa na mengi ya kuzungumza, lakini nitazungumzia katika Hifadhi ya Mazingira ukurasa wa 19. Katika Ilani iliyoletwa na Serikali, ninanukuu:

"Taifa letu sambamba na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka 2005, kwa kuanzia Serikali imepitisha mkakati wa kuhifadhi mazingira ya ardhi na vyanzo vya maji ambapo hatua mbalimbali zitachukuliwa ili kukabiliana na changamoto mbalimbali kama zifuatazo:-

(1) Uharibufu wa Mazingira na wa vyanzo vya maji utokanao na moto." Kwa kweli hili inabidi litiliwe mkazo sana hasa katika Mkoa wangu wa Lindi. Mkoa wangu wa Lindi Mwenyezi Mungu ameubariki kuwa na misitu ya kutosha ambayo inatusaidia kupata mvua za kutosha, lakini elimu ya mazingira haijafika kwa wakulima. Ukifika kule utakuta wananchi hawawezi kuanza kulima mpaka wachome moto. Hivyo, inaathiri uoto wa asilia na viumbe hai vidogo vidogo ambavyo viko katika ardhi. Hivyo naomba Waziri aliangalie na alipe kipaumbele na atembelee akaone hiyo hali kuanzia sasa hivi kwa vile ni msimu na wanatarajia kuanza kilimo.

(2) Mkoa wa Lindi, kumeingia balaa kubwa sana la ukataji wa miti ambao unachangiwa na Wizara ya Maliasili. Wanaharibu raslimali yetu ambayo tulikuwanayo, miti ya kutosha na hifadhi ya kutosha lakini sasa hivi ukienda Lindi hata kama ilitolewa Ilani kwa miti isikatwe lakini bado uharibifu unaendelea.

(3) Mkoa wa Lindi na Mtwara tuna fukwe safi sana, Mkoa wa Lindi na Mtwara tuna *beach* ambazo katika Afrika hakuna, lakini hazikutumiwa

kikamilifu. Matokeo yake hizo fukwe ni fujo ya ukataji wa miti ya mikoko na ni sehemu ya vyoo vya wananchi, lakini hii yote ni kutokana na wananchi hawa hawakupewa elimu ya matumizi ya fukwe.

Mheshimiwa Spika, sasa basi ninachosema ni kwamba ninaomba Serikali hii tukufu itilie macho mazingira Kusini ili uoto wa asilia uendelee kudumu, maji na mvua tuweze kuzipata za kutosha maana yake Mikoa mingine wanahangaika na ukame, lakini Lindi, Mtwara na Kusini yote, suala la ukame halipo.

Mwisho, napenda kusema tena kwamba umetokea uharibifu wa mazingira kwa wafugaji. Serikali naomba itilie mkazo na ilione hili. Ninashukuru Waziri wa Mazingira, alitupa nafasi sisi Kamati ya Mazingira kutembelea Mbarali na kweli tuliona uharibifu. Lakini kwa vile wale wafugaji hawakupewa mazingira, mazuri na elimu sasa wameamua kuhama kukimbilia Mkoa wa Lindi, je, Serikali badala ya kuzuia tatizo wanaongeza tatizo?

Tunachoomba, Serikali ifuatilie kwa makini kuona huu uharibufu wa mazingira ambao utaukumba Mkoa wa Lindi uweze kurekebishwa mapema iwezekanavyo kwa kuhakikisha kuwa wafugaji wanaotoka Ihefu na sehemu nyingine za Mbarali wawekewe mazingira mazuri.

Mheshimiwa Spika, wananchi hawajakataa wafugaji kuja katika Mkoa wa Lindi, lakini wawekewe mazingira mazuri. Mazingira ya kwanza ni kujua ni wapi watakaa, watengenezewe majosho na watoto wao wanaopita kuzunguka nao bila kupata elimu wapewe elimu, hili nalo vilevile ni changamoto.

Pili, hawa wafugaji wana uharibifu mkubwa wa mazingira kutokana wafugaji hasa Wasukuma hawapendi miti na ile miti wameikuta kule ipo kwa miaka, matokeo yake wakifika ni kukata miti na kutuletea uharibifu wa mazingira katika Mkoa wa Lindi. Kwa hili ninaomba Waziri wa Mazingira atembelee na akajionee uharibifu huo.

Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Mazingira kwa kuona hilo na ninapenda kutoa ujumbe mwingine. Kusini tuna bahari na tuna fukwe za bahari zetu, kuna miti aina ya mikoko. Kwa kweli wananchi wanakata ovyo na wanajaribu kutumia wizi wa kutoa hiyo miti kwa kutumia majahazi. Majahazi yanachukua miti yanapeleka nchi mbalimbali hasa Somalia, matokeo yake bahari inakula Vijiji, Vijiji mbalimbali vimeanza kuathirika kwa kuliwa na maji ya bahari na hivyo ningependa Waziri aungane na mimi akajionee hiyo hali ambayo ni ya uharibifu ya ukataji wa miti hovyo. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii angalau kuchangia kidogo kuhusu hotuba ya Mawaziri wawili ambao ni Waziri wa Mazingira na Waziri wa Muungano.

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru kwa hotuba yao ambayo ina mwelekeo kidogo, lakini naomba nitoe mawazo mawili au matatu ambayo ninaamini yanaweza sana yakasaidia shughuli zetu kwa faida ya nchi yetu na zaidi, mimi nitazungumzia kuhusu masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, Muungano huu uliopo ni Muungano ambao sote tunaukubali, ni Muungano ambao umezaliwa miaka 43 nyuma na hakuna anayebisha kwamba Muungano huu ni halali.

Kuna maneno ambayo yanazungumzwa kwamba pengine kulikuwa hakuna *ratification* na mambo kama hayo ni sawasawa, lakini katika masuala haya unapokaa sana, kuna mambo ambayo yanaitwa ***acquiescence,*** kwa maana hiyo, Muungano huu tunaukubali sote kwa misingi hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini napenda niseme tu kwamba Muungano huu ulitokana na Sheria Mama, naweza nikaiita *Articles of Union*. Sasa *Articles of Union* hizi ninavyofikiria mimi ndiyo *Grand norm* ya Muungano wenyewe. Kwa hiyo, ni lazima iheshimiwe, ienziwe na kama kuna matatizo, basi ni lazima yawe *addressed to,* ili tuweze kuondokana na matatizo ambayo yapo.

Lakini Sheria Mama hii yaani *Articles of Union* imesahaulika kabisa. kuna mambo ambayo yamo katika *Articles of Union,* lakini hayashughulikiwi na yamepuuzwa. Kwa maana hiyo, *Grand norm* yetu, hii *Articles of Union* ndiyo msingi mmoja mkubwa ambao unaleta matatizo ya Muungano.

Sasa hili ni kero moja ya msingi ambayo nahisi sisi kama ni Watanzania ni lazima tukae tutazame *Articles of Union* zile zilifanya nini? Zilisema nini? Zilitaka nini? Je, tumezitekeleza? Au kuna mambo ambayo tunayaendesha kinyume na *Articles of Union* zile? Sasa tukishafanya hivyo, mimi nahisi moja kati ya misingi mikuu ya kero zinaweza au linaweza likaondoka.

Sasa mimi ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba, *let us go back* kwenye *Articles of Union,* tuzitazame: Je, zina matatizo gani na zina makosa gani na halafu tu–*compare* na Katiba iliyopo kwa sababu Katiba ni *creature* iliyokuja au ni kitoto kilichokuja baada ya kuwepo hiyo *Articles of Union*.

Sasa Katiba ninavyohisi mimi ni kwamba ni ndogo kuliko hii *Grand norm* au kuliko makubaliano ya Muungano na pale ambapo Katiba inakwenda kinyume na *Grand norm,* nafikiri ni lazima tukae na turekebishe kwa faida ya Watanzania wote. Sasa hilo ni moja ambalo naiomba Serikali watazame kwa misingi hiyo kwamba hili ndilo tatizo moja kubwa ambalo lipo.

Mheshimiwa Spika, la pili, tutazame ile *nature* ya Muungano ambayo imekuwa *envisaged.* Ukitazama katika kifungu cha nne au Ibara ya nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano vifungu vidogo (1), (2) na (3) utaona kwamba katika Ibara hizi kuna *jurisdictions* mbili. Kuna *jurisdiction* au kuna mamlaka ya Serikali ya Muungano wa

Tanzania na kuna mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini katika Serikali ya Muungano wa wa Tanzania, ndani yake kuna *jurisdiction* nyingine mbili. Kwa yale mambo ambayo sio ya Muungano, basi yatashughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano na pia kwa mambo ya Muungano yatashughulikiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo, hapa *it is obvious* kwamba kuna mambo mawili au kuna *jurisdictions* mbili katika Katiba moja ambayo inashughulikia mambo ambayo sio ya Muungano na mambo ambayo ni ya Muungano kwa Tanzania Bara.

Halafu *jurisdiction* nyingine ambayo ni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hii inashughulikia mambo ambayo sio ya Muungano ambayo yanahusu Zanzibar. Kwa maana hiyo, ni wazi kila mtu anajua kwamba Jamhuri yetu ya Muungano ina *jurisdictions* tatu.

Ya kwanza, ile ambayo inashughulikia mambo ya Muungano, ya pili, ile ambayo inashughulikia mambo ambayo sio ya Muungano, lakini yanahusu Tanzania Bara na ya tatu, yale ambayo sio mambo ya Muungano lakini ni kwa Zanzibar. Kwa hiyo, *what is the end result* ya *jurisdictions* tatu hizi? Kila mtu anajua kwamba hayo mambo yalikuwa *envisaged* nyuma, ni kwamba kuwe na Serikali tatu. *It is very obvious* kwa msimamo huu na kwa maana hiyo, zile kelele ambazo tunapiga siku zote, zimekuwa *answered* katika Katiba. Sasa tunachotakiwa sisi ni *to put this into action, very simple.* Sasa ndiyo tukasema kwamba *jurisdictions* hizi ili kuondoa mambo ambayo yanaleta mgongano na yanaleta kero tui-*translate* vizuri na kwa nia safi kile kifungu cha Ibara ya Nne ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ambayo inatupa *jurisdictions* mbili kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kwa mambo ambayo sio ya Muungano kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi ninachosema ni kwamba mambo haya tuyatazame katika *connection* hiyo na tuwe wa kweli katika kuimarisha suala letu zima la Muungano.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu ambalo nataka nilizungumze ni kuhusu kero za Muungao, ingawa kuna wengine walisema sio kero, ni matatizo. Mimi naona ni sawasawa, ukisema kero au matatizo. Lakini *issue* ni kwamba, kuna *issues* ambazo pande zote mbili bado zina matatizo nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa kero hizi ni nyingi sana, hatuwezi kuzitaja katika nafasi hii au katika muda huu mfupi tulionao, lakini mimi nafikiri suala la kwanza kabisa, ikiwa kweli tunataka tuwe ni *genuine* katika masuala haya ya Muungano na tushughulike katika masuala haya, basi masuala kama yaliyoelezwa katika kitabu cha hotuba ukurasa wa 16 mimi nafikiri *with due respect* tungelisubiri kwanza kwa sababu hapa Mheshimiwa Waziri anasema kwamba ukurasa wa 16 chini *item number 23:* "Muungano wetu unakua na umepitia hatua mbalimbali, hivyo imejitokeza haja ya kuongeza maeneo mengine katika mambo ya Mungano."

Mimi nafikiri *statement* hii sikubaliani hata siku moja. Sikubaliani nayo kwa sababu moja kubwa, hivi sasa tuna matatizo tunayosema ni ya Muungano, sasa ikiwa kuna matatizo ambayo pande zote mbili, zinakubali kwamba kuna matatizo, kwa nini

hatuyatatui matatizo haya tukajua misingi yake, tukaweka misingi mizuri ya mambo mengine ambayo baadaye tunaweza tukayaongezea katika orodha ya Muungano au tukayapunguza katika orodha ya Muungano?

Mheshimiwa Spika, lakini ikiwa kila siku tutakaa, tutasema tu, kwamba tuongeze kwa sababu Muungano wetu unakua bila ya kutatua matatizo ambayo yapo, mimi nahisi tunalipeleka gari letu mahali pabaya. Kwa hiyo, *statement* hii nahisi kwamba tusiitekeleze, lakini kwanza tuondoe yale au tutatue matatizo na kero ambazo zipo, tujue ni sababu gani ambazo zimeleta matatizo haya. Je, tutafanya vipi na halafu baadaye tunaweza tukaongeza mambo ambayo tunahisi yaongezwe. Lakini hivi ni kuongeza au Waswahili wanasema kutia msumari wa moto katika kidonda! Hayo ni matatizo!

Mheshimiwa Spika, katika matatizo haya ya Muungano, kuna suala kwa mfano katika nyongeza ya pili katika ukurasa wa 130, katika nyongeza hii ya Katiba, inasema: "Mambo ambayo mabadiliko yake yatahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Bunge kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Zanzibar." Maelezo pale ni mambo nane.

Mheshimiwa Spika, lakini ukitazama namba tano na sita, madaraka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Zanzibar, mimi najiuliza hivi kweli Mahakama Kuu ya Zanzibar, kwa mfano tunataka kuibadilisha, kuna haja yoyote ya kupata theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Bara? Theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar! Haina maana, sasa hii ni kero.

Mheshimiwa Spika, kweli Mamlaka ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inahusu kitu gani kwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano kupata theluthi mbili ya Wabunge kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar na haya au ni mamlaka ya Serikali ya Mapunduzi ya Zanzibar ni mamlaka ya Zanzibar? Sasa haya ni mambo ambayo nayo ni kero. Tujaribu kuyatatua haya, halafu namna ya kuongeza mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo ni kero, kwa mfano kuna suala la Mambo ya Nje, kwa bahati imeelezwa katika hotuba ya Waziri, kuna wafanyakazi 30 tu katika Wizara nzima ya Mambo ya Nchi za Nje, maana yake amesema Mabalozi watatu, Naibu Waziri mmoja na wafanyakazi 26. Sasa tukisema kwamba Zanzibar mnaionea, nani hatakubali? 30 katika Wizara nzima ya Mambo ya Nje, haiwezekani! Tutatueni haya halafu ndiyo tufikirie kuongeza mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la mafuta na gesi yote ni mambo ya Muungano ambayo yamo katika Katiba. Leo gesi imeshachimbwa, kuna bilioni za pesa ambazo zipo, kwa nini Zanzibar hawapewi? Au angalau hawaambiwi fedha hizi katika mgao wa mambo haya, basi Zanzibar kuna hivi na hivi, au tuambiwe kwamba bado tunajadiliana katika *issues* hizi za mafuta, za gesi kwa hiyo, tusubirini.

Lakini kusubiri kuwe na maandishi maalim kwamba fedha zilizopatikana ni hizi. Lakini leo gesi imo katika Katiba, ni mambo ya Muungano. *Billions of money* zinapatikana, hatuna, hata Shilingi moja Zanzibar iliyopewa!

Sasa kwa nini tusiseme kuna kero za Muungano au kuna matatizo ya Muungano kama alivyosema Mheshimiwa Wilson Masilingi, *there are problems*. *To address* matatizo yetu kwanza, tuyatatue haya halafu ndio tuendelee. Kuna *encroachment* hivi sasa inafanywa.

Mheshimiwa Spika, ukitazama Mkataba wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuna mambo mengi ambayo si ya Muungano. Kwa mfano, Mkataba wa Afrika Mashariki unasema kwa mfano, utalii na wanyamapori, elimu na mafunzo, masuala ya miundombinu mambo kadha wa kadha. Mambo haya yanaingizwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ikiwa yanaingizwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo si mambo ya Muungano, Zanzibar iko wapi? Itashughulikiwa namna gani kwa sababu haya ni mambo ambayo yanashughulikiwa na Zanzibar, je, Zanzibar sasa itakwenda katika Jumuiya ya Afrika Mashariki namna gani ili kutetea haki hizi? Kwa sababu haki au masuala haya hayatetewi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ni Wazanzibar wenyewe, ni Serikali ya Zanzibar ambayo ifanye utetezi huo. Sasa hizo ndio kero za Muungano ambazo lazima tuzitatue tujue tutakwenda vipi au tutafanya namna gani.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba kwanza tuangalie upya Katiba na *Articles of Union*. Tukiziangalia upya hizi zinaweza zikatupa *green light* ya kitu gani tufanye. Pili, tuwashirikishe *stakeholders* wote ambao ni wananchi wote wa Tanzania nzima na tatu baada ya kushirikisha hawa na baada ya kutazama hayo ndio baadae Serikali zetu ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitakaa kwa kupitia Mawaziri Wakuu na vyombo vingine baada ya kupata maoni kwa *stakeholders* na watu wengine. Hhapo mimi nafikiri Muungano wetu tutaufanya uwe mzuri, sote tutaridhika na tutaendelea katika misingi mizuri ya Muungano, vinginevyo siku zote tutasema kwamba kuna kero za Muungano, Zanzibar inaonewa na mambo kama hayo.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais ya Muungano na Mazingira. Kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa jinsi alivyowasilisha bajeti yake kwa umakini na umahiri mkubwa. Lakini vile vile niwapongeze watendaji wa Wizara yake kwa maandalizi ya bajeti. Pia vile vile nampongeza Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano kwa kuanza kukabili matatizo ya Muungano kwa ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya kama Mheshimiwa Rais alivyoahidi alipolihutubia Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza ningependa kuchangia kuhusu mazingira. Kwa upande wangu sioni kama Muungano una matatizo makubwa sana, kwa hiyo, ningependa kuelekeza nguvu zangu kwenye eneo linalohusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, tatizo la uharibifu wa mazingira kwa hali ya sasa lina sifa kabisa za kuitwa janga la Taifa na ukiangalia kwa mienendo ya hali ya hewa ya nchi yetu na kwa majanga ambayo yanajitokeza tunahitaji kuweka nguvu kubwa ya kukabiliana na tatizo hili. Sasa nimeangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwenye maeneo mengi nikaona kwamba kuna maeneo ambayo yanahitaji kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu sote tunajua kwamba tayari kuna majanga dhahiri yanayotokana na uharibifu wa mazingira lakini vile vile kwenye Ilani yetu ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ukiangalia Ibara ya 112 imeeleza wazi kabisa kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaweka nguvu kubwa katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira na katika kuonyesha jitihada hizo Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge lako Tukufu tarehe 30 Desemba, 2005 alizungumzia, ukiangalia hotuba yake kuanzia ukurasa wa 48 hadi wa 51 alizungumzia mikakati na kuna maagizo waziwazi yamewekwa ambayo ameagiza Wizara inayohusika na Maliasili kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Kwa kuzingatia hayo bado Mheshimiwa Rais na Serikali yake akawa pia ameweka nguvu katika kuanzisha Wizara inayohusika na Mazingira moja kwa moja na tarehe 1 Aprili, 2006 Mheshimiwa Makamu wa Rais akatoa tamko linaloelekeza jitihada za muda mfupi wa kukabiliana na tatizo la mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwanza nilitaka niweke wazi kwamba uharibifu wa mazingira ambao unaathiri nchi yetu si ule unaotokana na wafugaji. Nasema hivyo kwa sababu ng'ombe wanakula nyasi hawali majani, kwa hiyo mara nyingi wafugaji hawaendi kwenye misitu wanakwenda kwenye nyika. Uharibifu wa mazingira unaoharibu nchi yetu ni ufyekaji wa miti ambao ndio chanzo cha mvua, ambao ndio huleta maji, kwa hiyo, tusiende kwenye jibu la haraka haraka kwamba wafugaji ndio wanaoathiri au kuharibu mazingira kwa kiasi kikubwa. Anayeharibu mazingira kwa kiasi kikubwa ni binadamu, shughuli zake kilimo, utafutaji wa nishati kuni, mkaa, mbao na shughuli zingine kama hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa napenda kuiomba Serikali ijielekeze katika utatuzi wa tatizo la uharibifu wa mazingira au utowekaji wa misitu katika kukabiliana na matatizo haya ambayo yanatokana na binadamu mwenyewe. Sasa nimeiangalia hotuba ya Mheshimiwa Waziri aliyewasilisha na nilitegemea mtu mwingine yeyote atakayeisoma au akisikiliza hotuba hiyo angeona kwamba msisitizo uko wazi katika kukabiliana na matatizo hayo, *expectations* zangu katika Wizara hii kwanza nilitegemea kwamba fedha nyingi zitengwe kwa ajili ya kukabiliana na uharibifu wa mazingira hasa unaoelekea au unaohusu tatizo la *deforestation,* shughuli nzima inayohusu urejeshaji wa misitu ya asili na ya kisasa au misitu ya kupanda na ambayo kwa sasa hivi inatoweka.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile baada ya fedha hizo nyingi kuwa zimetengwa, nilitegemea pia mgawanyo wa fedha hizo ulenge katika maeneo ambayo yana matatizo ya wazi au matatizo makubwa. Naweza kusema kwamba kwa mtazamo huu au usikilizaji

wa hotuba hii nikilenga katika maeneo hayo, nimeona kuwa kuna *gap* na ndio hasa nimeona ni vizuri nizungumzie hilo, kwanza kama wachangiaji wengine walivyosema tulivyosikia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwamba fedha ambazo zimetengwa ni kama shilingi bilioni tisa kwa ajili ya kukabiliana na tatizo zima la mazingira. Kwa ujumla pesa hizi ni kidogo.

Vile vile nimejaribu kuangalia jinsi Serikali ilivyojipanga kukabiliana na uharibifu wa mazingira kwenye maeneo mbalimbali. Katika kufanya hivyo nilirejea kitabu kinaitwa mpango wa Serikali wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi mwaka 2005 kwa kipindi cha mwaka 2006/2007, kitabu cha pili kinachozungumzia Mikoa.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu hiki Serikali imeainisha mikakati ambayo itawekwa katika kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira. Uharibifu wa mazingira umekuwa mkubwa sana na madhara yake yamekuwa wazi sana kwenye Mkoa wetu wa Shinyanga na Tabora, pia imeathirika sana kutokana na matumizi ya nishati ya kuni na mkaa. Misitu inatoweka kutokana na ukataji wa miti ovyo, watu wakijitafutia kuni au mkaa lakini vile vile kwa ajili ya shughuli za ujenzi kama ukataji wa miti kwa ajili ya mbao.

Mheshimiwa Spika, ukifika Wilaya ya Kahama sasa hivi utasikitika, kimsingi Wilaya ya Kahama na Urambo kwa sababu najua pia Wilaya ya Urambo ina-*produce* mbao kwa kiasi kikubwa sana ambazo ndio zinakuja kuuzwa kwenye sehemu mbalimbali za nchi yetu. Wilaya ya Kahama kwa miaka ya nyuma ilikuwa inapata mvua karibu kipindi chote cha mvua. Miaka ya karibuni tumeanza kupata matatizo ya mvua lakini ukiangalia tatizo kubwa ni ufyekaji wa miti. Sasa nilikuwa namwomba sana Mheshimiwa Waziri afanye jitihada za makusudi za kunusuru jangwa katika Mkoa huu. Wilaya ya Kahama ambayo ndio naielewa kwa uwazi na vizuri zaidi kuna Kata kwa mfano Kata kama ya Idahina, Igwamanoni, Segese, Chela, Lunguya, Kata hizi misitu yake imetoweka katika miaka ya karibuni kutokana na ukataji wa miti na kuchoma mkaa.

Mheshimiwa Spika, mkaa huu unaochomwa katika maeneo haya ndio unaouzwa kwenye soko la Mwanza na Mji wa Shinyanga. Sasa ukiangalia fedha ambazo zimewekwa kwa ajili ya kupanda miti kwenye maeneo hayo ni kidogo sana. Kwa kutumia kitabu hicho hicho ambacho nimekitaja hapa punde cha mikakati ya Serikali nimejaribu kuangalia uwiano wa kimikoa Mkoa wa Mwanza kwa mfano, umeweka mikakati ya kupanda miti milioni sitini kila Wilaya na pesa zilizotengwa ni karibu bilioni moja nukta nane kwa ajili ya zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Shinyanga pamoja na kwamba ndio ulioathirika zaidi na *deforestation* lengo lililowekwa ni kupanda miti takribani milioni kumi na moja na laki mbili kwa Mkoa mzima ambao ni kama wastani wa milioni moja na laki nne kwa kila Wilaya na pesa zilizotengwa ni kama milioni 856 tu. Sasa ukilinganisha na Mikoa mingine, kwa mfano, Mkoa wa Morogoro ambao umeweka lengo la kupanda miti milioni tisa kwa kila Wilaya na pesa zimetengwa shilingi bilioni 2.2 kwa ajili ya zoezi hilo. Sasa ukiangalia uwiano huu bado naona kwamba nguvu iliyowekwa katika zoezi zima la upandaji miti kwenye Mkoa wa Shinyanga ni kidogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba

Wizara ijaribu kuweka mkakati maalum wa kusaidia zoezi zima la upandaji miti katika eneo hili.

Vile vile elimu ya mazingira kwa wananchi hawa, ni kweli watu wanafyeka miti ovyo lakini kutokana na kutokujua umuhimu wa miti. Pesa ambazo zimetengwa kwa ajili ya zoezi hili na zenyewe ni kidogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa nashauri Serikali iweke maanani katika eneo hilo. Kwa mfano, fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira, elimu ya mazingira kwa Mkoa wa Shinyanga ni kama milioni ishirini na laki saba na elfu hamsini na mbili. Milioni ishirini ni pesa kidogo sana kwa Mkoa mkubwa kama huo na ambao umeathirika kwa kiasi kikubwa namna ile cha ufyekaji miti ovyo. Mkoa wa Mwanza kwa kulinganisha pia umetengewa kiasi cha shilingi milioni ishirini na laki nne ambazo pia ni kidogo sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba Wizara pamoja na kwamba pesa ambazo zimetengwa na Wizara hii kwa ujumla kama nilivyosema ni kidogo lakini bado ule mgawanyo wake katika maeneo mbalimbali umekuwa hautoshi.

Mheshimiwa Spika, pia kuna tatizo katika jitihada ambazo zimewekwa na Serikali katika kutafuta nishati mbadala. Ni kweli kuna *alternative sources of energy* ambazo zinaweza kusaidia kupunguza tatizo la wananchi kufyeka misitu kwa ajili ya mkaa, lakini nimeangalia kwenye mikakati ya Serikali hakuna fedha maalum za kutosha zilizotengwa kwa mfano kwa ajili ya kuhamasisha wananchi watumie majiko ya gesi kwa mfano, lakini vile vile pamoja na kuhamasisha wananchi watumie gesi pamoja na kupunguza ushuru kwenye majiko kama tulivyosikia kwenye bajeti iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Fedha bado wananchi hawana elimu ya kutosha ya utumiaji wa gesi kwa sababu ni kitu cha hatari, mara nyingi ikitumika vibaya inaweza ikalipuka na ikaleta maafa. Sasa ni pesa kiasi gani tumeweka kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi wetu ili waweze kutumia gesi, kama *alternative source of energy,* tunakuta kwamba pesa zilizowekwa ni *almost* hakuna.

Mheshimiwa Spika, vile vile nimeona mkakati ambao umewekwa wa kuhamasisha wananchi watumie majiko sanifu yanayotumia mkaa kidogo. Mkoa wa Mwanza nimeona wameweka kiasi cha majiko 3000 kwamba ndio yatakayowekwa kwa kuanzia.

Sasa mimi nikashangaa, majiko 3000 kwa Mkoa wa Mwanza ambao una watu takribani milioni tatu hivi hayatoshi chochote na bado watu wataendelea kufyeka misitu kwa ajili ya kujipatia mkaa mpaka hapo tutakapoamua kama Serikali kuwahamasisha wananchi hawa waweze kutumia majiko haya yanayotumia mkaa kidogo. Lakini vile vile tuwatafutie na tuwasaidie kupata nishati mbadala. Suala la kutafuta nishati mbadala kama makaa ya mawe nalo ni la muhimu sana lakini kwenye bajeti halijaguswa kabisa. Sasa naomba Mheshimiwa Waziri aboreshe maeneo hayo yawezekana kwamba katika bajeti hii inaweza ikawa sio rahisi lakini katika mwenendo wa siku za usoni maeneo haya yaangaliwe sana ili kuhami misitu yetu ambayo ndiyo inayoleta mvua, umeme na kuwafanya wananchi waweze kulima na kupata maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba niseme kwamba naunga mkono hoja kabla kengele haijagongwa, lakini vile vile nilikuwa naishauri Wizara iweke utaratibu

maalum wa kusimamia zoezi zima la upandaji miti ambalo litakuwa linaiwezesha Wizara kujua ni miti mingapi imepandwa na njia pia za kuhamasisha wananchi waweze kutunza miti ile. Lakini vile vile naiomba Wizara itupie macho kwenye uharibifu wa mazingira unaotokana na uchimbaji wa madini. Wilaya ya Kahama kuna madini mengi, kampuni zinazofanya *exploration* zinaharibu mazingira, zinaharibu ardhi pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa sababu muda umekwisha nimwombe tu Waziri atembelee yale maeneo ambayo *exploration* inafanyika, afike Kahama, Bulyankulu, Nyang'wale ataona jinsi ambavyo shughuli za binadamu zinaathiri mazingira na kufanya hivyo, naamini kabisa kwamba wewe kama Waziri na Serikali yako na Wizara yako kwa ujumla utaweza kuona ni namna gani unaweza kusaidia wananchi hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi hii na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyo mezani kwetu. Kwanza nianze kabisa kwa kusema nimevutiwa sana na jinsi hotuba ilivyoandaliwa na hata ilivyoletwa hapa kwetu na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na ninatambua kwamba yeye kama Profesa ameweza hata kui-*present* kiprofesha Profesa, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumshukuru Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa hotuba nzuri waliyoandaa na ni nzuri sana. Pamoja na watendaji wake wametufanyia kazi nzuri sana ambayo tunachotakiwa kufanya kwa kweli ni kuchangia hapa na pale ili kuifanya iwe bora zaidi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kusema nataka nitoe pole kwa Wabunge wenzangu wanaotoka Iringa na hususan wale wanaotoka Njombe na wananchi wa Njombe na Iringa kwa ujumla kwa kuondokewa na mwenzetu Mhadhiri mahiri Profesa Chachage. Mungu aiweke roho ya Marehemu mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, nataka vile vile niseme kwamba nadhani kama alivyosema mwenzangu mmoja huku nyuma, kwa kweli Wizara hii inastahili kupewa siku mbili, kwa kweli kuipa siku moja ni ku-*underrate* umuhimu wa Wizara hii, ina vitu viwili muhimu masuala ya Muungano na masuala ya mazingira ambayo ni *cross cutting,* inaangalia Wizara zingine zote kwa hiyo, kuipa siku moja ni kuwa *very unfair* kwa hiyo nami naunga mkono kwamba Wizara hii inastahili tupewe muda wa kuijadili kwa siku mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo sasa niseme tangu mwanzo kwamba mimi nitajikita kwenye masuala ya mazingira kwa sababu ni *professsion* yangu na masuala ya Muungano nitawaachia wenzangu kuchangia. Ningependa kuanza kwa kuangalia suala la uwezekano, nahisi kunaweza kuwa na mgongano mkubwa kati ya sera za kuhifadhi maji na vyanzo vya maji na miradi ya kilimo hasa umwagiliaji tunaouzungumzia na tumezungumzia siku mbili zilizopita pamoja na miradi ya maji.

Nasema hivi kwa sababu sote tumeona miradi ya maji iliyoletwa mbele ya Bunge ilikuwa mingi sana, ni nchi nzima. Tumeona vile vile wanaohitaji kujengewa malambo, visima virefu na vifupi na kwa kweli vyote hivi ni masuala ya maji, inategemewa hayo maji yanatoka wapi, vyanzo vyake viko wapi.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile umwagiliaji tunaouzungumzia, kama hatuko makini katika kuhakikisha kwamba vyanzo vya maji hayo vinahifadhiwi na kwamba tunapochukua maji kupeleka Vijijini tunachukua maji na kuacha wanayoita *environmental flows* kuhakikisha kwamba kuna maji yanabaki kwa faida ya mazingira na watu wanaoishi *down stream*. Nina hofu kwamba baada ya muda badala ya kutoa maji kwenye mabomba itatoka hewa kwa sababu tutatumia maji mengi kama hatukufanya utafiti wa kina kuhakikisha kwamba tuna uhakika na vyanzo vile na kiasi tunachokichukua kwa matumizi yetu ni *sustainable*. Malambo tunayoyazungumzia nahofia baada ya miaka miwili, aidha, yatajaa tope au yatabomoka. Nakumbuka bwawa la Kisongo pale nje ya Arusha lilivyobomoka baada ya kujaa matope na mabwawa mengi sisi sote tunajua kwamba baada ya muda mrefu hapa nchini huwa hayafanyi kazi. Matatizo yake ni kwamba hatufanyi *detailed environmental impact assessment. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu umwagiliaji, hata katika hotuba ya Kilimo na katika hotuba ya Maji sikuona msisitizo wowote kwenye masuala hayo lakini jana nilielezwa kwamba miradi ya maji na usimamizi wake, *(coordination)* itafanyika kwenye ngazi ya Kitaifa, Mkoa na Wilaya, lakini sote tunajua kwamba wataalam wa kufanya *EIA* hawapo au wapo kidogo sana. Pengine Wilayani hawapo kabisa, sasa nitataka kujua wakati Waziri atakapokuwa anajumuisha anieleze, anihakikishie kwamba miradi yote ile ya kilimo, umwagiliaji katika nchi nzima na miradi yote ya malambo na kadhalika watuthibitishie kwamba itafanyiwa *EIA* na watuthibitishie kwa utaratibu upi, watafanyaje kuhakikisha miradi yote hii ambayo itafanyiwa *EIA* kwa vipindi tofauti kwa mwaka wote huu, watuthibitishie itafanyiwa *EIA* kwa utaratibu upi, nitapenda sana Mheshimiwa Waziri anieleze hilo.

Mheshimiwa Spika, la pili ambalo linafanana na hilo, Mheshimiwa Waziri na mimi tunaelewa na wengi wetu inawezekana tunaelewa, ni kweli wataalam wa *EIA* hawapo, nashukuru kwamba katika kijitabu hiki ukurasa wa 22 ndio sasa tunaambiwa kanuni za usajili wa wataalam wa mazingira zimeandaliwa. Kwa kweli ni wataalam wa kutathmini athari za mazingira sio wataalam wa mazingira, nadhani ndio walivyotaka kusema. Sasa hawapo au wapo kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nilitarajia kwamba kwa vile tumeunda sheria sisi wenyewe juzi juzi hapa ambayo inataka kwamba programu za kumwagilia zifanyiwe *strategic environment impact assessment*. Lakini sikuona haya yakizungumzwa. Lakini vile vile wataalam hao watatoka wapi wa kufanya mambo haya? Nilitegemea kwenye hotuba hii nitaelezwa au tutaelezwa utaratibu wa kutengeneza au ku-*train* watu wa kufanya *environmental impact assessment,* lakini sikusikia hilo likisemwa. Sasa nitaomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho yake aniambie pamoja na lile la kwanza jinsi watakavyofanya *EIA* kwa nchi nzima kwa miradi yote ya maji na kilimo

lakini vile vile waniambie wataalam watatoka wapi kama kuna *training program,* tuambiwe na nitapenda kujua hawa watakuwa *trained* kwa utaratibu upi na wangapi tunawategemea watakuwa wamepatikana ifikapo mwisho wa mwezi.

Mheshimiwa Spika, la tatu ambalo ningependa kuzungumza ni kuhusiana na suala la vyura wa Kihansi, ni suala la mazingira najua linapewa fedha nyingi sana. Nalizungumza hili kwa sababu hata mimi najua mradi ule wa vyura wa Kihansi kwa sababu nilishiriki, *World Bank* walinipa kazi ya kufuatilia, ku-*monitor* vyura wa Kihansi na mazingira yao miaka ya 1999 hadi 2001. Kwa hiyo, nafahamu sana suala la mazingira ya Kihansi, ninachotaka kusema ni kwamba kilichofanyika tumehamisha vyura wachache wamepelekwa nje ya nchi. Kuna vyura wachache walibaki pale, tukaweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba mazingira yale pengine yataboreshwa yafanane na mazingira ya awali ili viumbe wale waliobaki pale waendelee kustahimili kuishi pale.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo ni kwamba kwa kweli vyura wale hawapo Kihansi pale, kama wapo basi ni kidogo sana lakini Waziri aniambie vyura wangapi wamebaki Kihansi. Kwa hiyo, tegemeo letu ni kwamba vyura tunaowazungumzia ni wale walio Marekani. Lakini mategemeo yetu ni yalikuwa kwamba kwa kipindi hiki tutaendelea kuandaa mazingira ya kuwarudisha vyura wale aidha, Kihansi au mahali pengine popote nchini ambapo kutaonekana kuna mazingira yanayofanana na mazingira ambapo vyura wale wanaweza kustahimili. Hili sijui limefikia wapi, inawezekana wale vyura wakakaa Marekani milele.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitegemea Waziri ataniambia vile vile mikakati inayofanywa kuhakikisha vyura hawa wanarudi na wakirudi tutawapeleka wapi. Nitaomba pia katika hilo nipate jibu.

Mheshimiwa Spika, halafu nije kwenye suala la mkaa wa mawe kama mbadala wa kuni au mkaa wa miti. Kule Ludewa, Mchuchuma naambiwa tuna *grade* tatu za mkaa, aina moja ni *domestic coal* na nategemea kuna mkaa vile vile Mbinga kule na maeneo mengi hapa nchini ambayo huenda tuna *domestic coal. Domestic coal* ni mkaa ambao una nguvu ndogo *(calorific value)* ambayo tunaweza kuitumia majumbani. Sasa tuna *source* kubwa pale Ludewa ya *domestic coal*.

Mimi nilitegemea kwamba utafiti ungefanywa ili tuhakikishe kwamba makaa ya mawe yale yanawekwa kwenye magunia, tunasambaza nchini kwa bei nafuu, wananchi watumie kama mbadala wa kuni na mkaa unaotokana na miti. Nitaomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri anieleze mikakati ambayo inafanywa ili kuhakikisha kwamba mkaa ule aina ile ya *domestic coal* inaweza kutumika hapa nchini ikiwa ni mbadala wa kuni na mkaa wa miti.

Mheshimiwa Spika, naomba pia niongelee kuhusu Usangu. Tumefanya vizuri sana kuondoa mifugo Usangu, lakini baada ya hapo je, *what next?* Mimi nilidhani kitu cha haraka haraka kufanya ni kufanya tathmini ya hali ya mazingira, hali ya maji, *flows* zilizopo sasa hivi tunaita *baseline,* kutafuta *baseline data* ikoje, lakini baada ya hapo kufanya programu ya kufuatilia mwenendo wa mazingira yale pamoja na mwenendo wa

maji utakavyokuwa unabadilika, unaongezeka au unaendelea kupungua na mazingira, je, yanaboreka au yanaendelea kuharibika? Sasa nitataka kujua kutoka kwa Waziri mikakati ipi inawekwa kuhakikisha kwamba hayo yanafanyika, tunakuwa na *baseline data* hali ilivyokuwa *immediately* baada ya kuondoa mifugo halafu mikakati inayowekwa na *indicators* za kufuatilia mabadiliko ya mazingira na ya upatikanaji wa maji ili tuweze kufanya mikakati maalum ya kuhakikisha mazingira yale yanaboreshwa kweli.

Mheshimiwa Spika, mwisho nilitaka nizungumzie juu ya kilimo cha mabondeni. Ni kweli taarifa iliyotolewa na Makamu wa Rais imeleta mchanganyiko kidogo kwa sababu watu wamepata hisia kwamba kilimo cha mabondeni marufuku kwa sababu kinaharibu vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Nyanda za Juu na ninakotoka mimi Ludewa kilimo cha mabondeni ni muhimu sana wakati wa kiangazi, lakini imetolewa *blank statement* kwamba kilimo kile hakifai. Mimi nilifanya utafiti Iringa wa kuangalia umuhimu wa kilimo kile, tuligundua kwamba kinawasaidia sana wananchi, kinahitaji tu kuboreshwa ili kiweze kuwa endelevu.

Kwa hiyo, kinachotakiwa ni kuamua, tunataka wananchi wale waruhusiwe kulima kwenye mabonde makubwa kiasi gani na umbali gani kutoka kwenye *banks* za mto ndiyo suala la muhimu. Lakini huwezi ukaweka *blank statement* kwamba kilimo cha mabondeni haiwezekani. Hata Bonde wa Mto Rufiji huwezi ukalima kama ni hivyo. Lakini ni bonde kubwa kiasi gani na umbali kutoka kwenye mto uwe kiasi gani. Kwa hiyo, haya mambo yasemwe mapema. Kwa sababu nimepata ripoti kutoka Ludewa kwamba wananchi wameambiwa hakuna kulima vinyungu mabondeni katika kiangazi hiki na muda wote unaokuja.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atoe *clarification* wakati anajumuisha hoja yake ili awajibu na wananchi wangu wa Ludewa waweze kujua maana yake nini? Makamu wa Rais alikuwa na maana gani aliposema kwamba ni marufuku kulima au tunaweka usimamizi katika kilimo cha mabondeni?

Mheshimiwa Spika, napenda kurudia kwa kusema kwamba baada ya hayo, hotuba ni nzuri na mipango ni mizuri. Lakini ningependa sana kupata majibu ya haya niliyoyasema na napenda kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HAROUB SAID MASOUD:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa shukrani kupata nafasi hii ili nami nichangie hotuba hizi za Mawaziri wawili ambazo zimetolewa asubuhi hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Waziri kwa utaalamu mkubwa alivyoisoma kwa dakika chache kabisa wakati ambapo hotuba ilikuwa ni ndefu lakini tumeielewa. *(Makofi)*

Pili, napenda kusema kwamba wakati ambapo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, Muungano alipokuwa anatoa hotuba yake nilitaka nitumie Kanuni, lakini nikamwonea huruma. Kwa sababu angeshindwa kujibu yale ambayo ningemwambia. Alitumia lugha kwamba Muungano wetu ni sawa sawa na wana ndoa wawili.

Mheshimiwa Spika, wana ndoa ni mwanamke na mwanaume. Sasa ningemuuliza Mheshimiwa Mbunge ni nani mwanaume kati ya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani angeshindwa kunijibu. Sasa nataka aelewe hivyo tu kwamba mara ya pili asitumie lugha hiyo kwamba Muungano aufananishe na wana ndoa wawili. Wana ndoa lazima walale katika kitanda kimoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa niendelee kuchangia kuhusu mambo ya Muungano. Hatuwezi tukazungumzia Muungano wetu kwa kuendelea hapo tulipo na tunakokwenda tu, lazima turejee nyuma. Mwenyezi Mungu alipomuumba kinyonga alimpa afanye ya peke yake, anapokwenda hatua mbili mbele anarejea hatua moja nyuma. Hii anatwambia sisi wanadamu kwamba msiende mbele tu moja kwa moja muangalie hayo mliyoyafanya nyuma na yanayotokea hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kinyonga lazima tumfuate. Sasa hivi tulivyo tunauangalia Muungano hapa tulipo tu. Kwa watu wa Zanzibar hatuelewi tunatoka wapi? Ni lazima tuelimishane, tueleze historia fupi ya Zanzibar ya karne hadi karne.

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Zanzibar katika karne za mbali kabisa huko kabla ya Seyyid Said bin Sultan hajaja Zanzibar mwaka 1804 walikuwepo watu wakiishi na wengi wao walikuwa ni jamaa wa Tumbatu, Washirazi, Wazigua na baadhi ya watu kutoka Tanzania Bara ingawa sasa hivi wale wasioelewa Zanzibar wanasema watu wa Bara kule Zanzibar ni wageni, si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Seyyid Said bin Sultan alifanya himaya yake Zanzibar na kuhamia Zanzibar mwaka 1832. Wakati wote huo Mfalme Seyyid Said bin Sultan alikuwa anaitawala Zanzibar na kukawa na Baraza la Kutunga Sheria miaka mingi iliyopita kuanzia mwaka 1926. Lakini muda wote huo ingawa Waafrika, Washirazi, Watumbatu walikuwepo katika Baraza hilo la kutunga sheria hakuwemo mtu hata mmoja mwenye rangi nyeusi yaani Mwafrika hadi mwaka 1947 wakati Marehemu Ameir Taju ndiye alikuwa Mwafrika wa mwanzo kuwekwa pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapo ndipo lilipoanza vuguvugu la kisiasa la chini kwa chini. Wakajiona Waafrika kwamba ni dhariri katika nchi yao. Lakini hata hivyo, mwaka 1955

kiliundwa Chama cha *ZNP* na mwaka 1957 *Afro Shiraz Party* nayo ikaundwa na uchaguzi ukaanza pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika chaguzi zote zilizopita Zanzibar matokeo yalikuwa yanaonyesha dhahiri kwamba *Afro Shiraz Party* ilikuwa na wanachama wengi. Nitatoa mifano midogo kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uchaguzi wa mwanzo mwaka 1957 kulishindanishwa viti vitano, katika viti vitano hivyo, vinne walipata *Afro Shiraz Party* na kiti kimoja kikapatwa na *Muslim Association* ambacho kikiongozwa na Chodrey na *ZNP* hawakupata kiti hata kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitazungumzia uchaguzi wa mwisho kabisa ambapo ulikuwa mwaka 1963 ambapo *Afro Shiraz Party* ilipata ushindi wa kura 87,405 sawa sawa na asilimia 54.2. Vyama viwili vya *ZNP* na *ZPP* wakapata kura 73,553 yaani vyama viwili hivyo *ZNP* na *ZPP* wakapata asilimia 45.79. Kwa nini nikasema hayo kudhihirisha kwamba *Afro Shiraz Party* iliongoza miaka yote hiyo hadi uchaguzi wa mwisho kabisa.

Mheshimiwa Spika, matokeo yake Serikali walinyimwa kuunda *Afro Shiraz Party* na ikatamkwa kwamba kwa sababu kulikuwa na Mkutano wa Katiba ambayo ulikuwa unafanyika London tarehe 20 hadi 24 Septemba, 1963 yalitoa maamuzi yafuatayo, Zanzibar ipate Uhuru Desemba, 10, 1963, lakini Sultan atabakia na ataendelea kuwa Mkuu wa nchi. Narudia tena hivyo Uhuru huo Sultan atabaki na ataendelea kuwa Mkuu wa nchi.

La pili, pia Sultan alikubaliwa kwamba ana haki ya kuteua mrithi wake milele na milele. Kwa nini *Afro Shiraz Party* wakataka kupindua? Kwanza, walidhulumiwa kura zao na hawakupewa Serikali, lakini kubwa zaidi la tatu, Mfalme aliambiwa ataendelea kuchagua mrithi wake. Ikaonekana hapa mambo hayo hayatakwisha mpaka Kamati ya watu 14 ambayo iliundwa na watu wafuatavyo, Said Washoto, Khamis Hemed, Seif Bakari, Said Bavai, Abdallah Natepe, Yusuf Hemid, Mohamed Abdallah, Pili Khamis, Haffi Suleiman, Hemed Ameir, Ramadhan Haji, Khamis Daruwesh, Seif Mafarumaru, John Okelo wakiongozwa na mwenyewe Marehemu Abeid Amani Karume. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka waelewe Watanzania na walioko nje ya Tanzania kuwa Mapinduzi yalikuwa kutekeleza yale ambayo yalikuwa dhuluma katika nchi ile ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ndiyo maana pale Zanzibar wakaungana na Serikali ya Tanzania Bara. Sasa nashangaa kuna baadhi ya watu miaka yote hiyo 42 Muungano huu upo, unaendelea, unadumu, unaimarika, kama kuna kasoro ndogo ndogo ndani miongoni mwetu nasema bado si sahihi kutamka mtu kwamba anataka Serikali moja, anataka Serikali tano na anataka Serikali sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo sahihi kabisa ndani ya Bunge hili kusimama Mbunge akasema watu wa Bara wanataka na wao waingie kwenye Baraza la Wawakilishi, watu wa Bara gani wanaotaka kuingia kwenye Baraza la Wawakilishi? Nani mtu wa Bara aliyetamka na naomba kama nafasi ipo wachangie waseme na wao wanataka kwenda Zanzibar kuingia kwenye Baraza la Wawakilishi, si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo yanayotuharibu na haya ndiyo yanayotukoroga. Siasa waangalie siasa ya kweli, siasa siyo utumwe useme maneno yawe dhidi ya maneno ambayo upinzani wako mwenyewe unazungumza vinginevyo.

Mimi namshukuru Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, amezungumzia vizuri kabisa na ameeleza kasoro ndogo ndogo ambazo Serikali zetu mbili zikae, ziyachambue na yale yamezungumzwa na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, ndani ya Bunge hili. Ndiyo kwa maana hiyo akachaguliwa Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi kuwa Waziri Maalum wa Mambo ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, ametoa agizo maalum kwamba wakae kila baada ya muda Waziri Mkuu na *Chief Ministry* wa Zanzibar ili kutafuta maoni, siyo wakae pekee yao wadhani watapata maneno. Wakae wao, wachukue maoni kutoka kwa watu. Halafu baadaye turekebishe, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nashangaa mtu anasema Serikali moja, Serikali tatu. Lakini sasa tujiulize baada ya Muungano huo kweli tumerudi nyuma, kweli Wazanzibar au watu wa Tanzania Bara hawakufaidika na Muungano huu. Mimi nasema kuwepo kwetu hapa sisi watu wa Zanzibar ni ushahidi tosha kwamba Muungano ni bora na wala hakuna kitu imara kuliko huu Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi mara ya mwanzo kabisa kuiona Tanzania Bara ilikuwa mwaka 1965. Miaka yote hiyo nimeishi sijui Tanzania Bara nasikia tu, nilikuwa nimekuja katika mashindano ya mbio katika uwanja wa Moshi na nilikuwa mkimbiaji mzuri sana na kesho kutwa nitawaonyesha watu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara ya kwanza wakati huo na si pekee yangu ni wengi. Lakini tujiulize kabla ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar tulikuwa tukilishwa na nani sisi? Chakula chetu mpaka maharage, vitunguu, viazi na vitu vingine tulikuwa tukiagiza kutoka Misri na Pakistan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tunaona fahari tunapiga simu tu Kyela tuletewe mchele Zanzibar wa tule na bwana. Leo Zanzibar tunapiga simu Iringa tuletewe viazi ulaya, tuletewe vitunguu, hatuviagizi kwa fedha za kigeni, bado kuna watu wanabughudhi wanasema hawajatosheka. Mimi nasema hao wana *agenda* yao ya siri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wako ambao vile vile hawaoni, lakini mimi naunga mkono sana Muungano, kasoro ndogo ndogo tukae kitako, tuzungumze na hapa tuzungumze siyo unaponda wakati cha kuponda huna kabisa. Hebu tuangalie biashara

zimeimarika. Lakini vile vile kuna majengo mangapi yamejengwa tena siyo kipindi cha nyuma cha wakati huo. Tukumbuke miaka mitatu nyuma hapo Zanzibar. Tukienda Pemba huko nyumba za majeshi, nyumba za polisi mpaka Wawi zimejengwa nyingi.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Capt. John Chiligati, alipokuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi wakati ule amezijenga nyumba mpaka akina Mheshimiwa Profesa Philemon Sarungi, amejenga nyumba. Tukija Unguja kila mahali nyumba za askari ziko nyingi na ofisi kubwa kubwa lakini ofisi kubwa zaidi ya Bunge ipo Zanzibar Tunguu pale, ofisi ya Uhamiaji, zimejaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tukiangalia hivyo bado tunasema tumeminywa, tumedhulumiwa, aliyewadhulumu ni nani? Kasoro ndani ya nyumba zetu wenyewe zipo, haziwezi kukosekana hata siku moja. Hakuna mtu hata mmoja hapa aliyekuwa hana tatizo ndani ya nyumba yake. Lakini tunakaa pamoja wewe na familia yako mnazungumza, mnapanga na mnapangua ili kurekebisha yale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa sababu hotuba ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, aliyeitoa hapa tarehe 30 Desemba, 2005 na tukiangalia na hotuba ambayo imesomwa hapa leo, tumeambiwa kwamba hata zile Wizara ambazo si za Muungano wakae pamoja kutazama jinsi gani wataweza kusaidiana.

Mheshimiwa Spika, sasa natamka hapa kwa kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano aliangalie kwa jicho la huruma ombi langu hili ninalotaka kusema hapa na nalitoa si kwa sababu kama Haroub Said Masoud na kama Mbunge wa Jimbo la Koani, nalitoa hapa kwa sababu ya Muungano huu uliokuwepo leo hapa. Si mimi wala si yeye Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Muungano tusingekuwepo hapa leo kama si Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964 yaliyoongozwa na Marehemu Abeid Amani Karume ambaye huyo huyo walimsaliti, walienda kumuua hadharani.

Sasa huyu amezaliwa Kiongoni, Kiongoni iko katika Jimbo la Koani namwambia Mheshimiwa Waziri. Hilo Jimbo la Koani kuna barabara ambayo haipitiki hata kidogo. Kilometa nne tu kutoka Koani kwenda Jumbi ambayo inapita pale kwenye shamba lake mpaka leo lipo namwomba Mheshimiwa Waziri akae na Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu barabara ile itafutiwe fedha popote pale ijengwe toka Koani kwenda Jumbi hapo tutaimarisha zaidi Muungano wetu kwa kumkumbuka Marehemu Abeid Amani Karume.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na ninawatakia kila la kheri yeye na Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza ofisi hii ya Makamu ya Rais juu ya utendaji wake mzuri ambao kila Mtanzania anauona. Yote hayo inaongozwa na Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein. Mheshimiwa Makamu wa Rais kwa jitihada kubwa anafanya kazi kwa bidii kwa kutembelea sehemu mbalimbali na kuona matatizo ya wananchi na kuyapatia ufumbuzi. Napenda kumshukuru sana na kumpongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kumpongeza Makamu wa Rais, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wetu wawili, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa kazi zao nzuri ambazo wanazifanya kwa ushirikiano mkubwa na wananchi. Hakuna asiyejua ushirikiano wao mkubwa na wananchi katika kutatua matatizo mbalimbali ya wananchi na vile vile kwa kushirikiana na watendaji wao akiwemo Katibu Mkuu, Sheikh Abubakar Rajab na watendaji wengine napenda kuwapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye hoja. Napenda kuchangia moja kwa moja leo sitapenda kuchangia kuhusu Muungano kwa sababu wenzangu wengi wameshachangia kuhusu Muungano.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Mradi wa *TASAF.* Katika kitabu chetu hiki tumeonyeshwa hapa kwenye ukurasa wa 14, naomba kunukuu: "Serikali imechukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba miradi ya pamoja inaandaliwa na kutekelezwa katika pande zote mbili za Muungano hii ikiwa ni pamoja na Mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)* ambako jumla ya miradi 76 ilitekelezwa Zanzibar mpaka sasa ambayo kwa upande wa Unguja ni miradi 43 na Pemba miradi 33."

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inavyoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuanzisha mradi huu wa *TASAF* kama tunavyoelewa kwamba mradi wa *TASAF* ni mkombozi wa jamii na ni mkombozi wa wanyonge. Mradi huu wa *TASAF* uko Tanzania nzima ikiwemo Pemba na Unguja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya *TASAF* wananchi walikuwa katika hali duni lazima tukubali. Lakini Mradi huu wa *TASAF* umetukomboa hasa sisi kule Pemba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Awamu ya Kwanza ya *TASAF* ilivyoanzishwa miaka mitano iliyopita kulikuwa na miradi mingi tu ambayo ilikuwa imetekelezwa na wananchi walishirikishwa kikamilifu tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tumo kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwetu katika Kisiwa cha Pemba kumetekelezwa miradi mingi ambayo ipo katika Majimbo tofauti. Mimi nitasemea upande wa Kusini Pemba kwa

sababu upande wa Kaskazini Pemba yupo mwenzangu na yeye anaweza akazungumza. Lakini nitazungumza kwa upande wa Kusini Pemba.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua katika upande wa Kusini Pemba tuna Majimbo tisa, Jimbo la Chake chake, Jimbo la Ziwani, Jimbo la Wawi, Jimbo la Chonga, Jimbo la Chambani, Jimbo la Mtambile, Jimbo la Kiwani, Jimbo la Mkanyageni na Jimbo la Mkoani. Katika awamu iliyopita, nilizungumzia Majimbo yote ingawa Wabunge wao wapo hapa lakini naona hawatetei hayo Majimbo. Mimi nasema kama Mbunge wa Viti Maalum Kusini Pemba naingia kwenye Majimbo yote kwa sababu kuna wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi walitekeleza miradi tofauti ikiwemo ya shule, miradi ya vituo vya afya, miradi ya barabara, madaraja, maji na kadhalika na kila Jimbo kati ya hayo Majimbo ya Pemba napenda kusema haikukosa miradi angalau miwili. Lakini napenda kusema kwamba katika Jimbo la Wawi katika Awamu ya Kwanza ya *TASAF* hakuna hata mradi mmoja uliotekelezwa. Nilipokuwa Mbunge wa Jimbo la Wawi hapa nilitetea toka miaka yote mitano nilikuwa natetea miradi hii ya Jimbo la Wawi lakini haikutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kwa jitihada ya Serikali mara hii isilale kiporo, miradi ya Jimbo la Wawi nayo itekelezwe ipasavyo. Miradi yao waliyoitafakari kule ni Mradi wa Maji katika Kijiji cha Kilimahodi, Mvumoni na mradi wa shule katika Shehia ya Wawi. Naomba sana watendaji wasiisahau sasa Wawi kwa sababu wananchi wa pale watajisikia vibaya. Tanzania nzima ina miradi ya *TASAF,* lakini Wawi pekee yake hakuna miradi ya *TASAF.* Napenda kusisitiza Serikali isisahau Jimbo la Wawi. Kwa sababu haya mambo niliyaanzisha mimi kuyatetea. Kwa hiyo, nataka niyamalize miradi itekelezwe katika Jimbo la Wawi hasa kuhusu maji. Akinamama wanaenda mbali kuchota maji na muda mwingi wanautumia kule mabondeni kutafuta maji, tuwahurumieni akinamama na wanafunzi wanaenda sehemu ya mbali kutafuta elimu. Kwa hiyo, tuwahurumie pia na wanafunzi, tuwajengee shule karibu na maeneo yao wanayoishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TASAF* ya Awamu ya pili imeingia na imepiga hodi katika Kisiwa cha Pemba, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu ya Nne, hongera. Najua sasa hivi itamaliza matatizo yote.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ambayo mara hii itatekelezwa tunashukuru kwamba itamalizwa ile ambayo pengine ilikuwa haijatekelezwa kama nilivyoomba. Lakini sasa imekuja na mfumo mwingine mzuri zaidi kuwashirikisha jamii zaidi katika vikundi mbalimbali. Vikundi vya akinamama, vikundi vya walemavu, waathirika wa UKIMWI, vikundi vya wajane na vikundi vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *TASAF* imehamasishwa tukiwemo na sisi Waheshimiwa Wabunge kwa sababu tuko kwenye Kamati. Tumewahamasisha sana wananchi sasa hivi wameshajitokeza kwa wingi na wameshaunda vikundi vyao tofauti na vilevile wameshachagua miradi yao na vile vile wameshajaza fomu za kuomba fedha hizo.

Naomba Serikali ifuatilie, isije ikawa kama awamu ile ya kwanza ikawa kwa muda mrefu fedha zilikuwa zinachelewa chelewa kidogo. Kwa hiyo, fedha zipelekwe kwa haraka haraka, miradi hii ya *TASAF* katika Kisiwa cha Pemba izidi kuwakomboa wananchi hususan wanawake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja katika mradi wa chumvi. Katika kisiwa chetu cha Pemba au Tanzania kuna miradi tofauti ya ukulima wa chumvi, lakini katika kisiwa chetu cha Pemba kwa sababu ni Kisiwa kama tunavyojua bahari. Kwa hiyo, kimezungukwa na wananchi mbalimbali wanajishughulisha na biashara zao za ukulima wa chumvi wakiwemo akina baba, akina mama na vijana. Hilo ni moja kati ya biashara zao ambazo zinawapatia maslahi yao ya kila siku na ni ajira kwa kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kulikuwa na mradi huu wa *NIGP* ambayo kila siku nilivyokuwa Mbunge wa Wawi hapa kila siku natetea hilo kwamba kile kiwanda wakati ule hakukuwa na mashine ya kuingiza *iodin*e katika chumvi. Kila siku nikawa napewa ahadi ahadi. Lakini nashukuru Serikali imeona na kwamba sasa hivi katika kiwanda kile ambacho kiko katika kijiji cha Wawi kimepatiwa mashine mpya za kisasa ambazo zimetolewa na *UNICEF* na vilevile *NIGP* wao wanashughulika kwa matengenezo na matayarisho ya mashamba ya wakulima. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali imetuona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru sana wanavijiji au wananchi wa Pemba wanaendelea kufanya biashara zao kwa umakini zaidi. Kwa sababu kama tunavyojua chumvi ikiwa haijatiwa *iodine* inawezakana ikaleta matatizo ya goita. Hata siku moja niliuliza hapa nikaambiwa ni kweli. Kwa hiyo, sasa hivi wataweza kuuza chumvi yao hapa Tanzania na vile vile wanaweza wakauza chumvi yao nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wakati kinatayarishwa kiwanda kile akinamama pale walikuwa wanafanya kazi za kila siku wanaenda halafu wanarudi nyumbani, lakini sasa naomba kiwanda hiki kiweze kuwaajiri akinamama wengi kwa sababu akinamama wako makini na wanaweza kufanya kazi katika kiwanda cha chumvi ili na wao wapate ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa sina mengi kuhusu *TASAF* na mradi wa chumvi ilikuwa ni kuwatetea wananchi wangu wa Pemba . Kwa hiyo, nashukuru sana na naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia ambao ni kama dakika saba hivi au sita hautoshi kuruhusu mchangiaji yeyote aweze kuchangia kabla ya kusitisha shughuli za Bunge kwa asubuhi hii. Kwa hiyo, nataka tu nikumbushe mambo mawili.

Moja, tutakuwa na nafasi ya wachangiaji watatu tu pale kuanzia saa 11.00 jioni, nao ni wafuatao ni Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Sameer Lotto na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. Ni bahati mbaya hatutaweza kuwafikia Mheshimiwa Mariam Mfaki na Mheshimiwa Ali Khamis Seif.

La pili, ni kuhusu Kamati ya Matumizi, naomba wote ambao wanataka kuchangia katika Kamati ya Matumizi kwa usahihi waviangalie vifungu. Ijumaa nilizungumza na baadaye Naibu Spika wakati sipo alikumbusha. Si sahihi kusimama kwenye mshahara wa Waziri halafu ukazungumzia jambo lolote unalopenda si sahihi kikanuni. Inabidi ulenge katika kifungu kinachohusika na suala ambalo unataka kupata maelezo ama ufafanuzi. Natoa tahadhari hiyo kwa sababu nitashikilia msimamo huo kwa kuongoza Kamati ya Matumizi hapo jioni.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kwa kuwa muda hautoshi kuendelea. Sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.54 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kukushukuru kupata nafasi hii ya kwanza katika kipindi hiki cha mchana cha Bunge lako Tukufu kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuishukuru hotuba ya Wizara ya Mazingira na Muungano ambayo imewasilishwa leo asubuhi ikiwa ni nzuri yenye kutuonyesha tulikotoka, tulipo na tunakoenda na ambayo kwa kweli ime-*cover* masuala ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM pamoja na MKUKUTA. *(Makofi)*

Vile vile nichukue nafasi hii kumshukuru Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo Wizara hizi mbili zipo chini ya ofisi yake na jitihada kubwa ambazo anazifanya katika kuendeleza Wizara hizi mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nishukuru pia maoni ya Kamati husika ya Mazingira na Kamati ya Katiba na Sheria na utawala juu ya masuala ya Muungano.

Mheshimiwa Spika, nishukuru na kutambua pia maoni ya Kambi ya Upinzani. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tuna kipengele kinasema uhuru wa maoni. Kwa hiyo, nitambue uhuru wa maoni waliokuwa nao Kambi ya Upinzani bila kujali yaliyomo ndani yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kusema nadhani siku moja kuchangia Wizara hizi nyeti mbili ndani ya nchi yetu hazitoshi. Kwa hiyo, naomba kutoa rai ili tujaribu kuyaangalia haya masuala yote ya Muungano na Mazingira ni mambo ya msingi sana katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira kama tulivyoambiwa kwenye hotuba ni suala la mtambuka *(cross cutting)* ambalo ni muhimu sana. Mimi nilikuwa najaribu kufanya utafiti kidogo na kutafakari juu ya suala zima la uharibifu wa mazingira na nikawa najaribu kutafakari ni sababu zipi ambazo zinapelekea uharibifu wa mazingira

ambao kila siku tumekuwa tukiuzungumzia na kwa kuwa tunahitaji masuala ya *sustainable development* katika nchi yetu basi suala la mazingira ni la msingi sana.

Mheshimiwa Spika, katika sababu ambazo nimeziona ni pamoja na suala la umaskini. Vile vile kuna suala la vyanzo vya mapato. Watu wetu wanahitaji vyanzo vya mapato na wanadhani wakati mwingine njia pekee ni kuingia katika mazingira na kuwekeza humo kwa njia moja au nyingine. Sababu nyingine ambayo nimeiona wakati mwingine inatokana na desturi au mila ambazo tumezizoea na sasa umefika wakati basi kama hizo ndizo sababu ni muhimu sisi kama Serikali, kama viongozi na wananchi tujitahidi kuwapa wananchi wetu mbadala wa vile vyanzo ambavyo vinapelekea uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika mkoa ambao natokea mimi mkoa wangu wa Iringa, kwa kweli vijana wengi kutokana na ukosefu wa ajira utakuta wanafanya kazi za kuchoma mkaa, kufyatua matofali pembezoni mwa vyanzo vya maji. Hii yote ni kutokana na kutafuta riziki katika njia ambayo ni halali. Ni kweli kabisa wanatambua kwamba si sawa na hivyo tunahitajika tuwape mbadala lazima kuwepo na mbadala wa matatizo haya. Kama ni kufyatua matofali, kama ni suala la mkaa basi ni wajibu wa Serikali na vyombo vinavyohusika katika kurekebisha matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo hata akinamama ambao wengi wao wako vijijini na hasa katika mkoa wa Iringa wametambua baada ya kupata elimu ya kutosha juu ya masuala ya mazingira kwamba kilimo cha vinyungu si sawa kwa sababu kinaharibu mazingira. Akinamama hawa wamenituma nije hapa nilete ujumbe wao wanasema sasa mbadala wa kilimo cha vinyungu na kwa kuwa wanahitaji chakula ni nini? Kwa hiyo, na mimi nawasilisha salaam hizo kwa Serikali. Serikali tunapaswa tubuni mbinu kama ni masuala ya *irrigation,* kama ni masuala ya mbadala juu ya masuala haya ya kilimo ni lazima tuyaangalie.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo mimi nilikuwa nimeliona na kupata uzoefu kidogo katika nchi chache ambazo nimewahi kuishi kama miaka mitano nimewahi kuishi katika nchi ya Urusi na Uingereza. Wao katika *policy* za mazingira walikuwa wana kitu kinaitwa *re-cycling policy. Re-cycling policy* hii ni *polic*y ambayo ilikuwa inasaidia suala la mazingira likaimarishwa kupata *sustainable development*. Kimsingi katika maeneo kama viwanda kunakuwa na *output* yaani taka ambazo zinakuwa hazihitajiki baada ya kazi za malighafi ambazo ni muhimu. Zile taka huwa zinaangaliwa na kupimwa na wakati mwingine zinarudishwa tena kutengenezea malighafi nyingine, hiyo ndiyo *re-cycling policy*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kuna viwanda ambavyo vinatumia tuseme maboksi, karatasi, zile karatasi zinazobaki zinarudi tena. Sambamba na hilo wamekuwa wakiitumia *re-cycling policy* vizuri sana katika maeneo ya taka za nyumbani. Taka za nyumbani zina aina nyingi, kuna taka ambazo zinaweza zikawa ni vitu kama chupa, *metals,* lakini kuna taka ambazo zinatokana na mazao kama maganda ya viazi na kadhalika. Taka zile zimekuwa zikikusanywa na kutengenezewa mbolea. Kwa hiyo, suala la *re-cycling policy* katika

suala zima la mazingira nadhani nalo limefika wakati katika nchi yetu hasa katika wakati huu wa utandawazi ni lazima lipewe kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, binafsi nadhani suala hili la mazingira wakati mwingine tunajua tumewaachia wataalamu wetu. Ni jukumu nadhani la taasisi, ni jukumu la *Local Government Authorities* katika nchi yetu kuangalia sana suala hili la mazingira. Utakuta wakati mwingine hata Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali kwa kweli yamewekeza kwenye mazingira bado ni machache sana. Kwa hiyo, nadhani wakati umefika sasa Serikali ikiwezekana kutoa *incentives* kwa Mashirika ili kuwekeza katika suala la mazingira hiyo itakuwa ni jambo la muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote viwanda ambavyo tunavyo, viwanda vingi sana tulivyokuwa navyo vinatumia maji kwa wingi sana. Pamoja na kwamba wanalipa gharama za maji pamoja na kwamba wanalipa hata masuala ya kodi mbalimbali lazima tuangalie kwamba wawe wanalipa kiwango fulani ambacho kinaingia kwenye mazingira. Tunavyo viwanda kama *TBL, Cocacola* hivi ni viwanda ambavyo vinatumia malighafi ya maji kwa kiasi kikubwa sana. Kwa hiyo, lazima kuwepo na *re-cycling policy* kuhakikisha kwamba masuala ya *sustainability* ya maji yanaendelea kudumu. Kwa hiyo, nilidhani tubuni *formula* au *policy* ambayo itasaidia.

Mheshimiwa Spika, labda pia niongelee suala la upandaji miti. Tumekuwa ni watu wazuri sana kupanda miti. Tunaambiwa wakati mwingine tumepanda miti elfu kadhaa, milioni kadhaa katika nchi yetu. Lakini hili suala la miti pamoja na upandaji wake kitendawili kimebaki pale kwenye miti ile kufika kudumu ili kufika wakati wa kuvunwa bado imekuwa ni kitendawili. Yamkini wakati mwingine ni kwamba bado tunategemea mvua, sasa nikawa najiuliza kwamba hivi tukisema tunapanda miti labda tunaendelea kutegemea mvua katika zile nchi zipo katika jangwa la Sahara wao inakuwaje masuala ya mazingira? Maana yake bila shaka wanakuwa na mikakati ambayo ni dhahiri. Niliwahi kuonana na Wabunge wa nchi za Algeria na Libya na nchi zile zingine ambazo zipo katika jangwa la Sahara waliwahi kusema tatizo la maji katika nchi yao hakuna pamoja na kwamba wapo katika maeneo ya jangwa. Lakini sisi tupo katika maeneo ya *equatorial* na kuna uwezekano mkubwa wa kupata mvua, bado suala la mazingira na la maji limekuwa ni kitendawili. Nilidhani ni muhimu sana tukaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo nilikuwa naomba pia kusema kwamba ni kweli tunajitahidi kuwaambia watu wasikate miti ovyo na kule vijijini wakati mwingine tunazuia wanavijiji na wananchi wasikate miti ovyo. Unamkuta mama amebeba kuni, anabeba kuni kwa kujifichaficha ukuni wenyewe ni mmoja maana yake kichwa chake uwezo wa kubeba matani hana, anabeba kakuni kamoja tu akapike chakula na watoto wake na familia yake. Lakini zipo taasisi ambazo zinakata matani matani ya miti. Magereza tunaomba watuonyeshe kuni wanachukua wapi, mashamba yao yako wapi na wanapika ugali kwa ajili ya wafungwa kila siku. Viwanda kama vya Sigara watuonyeshe kuni wanapata wapi, mashamba yao yako wapi? Viwanda na wakulima wakubwa wa tumbaku viwanda vyao na sehemu wanakochukulia kuni ni wapi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, utakuta tuna mkandamiza sana huyu mwananchi ahaa kuni msikate lakini yeye anabeba kamoja tu tena anabeba kichwani. Kwa hiyo, nilidhani tujaribu kuangalia na kuwatafutia suluhu.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo pia nimeombwa niiombe Serikali kwamba mafuta ya taa yatasaidia sana suala zima la kusaidia kupunguza matumizi ya kuni kwa hiyo, wanaomba kodi ya mafuta ya taa ifutwe pamoja na gesi. Katika mkoa ambao natoka mimi tunayo milima ya Livingstone. Milima hii ina vyanzo vizuri sana vya maji pamoja na milima ambayo ipo katika Wilaya ya Kilolo, milima ya *The Eastern Alp Mountains* na milima ya Udzungwa. Kwa hiyo, tulidhani wakati umefika sasa wa Serikali kujaribu kuangalia na tusiachie Mashirika ya Nje kama Mashirika ya *WWF* ambayo yamejikita sana. Ipo haja ya Serikali kutenga kiwango kizuri tu na mpango shirikishi ambao upo kwa sasa lakini tuendelee kuwahimiza watu wetu ili waendelee kutunza maeneo haya muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya yote niseme kwamba Wizara hii kwa sababu ni nyeti sana na muhimu sana katika nchi yetu inatakiwa Wizara ya Mazingira ipewe ushirikiano mkubwa sana na Wizara zingine kama Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maji. Mpaka sasa masuala ya Mazingira katika nchi yetu bado nilidhani tunawaachia wataalam. Viwanda vingine vimejengwa karibu ya makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *pollution* ya hewa. Watu wetu hospitali ukienda wanakwambia labda mtu anaambiwa nimegundulika nina *TB*. Anasema taja historia yako. Anasema aaha, mwaka fulani niliwahi kukaa sehemu fulani kulikuwa kuna Kiwanda cha Sementi, kwa hiyo, inawezekana lile vumbi. Kwa hiyo, wale *polluters* wa hali ya hewa tuangalie ni jinsi gani tunaweza tukapunguza *air pollution*, ni viwanda vingi sana, wananchi wanapata athari na kwa kuwa athari za kimazingira ni za polepole *gradually* haziko *immediate*.

Kwa hiyo, inachukua muda mrefu sana watu kugundua kwamba amepata athari kutokana na suala zima la mazingira. Kwa hiyo, wanasheria tunaomba wajitahidi na ziwepo hizo sheria na tuwaone watu hawa ambao wana-*pollute* hiyo hewa katika vyombo vya sheria na wananchi ambao wanapata matatizo basi wapate nafasi ya kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema bila kusahau zile Wilaya ambako wanalima sana vinyungu na milimani ambako inapita naomba nizitaje. Wilaya hiyo ni Wilaya ya Kilolo, Makete, Njombe, Ludewa, Mufindi, Iringa Vijijini na Iringa Mjini. Tunaomba sana suala hili la mazingira liweze kupata kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuchukua nafasi hii kuunga mkono hoja na nadhani fedha walizoomba wanapaswa wapate. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SAMEER I. LOTTO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi kuweza kuchangia.

Nitakachoongea nitasisitizia yale niliyokwisha kuongea katika mkutano huu pale awali ni kushusha watu milimani. Nitakwenda kwenye pointi moja kwa moja. Wanajimbo la Morogoro Kusini Mashariki wengi wao asilimia zaidi ya 50 wanaishi kwenye milima. Sasa hivi tunaambiwa washuke milimani, watu hawa wanaishi kwenye milima hiyo kwa zaidi ya karne moja na kuendelea. Mimi nimewakuta na nitawaacha na naamini wataendelea kukaa milimani hapo. *(Makofi)*

Sasa tutafute njia mbadala sio lazima tuwahamishe. Nilipoongea siku ile nikasisitiza kwamba watu hawa wapewe maeneo yale wawe wanapanda miti ya kudumu. Sasa hivi tunaambiwa kuna bajeti ya kupanda miti. Wapewe wale fedha wakapande miti wenyewe, wapande miti ya kudumu pale. Wapande mifenesi, michungwa huku chini milimani wakishushwa huku kama miundombinu itakuwa sahihi watakuja, watapanda mazao ya muda mfupi mfupi. Lakini tunaambiwa waondoke huku chini wanapopelekwa hakuna maandalizi yoyote, watakwenda wapi hawa? Kule kuna makaburi yao, kuna mizimu yao kule juu. Hili naomba jamani nalisisitiza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi nikimnukuu Balozi hapa akiinukuu *Financial Times* ikimnukuu Waziri Mkuu alisema kwamba vipi tutafurahisha watu wa nchi nyingine na kuwanyima watu wa nchi yetu yalikuwa yanazungumziwa maji ya Ziwa Victoria. Lakini hapa sasa mimi naiweka kinchi sio Kimataifa bali Kitaifa. Vipi wananchi wa jimbo langu wata-*sacrifice* mashamba yao kwa sababu watu wa Dar es Salaam wapate maji, kwa sababu watu wa Dar es Salaam wapate umeme? Mimi nasema tena natetemeka hapa kwa sababu ya jazba kwamba watu wangu jamani watabaki pale naomba tusaidiane tukae. Tena nashukuru hapa naona Waziri wa Mazingira anaiandika andika sijui wapi nafikiri ataniita pembeni baadae tukae tulijadili. *(Makofi/Kicheko)*

Nasema kwamba *Kyoto Protocol* ambayo ililenga kusaidia wananchi ili nchi zetu ziweze kutoa *green* zaidi ili tuweze kutoa *carbondioxide,* hii imekwenda wapi? *Kyoto Protocol* imechangia vipi katika sisi Tanzania hapa? Naomba tusaidiwe. Wananchi watapanda miti wenyewe kule, watapanda miti yao. Tusaidieni hapo. Mimi sitoondoa shilingi wala sitoondoa thumuni. Sasa nashangaa hapa Amina thumuni haijui na hajawahi kuitumia. Lakini thumuni ni nusu ya shilingi. Sasa mimi nasema kwamba jamani Waziri anayehusika njoo tukae tuongee, tutafute ufafanuzi naamini unaniandikia mimi hiyo. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Suala la pili ninalotaka kuongelea ni kuhusu katika hii Mazingira kama tunavyofahamu ni *issue* mtambuka, zaidi nitazungumzia mkaa na mbao. Toka zoezi la mkaa na mbao haramu kuwekewa mkazo wa kusimamishwa na kunyang'anywa wananchi inafika miezi minne nafikiri. Je, ni mikaa mingapi imekamatwa na mbao ngapi zimekamatwa na ziko wapi? Maana yake inawezekana na naamini iko hivyo watendaji wanachukua zile mbao na ile mikaa wanatumia wao, wanauza. Sasa kama tutaruhusiwa tukae na Madiwani wetu tuorodheshe watu walionyang'anywa mbao au mikaa, tuangalie kama mikaa hiyo ipo na mbao hizo zipo. Maana yake naamini hazipo lakini tupo tayari kufanya uthibitisho wa hilo pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naongea kwa ukali na watendaji waongo wanatudanganya. Siku zile niliposimama nikasema hivi hivi nikasema watendaji waongo wanatudanganya.

Nasikitika kwamba *Chief Whip* yupo hapa, hanipi mwongozo wa Spika kwamba nitoe ushahidi. Lakini hata ndugu yangu Mheshimiwa Haroub Said Masoud, hapa hataki nitoe ushahidi kwa sababu ushahidi upo. Hawataki nitoe ushahidi lakini ushahidi upo kwamba tunadanganywa kuanzia ngazi ya vitongoji mpaka ngazi ya Wizara. Niambiwe nitoe ushahidi nitatoa ushahidi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sitoongea sana namaliza. Nasema kuhusu sungura. Mwenzangu pale leo ameongelea chura, mwingine dada yangu kule anaongelea mjusi, mimi naongelea sungura. Sungura tunasema ni mdogo lakini mapaja yake yanakwenda. Juzi kwenye Miundombinu yanakwenda Kilimanjaro. Nikaona tena kwenye Kilimo yanakwenda Iringa mapaja hayo. Sisi tunagaiwa sungura aliyebakiwa bila mapaja. Tukiangalia kwenye Maji yamekwenda Bunda, sasa hili sijui wapi lakini mimi naomba Rais kama ujumbe wangu unafika angalau kwa mwaka mmoja na mimi niwe Waziri nipate hayo mapaja kwa ajili ya jimbo langu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hayo yangu machache. Ahsante na nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sameer Lotto na tutazidi kukuombea ndoto zako siku moja zitimie. Pia umeokoa muda kwa hiyo si ajabu tukapata na msemaji mwingine ngoja tuone. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kama walivyokushukuru wenzangu kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais. Mimi nitakuwa sina mambo mengi, nina mambo matatu tu kama wakati utaniruhusu. Jambo la mwanzo ni suala la Muungano kama lilivyozungumzwa hapa. Suala la pili litakuwa ni Katiba, lakini la tatu kama wakati utaniruhusu basi nitazungumzia kuhusu historia ya kujirejea.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa mimi nichukue nafasi moja kwa moja kuishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuhimili, kumudu, kuuenzi na kuudumisha Muungano huu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Muungano wa Serikali mbili ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hiyo maalum kwa sababu hali ya Tanzania hasa Zanzibar ndani ya Jamhuri ya Muungano. Wazanzibar tumechukua nafasi kubwa ya kujivunia na pia tumechukua nafasi kubwa ya kudumisha Mapinduzi yetu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini tukizingatia masuala yaliyozungumzwa hapa kuhusu kero. Nashukuru sana Rais wa Awamu na Nne kwa kuunda Kamati katika Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Waziri Kiongozi kushughulikia kero za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili Jamhuri iende vizuri. Lakini wakati tukifanya hayo wewe utakuwa shahidi kwamba ndani ya Ofisi hii ya Makamu wa Rais katika michango mbalimbali. Kuna wajumbe hapa wanazungumzia kuhusu Muungano waulizwe wananchi. La ajabu ni kwamba wanaotoa hoja hizi wanatumia sana Tume za Jaji Francis Nyalali na Jaji Robert Kissanga. Lakini mwenzetu anaposimama hapa akatuambia kwamba anataka waulizwe wananchi taabani yeye anawakilisha wananchi angetuambia

basi na yeye ametumwa na wananchi gani ambao wanataka waulizwe ndani ya Bunge hili.

Lakini wenzetu hawatuambii wananchi gani wanataka muundo wa Serikali ya Muungano uzungumzwe. Lakini tunapozungumzia hizi ripoti za Jaji Robert Kissanga mimi ninavyofahamu kwa taaluma yangu ndogo Serikali inapotoa nafasi ya kuunda Tume na inapofika Tume ile kupeleka ripoti, ripoti ile si *Quran,* ripoti ile inajadiliwa na wananchi wa nchi husika. Sasa ripoti zote hizi mbili badala ya kupelekwa wanaoamua wenye uamuzi wa mwisho ni wananchi sio wanaoandika ripoti na ripoti zote mbili hizi wananchi wameamua zote mbili inayozungumzia muundo wa Muungano Serikali ngapi, wananchi wameamua Serikali mbili. Wale waliozungumzia suala la Muungano wenyewe asilimia ngapi, sote tumeambiwa, lakini humu ukisoma ripoti ya Mkuu wa Upinzani badala ya kuzungumzia hali halisi ilivyo naomba ninukuu kipengele kimoja Mheshimiwa Spika, badala ya kutilia mkazo basi anasema, Mheshimiwa Spika, inasemwa, hilo inasemwa maana yake uzito wake mdogo. Sawa sawa na eti, ndiyo maana yake. Inasemwa kuwa asilimia 96 ya wananchi waliohojiwa Zanzibar walitaka muundo wa Serikali mbili na asilimia 84 wananchi waliohojiwa Tanzania Bara walitaka Muundo wa Serikali mbili. *(Makofi)*

Wananchi wameshasema na muundo wa Serikali mbili ndio utakaobakia katika Jamhuri ya Muungano ndani ya Chama cha Mapinduzi. Sasa kama kuna mtu ana muundo wa Serikali Tatu, Nne hapa ndio pahali pake pa kusema. Waliosema wote hawajatuambia wanataka muundo wa Serikali ngapi, wanasema wananchi wanataka. Wewe unataka ngapi? Sema wewe mwenyewe unataka ngapi basi tuambie. Watu wanaogopa kivuli vyao, hili ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sisi tumeletwa hapa kuja kuishauri Serikali, waishauri Serikali wao wanataka muundo wa Serikali ngapi? Wanaogopa nini? Wasiogope kivuli chao. Hapa ndio mahali pa kusema. Lakini wanazunguka wananchi wahojiwe, lakini wananchi wameshahojiwa, lakini waache kuhusu hizi ripoti za Tume za Tume za Majaji.

Mheshimiwa Spika, kinachoshangaza kuna ripoti nyingine ya Jaji Francis Nyalali ndani ya ripoti yake ya 1992 wenzetu hawa hawasemi kuhusu Mfumo wa Vyama Vingi ulivyoanzishwa maana ripoti hii ndiyo inasema uanzishwe Mfumo wa Vyama Vingi ndani ya Jamhuri ya Muungano. Hawajasema kwamba asilimia 80 ya wananchi wa Tanzania wamekataa kuunda Vyama Vingi, hawasemi kwa sababu hili lao. Lakini Jamhuri ikasema hapana, tuingie katika Vyama Vingi kwa sababu tufuate ulimwengu unakwenda wapi na hilo wamelitaka wenyewe hili.

Sasa leo kuzungumzia mfumo wa Muungano hapa tuambie basi mingapi mnataka. Lakini kwa sababu hili limewashinda nao wameona hawajafaidika wameanzisha sera nyingine. Naomba ninukuu. Katika mmoja wa wajumbe alipokuwa anachangia hotuba ya Waziri Mkuu alisema hivi maana huku kwenye Muungano wameshaondoka sasa wamekwenda kwenye sera. Naomba ninukuu: "Ni dhambi kwa chama chochote, nasema dhambi kwa mawazo yangu chama chochote kuwa na mfumo wa Serikali katika nchi yetu. Kwa yule anayesema Serikali moja, yule anayesema Serikali mbili, yule anayesema Serikali tatu, lazima tupate *mandate* ya wananchi wanataka mfumo gani wa

Serikali ili hatimaye kusiweko chama chochote ambacho katika sera zake kitakuwa kinazungumzia mfumo wa sera kwa sababu tayari utakuwa umeshaamuliwa na wananchi.

Mheshimiwa Spika, haya ni mambo ya ajabu sana na yanasemwa ndani ya Bunge Tukufu kama hili. Tumekubali kuwa na vyama vingi sisi wenyewe, sasa kama una Sera katika chama chako, usimwambie mwenzio asiwe na Sera. Chama cha Mapinduzi, kina Sera. Sera ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali mbili, amani na utulivu. Sasa kama chama chako hakina Sera, usitake kushawishi watu wasiwe na chama chenye Sera, hapana. Vyama vinakuwa na Sera, si Tanzania tu, ulimwengu mzima, utakwendaje kwa wananchi bila kuwa na Sera, bila kuwaambia utakachokifanya, bila kuwa na Ilani ya Uchaguzi, huu ndiyo mfumo wa vyama vyingi. Sasa wameondoka huku, wanakwenda kwenye Sera. Kama huna Sera endelea na Sera yako ya mawe. Chama cha Mapinduzi, kimeendelea kushinda kwa sababu ya Sera zake, hakikushinda ovyo ovyo tu, hapana. Wananchi wamekataa vyama vingine, kwa sababu ya Sera zao. Hakuna Sera ya matusi katika nchi hii, hakuna Sera ya ugomvi katika nchi hii, hapa pana Sera ya amani na utulivu na Sera ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine linalonishangaza, Muungano huu unazungumzwa sana, lakini *wallahi* hakuna watu waliofaidika na Muungano kama Zanzibar. Wapemba wako Somali, wapemba wako Mbeya, Kyela na kwingineko. Wamejaa katika Tanzania, wako huru. Sasa mimi naona ajabu watu wanatafuta Muungano gani tena!

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge kifungu gani?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, kifungu cha 50, Mbunge asiseme uongo Bungeni. Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, anapozungumza anasema kuna chama chenye Sera ya Mawe. Tungependa kujua ni chama gani kina Sera ya Mawe na tungependa kujua ni nani anayekataa Muungano? Anatumia hiyo kwa kutumia pia kifungu cha 54 kuweka jambo sawa. Upinzani haujakataa Muungano, lakini pia si sahihi kwa Muungano kuelezwa kwa sura anayoifahamu tu Mheshimiwa Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. Sisi tumesema Muungano wa Serikali tatu, sasa kama haufai ni Sera yetu, ni utaratibu wetu na yeye pia anatakiwa kuwa na utaratibu wake. Kwa hiyo, tulitaka kuweka sawa hilo. Lakini pia tulitaka kujua ni Sera ipi hiyo ambayo inahusika na mawe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge asante. Mimi nilivyomsikia Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, alisema kama huna Sera ndiyo uchague hiyo ya mawe. Ndivyo alivyosema, hakutuhumu chama chochote kwamba, kina Sera ya Mawe. La pili, kuhusu alichokuwa ananukuu kwenye *Hansard,* alikuwa anamjibu, nilivyoona mimi, Mbunge wa chama kingine, sio CHADEMA. Alikuwa anamjibu Mbunge wa *CUF*. Kwa hiyo, CHADEMA inajulikana kabisa nchi nzima kwamba, ndiyo chama chenye Sera ya Serikali tatu, imo kwenye Ilani yao. Lakini yeye alikuwa hasemi hilo, alikuwa anazungumzia Chama cha *CUF*, ambao ndiyo wachangiaji wake walikuwa wanahoji na kuomba kwamba, suala la Muundo wa Muungano lirejeshwe kwa wananchi. Sasa hao nao ndiyo Sera yao hiyo.

Hiyo ndiyo alikuwa anaihoji, kwa hiyo, hakuna chochote alichoharibu, naomba uendelee Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. *(Makofi)*

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa ufafanuzi, lakini pia naomba dakika zilizopotea uniongezee hapo baadae.

Mheshimiwa Spika, Katiba ni uskani, mwongozo, dira na Katiba ni heshima. Bunge ni sehemu ya Katiba, Serikali zote mbili ni sehemu ya Katiba, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Spika, ni sehemu ya Katiba na wao ni moja kati ya wasimamizi wa Katiba hiyo.

Nitakayoyazungumza sasa hivi, nakuomba kwa hisani yako, univumilie kidogo, nikikugusa. Hali kadhalika namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu, naye anistahimilie nikimgusa.

Mheshimiwa Spika, Wabunge kuwa halali kuingia ndani ya Bunge hili, kuna utaratibu wake. Utaratibu wa Bunge hauna tofauti sana na utaratibu kwa sisi wa Waislam, tunapotaka kuingia Msikitini. Unapotaka kuingia Msikitini lazima utie udhu, unawe mikono, unawe uso, viganja na mambo mengine, lakini ukishajitia udhu kuna tatizo moja usi-*huduth.* Ku-*huduth* ukishajitia udhu, ni kutoka upepo sehemu yako ya siri. Kwa hiyo, udhu unakuwa haupo, inabidi ukatie tena. Sawa sawa na Bunge, Waheshimiwa Wabunge kuingia ndani ya Bunge, hili mchakato wake ni mkubwa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, nadhani lugha hiyo sasa inakwenda kwingine, nadhani unaweza ukaijenga hoja bila kutumia maneno hayo.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, naondoa hoja yangu hiyo. Lakini nakuja kwenye mchakato wa kuingia Bungeni. Tunapita sehemu nyingi, kwenye kura za maoni na mambo mengine hadi kuingia katika Bunge, hali kadhalika tunakula kiapo. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukurasa wa 88, kifungu cha 103, kwa ruhusa yako naomba kunukuu: "Kutakuwa na Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambaye ndiye atakuwa Rais wa Zanzibar na Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na vilevile Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi."

Mheshimiwa Spika, lakini kifungu cha 104 ukurasa wa 89 kinazungumza kwamba, naomba ninukuu: "Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, atachaguliwa na wananchi katika Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Zanzibar na kwa kufuata utaratibu uliowekwa, kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi Zanzibar, inayohusu uchaguzi wa ujumla au uchaguzi wa Kiongozi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar."

Mheshimiwa Spika, Rais wa Zanzibar yupo, amechaguliwa kihalali, lakini kifungu cha 26(1), naomba ninukuu kinasema kwamba: "Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kuitii Katiba hii na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania."

Mheshimiwa Spika, Chama cha *CUF*, kimekiuka Katiba, kimekiuka vifungu namba 26, 103 na 104, baada ya uchaguzi halali uliofanyika Zanzibar kwa kutangaza kuwa, hawamtambui Rais wa Zanzibar. Kwa maana hiyo, kwa sababu chama hiki kina Wabunge ndani ya Bunge hili, Wabunge hawa, kwa maoni yangu, si halali kuwemo ndani ya Bunge hili, kwa sababu chama chao kimekiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa maana hiyo, naomba mwongozo wako na hatua za kinidhamu zichukuliwe kwa Wabunge wa Chama cha *CUF*, sisemi wa Zanzibar, nasema Chama cha *CUF*. Kwa sababu Chama cha *CUF,* ndicho kilichotangaza kutomtambua Rais wa Zanzibar, aliyechaguliwa kihalali na kuwemo ndani ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano.

Lakini kama hilo halitoshi, Kanuni kifungu cha 25, kinatuambia hivi, naomba ninukuu: "Mimi (Mbunge atataja jina lake), naapa kwamba, nitakuwa mwaminifu kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuitumikia kwa moyo wangu wote na kwamba, nitaihifadhi, nitailinda na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, iliyowekwa kwa Mujibu wa Sheria."

Mheshimiwa Spika, Chama cha *CUF* hawaitetei, hawauingi mkono na hawamtambui Rais wa Zanzibar. Kiapo cha Wabunge wa Bunge hili kutoka Chama cha *CUF,* si halali na kwa maoni yangu, ni cha kejeli. Kwa sababu chama chao kimetamka hadharani na baya zaidi, ndani ya Bunge hili, mmoja kati ya Wabunge hao, ametamka hadharani kwamba, simtambui Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ni jeuri ya Kikatiba na hili nalisema kwa sababu wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Makamu wa Rais, viapo vyenu ni tofauti na sisi. Viapo vyenu Waheshimiwa ninyi mnapoapa, Rais anawakabidhi Katiba pale pale, kwa maana ya kuisimamia. Sisi tunapoapa, tuna mikoba yetu ya kupewa pale, kuna tofauti hapa.

Naomba sasa kwa kutumia vyeo vyenu, muilinde Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hasa tukiwa ndani ya Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambalo linatumia haki zote za wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, katika mchango wake, amedai Mwongozo wa Spika, kuhusu uhalali wa Wabunge wa *CUF*, kuwemo humu Bungeni. Mwongozo wa Spika unasema, wao ni halali. Kinachozingatiwa hapa ni kwamba, waliapa kama kila mmoja wetu alivyoapa, waliapishwa kama Wabunge.

Hayo mengine yanayokuja sasa, itabidi yachukuliwe utaratibu unaostahili, ili kauli hizo ndiyo ziweze kupelekwa mahali zionekane kwamba, zimetengua Ubunge wao. Kwa hivi sasa ni Wabunge halali wa Bunge hili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hadi hapo, hakuna nafasi tena ya kuendelea na mjadala kwa wachangiaji wa kawaida. Kwa hiyo, tuendelee na hatua inayofuata ya kujibu hoja. Tulipanga nusu saa kwa Waheshimiwa Mawaziri wawili, kwa hiyo, anaanza Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kuhusu Muungano, halafu atamalizia Mhesimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, kuhusu Mazingira. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Waziri wa Mazingira, kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya katika suala zima la usimamizi na uendelezaji wa mazingira hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, leo ningependa kuchangia kuhusu suala la *Environmental Impact Assessment (EIA)*. Katika suala hili ningependa kuishauri Serikali kuwa, hii *EIA* iwe inafanywa na Serikali na si wawekezaji au watu wanaotaka kuanzisha chochote katika nchi hii. Kwa kawaida wawekezaji katika Sekta ya Madini, wamekuwa wao ndio wanaofanya *EIA*. Jambo hili limekuwa likileta hofu na malalamiko kwa wanachi, kwani wawekezaji hawa wamekuwa hawatoi ripoti halisi, inayoonyesha uharibifu utakaotokana na uwepo wao katika eneo hilo. Hili linaweza kuepukwa, iwapo Serikali itaamua *EIA* iwe inafanywa na Serikali na si kufanywa na wawekezaji moja kwa moja au kufanywa na kampuni ambayo hata hivyo inagharamiwa na wawekezaji hao.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuzungumzia suala la utafiti wa matumizi ya kemikali katika viwanda. Katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwepo na ongezeko la viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali, sambamba na ongezeko la migodi na shughuli nzima ya utafutaji wa madini. Katika kufanikisha shughuli hizo, wamiliki wamekuwa wakitumia kemikali mbalimbali, swali langu ni je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na zoezi la utafiti wa kina na wa mara kwa mara ili kuhakikisha madawa na kemikali hizo, ambazo ni sumu kali yanabadilishwa au kupiga marufuku?

Mheshimiwa Spika, je, hadi sasa Wizara ina wataalam wangapi wa masuala ya utafiti wa kemikali; ni wa viwango vya elimu ya kiasi gani na huwa wanahakikisha vipi kuwa kemikali hizo hazitumiki? Sambamba na hilo, ni kiwanda au mwekezaji gani aliyewahi kuchukuliwa hatua kutokana na matumizi ya kemikali zilizopigwa marufuku?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika hoja ya bajeti ya Mazingira. Naunga mkono juhudi kubwa, ambazo Serikali imezifanya ili kuokoa na kulinda mazingira ya nchi yetu. Hata hivyo, napenda kushauri yafuatayo, ambayo ni imani yangu kuwa tukijipanga vizuri tutafanikiwa:-

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali yetu sasa ione umuhimu wa kutumia nishati ya jua, ambalo tunalipata kwa wingi sana nchi nzima. Naomba tujifunze matumizi mazuri ya nishati hii. Nchini Israel ambako hawapati mvua nyingi, nchi yao eneo kubwa

la ardhi ni jangwa, maji yao hupatikana kutoka *Jordan River*. Pamoja na hali hiyo, nchi hiyo haina tatizo la umeme wala uhaba wa maji. Naomba ufike wakati sasa, tupeleke wataalam wetu huko, wakaone wenzetu wanaishi vipi. Kwa kuwa Israel hawana misitu wala vyanzo vingi vya maji, lakini jambo la ajabu wanajitosheleza kwa chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, nashawishika kuona kuwa, nishati mbadala ya jua sasa ilete vifaa vyake na kodi iondolewe kabisa ili wananchi waweze kuitumia. Kwa kufanya hivyo, nishati itokanayo na maji, itumike viwandani, hospitalini, vyuoni, mashuleni, majeshini, makambini na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, pili, ili kunusuru misitu, wananchi wafundishwe kutumia kinyesi cha ng'ombe, *biogas* katika matumizi ya kawaida kwa vile nishati hiyo nayo ni nyingi. Naomba tujifunze matumizi mazuri ya nishati hii, kwa wenzetu wa India. Aidha, nashauri ufike wakati sasa, nishati mbadala zitumike kwa wananchi wengi na kwamba, endapo wachache watasalia, watumie makaa ya mawe. Kwa kufanya hivyo, naamini kabisa tutayaokoa mazingira ya nchi yetu. Jambo kubwa ni elimu na upatikanaji wa nishati hizo mbadala.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu uharibifu wa msitu wa Namlonga. Msitu wa Namlonga upo katika Kijiji cha Namlonga Kata ya Ruanda – Mbozi. Inaonekana kama Serikali ya Wilaya na Mkoa zimeshindwa kukabiliana na ukataji wa miti ovyo katika vilima vya Namlonga. Miti hukatwa kwa wingi sana, kwa ajili ya mkaa na inasemekana kwamba, zaidi ya magunia 50 hadi 80 ya mkaa husafirishwa kwa siku. Hii ni hatari sana. Wachoma mkaa wakipewa maagizo hawatekelezi, hukaidi maagizo ya Serikali na hutembea na silaha, tayari kukabiliana na dola. Hali hii imeshatokea, Afisa Mtendaji wa Kijiji aliwahi kutekwa, alipigwa na kunyang'anywa baiskeli na wachoma mkaa. Pia inasemekena kwamba, wanajeshi wa kikosi cha 44 KJ – Mbalizi Mbeya, ndio huwatuma wachoma mkaa kufanya kazi ya kuchoma mkaa kwa ujira mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, Serikali kwa kupitia Wizara ya Mazingira, iingilie kati suala hili kwa kutoa maelekezo makali sana kwa uongozi wa Mkoa Mbeya ili uhakikishe unasimamia kwa ukaribu suala hili. Kama ushauri huu hautofanyiwa kazi, basi msitu wa Namlonga, ambao ni mkubwa sana na ambao pia ni chanzo kikubwa cha mvua, utateketea.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu suala zima la mazingira. Katika suala zima la mazingira nitazungumzia kuhusu wananchi wachimbaji wafuatao:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, wachimbaji wa mchanga kwa ajili ya ujenzi. Kuna baadhi ya hawa wachimbaji ambao wanachimba kokoto katika maeneo ambayo Serikali

haijaruhusu kuchimba mchanga. Wao wanachimba kwa wizi tu, wanachimba sehemu ambazo ni karibu na makazi ya wananchi, kiasi cha kusababisha mmomonyoko wa udongo.

Mheshimiwa Spika, pili, wanaojiita wachimbaji wadogowadogo wa madini. Hawa wanachimba sehemu ambazo hata wao wenyewe hawana hakika kuwa watakapochimba watapata madini. Hii husababisha uchimbaji holela ambao husababisha uharibifu wa mazingira. Pia hawa ndio chanzo cha kukata miti ili wapate sehemu ya uchimbaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukataji miti ovyo, wapo baadhi ya wananchi, ambao hukata miti ovyo kwa ajili ya kuni, mkaa au kwa ujenzi. Miti wanayoikata pia hawafahamu ina thamani gani kwa Taifa. Nashauri Serikali, iwaelimishe zaidi wananchi umuhimu wa kuitunza miti na pia kuhakikisha wanahamasishwa upandaji wa miti ile ambayo ni maalum kwa matumizi ya kuni, mkaa au miti. Wananchi wahamasishwe kukata na kupanda miti, wananchi wengi hawana elimu ua utunzaji wa mazingira yetu. Mfano, katika sehemu ya mpakani ya Tanzania wa Kenya, ambayo ipo sehemu ya Mkoa wa Tanga, kati ya Jimbo la Mkinga na nchi ya Kenya kwa sehumu ya Lunga Lunga. Kuna wananchi ambao wanaishi sehemu ya Tanzania, wakati wao ni raia wa Kenya. Wao wanaingia Tanzania kupitia mpaka wa Tanzania - Horohoro. Hawa huchangia kwa kiasi kikubwa, kuchafua mazingira yetu kwa kukata miti ovyo kwa ajili ya mkaa, kuni na kwa ujenzi na husafirisha vitu hivi kwa njia ya panya kuuza nchini kwao Kenya.

Kwa hiyo, hawaoni umuhimu wa kupanda miti tena baada ya kuikata na ukizingatia hawa sio Watanzania na hawana uchungu na Tanzania. Naomba Serikali idhibiti hawa raia wa Kenya, wanaoingia Tanzania na kujifanya ni Watanzania, ukizingatia pia hawaeleweki kutokana na hufanana kwa lugha zao. Serikali iandae vitambulisho ili kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, ahsante naunga mkono hoja.

**MHE. HASSAN C. KIGWALILO:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja. Hotuba ni nzuri na kamilifu. Ninawapongeza Mawaziri, pamoja na Wataalam walioandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira sio lelemama ni mapambano makubwa ya kuwarekebisha wananchi, kulinda mazingira, kutunza misitu, vyanzo vya maji, hata katika uchimbaji wa madini, ujenzi wa viwanda na kadhalika. Haya yote yanaathiri sana mazingira, kama hatua za tahadhali hazitachukuliwa wa wakati wa maamuzi ya kibiashara au kiuchumi yanapofanywa. Ninaishauri Serikali, ifuatilie kwa karibu sana, namna ya kuwasaidia wananchi katika kutunza mazingira kila Wilaya na kila Jimbo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa mfano wa Jimbo langu la Liwale, ambalo lina eneo la kilomita za mraba 39,000. Asilimia 53 ya eneo hilo ni Hifadhi ya Wanyamapori, yenye misitu mikubwa na miti mingi. Nina wasiwasi mkubwa sana wa namna biashara ya ukataji wa magogo inavyofanywa juu ya hifadhi ya mazingira. Sio

hivyo tu, ukataji wa magogo, haunufaishi wananchi wa maeneo ambao ndiyo watakao athirika hapo baadae kwa kukosa mvua, endapo misitu hiyo itaendelea kukatwa kiholela. Ninaishauri Serikali, ifuatilie kwa karibu biashara hii ya magogo, kwani inaonyesha Serikali ina kigugumizi kusitisha ukataji wa magogo.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa wafugaji wameanza kuvamia Mikoa ya Lindi na Mtwara, kutafuta malisho ya mifugo yao. Ninaiomba Serikali, iangalie hali ya kila Wilaya namna ya kutekeleza na Wabunge wahusishwe, wanapotafutiwa wafugaji maeneo ya malisho kwa mifugo yao. Pia ninashauri badala ya kuhamisha mifugo, kwa nini maeneo yenye nyasi au majani ya kutosha, wapewe tenda za kusafirisha majini au nyasi hizo kwa maeneo ya wafugaji? Hii itakuwa ni biashara, kwani wafugaji hawatalisha mifugo yao bure. Wafugaji wakiona kuna gharama ya kulisha mifugo yao mingi, watalazimika kuwafanyia *family planning,* ili wawe na ng'ombe wachache na wenye afya. Kuhamisha mifugo kufuata malisho, sio jawabu la kudumu kwani hata watakaohamia pia wataharibu mazingira na kutengeneza jangwa baada ya muda si mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, Mikoa ya Kusini tunahitaji mifugo, lakini Serikali itaisaidia sana mikoa hiyo kama ng'ombe au ufugaji huo utafanywa na wenyewe, ambao wataweza kuendeleza kutunza mazingira. Eneo kama Wilaya ya Liwale, hakuna vyanzo vingi vya maji hivyo, wafugaji wakienda kiholela, vyanzo vya maji vitatoweka baada ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali imepania kufuatilia hifadhi za mazingira, naomba pawe na wataalam kwa kila Wilaya, watakaofuatilia hifadhi za mazingira kwa karibu na wapewe nyezo za ufuatiliaji kama usafiri wa uhakika, kwani hivi sasa hifadhi ya mazingira inafanywa na viongozi wa Wilaya/Wabunge na kadhalika, ambao si wataalam. Kwa mfano, Liwale mazingira hayajaathirika sana ukilinganisha na maeneo mengine, tishio kwetu ni ukataji holela wa magogo. Hivyo, ninaishauri Serikali, ipatapo wataalam, miongoni mwa Wilaya za kufikiriwa kupata haraka wataalam hao, iwe Wilaya ya Liwale, ambayo iko hatarini kuvamiwa na wale wanaofanya biashara ya kukata magogo, bila kujali mazingira.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MONICA N. MBEGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Pili, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kazi nzuri mnayofanya katika Wizara yenu.

Tatu, nachangia suala la vinyungu (bustani za kiangazi katika mabonde ya mito). Mkoa wa Iringa pia Mkoa wa Ruvuma ni mikoa maarufu sana kwa kilimo hicho. Kilimo hicho kimesaidia sana katika suala zima la kupata chakula na hivyo kuwawezesha wananchi kujikwamua na umaskini. Naomba utoe tamko, je, wananchi wamezuiwa kabisa au wafuate taratibu za mita 100 kutoka mtoni?

Naomba pia utoe tamko la kupiga marufuku upandaji wa miti inayoitwa Miti Ulaya, kwani inaharibu kabisa ardhi kwa kutoa rutuba yote na pia kunyonya maji. Ni vizuri miti yote ikatwe na mingine inayohifadhi rutuba na maji ipandwe.

Mheshimiwa Spika, suala la mkaa na kuni, bado halijaeleweka vizuri au Watendaji wanaelewa, lakini wanatumia tangazo la hifadhi ya mazingira, kwa kuzuia kukata miti ovyo, kwa ajili ya mkaa na kuni kwa manufaa yao. Ninajua wananchi wameruhusiwa kuendelea kutumia nishati hiyo, lakini wauzaji wafuate taratibu. Hivyo, kwa sasa wananchi wananyanyasika sana, hasa katika Manispaa ya Iringa, ambapo hata wale wanaouza kwenye makopo, wanashikwa na kutakiwa kulipa faini. Nadhani si haki, kwa sababu huyu ni mtu wa mwisho, anayepaswa kudhibitiwa ni yule anayekwenda msituni, kutafuta kuni na mkaa. Naomba wananchi waeleweshwe, wafuate taratibu zipi na pia watendaji wanyanyasaji wakemewe.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Pia nawapongeza Wataalam wote walioko chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais.

Naomba nichangie juu ya mazingira katika Wilaya ya Kiteto. Kuna uharibifu mkubwa wa mazingira Wilayani Kiteto. Tuna msitu wa asili, ujulikanao kama *SULEDO*, ambao ni maarufu sana na uliwahi kupata zawadi Kimataifa. Tuna hifadhi ya wanyama pori ya mbuga ya Martagos ambayo imepakana na msitu wa *SULEDO.* Sehemu zote hizo, zimevamiwa na mpaka sasa, watu wanaendelea kufyeka.

Tume imeundwa na imeshakamilisha taarifa yake na kumkabidhi Waziri wa Mazingirsa. Ombi langu ni utekelezaji wa taarifa ya Tume, ufanyike kwa haraka iwezekanavyo ili wavamizi wote waweze kuondolewa maeneo ya hifadhi katika mbuga ya Martagos na hifadhi ya msitu wa asili *SULEDO.*

Mheshimiwa Spika, naomba ili tuweze kuweka mazingira mazuri katika Wilaya ya Kiteto, wataalam wafike Kiteto na kuanza kupanga matumizi bora ya ardhi. Bado Kiteto inawezekana kutunza maeneo muhimu ya hifadhi, wafugaji na maeneo ya wakulima.

Mheshimiwa Spika, naomba Wilaya ya Kiteto iwe ya mfano kwa Taifa kwa mpangilio ya maeneo. Kwani maingilio bado ni mdogo. Ningefurahi kupata jibu la hili leo jioni wakati wa majumuisho kwani ni muhimu sana.

**MHE. DR. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba nimpongeze Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), kwa hotuba yao nzuri na mahiri.

Napenda nichangie upande wa mazingira. Tafsiri ya jumla ya mazingira, ni nchi kavu, maji na hewa (anga), pamoja na viumbe vyote vilivyoko kwenye maeneo hayo. Katika nchi kavu, viumbe ambavyo vinaathirika sana ni misitu, ardhi na wanyama pori.

Nchi yetu sehemu kubwa ya misitu imeathirika sana kwa ukataji miti ovyo, pamoja na uchomaji moto. Katika Wilaya ya Chunya, misitu iliyokuwepo miaka ya nyuma, hivi sasa inatoweka kwa kasi kubwa sana. Sababu kubwa zaidi ni miti kwa ajili ya mbao, miti kwa ajili ya kuni na mkaa, miti kwa ajili ya ujenzi wa nyumba na miti kwa ajili ya kujengea mazizi ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, upande wa ardhi, ambayo ndiyo inabeba rasilimali karibu yote, imeathirika vibaya sana. Baadhi ya athari zilizotokea kwenye Wilaya ya Chunya ni pamoja na mmomonyoko *(Soil Erosion)*, inayotokana na mifugo, kilimo kisichoendelevu, uharibifu wa ardhi yenyewe kwa uchimbaji wa kutafuta dhahabu *(Land degradation/deformation),* uanzishaji wa miradi bila kufanyiwa upembuzi yakinifu, ambako inabidi uchimbue ardhi na kilimo cha kuhama hama *(Shifting Cultivation).*

Ninaishauri Serikali, isisitize hatua ya kufanya *Environmental Impact Assessment,* kabla ya mradi wowote kuanza kutekelezwa. Vile vile maeneo ambayo ni vivutio vya utalii, yahifadhiwe. Maeneo hayo ni kama milima, vyanzo vya maji na mabonde. Ziwa Rukwa hivi sana linaelekea kupungua kina, kwa sababu ya ujazo wa udongo, mchanga na takataka zinazosababishwa na mifugo toka milimani. Naishauri Serikali, ichukue hatua za makusudi, kulilinda ziwa hilo. Ili kufanikisha hatua za hifadhi, Serikali iwawezeshe wagani walioko kwenye maeneo husika, kwa kuwapatia nyenzo za usafiri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JANETH M. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nawapongeza wahusika wote katika Wizara hii, wakiwemo Mawaziri, Katibu Mkuu na watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, nazungumzia kuhusu uharibifu wa mazingira Mkoa wa Dar es Salaam. Mkoa wa Dar es Salaam, una mito mingi na mabonde mengi, yakiwemo Mto Msimbazi, Mto Ng'ombe na kadhalika, lakini mito hii ambayo iko Mkoani Dar es Salaam na maeneo mengine, ambayo sikuyataja, imegeuzwa kuwa ni sehemu ya kutupia takataka na hakuna taasisi yoyote inayotupia macho maeneo hayo. Mfano hai ni eneo la Kigogo Darajani na Jangwani katika Kata za Mchikichini, katika Manispaa ya Ilala na Kigogo Darajani mkabala Magomeni/*Morogoro Road* na Kajima, ambapo kuna magari makubwa ambayo huwa yanamwaga takataka (pumba za mpunga). Pia wakati huo huo, huwa wanasafirisha mifuko ya *plastic,* iliyotumika kuhifadhia kemikali, ambazo ni hatari kwa maisha ya binadamu na viumbe hai.

Mheshimiwa Spika, sasa nauliza; je, Wizara hii ya Makamu wa Rais, Mazingira, inachukua hatua gani katika kuwaelimisha wananchi, juu ya athari za kutotunza mazingira na pia wajue sheria ambazo zinaweza kuchukuliwa endapo taratibu zitakiukwa?

Mheshimiwa Spika, utunzaji wa mazingira na usafi katika maeneo yaliyo na vyanzo vya maji na pia na kasi ya upandaji wa miti, uende sambamba na uwekaji wa mbolea. Pawepo na wakaguzi wa mazingira katika kila Kata hapa nchini, kwa lengo la kuzuia uharibifu wa maizngira. Miti ipandwe kwa kila kaya, kila mtaa uwe na programu yake ya upandaji wa miti, kila Wilaya nayo iwe na programu yake ya upandaji miti na

Mikoa kwa ujumla, kuwe na takwimu sahihi. Lengo/matarajio ya upandaji, hali halisi na taarifa ya utekelezaji kwa kila mwaka kwa kila mtaa nchi nzima.

Sheria kali zichukuliwe, kwa watakaofanya uchafuzi kwenye mito na mabonde. Vile vile uchafu ukomeshwe katika kila mtaa na kanuni za afya zifuatwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MIZENGO K. P. PINDA:** Mheshimiwa Spika, Mikoa ya Rukwa, Kigoma na Kagera inakabiliwa na matatizo makubwa sana, yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira, unaosababishwa na wakimbizi. Ninaelewa kwamba, wakimbizi hawa wako nchini kwa ridhaa ya Serikali, lakini tunafanya nini na uharibifu huu mkubwa wa ukataji wa miti katika nchi yetu? Ninashauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), iitake Jumuiya ya Kimataifa, isaidie kutoa mchango wa hali na mali, utakaowezesha kupunguza uharibifu wa misitu na vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Rukwa, unakabiliwa na tatizo kubwa la wafugaji wahamiaji, wengi kutoka Mikoa ya Mwanza, Shinyanga na kadhalika. Wahamiaji hawa, wanakata miti kwa wingi kwa ajili ya kilimo na mahitaji ya kuni kwa ajili ya nishati. Aidha, kutokana na idadi kubwa ya mifugo, inayokadiriwa kuwa zaidi ya 600,000 kuna uharibifu mkubwa wa ardhi. Mifugo karibu yote hiyo, iko katika Bonde la Ziwa Rukwa na Kipeta. Vyanzo vya maji ambavyo ni muhimu hata kwa wanyama katika mbuga ya wanyama ya Taifa ya Katavi, navyo sasa vimeharibika kabisa na kusababisha madhara makubwa kwa wanyama na viumbe hai vingine, ambavyo vinakufa kwa wingi kutokana na vyanzo vya maji. Ninaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), isaidie kuandaa Mpango Maalum wa Hifadhi ya Mazingira Mkoani Rukwa, ili kuuokoa Mkoa huu kugeuka kuwa jangwa katika miaka michache ijayo.

Mheshimiwa Spika, Ziwa Rukwa ni zuri, ndiyo ziwa pekee lenye mamba wengi na pia kivutio muhimu cha watalii katika Bonde letu la Ufa. Ziwa hili sasa liko hatarini kutoweka, kutokana na kujaa tope kwa kasi kabisa. Ujazo huu unatokana na matope yanayoingizwa ziwani, kupitia mito ambayo vyanzo vyake vimeharibiwa na shughuli za binadamu na mifugo katika eneo hilo. Naomba ofisi yako itusaidie kufanya uchunguzi wa kina wa matatizo haya na namna bora ya kuhifadhi ziwa hili. Kwa sasa tunaambiwa, kina cha maji kirefu kabisa, hakizidi mita kumi. Hii ni hatari. Baada ya uchunguzi, Serikali ianzishe Programu Maalum ya kuendeleza ziwa hili zuri.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba suala la *Lake Tanganyika Integrated Regional Development Programme (PRODAP),* liangaliwe kwa umakini mkubwa, kwa kuwa kuna ucheleweshaji wa Mradi huu. Tukichelewa mpaka Novemba, 2006, *AFDBs Project will expire.* Kwa hiyo basi, watu wa Kigoma Mjini watapata hasara!

Mheshimiwa Spika, pia naomba nichukue nafasi hii, niwapongeze watu wa *TACARE,* kwa kazi nzuri ya kutunza mazingira, hasa msitu uliopo katika Msitu wa Katonga katika Manipsaa ya Kigoma. Naomba Serikali iwatambue watu wa *TACARE*,

kwa kazi nzuri wanayoifanya ya mazingira. Katika Mkoa wa Kigoma, hii *TACARE* ni *JANE GOONE* wa Chimpanzee.

Mheshimiwa Spika, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), ifanye mpango wa kuhakikisha kila Halmashauri ambayo ina msitu, kuwe na ufuatiliaji wa kina katika hili.

Mheshimiwa Spika, Kigoma imeathirika sana na mazingira kutokana na wakimbizi. Naomba Serikali itufikirie watu wa Kigoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nawapongeza Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, Mheshimiwa Dr. Husseni Ali Mwinyi na Watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kazi nzuri ya kuandaa bajeti na hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia kwa uamuzi mbalimbali, ambao wanaendelea kuchukua kwa lengo la kuhifadhi mazingira, hususan hatua ya kuhamisha wavamizi katika maeneo Oevu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia maeneo yafuatavyo: Kwanza, umwagiliaji usio endelevu. Iko haja kubwa sana, kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, ili kufanikisha suala hili. Kuna haja ya kuangalia *bylaws* zilizopo katika kilimo na kutunga sheria nyingine, hususan sheria ya umwagiliaji, ambayo pamoja na mambo mengine, itabidi izingatie suala zima la kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kilimo cha mseto. Suala hili bado halijapewa msukumo unaostahili na baadhi ya watu wanadhani kuwa ni suala jipya. Nilitembelea vijiji vilivyoathirika na kuwepo kwa wakimbizi katika Mkoa wa Kigoma na hasa Kijiji cha Kasanda, nikajionea jinsi *NGO* ya REDESO inavyofanya kufufua kilimo cha mseto na kujaribu kurejesha mazingira yaliyoharibiwa na kuwepo kwa wakimbizi. Lakini zaidi, kilimo kisichozingatia hifadhi ya ardhi na uoto wa asili. Naomba Wizara yenu, iwatembelee *REDESO* - Kibondo, mwone kazi yao na muwasaidie.

Mheshimiwa Spika, suala la tatu, ni kuwa Mkoa wa Kigoma, unaweka mkazo sasa katika Zao la Michikichi *(Palm Oil Trees).* Kuna Mradi unaoitwa, *Farming for Energy,* kilimo kwa ajili ya nishati, ambao unaitwa *FELISA,* lengo la Mradi ni kuendeleza Zao la Michikichi kwa lengo la kuzalisha mafuta ya chakula, mafuta ya kuendeshea magari *(Biodisel)* na kuzalisha umeme. Mradi unakabiliwa na upungufu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, wakati Mheshimiwa Rais alipoutembelea Mkoa wa Kigoma, kwa ziara ya kutoa shukrani, nilimweleza juu ya Mradi wa *Farming for Energy,* akashauri wajaribu kuzungumza na *GEF.* Napenda kujua jinsi *GEF*, inavyoweza kusaidia suala la kilimo cha michikichi Mkoani Kigoma.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii, niweze kuchangia katika hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), iliyowasilishwa hapa Bungeni. Aidha, nampongeza Waziri wa Wizara hii, pamoja na wataalam wake, kwa kuandaa bajeti hii na kuiwasilisha kwetu.

Mheshimiwa Spika, naomba niende moja kwa moja kwenye mchango wangu. Suala tathmini ya tahadhari za mazingira hapa Tanzania ni suala ambalo halitiliwi maanani na Serikali halipi uzito wa kutosha. Taarifa zinazotolewa, hazilingani na hali halisi ya kile kilichoko kwenye *ground.* Wanaopewa jukumu la kufanya *Environmental Impact Assessment*, wanajali sana maslahi yao na wale wanaoomba kufanyiwa *EIA*, wanatumia ujanja mwingi, kuwaweka sawa wataalam ili azma yao ifanikiwe. Hali hii ndiyo imesababisha, baadhi ya viwanda kujengwa katikati ya makazi ya watu na viwanda vingine kujengwa kwenye vyanzo vya maji.

Mhsehimiwa Spika, nashauri Shirika la Mazingira *NEMC,* lipewe meno, lifanye kazi zake kikamilifu na kutimiza wajibu wao, kusaidia uhifadhi wa mazingira ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, utupaji wa taka ngumu. Mfumo wa utupaji taka hapa nchini, bado ni duni sana. Pamoja na baadhi ya Manispaa kuwa na utaratibu wa kukusanya taka ngumu majumbani, lakini taka hizo zinakwenda kutupwa maeneo ambayo siyo sahihi.

Madampo mengi, yapo jirani na mito na mengine yapo jirani na makazi ya watu. Serikali itafute njia nzuri ya kuteketeza taka ngumu, ili kuondoa usumbufu kwa wananchi na matatizo ya milipuko ya magonjwa yanayosababishwa na mlundikano wa takataka hizi katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vyanzo vya maji vingi vimeharibiwa kutokana na kutokuwepo taratibu za umakini za Serikali kuyahifadhi maeneo haya. Ni ajabu, pamoja na kuwa hali ya ukame inalitishia Taifa hili, lakini bado Serikali inawaachia wananchi kuendelea kufanya shughuli za kilimo jirani na maeneo haya na mengine wanafanya ni mashamba.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali, baada ya kufanya utafiti wa kina na kujua tuna vyanzo vingapi vya maji na viko wapi, Serikali itoe hati za maeneo hayo, kumilikiwa kisheria kama vyanzo vya maji na watu wote wanaoish jirani, wahamishwe na kupatiwa maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, kupigwa marafuku mifuko ya rambo na bidhaa zinazowekwa kwenye mifuko kama maji na *juice,* naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa kutoa tamko kuhusu uhifadhi wa mazingira hapa nchini, hasa kuondoa kero kubwa ya mifuko ya nailoni, ambayo kwa kweli inachafua mazingira yetu kila kona. Tunatambua fika kwamba, wapo watu watakaokaidi na kupinga amri hiyo, kutokana na kuwa na maslahi binafsi kwenye mifuko hiyo, hasa wafanyabiashara ambao wanatengeneza na kusambaza bidhaa hizo.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni tumesoma kwenye vyombo vya habari, wafanyabishara hao, wameanza kulaani kauli ya Serikali na kuona kwamba, kauli hii imewahi kutolewa hivyo, wapewe muda wajiandae. Natoa rai kwa Serikali, iheshimu maamuzi yake yenye busara, iangalie maslahi ya Taifa na siyo ya watu wachache, ambao ni wafanyabiashara, wasiojali mazingira yetu. Ni tegemeo la Watanzania, muda uliotamkwa ukifika, sheria itachukua mkondo wake, kuhakikisha utekelezaji wa tamko la kuhifadhi mazingira unafuatwa. Wakati wafanyabiashara wasiojali mazingira wanasema, Serikali imewahi kutoa tamko, wananchi wapenda mazingira ya nchi yetu, tunaona tunachelewa sana kuchukua hatua hadi athari zimekuwa nyingi.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na ninaunga mkono hoja.

**MHE. DR. MZERU O. NIBUKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hotuba ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira).

Mheshimiwa Spika, mazingira ni jambo lenye umuhimu wa pekee na naweza kusema mazingira ni uhai. Mazingira ni jambo lenye nadharia pana sana, lakini mimi napenda kuchangia kwa kiasi fulani kuhusu hifadhi ya misitu na maji. Kama ambavyo nimegusia hapo juu kwamba, tunahitaji sana kutunza mazingira yetu, kwa nguvu kubwa, lakini nguvu hizi siziwe za unyanyasaji kwa wananchi wetu, nchini kote. Moja katika hili, ningependa kuishauri Serikali au Wizara ya Mazingira kwamba, wananchi wapate elimu ya kutosha, kwa kuwatumia wataalam wetu wa misitu, kuwaelewesha wanavijiji ili wafahamu umuhimu wa mazingira, kwa maana wasikate miti ovyo, wasilime kwenye vyanzo vya maji au kandokando ya mito, ambayo inatoa maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Lakini pia wapande miti kwa kadri ya uwezo wao. Hivyo basi, tutumie ule usemi wa panda mti kata mti. Pili, tuwaelimishe wananchi wasijenge majumba ya kuishi ndani ya mita 500 ili kuzuia uchafuzi wa vyanzo vya maji, pamoja na mito au mabwawa.

Mheshimiwa Spika, jambo la tatu kubwa katika nchi yetu ni kuhusu matumizi ya mkaa, ambayo naweza kusema ndiyo nishati muhimu na kubwa kuliko zote katika nchi yetu kwa hivi sasa. Nashauri suala la matumizi ya mkaa, liendelee sambamba na elimu kwa wananchi, kwa vile bado hatujapata nishati mbadala, la sivyo tutaleta usumbufu mkubwa mno, kwa wananchi wetu, hasa ukizingatia watendaji wetu wakishapewa maagizo, basi maagizo hayo huyatumia vibaya, kiasi cha kuwanyanyasa wananchi wetu. Kwa mfano, mkaa hivi sasa unakamatwa, lakini mkaa haupelekwi Mahakamani, ambako sheria itachukua mkondo wake. Naomba jambo hili litazamwe kwa macho mawili, mpaka hapo Serikali itakapopata nishati mbadala.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuwahamisha wananchi kwenye sehemu zenye vyanzo vya maji, pia linahitaji umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, kabla ya utekelezaji wa jukumu hili, naomba mambo muhimu yafuatayo yatekelezwe: Kwanza, tufanye utafiti wa kutosha. Pili, tuandae mahali ambako wananchi hawa watapelekwa, kwa maana ya viwanja vilivyopimwa na hasa *garden plots.* Tatu, Serikali iandae malipo ya kutosha angalau ya kuwawezesha kujenga nyumba za kuishi na wala sio fidia. Nne, wananchi wapewe muda wa kutosha

kule wanakoenda ili waweze kupata muda wa kutosha kujenga nyumba hizo na wala isiwe zimamoto, kiasi cha kuwanyanyasa wananchi wetu katika nchi yao ya asili na kuzaliwa. Tano, sehemu wanakopelekwa, waandaliwe miundombinu na sehemu zenye mahitaji muhimu kama maji, shule, zahanati au kituo cha afya ama hospitali na huduma nyingine. Sita, maamuzi mengi yanayofanywa na Serikali, mara nyingi hayawahusishi wawakilishi wa wananchi kama Wabunge na Madiwani, badala yake dola inachukua mkondo wake bila hata wawakilishi hawa kujua kikamilifu. Badala yake, wao wanasikia hewani, kwa hali hii hatuwezi kufika tunakotaka kwenda. Hivyo basi, Serikali iwape maelekezo hawa watendaji kama Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa, kila wakati watoe maamuzi shirikishi na wala sio amri tu.

Mheshimiwa Spika, kama ushauri huo hautafuatwa na badala yake kuleta kero kwa wananchi na mimi sitakuwa na ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, pamoja na Wasaidizi wake, kwa maandalizi mazuri ya hotuba ya bajeti kwa kipindi cha 2006/2007.

Nchi yetu inakabiliwa na uharibifu wa mazingira, kutokana na sababu za uelewa mdogo wa wananchi, juu ya kuboresha mazingira au mazingira ni kitu gani? Kwa sababu hizo, hatua kadhaa zinahitajika, ikiwa ni kutunza na kuboresha mazingira kwa ujumla. Jamii ielimishwe kuanzia ngazi ya kaya kwamba, mazingira ni nini, umuhimu wake na madhara yake, hasa unapoharibu mazingira. Kazi hii ifanywe na Wizara, itoe elimu kwa njia ya vipeperushi, semina, makongamano na hata ujumbe, kupitia mamlaka husika kwa ngazi za kitongoji, kijiji, kata na kadhalika. Vilevile maeneo yaainishwe na Serikali Kuu, kupitia Wizara katika kila eneo, matumizi yake na faida zake juu ya kutunza mazingira ili kujenga uelewa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. FATMA MUSSA MAGHIMBI:** Mheshimiwa Spika, maneno yote yamezungumzwa na wasemaji wa Kambi ya Upinzani, kuna masuala mawili naomba nipate majibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Kwanza, kwa nini Bunge hili limeshindwa kupiga marufuku mifuko ya nailoni kuingizwa nchini, je, Bunge limeshindwa kutunga sheria ya kupiga marufuku? Hebu twendeni Iringa tukaone kulivyo safi, wao wametunga sheria ndogo ya kupiga marufuku mifuko hiyo ya nailoni au Bunge lina *hold shares* katika kiwanda cha mifuko?

Pili, kwa nini Serikali inasita kuwaonesha *Articles of Union* wananchi ili kuondoa maneno yasiyokwisha; Serikali itapoteza nini kuwa wazi?

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, anomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa ibara ya 54(1), inamtaja Rais wa Zanzibar, kama mmoja wa Wajumbe wa Baraza la Mawaziri; na kwa kuwa Katiba ya sasa, haimtaji tena Rais wa Zanzibar kama Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; je, nini hasa:-

- Hadhi ya Rais wa Zanzibar katika Baraza la Mawaziri na pale inapotokea Rais hayupo na Baraza la Mawaziri linakutana, yeye anakuwa Mwenyekiti au Waziri Mkuu na ikiwa hivyo ndivyo, je, hali hiyo haimwondolei hadhi yake kama Rais wa Zanzibar?

- Kwa kuwa Ibara ya 47(1), inatamka kuwa Makamu wa Rais atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu Mambo yote ya Jamhuri ya Muungano kwa ujumla, je, kifungu hiki tafsiri yake halisi ni nini? Kama anashughulikia masuala ya Jamhuri ya Muungano, je, haina maana kuwa ameondolewa mamlaka ya kushughulikia masuala yasiyo ya Muungano, kwa maana ya mambo ya Zanzibar na hata ya Tanzania Bara? Utata huu unatatuliwa vipi ili nafasi ya Makamu wa Rais iweze kufanya kazi pande zote za Muungano?

Mheshimiwa Spika, mazingira ni kweli yanahitaji kutunzwa na kulindwa. Hata hivyo, mazingira yako kwa ajili ya binadamu. Tumefikia hali mbaya ya mazingira kutokana na kutokuwa na mipango bora na endelevu toka mwanzo. Hivyo, ni hatari sana kufanya maamuzi ya zimamoto, yasiyozingatia sheria au sheria ndogo na/au ambayo hali iliyoko imesababishwa na maamuzi na usimamizi mbovu wa vyombo vyetu mbalimbali. Matokeo ya maamuzi yetu, hayapaswi kuathiri wananchi wasio na makosa.

Serikali badala ya kutoa tu matangazo ya kupiga marufuku au kuondoa mifugo maeneo fulani fulani kama ilivyotangazwa, imechukua hatua gani ya makusudi, kuweka kinga kwa wanaoathirika? Kwa mfano, Serikali ilichukua maeneo ya wafugaji katika Wilaya ya Hanang, bila kujadiliana, yenye eka zaidi ya 100,000 na kuwafanya wafugaji wa jamii ya Wabarbaig wawe *displaced* ndani ya nchi yao na leo wanafukuzwa maeneo walikokimbilia kama Morogoro, Mbeya na kwingineko. Isitoshe, leo maeneo hayo ya *Hanang Wheat Complex* yanabinafsishwa.

Ninapenda kupata maelezo ya kina, ni kwa nini wananchi hawa wanahangaika, ambao hawakupata fidia ya aina yoyote, wasirudishiwe ardhi yao badala ya kubinafsishwa? Nisipopata maelezo ya kina, nina nia ya kutoa shilingi kwa mujibu wa Kanuni ya 81(2)(c). Kero moja kubwa katika miji yetu mingi ni namna ya kushughulikia taka ngumu mijini, licha ya uchafuzi na uharibiufu wa mazingira. Taka ngumu ni hatari kwa afya za wananchi. Pamoja na itifaki mbalimbali tulizoridhia, ninapenda kufahamu Serikali ina mpango gani wa makusudi wa kuanzisha *recycling plants* za taka ngumu badala ya kuacha mamlaka za miji na Halmashauri kuhangaika na tani kwa tani za taka mbovu na hatari, ambayo hawana madampo ya kuyatupa kwa vile madampo hayo yana athari kwa wananchi wanaoishi maeneo hayo. Jiji la Dar es Salaam peke yake inakisiwa kuzalisha tani zaidi ya 200,000 za taka ngumu. Fedha nyingi zinazotumika kwenye semina za mazingira ni kwa nini zisielekezwe kwenye mpango wa makusudi wa *recycling plants?*

Mheshimiwa Spika, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Suala la mazingira ni suala mtambuka. Tunashukuru Serikali kulipa suala hili umuhimu wa pekee mpaka kuundiwa Wizara.

Madhara yatokanayo na uchafuzi wa mazingira, yanatugusa wananchi moja kwa moja, ingawa siyo kwa kuonekana kwa macho. Kwa mfano, athari ya moshi kutoka kiwanda cha *Cement* pale *Wazo Hill,* unaweza usionekane mara moja, lakini baada ya muda wakazi wa Boko wanaweza wakaathirika kiafya kwa maradhi ya *cancer* au *TB*.

Mabwawa ya chumvi yaliyoko chini ya kiwanda hicho maeneo ya Kunduchi, lazima yatakuwa na mabaki ya zebaki kutokana na maji yanayotiririka kutoka kiwandani hadi kwenye mabwawa hayo, lazima yatazoa mabaki hayo na kuingiza kwenye chumvi inayovunwa hapo.

Tunaishukuru Serikali kupunguza bei ya mafuta ya taa na gesi ya majiko. Ili kuwawezesha wananchi wa kawaida kutumia mafuta ya taa natoa ombi pia kuwa majiko ya mafuta ya taa, maarufu kama majiko ya Mchina, yafutiwe kodi, yaingizwe kwa bei nafuu ili wananchi wote waweze kumudu kuyanunua.

Kilimo kama cha tumbaku, kinafaa kifanyike kwa kuvuna miti kwa mtindo wa *fallow system*. Hii itawezesha mashamba/misitu ya miti ku-*regenerate* kwa miaka kadhaa kabla haijavunwa tena.

Viwanda hivyo vyenye kutumia kuni nyingi, kama kuchemcha chumvi kwa mfano, *Uvinza Salt Mine,* vilazimishwe kuwa na *Plantations* za miti.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, katika kupambana na uharibifu wa mazingira, vipo vikundi vya vijana, ambavyo vimeweza kujiunga katika Wilaya ili kushughulikia suala zima la kupambana na uharibifu wa mazingira, ambao unakwenda sambamba na ukataji wa miti kwenye vyanzo vya maji. Hali kadhalika, tatizo la uchomaji moto mapori katika Wilaya ya Kibondo ni hali ambayo imekuwa kichocheo kikubwa cha uharibifu wa mazingira. Ili kupambana na hali hiyo, vikundi ambavyo vimesajiliwa na mimi Mbunge niliagiza vikundi hivyo vianzishwe, ninayo orodha ya vikundi 15 hadi sasa. Vikundi hivyo, vinajihusisha na upandaji wa miti mahali palipoharibiwa, pamoja na kuimarisha vyanzo vya maji kwenye vijiji hadi kwenye Kata. Ombi maalumu kwa Wizara ya Mazingira, ni upendeleo wa pekee kwa hivi vikundi, kwa kuwezeshwa kifedha ili viweze kufanya kazi kwa ari mpya, kasi mpya na nguvu mpya.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa linaloikabili Wilaya ya Kibondo la ukosekanaji wa maji ni pamoja na vyanzo vyake kuharibiwa. Sasa hivi vikundi hivyo, vinalo zoezi la kupanda miti kwenye milima na kwenye vyanzo vya mito. Aidha, ninatoa ombi kwa Waziri kuitembelea Wilaya ya Kibondo ili kuwatia moyo hawa vijana ambao wamejiunga kwenye vikundi.

**MHE. AHMED M. SHABIBY:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu, kwa kunipa nguvu, pamoja na nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya mazingira lau kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, vile vile, napenda kumpongeza mtoa hoja, kwa hotuba nzuri aliyoitoa kuhusu mazingira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na yote niliyozungumza, napenda kuishauri Serikali kuhusu mazingira hasa katika Jimbo la Gairo. Gairo ni moja ya Majimbo makubwa nchini na ambalo lina milima mingi maarufu kama Milima ya Ukaguru na Rubeho. Katika Jimbo la Gairo, ikumbukwe ndiko kunakotoka vyanzo vingi vya maji pamoja na kuwa mji wenyewe wa Gairo hauna maji. Pamoja na hayo, mito inayotoka Jimbo la Gairo ni karibu yote ambayo ipo katika Wilaya ya Kilosa, ambayo ni Mto Mkondoa, Mto Msowelo, Mto Mvumi, pamoja na Mto Rudewa. Mito yote hii inaungana na kutengeneza Mto Wami na vyanzo vyake vikuu vinatoka Jimbo la Gairo, Tarafa ya Nongwe, umbali wa kilomita sabini kutoka Tarafa ya Gairo.

Mheshimiwa Spika, cha kushangaza, pamoja na umuhimu wa mito hiyo katika vyanzo vyake, lakini inaonekana Serikali haichukulii umuhimu wa kutosha wa kutunza mazingira ya vyanzo hivyo, wala haifuatilii kabisa na imefikia hatua kina cha maji katika vyanzo hivyo kinapungua. Kama nilivyozungumza mwanzo pamoja na kuwa maji hayo hayatumiki, kwa kiwango kikubwa katika Jimbo la Gairo yanakotoka lakini huko yanakokwenda, kuna Watanzania wengi ambao wanayahitaji kwa matumizi ya aina tofauti.

Mheshimiwa Spika, cha ajabu, hakuna utunzaji wa mazingira wa vyanzo nilivovitaja, pamoja na vingine vingi vidogo vidogo na kile kinacholeta maji Gairo. Naiomba Wizara ya Mazingira, ichukue hatua za haraka, kuvinusuru vyanzo hivi haraka iwezekanavyo, pamoja na chanzo cha maji Gairo.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itachelewa, basi suala hili litakuwa ni kero kwa Watanzania wengi, sio wa Jimbo la Gairo tu, tayari ukataji miti umefanyika na hakuna upandaji miti wowote. Pamoja na kuwa mimi binafsi kama Mbunge, natumia nguvu ya ziada kuelimisha wananchi juu ya athari za mazingira, lakini tunahitaji nguvu zaidi ya Serikali na hasa katika upandaji miti kutokana na mazingira ya milima.

Mheshimiwa Spika, nashukuru tena kwa kupata nafasi hii na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kuwapongeza sana Mawaziri wote wawili wa Mazingira na Muungano. Hotuba yao ni nzuri, ya kina na imezingatia mambo yote yanayohusu mazingira na mambo ya muungano.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, kwa kasi aliyoingia nayo katika shughuli za kumsaidia Mheshimiwa Makamu wa Rais,

upande wa hifadhi ya mazingira. Tumeshaona jitihada za makusudi, anazoendelea nazo, kuanzia mifuko ya *plastic*, maji machafu yanayotiririshwa na viwanda na watu binafsi, shughuli za uhifadhi wa misitu na mambo mengine mengi. Wananchi wengi sana katika maeneo mbalimbali, wanaona jitihada zako, wakiwemo wananchi wanaoishi kando kando ya msitu wa Mgori. Wakati wa sikukuu ya mazingira, uliwaongezea kasi ya kujiona kwamba, huo msitu ni mali yao na kuendelea kuumiliki na kuutunza vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, Iramba Mashariki, kuna misitu mikubwa miwili ya asili, ambayo inasimamiwa na Wahadzabe, pamoja na Wanyisanzu, wanaoishi Tarafa ya Kirumi, Kata za Mwangeza na Nkinto. Ambao kwa miaka yote wamekuwa wanahakikisha, waovu hawaingii humo na kuvuna misitu bila vibali vya Serikali na pia kuharibu maliasili ya kale zilizomo humo, kama vile mapango yenye picha za kale, ngoma kubwa za kale na silaha walizokuwa wanatumia mababu zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa, kwenye fedha ambazo ofisi ya Makamu wa Rais itatenga, kwa ajili ya kuhifadhi mazingira, ikiwepo misitu ya asili, misitu hii inayosimamiwa na Wahadzabe na Wanyisanzu, ipewe fedha ili kuwasaidia wao katika shughuli nzito waliyonayo ya kutunza maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, naomba nikufahamishe kwamba, wenzetu Wahadzabe wanategemea misitu hiyo kwa kupata asali, matunda, mizizi na kuvuna wanyama waliomo ndani kama chakula chao. Kwa hiyo, wakipata msaada wa fedha, wataiendeleza misitu hiyo ili waendelee kupata mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Ofisi ya Makamu wa Rais, ianzishe mpango wa makusudi wa kutenga fedha kwa ajili ya kuanzisha vitalu vya miche mashuleni na kwenye vijiji ili kuharakisha kasi ya upandaji miti maeneo yote Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri Ofisi ya Makamu wa Rais, ihakikishe Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya na Wakuu wa Idara za Misitu, Wanyamapori na Uvuvi, wanashiriki kikamilifu kwenye suala la uhifadhi wa mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Muungano, kwa kazi anazozifanya. Namshauri ahakikishe Muungano unadumu na zile kasoro ndogo ndogo zilizopo, zinajadiliwa na kutatuliwa haraka. Pia nashauri kama inawezekana, vianzishwe vipindi vya radio vya kuzungumzia mambo yote mema yanayohusu Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri vikao vya mara kwa mara viwe vinafanyika kati ya Tanzania Bara na Zanzibar, kuzungumzia mambo yote yanayohusu Muungano ili kuziba nyufa chache zinazoletwa na watu wachache wabaya.

Mheshimiwa Spika, nauunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:-** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nami nafasi hii, ili nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu.

Nampongeza sana Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa hotuba yake nzuri na ninaiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, naomba nijikite kidogo katika hali halisi ya Jimbo langu la Bukene, nimesikiliza hotuba kuhusu mazingira hasa ukizingatia Jimbo langu, naona hakuna sehemu iliyotajwa. Kwa misingi hiyo basi, naomba nami nipate semina, warsha au mafunzo ya mazingira ili Kata kama za Mwamala, Igusule, Sigili, Ikindwa, Uduka na Karitu na kwa ujumla wake, Jimbo lote la Bukene, umuhimu wa miti ueleweke vizuri na hivyo mwisho wa siku, watu katika sehemu nilizozitaja, waweze kupanda miti na hivyo kuhifadhi mazingira.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo langu kuna vianzio vya maji katika Kata hasa ya Semembela na Isagenhe na jirani zao wa Ipala, Nzega. Naomba mafunzo ili wananchi wajue kuhifadhi vyanzio vya maji na hivyo, watumie kwa uangalifu, tusije adhirika hapo baadaye, sisi wenyewe, watoto wetu na kizazi kijacho, yaani wajukuu na vitukuu.

Mheshimiwa Spika, suala la mkaa na kuni linanitatanisha sana, sasa Wizara inawatayarishaje wananchi kuwa na kitu mbadala ili wasikate miti kwa matumizi ya mkaa au kuni, hasa ukizingatia gharama za umeme au vyombo/mashine za kutumia sola? Kwa misongo hii, naomba vyombo/mashine au majiko yanayotumia sola/umeme/gesi, ili wananchi wanunue na kutumia. Hivyo, tutaacha kutumia mkaa/kuni na ndiyo tutalinda mazingira na pili miti ipandwe mingi. *NGOs* na *CBOs* zipewe nafasi na ziwezeshwe kufanya kazi hii.

Mheshimiwa Spika, *NGOs* na *CBOs* zisipangiwe na Wakuu wa Wilaya, wafanye nini na wawe wapi, *NGOs* na *CBOs* zifanye yale matatizo ambayo yapo *at a particular area/issue.* Naomba wakati Waziri akijibu, alieleze Bunge lako Tukufu, utaratibu wa kazi za *NGOs* na *CBOs.* Baada ya kuandikishwa, zinatakiwa zifanye nini kiutaratibu, ili zifanye kazi zake kama zilivyoandikishwa.

Mheshimiwa Spika, suala la *NGOs* na *CBOs* haliko kwangu ila nimelipata kwa vijana ambao wako Chalinze, wanaambiwa waondoke Chalinze kwani hawajapangiwa hapo. *Registrations* wanayo, wateja wao wanawahudumia kwa kujitolea na hawana wala baiskeli, hata dawa za wagonjwa wao wa UKIMWI, wanasaidiwa na wasamaria wema, wanaopita hapo hasa ukizingtia kuna pesa nyingi za UKIMWI. Niko tayari kukueleza zaidi, iwapo utataka hivyo, ili kusaidia *NGOs* na *CBOs* nyingine bila kugombana na watawala, yaani Wakuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA: -** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwako, kwa kasi na viwango *(Standard and Speed).*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mazingira, inahitaji ushirikiano mkubwa na Wizara mbalimbali katika kuleta uhai wa nchi na wananchi kwa ujumla. Elimu ya

Mazingira, itengenezwe mitaala makini, kuanzia shule za msingi ili kuweka misingi bora ili uelewa wa mazingira uanzie katika ngazi ya chini. Kwa kutoa mafunzo kwa wanakijiji kupitia watendaji wa Serikali za Vijiji (*Village Ward Attendance*), hii itasaidia uhamasishaji wa elimu na utumiaji bora wa mazingira.

Ujenzi wa barabara na uchimbaji wa kokoto, uendane na uwekaji mazingira kwa kuhakikisha pale barabara au mahali unapoishi, baadhi ya mahandaki yazibwe ili mazingira yarudie katika hali nzuri.

Ukataji wa mikoko umekithiri katika Fukwe za Kilwa Mtoni hadi Lindi na Mtwara kuleta athari mbaya sana. Baadhi ya vijiji kama Kijiweni *(Mzungu Bay),* Kitomungu na kadhalika, tayari vinaliwa na maji. Naomba Serikali ilione hilo na kunusuru maisha ya watu walio hatarini kuchukuliwa na kufunikwa na maji.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Ruangwa, hivi sasa kuna wachimbaji wadogo wadogo wa madini, ambao wanachimba na kuacha mapango makubwa, hivyo kuleta uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, wafugaji wa Tanzania, ambao nao wanayo haki ya kukaa popote Tanzania, lakini cha msingi ni Serikali kuweka mkakati wa kuwaweka wafugaji, wawekewe mazingira nao wafaidike na ufugaji wao ili kuondoa kero hii na wafarijike na nchi yao. Wizara ya Elimu itoe elimu kwa watoto wa wafugaji, Wizara ya Maji iweke mazingira bora ili wafugaji watulie sehemu moja na mwisho kabisa, Wizara ya Maliasili nayo iangalie fujo za ukataji miti ovyo ili kuzuia uharibifu wa mazingira hasa katika Mkoa wa Lindi. Waziri wa Mazingira, aelekeze wataalam wake, waende wakajionee na kuleta nusura ya hii hali.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kushukuru na kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii, kumpongeza kwa dhati, Mtanzania Profesa Anna Tibaijuka, kwa kuteuliwa na kuchaguliwa kwa mara ya pili kuwa, Mkurugenzi Mtendaji wa *UN–HABITAT*. Mama huyu, amefanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa, kuhakikisha wananchi wanaishi katika makazi bora na bila kuathiri mazingira.

Mheshimiwa Spika, suala la mazingira ni mtambuka na hivyo, linahitaji kupewa kipaumbele kinachostahili. Ni jambo la kusikitisha kuona bajeti ya Wizara hii, ikiwa finyu mno, yaani shilingi bilioni 14 tu. Kwa fedha chache kiasi hiki, kamwe hatutakidhi kuhifadhi mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, uchafuzi wa mazingira umepelekea nchi yetu kutumia fedha nyingi, kutibia magonjwa ambayo yasingekuwepo kama mazingira yangekuwa safi.

Mfano, kila leo watu wanapata kipindupindu na *other waterborn diseases*. Je, Wizara ina mpango gani wa kuhakikisha vyanzo vya maji havichafuliwi?

Mheshimiwa Spika, pamoja na Waziri na Wizara kuwa na mikakati kuhusu mifuko ya *plastic*, maarufu kama Rambo, kuongezwa ushuru hadi asilimia 120, bado si la ufumbuzi. Mifuko bado inazagaa, ni kwa nini Serikali isifute kabisa uagizwaji wa mifuko hiyo?

Mheshimiwa Spika, suala la Muungano nalo ni matatizo makubwa, kila pande zinalalamika kwa mfano, Tume ziliundwa kama ile ya Jaji Nyalali na ile ya Jaji Kisanga, zote zikishauri Serikali tatu, lakini kwa mshangao wa wengi, Serikali ilikataa ushauri huo. Tatizo kubwa, Serikali yetu haikubali kufuata ushauri wa kitaalamu na badala yake hufanya maamuzi kwa utashi wa kisiasa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetoa matamko mbalimbali, hasa yale ya kuzuia watu katokata miti kwa ajili ya kuni, bila kutoa nishati mbadala. Sasa Serikali inataka wananchi hawa wapikie nini, hususan vijijini? Kimsingi kuni huwa ni kavu hivyo, hata zikikatwa haziharibu mazingira.

Mheshimiwa Spika, lakini pia inashangaza kwa hatua za Serikali kuwa na *double standards* katika maamuzi yao mfano, Waziri Mkuu alitoa tamko la kuwaondoa wale wote waliokuwa wakichimba kokoto kule Boko. Je kule Boko mazingira hayaharibiki?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la *NEMC* ni jambo la kusikitisha, kuona Baraza hili halina nguvu/*mandate* ya kupambana na uharibifu wa mazingira, kwa mfano, wakati kunakuwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira, Baraza hili linapojaribu kuingilia kati, wanakumbwa na malumbano mengi.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Wizara ya Mazingira, iongezewe bajeti, lakini pia ile ya Muungano iongezewe, kwani ina mambo mengi ya kushughulikia mfano, mjadala wa namna au mfumo wa Muungano wetu Kitaifa. Nashukuru sana.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya na Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, kwa hotuba yao nzuri.

Pia niendelee kuwapongeza Mheshimiwa Rais na Makamu wa Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Waziri na Wabunge wenzangu, kwa kuchaguliwa kwao kuingia Bungeni. Bila kuwasahau wapiga kura wangu na wananchi wote kwa ujumla wa Jimbo/Wilaya ya Bukombe, kwa kunichagua na kuniunga mkono kuwa Mbunge wao. Baada hayo, naomba nitoe mchango wangu kuhusiana na hotuba hii ya bajeti hasa upande wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, uchimbaji wa madini unasababisha uharibifu wa mazingira kweli kweli. Najua katika mikakati ambayo ilishatolewa ni pamoja na kuwaondoa wachimbaji wadogo wadogo walioko Matabe - Biharamulo. Mkakati huu ni mzuri, lakini lazima tuangalie hatima yake ni nini, kwani watu hawa mara nyingi ni wakazi wa

Mji wa Uyoni, Ushirombo, Masumbwe, Lulembela na sehemu nyingine Wilayani Bukombe. Watu hawa bila kuandaa Mkakati Kabambe, tutaongeza wimbi la ujambazi Wilayani Bukombe.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, Wizara hii ishirikiane na Wizara ya Nishati na Madini, uandaliwe utaratibu wa kuwawezesha wachimbaji wadogo wadogo katika migodi ambayo ina dhahabu za kutosha, lakini uhaba wa vifaa unakwamisha maeneo hayo. Maeneo hayo ni Kelezia, Katente Na. 9, Shenda, Mwabomba na Butambala. Watu hawa watarejea wenyewe bila kutumia nguvu.

Mheshimiwa Spika, suala la uharibifu wa mazingira unaofanywa na wafugaji, niiombe Wizara hii, ishirikiane na Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo, lipo eneo ambalo ni hifadhi ya Halmashauri ligawiwe wafugaji ili waweze kuondoka/kutovamia maeneo ya *game reserve,* hasa Kigosi/Myowosi. Lakini pia wafugaji wakipatiwa malambo na mabwawa ya kutosha, hili suala litakwisha.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kama Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari, tuwasiliane namna ya kusaidia wachimbaji hawa. Kwa kufanya hivyo, Bukombe itaendelea kuneemeka na kuleta maisha bora kwa kila Mtanzania.

**MHE. PROF. FEETHAN F. BANYIKWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ya Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya, kuhusu Mazingira.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Ngara, lilivamiwa na wakimbizi kutoka Burundi, Rwanda na *DRC.* Wakimbizi hawa walipokelewa na Serikali ya Tanzania na hapa naipongeza Serikali, kwa kuweka utaratibu mzuri wa kuwapokea wakimbizi. Pamoja na pongezi hizi kwa Serikali, niseme kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, wakimbizi hawa wamekata miti sehemu yote ya Kata ya Rusumo. Si hivyo tu, vile vile wameuwa wanyama katika mapori ya Hifadhi ya Burigi. Wananchi wa Ngara, wanaomba Serikali isaidie kuboresha mazingira ya Ngara, hasa Kata ya Rusumo ili wananchi waweze kupanda miti kwa wingi, kwa sababu Wakimbizi wamejazana katika Wilaya ya Ngara na wanaleta uharibifu mkubwa wa mazingira. Wananchi wa Ngara, pia wanaomba barabara ili waweze kujiletea maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Wakimbizi wameleta ng'ombe wao. Itabidi Serikali itoe maelekezo kuhusu suala hili ili hawa Wakimbizi warudishwe kwao, pamoja na ng'ombe wao, kwa sababu hawa ng'ombe wanaharibu mazingira, wanaleta mmonyoko wa udongo na wanamaliza malisho ya ng'ombe wa wakazi wa Ngara. Kama tunataka mazingira ya Ngara yawe bora, inabidi basi hawa ng'ombe wa kutoka Rwanda, warudishwe Rwanda ili tulinde mazingira ya wakazi wa Jimbo la Ngara.

Mheshimiwa Spika, Wakimbizi wanaleta magonjwa mengi kutoka kwao na kwa sababu wanakaa wamerundikana katika makambi, wanasababisha milipuko ya magonjwa hasa ya Kipindupindu na UKIMWI. Hii yote inaleta uchafuzi wa mazingira. Sasa kwa

wale wakazi wa Ngara, ambao wameathirika, wafanyeje? Ni lazima Serikali angalau itoe fidia kwa kuboresha miundombinu hasa barabara na hospitali.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, naomba kuelimishwa, ni ajira ngapi zitapotea kwa kufunga viwanda vya mifuko ya plastiki na kodi kiasi gani kitapotea kwa zoezi hili na je, haingekuwa sawa wananchi kupewa elimu ya mazingira badala ya kuvifunga?

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, natoa pongezi za dhati, kwa Serikali kwa ujumla wake, juu ya utendaji wake wa hali ya juu. Pia pongezi kwa wanachama na Wajumbe wa Mkutano Maalum wa Saba wa CCM, uliofanya kazi nzuri sana ya kumchagua Mwenyekiti Mpya na kuidhinisha uteuzi wa Sekretarieti mpya. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mazingira, kwa kazi nzuri anayoifanya.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu katika mazingira ni kuhusu vyanzo vya maji kule jimboni kwangu Hai, ambapo tunavyo vyanzo vingi sana vya maji tangu enzi na enzi, lakini kutokana na uharibifu wa mazingira uliofanyika kwa miaka mingi, baadhi ya hivi vyanzo vimekauka kabisa na vichache vilivyobakia, viko hatarini kukauka, tusipochukua hatua za dharura, za haraka na za kudumu. Mnamo mwezi Machi, 2006, mimi pamoja na Watendaji wa Halmashauri wa Idara ya Misitu, tulitembelea vyanzo vyote vya maji, ikiwa ni kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliyonipa alipotutembelea hapo mwanzoni mwa mwezi Februari, 2006.

Ombi langu ni Wizara ya Mazingira, kutusaidia kuweka mipaka pamoja na *beacons* katika vyanzo vyote vya maji, kuanzia vilivyopo ukanda wa milimani na ukanda wa tambarare, pamoja na kuweka sheria kali ambazo zitalinda na kuviendeleza hivi vyanzo ambavyo ndivyo vyanzo vya mito mingi. Baadhi ya vyanzo, tumekwishaanza kuweka *beacons* lakini kutokana na vyanzo kuwa vingi tutahitaji msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, kinchi kwa ujumla, Elimu ya Mazingira ni muhimu sana ikaimarishwa kuanzia Elimu ya Msingi hadi Vyuo vya Elimu ya Juu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Spika, vipo vijiji zaidi ya 16 ambavyo vimeathirika sana na uharibifu wa mazingira. Vijiji hivyo ni Nyakitonto, Mgombe, Nychenda, Kitagake, Shunga, Buhoro, Mwali, Nyarugusu, Makere, Nyamidaho na kadhalika. Je, Wizara ina mkakati gani wa kurejesha mazingira kama yalivyokuwa kabla ya ujio wa Wakimbizi?

Mheshimiwa Spika, Katika Wilaya ya Kasulu, ambayo imeathirika vibaya, nini hasa programu ya Taifa katika maeneo haya? Kwa hali hiyo, ninaomba gari moja kwa ajili ya Ofisi ya Maliasili, kwa ajili ya *forestation* Wilayani.

**MHE. BUJIKU P. SAKILA:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kwimba ni kame, juhudi zilizokwisha fanywa ni kupanda miti chini ya Mradi wa *Kwimba Reforestation Project (KRP).* Wananchi waliitikia vizuri sana, lakini Mradi huu ulihamishiwa Wilayani. Tunaomba tufahamishwe kuwa tulikosa kosa gani kwa kuwa hadi Mradi unahamishiwa Magu, wananchi walikuwa bado wanaendelea kupanda miti kwa wingi na katika vikundi vikundi.

Mheshimiwa Spika, kama Mradi huo usingelihamishiwa Magu, basi uanzishwaji wa *SACCOS* Kwimba, usingelikuwa mgumu.

Mheshimiwa Spika, kama kutakuwa na jibu, naomba kufahamishwa mwenye kosa alikuwa nani, kwani Mradi huo ulikuwa bado unahitajika; tuarifiwe, mwenye kosa ni nani; Wananchi au Watendaji wa Halmashauri ya Wilaya au wa Mradi?

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Biogas,* tulipata ufadhili wa *Biogas* kutoka *UNDP,* tunashukuru sana. Licha ya wananchi kufurahia sana Mradi huu, Mradi umeshindwa kuendelea. Tatizo moja la Mradi huo ilikuwa ni matangi ya kuhifadhia gesi.

Mheshimiwa Spika, ombi letu Mradi huo ilikuwa uwe kama wa Migesado. Matangi ya kuhifadhia gesi yawe ya kudumu, yaani ya *block*. Lakini kwa ushauri wa watu wa Chuo Kikuu cha Sokoine, ulibadilishwa, matangi ya plastiki yakaletwa. Matangi hayo yalikuwa yana uwezo wa kudumu kwa miaka miwili na nusu tu. Mradi huo ulikwama kuendelea kutokana na matangi ya plastiki. Tunaomba kupitia Wizara hii, Mradi huu urejeshwe tena na uje na badiliko la matangi ya kuhifadhia gesi, uje na matangi ya kudumu ya *block.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii na kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya na Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, natanguliza kusema kwamba, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri, kwa hotuba yake zuri sana, yenye matumaini kwa Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mazingira ni uhai, kwa hiyo, lazima tulinde na tuwe na mikakati ya kulinda mazingira. Kwa kuwa kuna mikakati iliyowekwa, basi iliyobaki ni kupeleka elimu vijijini ili wananchi wasaidie kulinda mazingira.

Mheshimiwa Spika, kuna hujuma kubwa ya watu wanaoshambulia misitu, kwa kukata mbao za miti ya asili na wengine kuvuna miti ya aina ya Msandali, ambapo uvamizi huo umefanyika katika Mlima Kilimanjaro na Mlima Ketumbeine, kukata miti

ya Msandali. Ninaiomba Serikali ifuatilie jambo hilo ili kuhifadhi mazingira na mti wa Msandali usipotee kabisa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni uchomaji wa mkaa, ni kweli bila mkaa, kuna maeneo mengine hawawezi kupata huduma ya kupika chakula. Ni afadhali sasa, Serikali itafute namna ya mbadala ya kupata nishati ya kuni, la sivyo, misitu itaisha.

Mheshimiwa Spika, ombai langu lingine ni kuhusu kilimo cha kwenye maeneo ya kandokando ya mito. Kwenye Mto Simba ambao uko *West Kilimanjaro* na Ngarenairobi, wakulima wamelima kandokando ya mto huo na kusababisha udongo kuteremkia kwenye mto na kuharibu maji yanayotumiwa na wananchi walioko chini, kama Tingatinga na Kijiji cha Ngereyani. Maji wanayotumia wananchi hao, siyo mazuri kabisa, kwa sababu yanachafuliwa na wakulima wanaolima kandokando ya mto huo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni suala la ufugaji. Ni kweli mifugo huhamishwa maeneo mengi ya Tanzania. Uharibifu wa mazingira hautokani na mifugo tu, waharibifu wakubwa ni wakulima wanaotafuta mashamba na kuingia maeneo ya wafugaji. Naomba Serikali iwahamasishe wakulima kutoingilia maeneo ya wafugaji.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, uharibifu wa Mazingira unaofanywa na wafugaji (Wasukuma), waliohamia mamia kwa mamia katika Mkoa wa Rukwa na ng'ombe kwa mamilioni, tunaomba mpango ufanyike waondolewe katika misitu ya Kalambo, Lwafi na Bonde la Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imewaondoa katika Bonde la Ruaha, wahamiaji wafugaji wengi wamekimbilia Chunya na Rukwa. Tafadhali waondolewe, warudi walikotoka, Mikoa ya Shinyanga na Mwanza. Watu hawa hawaelewi somo lolote la uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, wahamiaji wanavunja Sheria Na. 5 ya Vijiji, lakini wanatoa rushwa na hongo kwa viongozi wa Vijiji na Wilaya hivyo, kuendeleza kero katika Jimbo la Kalambo. Ninaomba wasitetewe na wafanyakazi waovu wanaopokea rushwa, mfano ni kesi ya wafugaji Mkoa wa Rukwa, niliyoiwasilisha kwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, katika utunzaji wa mazingira, tunaomba Ofisi ya Mkamu wa Rais, itusaidie tupande miti katika eneo la Katuka, eneo la vyanzo vya mito mingi ili tuweze kulinda vyanzo hivyo, pia tuweze kupata maji mengi kwa matumizi mengine ya binadamu. Mitu ukipandwa eneo hili, utatupatia rasilimali mbao ili kusaidia kuondoa umaskini wa wananchi wa Jimbo la Kalambo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, mimi naiomba Serikali, kuhusu mazingira, waweke mikakati katika Mkoa wa Kagera, kuhusu vyanzo vya maji katika mito, Ziwa Victoria, pamoja na Pori la Biharamulo. Kwa sababu Serikali huwa

inaweka maandalizi na mikakati lakini haitekelezeki. Sasa naomba Waziri, afanye hima katika Mkoa wa Kagera, msipasahau kuna kipindi waliunda vikundi vya usafi wa mazingira sikujua viliishia wapi. Naomba hiyo mikakati kama ipo, iendelezwe, hata hivyo vilikuwa vinasaidia sana.

Mheshimiwa Spika, naomba viendelezwe kama ilivyokuwa mwanzoni. Hata hivyo, huo mkoa unasahaulika kwa kila kitu, naomba Serikali itukumbuke hata angalau tuwe na mikakati kama hiyo niliyoisema ya vile vikundi.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru tukikumbukwa Mkoa wa Kagera.

**MHE. DR. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda nichukue fursa hii kupongeza juhudi kubwa zilizokwisha fanywa na Mheshimiwa Makamu wa Rais katika kuhakikisha Muungano wetu unadumu na kustawishwa na pia kwa ujasiri wake mkubwa wa kukabiliana na uharibifu mkubwa wa mazingira uliofanywa na unaoendelea kufanywa sehemu mbalimbali za nchi. Hali kadhalika, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, wenye dhamana ya masuala ya Muungano na yale ya Mazingira, pamoja na Makatibu Wakuu na Watendaji Wakuu wao wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya katika kipindi hiki cha Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, napenda kukuhakikishaia kuwa, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbozi ni kati ya maeneo kadhaa nchini, yaliyopendelewa kuwa na mazingira ya kipekee, kwa kujaliwa kuwa na milima na mabonde, yenye vyanzo vya mito na maziwa ya kipekee kabisa, misitu asilia yenye uoto wa asili wa miti mbalimbali na Bonde la Ufa lenye, kupewa jina la *Msangano Trough,* kwani huonekana kwa mvuto wa aina yake.

Mheshimiwa Spika, ni katika eneo hili na hasa katika Jimbo la Mbozi Magharibi, ambako hupatikana hifadhi za misitu *(Forest Reseve),* kama ile ya safu za milima za kingo za Bonde la Ufa hilo, ikiwa ni pamoja na Isabilo - *Msangano Forest Reserve, Uwanda Forest Reserve (Rukwa Valley Plain)* na *Manyika Plain (Ufipa Plateau)*. Kwa bahati mbaya sana, hivi sasa kutokana shughuli za binadamu, kuna uharibifu mkubwa kabisa wa mazingira kutokana na yafuatayo:-

- Ukataji Mkubwa wa magogo ya mbao, unaofanywa na watu wasioruhusiwa kisheria.

- Kilimo kisichofuata utaratibu na hivyo kusababisha mmonyoko mkubwa wa ardhi.

- Kilimo na ujenzi holela kwenye vyanzo vya mito, kinachosababisha kukauka kwa vyanzo hivyo mfano, ni pale Vwawa Mjini na *Mbozi Mission*, ambapo kuna vyanzo vya Mto Nkana, ambao ni mto wa pili kwa ukubwa Wilayani Mbozi, ambao miaka ya nyuma ulikuwa haukauki, lakini kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni, kati ya Julai na Desemba umekauka. Pia mto Halungu nao umeingiliwa na uharibifu wa aina hiyohiyo.

- Ukataji miti kiholela kwa ajili ya kilimo cha kuhamahama kijulikanacho kama Ntemele, hasa Uwanda wa Juu wa Jimbo, ambacho huaminika kurutubisha ardhi.

- Uchomaji misitu kiholela kwa madhumuni ya kufukuza wanyama wakali kama fisi, wanaovamia mifugo yao na kurahisisha uwindaji wa kurina asali. Tatizo hili ni kwa jimbo zima wakati wa kiangazi.

- Uwingi wa mifugo kupita uwezo wa ardhi iliyopo, baada ya wahamiaji wa kutoka Kanda ya Ziwa kuvamia Jimbo hili, hususan Tarafa ya Kamsamba na Ivuna na hivyo kusababisha eneo kandokando ya Ziwa Rukwa kubaki jangwa, baada ya mifugo kula uoto asilia na wafugaji kukata miti ovyo, hata kusababisha wanayama wasiopatikana eneo lingine lolote duniani kasoro *Uwanda Game/Forest Reserve* kuanza kutoweka.

Mheshimiwa Spika, hali hii inatishia Jimbo la Mbozi Magharibi kugeuka jangwa katika kipindi cha miaka michache ijayo. Kilio cha wananchi wa Jimbo la Mbozi Magharibi, ni kuiomba Serikali ichukue hatua za haraka kuhakikisha hilo halitokei, kwa kuchukua hatua za makusudi kutekeleza yale yote yaliyoagizwa na Makamu wa Rais katika hotuba yake ya hifadhi ya mazingira hapo tarehe 30 Aprili, 2006.

Mheshimiwa Spika, narudia kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii, kwani ni hoja nzito na ina manufaa kwa jamii.

Mheshimiwa Spika, ninataka kuchangia suala la uharibifu wa mazingira ya bahari, vilevile suala la uvuvi haramu wa kutumia mabomu. Suala la mazingira ya bahari haliachani na suala la uvuvi wa kutumia mabomu baharini. Wizara hizi mbili; Maliasili na Utalii na Wizara inayohusika na Mazingira, inabidi wakae meza moja ili kusuluhisha hoja hii, ambayo ninataka kuisema.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze na uharibifu wa mazingira ya bahari. Bahari yetu ya Hindi upande wa Tanzania katika maeneo ya Tanga, Dar es Salaam, Mafia, Kilwa, Lindi na Mtwara, yameharibiwa sana na wavuvi wanaotumia mabomu ya baruti kwa kuvulia samaki, hivyo, kuathiri au kuleta madhara kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kimazingira. Kijamii; vifo, majeruhi na ulemavu ambao umetokea kwa raia. Kiuchumi; kumekuwepo na upungufu wa samaki katika bahari kwa sababu mazalia ya samaki na samaki wote wadogo wanauawa. Kiutamaduni; kwa siku za usoni, hatutakuwa na samaki katika mwambao wa Bahari ya Hindi. Kimazingira; mazalia ya samaki (matumbawe), yanaharibika au yanaharibiwa kwa kupigwa mabomu hivyo kuharibu mazingira.

Pamoja na Serikali kufanya jitihada ya kuzuia uharibifu huo wa kutumia mabomu kwa uvuvi, lakini uvuvi huo unaendelea na watu wanakula samaki wenye sumu kila siku.

Kwa mfano, kampeni za Kitaifa zilifanywa Lindi na Mtwara tarehe 3 Aprili, 1998 hadi 18 Aprili, 1998 katika mwambao wa Bahari ya Lindi na Mtwara. Si hao tu, kampeni za Kimkoa zilifanyika tarehe 20 Aprili, 1998 hadi 1998 tarehe 10 Mei, 1998. Kampeni za Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na wananchi wenyewe pia wanafanya kampeni Lindi na Mtwara, lakini bado uvuvi haramu unafanyika na hivyo kuathiri mazingira ya bahari. Katika kampeni hizo za kuzuia uvuvi haramu, ushahidi umepatikana kwa kuwakamata watu wa Lindi na Mtwara kama ifuatavyo: Wavuvi haramu 300; Unga aina ya *Amonium Nitrate* kilo 202; *Magnum Blusta Explosive* 113 na tambi za kuwashia baruti 36 na kadhalika.

Katika upande wa Mtwara na Lindi, vijiji vilivyohusika ni Mkoani Mtwara ni Msanga Mkuu, Tangazo, Ng'wale, Mahurunga, Nalingu, Chuno, Sinde, Shangani, Ng'ao, Ufukoni, Mkungu, Kiyanga, Naumbu, Mbuo, Namgogoli na Mikindani. Mkoa wa Lindi, vijiji vilivyohusika ni Kilwa, Songosongo, Kijiweni, Mchinga na Sudi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pongezi za dhati kwa hawa wafuatao:-

Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Makamu wa Rais, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Samuel Sitta, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Anna Makinda, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Job Ndugai na Mheshimiwa Jenista Mhagama, Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa nyadhifa zao na Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kuchaguliwa na wananchi wenu, kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda niwashukuru wananchi wa Jimbo langu wa Kwahani, kwa kunipa kura zao ili niweze kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Wachangiaji waliochangia katika eneo la Muungano, nitaomba niwataje wale waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa maandishi ni hawa wafuatao: Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Ania Said Chaurembo, Mheshimiwa Omar Ali Mzee, Mheshimiwa Omar Yusuf Mzee, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Dr. Harrisson G. Mwakyembe, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Usi Ame Pandu, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Ameir Ali Ameir, Mheshimiwa Ali Juma Haji, Mheshimiwa Maua Daftari na Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa.

Waliochangia kwa kuzungumza ni Mheshimiwa Ramadhani A. Maneno, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Haroub Said Masoud na Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru wote, kwa michango yao mizuri na niseme kwamba, Serikali itazingatia maoni yote yaliyotolewa. Sasa na mimi nachangia hoja iliyo mbele yetu, kwa kutoa majibu yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, alitoa hoja nyingi na alieleza kwamba, wanataka majibu ya kina na si ya kisiasa, naomba nimjibu kama ifuatavyo: Kabla sijaanza kujibu hoja hizo, nachukua nafasi hii, kumshukuru kwa kunipongeza kushika wadhifa nilionao na vilevile nimhakikishie kwamba, hana haja ya kunipa pole kwa nafasi hii, kwa sababu ninavyo vyombo madhubuti kabisa vya kunisaidia. Tuna Sekretarieti ya Muungano katika Ofisi ya Makamu wa Rais, ambayo inafanya kazi hii, tuna Tume ya pamoja ya Fedha chini ya Wizara ya Fedha na sasa hivi kuna vikao maalum vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, ambavyo kwa kweli, vimetusaidia kwa kiwango kikubwa kutatua kero zinazoukabili Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, nimefarijika kusikia kwamba, kila mmoja wetu, ameunga mkono kuwepo kwa Muungano, pande zote mbili za Bunge lako zimeunga mkono kuwepo kwa Muungano, hakuna mtu ambaye amesema angependa Muungano usiwepo. Kwa hiyo, inaonekana kwamba, Muungano tunaukubali, matatizo ya Muungano tuyashughulikie yaishe ili tuweze kudumisha na kuuenzi Muungano wetu.

Mheshimiwi Spika, Muungano wetu una faida nyingi, kwa bahati mbaya sana, tunapozungumzia Muungano, mara nyingi hatuzungumzii faida, tunazungumzia kero tu. Lakini kama tutalinganisha faida na kero za Muungano, faida ni nyingi zaidi. Tuna faida za kiusalama, kiulinzi, kiuchumi, kijamii na za kiutamaduni. Bila shaka Watanzania wapande hizi mbili ni wamoja na kwa hiyo, Muungano una kila sababu ya kuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika hoja. Hoja ya kwanza katika hotuba ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa sita inaonyesha matokeo ya Tume ya Jaji Kissanga na hoja yao ni kwamba, Muungano huu ilibidi waulizwe wananchi wanataka Muundo gani wa Muungano. Naona mantiki wanayoitoa hapa ni kwamba, Muungano hawana tatizo nao, tatizo walilonalo ni Muundo wa Muungano na wamependekeza kwamba, wananchi ndiyo waulizwe, watoe jibu wanataka Muungano wa aina gani.

Sasa jibu wamelitoa wao wenyewe, katika Hotuba ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ukurasa wa sita, anaonyesha matokeo ya Tume ya Jaji Kissanga kwamba, asilimia 96.5 ya wananchi wa Zanzibar, wanataka Serikali mbili na asilimia 84.9 ya wananchi wa Tanzania Bara, wanataka Muundo wa Serikali mbili. Sasa wanaonyesha

katika hoja hii kwamba ,matokeo ya utafiti huo na matokeo ya maoni ya wananchi si muhimu. Kilicho muhimu ni mapendekezo ya ile Tume ya Jaji Kissanga, ambapo si sahihi. Kama lengo ni kutaka kujua wananchi wanataka Muundo gani, jibu limepatikana hapa, kwa kiasi kikubwa sana wanataka Muundo wa Serikali mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka ninukuu katika hiyo hiyo *speech* ya Kambi ya Upinzani, ukurasa wa nne, *paragraph* ya kwanza, inasema hivi: "Wananchi wa pande zote za Muungano, waamue ni aina ipi ya Muungano na Serikali ngapi ziwepo." Jibu limeshapatikana. Aidha katika ukurasa huo huo wa nne, *paragraph* ya pili inasema: "Kama tutakuwa na Mamlaka tatu tofauti, kuna faida kubwa kwa udugu wetu tuliokuwa nao." Kama kutakuwa na Mamlaka tatu tofauti hii maana yake ni kwamba, wanaotaka Muundo wa Serikali tatu ni wao si wananchi. Kwa hiyo, mnaposema kwamba, wananchi waulizwe, wananchi walishaulizwa na walishajibu. Sasa hoja ni kwamba, kuna kikundi fulani cha Watanzania, wanataka Muundo wa Serikali tatu na sisi tunasema tuzungumze, ndiyo maana kuna vyombo vya kuzungumzia matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais, alisema tatizo si Muundo, tatizo lipo katika utendaji. Sasa nataka niingie katika hoja za kiutendaji, ambazo kwa kweli zimeoneka wazi kabisa, endapo zitashughulikiwa, tutaondokana na matatizo katika Muungano wetu. Kuna hoja humu inayohusu Majeshi ya Ulinzi na Usalama, kuwepo kwa Vikosi Maalum Zanzibar, Kikosi cha KMKM, *Volunteer* na JKU vinakwenda kinyume na utaratibu kwamba, hivi vikosi havina Mwongozo wa Amiri Jeshi Mkuu. Suala hili ni sahihi, lipo katika Tume ya Mheshimiwa Shellukindo, amelieza kwamba, kuna kasoro hii katika utendaji wetu. Lakini vile vile Katiba hapa ya Zanzibar, inampa Mamlaka Rais wa Zanzibar, kuunda Idara Maalum na ametumia kifungu hiki cha Katiba ya Zanzibar, kuunda Idara tatu ninazo zizungumzia. Lakini hapa mazungumzo yanawezekana, tunaweza kuboresha ili kama kuna kasoro, iondoke. Kwa sababu hii ni moja ya ajenda, zitakazokuja katika Vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri Kiongozi. Kwa hivyo bado masuala haya yanazungumzika na ni zaidi ya kiutendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja Mzungumzaji wa Kambi ya Upinzani anauliza, Rais wa Zanzibar ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri, lakini mbona haji Bungeni kujibu maswali. Nataka nimfahamishe kwamba, ujumbe wa Baraza la Mawaziri si lazima uje Bungeni na si peke yake. Rais ni Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri, Makamu wa Rais ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri na Rais wa Zanzibar ni Mjumbe wa Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, kutokuja kwake Bungeni, kwa kweli hakuna kanuni yoyote iliyovunjika, kwa sababu Mawaziri waliobaki, kuanzia Waziri Mkuu, wanafanya kazi hiyo ambayo wao, kwa nyadhifa zao, wasingeweza kuingia katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasemekana katika hotuba hii vilevile kwamba, Makamu wa Rais hana uhusiano wa kikazi na Serikali ya Zanzibar. Nataka kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mheshimiwa Makamu wa Rais ni Msaidizi Mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, anafanya shughuli zote ambazo ataagizwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Lakini vilevile amepewa Mamlaka Maalum, kusimamia na kuratibu masuala yote ya Muungano, pamoja na

Mazingira. Kwa hiyo, kazi za Makamu wa Rais, ziko wazi katika Katiba, lakini anafanya kazi zote ambazo anapewa na Mheshimiwa Rais.

Kuhusu Katiba kutamka kwamba, Mgombea Mwenza atatoka upande wa pili wa Muungano na wala sio rai wa upande wa pili wa Muungano, Mheshimiwa Mbunge, anaona ni kasoro. Nimfahamishe tu kwamba, hakuna uraia wa Zanzibar wala hakuna uraia wa Tanzania Bara, kuna uraia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Zanzibar kuna ukazi wa Zanzibar, hilo tunakubali lakini uraia ni wa Tanzania. Kwa hiyo, Katiba haijakosea kusema kwamba, Mgombea Mwenza atoke upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Serikali italeta lini *Articles of Union* Bungeni, ili kutazamwa upya kwa njia ya Semina na kadhalika? Tunasema *Articles of Union* ziko wazi kabisa. *Articles of Union* ndiyo msingi wa Muungano wetu na matatizo haya ambayo tunazungumzia, mafanikio yake yametoka na *Articles of Union.* Kuna baadhi ya *Articles of Union,* utekelezaji wake unahitaji kurekebishwa. Kwa hiyo, tunasema kuletwa Bungeni kwa njia ya semina wala si tatizo, ofisi yangu imejizatiti, baaada ya Bajeti hii, tutaweza kukutanisha Asasi mbalimbali, Wizara za pande mbili, Idara na Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali. Lakini vilevile tutafanya semina hizo, kwa Wabunge na Wawakilishi ili wautambue vizuri Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuridhiwa kwa masuala ya Muungano, yaani *Articles of Union,* awali zilikuwa 11 na sasa hivi ziko 22. Kuna hoja kwamba, utaratibu gani ulitumika kuziongeza. *Articles of Union* ni kweli zilivyoanza zilikuwa 11, lakini utaratibu wa kuongeza *Articles of Union* uko bayana kabisa. Kwamba, inapozuka haya ya kuongeza *Articles,* basi utaratibu wa kuleta Bungeni na kupitishwa kwa *two third,* pande zote mbili za Muungano, unatekelezwa na hiyo imekuwa ikitekelezwa na ndiyo maana sasa hivi tuna *Articles* 22 na kama itatokea haja ya kuziongeza tena, basi utatumika utaratibu huo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja kwamba Muungano haukuridhiwa na Baraza la Mapinduzi. Tunachotaka kusema ni kwamba, baada ya makubaliano ya Muungano, utaratibu ulifanywa wa kuridhia Muungano wetu.

Kwa upande wa Bara, yaliletwa katika Bunge la Jamhuri na kwa upande wa Zanzibar, kipindi hicho kulikuwa hakina Baraza la Wawakilishi, kwa hiyo, kazi hiyo ikafanywa na Baraza la Mapinduzi. Kwa hiyo, hakuna suala kama hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ile hoja ya kutaka *Original Copy* ya *Articles of Union* na kadhalika. Napenda kusema kwamba, hilo suala liko Mahakamani na isingekuwa vyema kulizungumzia.

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwa kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Wabunge wengine. Mheshimiwa Mgana Msindai, alitaka vianzishwe vipindi vya redio na *TV* kuhusu Muungano. Tunasema kwamba, hili tumejizatiti, tumeandaa hivi sasa masuala ya Muungano yatatoka katika magazeti, vipindi vya redio,

televisheni, tutakuwa na *website* tutaweka ukurasa katika tovuti ya Taifa, kuhusu masuala ya Muungano. Vikao vya mara kwa mara vifanyike kati ya pande mbili, hilo linafanyika na kama nilivyosema, kuna asasi nyingi sana ambazo sasa hivi lengo ni kuzikutanisha, Wizara, Idara na vilevile kuna vile vikao vya Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi, bila shaka mengi yatazungumzwa na tutaweza kutatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, alitaka maelezo katika maeneo yafuatayo: Anasema kuna mambo katika *Articles of Union,* ambayo yamepuuzwa. Kwa bahati mbaya sana, hakuwa *specific* kutaja ni mambo gani, lakini mimi ninachoweza kusema ni kwamba, *Articles of Union* zote 22, zinashughulikiwa kikamilifu. Lakini, lazima tukiri kuwa, kuna maeneo yana mapungufu na hilo si siri, ndiyo maana umeandaliwa utaratibu wa mazunguzo ili tuweze kurekebisha. Lakini, hakuna kipengele maalum katika *Articles* hizo, ambacho tunasema kwamba, kisishughulikiwe kabisa na hakuna sababu za kufanya hivyo. Vile vile anahoji kwamba, tusiongeze maeneo mengine katika *Articles of Union,* kabla hatujarekebisha haya ambayo yana kasoro za sasa hivi. Tunachosema ni kwamba, Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, wakati anachangia alisema, ipo haja, samahani kidogo, nirudi nyuma niseme kwamba, alinukuu hotuba yangu kwa kusema kwamba, ukurasa wa 16 ile aya ya 23 inasema, sasa ni wakati muafaka wa kuongeza hizi *Articles*, ulikuwa ni ushauri ambao utafuata taratibu, endapo utaridhiwa.

Mheshimiwa Spika, lakini Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, ametoa mfano mzuri sana, Sasa hivi Baraza la Mitihani ni Chombo cha Muungano. Wanafunzi wanaomaliza Darasa la Saba Zanzibar, wanafanya mtihani unaotoka Baraza la Mitihani, *Form Four*, Mtihani unaotoka Baraza la Mitihani. Sasa, kama Mitaala itakuwa tofauti, bila shaka kutakuwa kuna tatizo la ufaulu. Kwa hiyo, hili ni wazo na ndio maana tuko wazi, kila ambaye atakuwa na maoni mazuri, angependa kuyatoa, tutayapokea, tutayapitisha katika utaratibu unaofuatwa, unaotakiwa ili hatimaye kama ipo haja ya kuongeza vipengele hivi kwa madhumuni ya kuboresha, kwa madhumuni ya kujenga, si kubomoa, basi bila shaka tutauleta na ili Waheshimiwa Wabunge, waweze kuuridhia endapo itaonekana una manufaa.

Mheshimiwa Spika, ili kuondoa mgongano, kuwe na Serikali tatu, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary alilisema hili wazi, kwa hiyo, ni dhahiri kabisa kwamba, haya ni matakwa yao, si matakwa ya wananchi kama nilivyoeleza awali.

Wafanyakazi wa *Foreign Affairs* wako 30 tu, anaona hiyo si haki kwa Zanzibar. Nataka niseme hili jambo pia liko katika ajenda. Kuna suala zima la nafasi za Zanzibar katika Utumishi wa Umma. Serikali ya Jamhuri ya Muungano, inahitajika iwe na wafanyakazi kutoka pande zote mbili za Muungano. Sasa, kuna baadhi ya Wizara ambazo ni kweli lazima tukiri kwamba, pengine idadi ya Wazanzibari ni ndogo, kwa hiyo ni suala linalozungumzika, litapelekwa, litaingizwa katika ajenda, tutazungumza, tutatengeneza utaratibu mzuri zaidi wa kuwa na wafanyakazi wa kutosha wa pande zote mbili za Muungano katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivi, sasa utaratibu unaotumika ni wa kutangaza nafasi na watu wanashindania. Kwa hiyo, bila shaka kutokana na uwiano ambao sio mzuri wa kielimu, bila shaka kutakuwa kuna idadi

ndogo zaidi kwa wanaotoka Zanzibar. Lakini, ni suala ambalo linazungumzika na litazungumzwa ili lirekebishwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *East African Community*, tuseme tu kwamba, masuala yote yanayohusu Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ni masuala ya Muungano. Kwa hiyo, endapo Serikali ya Tanzania, itaingia katika *East African Federation*, basi Zanzibar itakuwa ni sehemu ya Tanzania katika hilo. Lakini, hakuna haja ya kuwa na wasi wasi, kwa sababu ilivyo hivi sasa, kuna mashauriano yanafanyika kuhusu Mikutano hiyo ya *East African Community,* inayoendelea. Mawaziri husika wanakutana, hata kama sio suala la Muungano, iwe suala la kilimo au iwe suala la biashara, bado kuna majadiliano ya awali kati yetu sisi, kwa maana ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kabla ya kwenda katika vile vikao vya *East African Community*. Kwa hiyo, hatudhani kwamba, kuna tatizo hapa la kuikosesha haki, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa kuna suala la mwisho la Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary kwamba, tuangalie upya, *stake holders* wote washirikishwe, yaani maoni ya wananchi ndiyo yapelekwe kwenye vikao vya Waziri Mkuu na Waziri Kiongozi. Sisi tunakiri kwamba, hiyo ni moja ya njia, wananchi wanatoa maoni, Asasi mbalimbali, *NGOs* zinafanya mikutano, wanaotoa maoni. Juzi *REDET* wamefanya mkutano wametoa maoni na Waheshimiwa Wabunge humu, wanazungumza wanatoa maoni. Sisi kazi yetu ni kuyakusanya, kuyatengenezea ajenda na kuyapeleka katika vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, masuala ya kutozwa kodi Zanzibar halafu ukija Bara unatozwa tena, ni kwa sababu wananchi waliyazungumza, tukayatengenezea ajenda tukayapeleka, yamezungumzwa na tumaeunda Kamati ya kurekebisha. Kwa hiyo, asiwe na wasi wasi kuhusu wananchi kutoshirikishwa, kwa kweli watashirikishwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Haroub Said Masoud, alinipongeza na mimi namshukuru kwa pongezi zake, lakini la mwisho alitaka msaada kwa Zanzibar, kwa maeneo yasiyo ya Muungano na alitaja hususan barabara ambayo angependa Serikali ya Muungano isaidie.

Mheshimiwa Spika, ninachosema hapa ni kwamba, sasa hivi tumetengeneza Mkakati unaoitwa *Joint Assistant Strategy*, ni Kamati ya pamoja inayobuni miradi na kuiuza kwa Wafadhili, ili zinapotoka fedha tuseme za barabara, basi kuwe kuna *component* ya Zanzibar. Tunapotoa fedha ziwe kwa jambo lolote la kimaendeleo, kuwe kuna *component* ya Zanzibar. Bila sahaka fedha hizi zinaweza zikatumika katika kurekebisaha hizo barabara, anazozizungumzia. Hii ni pamoja na Miradi kama ya *TASAF* na *SELF* kama tulivyozungumza.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar, ametoa pongezi na amesema kwamba, *TASAF* imekuwa ukombozi Visiwani Zanzibar. Tunashukuru na tunakiri kwamba, hilo ni kweli. Miradi mingi imetekelezwa Unguja na Pemba kupitia fedha za *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, sitoweza kuyajibu yote, lakini kwa kuwa bado nina muda kidogo, naomba niendelee kujibu hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge wengine. Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mbunge wa Mtoni Zanzibar, amesema kwamba, Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa, alipokuwa akifungua barabara ya Amani – Mtoni, kwa awamu ya kwanza, alisema ujenzi wa barabara hiyo kwa awamu ya pili utamalizika kabla hajaondoka madarakani, naomba Waziri wa Muungano aeleze ahadi ile ya Rais, itatekelezwa lini.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme kwamba, tumepokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge na mimi namhakikishia kwamba, nitalifuatilia suala hili ili niweze kumpatia majibu kwa mujibu wa ahadi iliyotolewa na Mheshimiwa Rais Mstaafu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, ametaka mgao wa asilimia 4.5 wa misaada, anaomba Kamati iliyoundwa ikamilishe kazi na ikiwezekana Wizara iangalie kima hicho kizidishwe. Tunachosema hapa ni kwamba, kweli ipo Tume ya Pamoja ya Fedha, ambayo awali iliweka misaada, mikopo na faida ya Benki Kuu asilimia 4.5, iwe ndiyo mgao wa Zanzibar. Sasa hivi wanajaribu kuangalia upya asilimia hii irekebishwe kwa sababu hiyo iliwekwa muda uliopita na ilikuwa ni ya muda. Kwa hiyo, sasa hivi wamemaliza kazi hiyo kwa kutumia *Consultant* na watatoa taarifa yao rasmi kwa Serikali, vikao husika vitapitia na hatimaye tutatoa maamuzi ya kiwango hicho cha asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, vile vile ametaka fedha zilizotolewa na Waziri Mkuu, shilingi milioni 500 kwa ajili ya mikopo ya vijana katika Mikoa, basi na Zanzibar nao wapate angalau shilingi milioni 100 kwa kila mkoa. Napenda niseme kwamba, hoja hii tumeipokea, tutaifikisha ili iweze kufanyiwa kazi. Aidha, kulikuwa na Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, yeye alisema Muungano umesababisha watu kuingia Zanzibar kiholela kutoka Tanzania Bara, baada ya kuondoa hati ya kusafiria, yaani *Passport*, jambo ambalo limesababisha kukithiri kwa majambazi na vile vile angependa vitambulisho vya uraia vitolewe.

Mheshimiwa Spika, katika hili, napenda nimjibu tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, si kweli. Sote tunajua kukithiri kwa majambazi ni tatizo la nchi nzima. Imetokea na sasa hivi suala hili limeshashughulikiwa na tunakiri kwamba, maeneo mengi sasa hivi yako salama kwa juhudi zilizofanywa na Jeshi la Polisi. Kwa hiyo, inapotokea kwamba, kumetokea ujambazi, si kwa sababu ya kuondolewa *Passport*. Kwa sababu, hata sehemu za Ngara, Dar es salaam, imetokea katikati hapa kukithiri kwa ujambazi, jambo ambalo naipongeza Serikali kwa kulishughulikia. Lakini, tuseme tu kwamba, ni kweli vitambulisho vya uraia vinahitajika. Jambo hilo linashughulikiwa na Wizara ya Mambo ya Ndani na bila shaka, vitaweza kutoka ili kulinda watu wanaotoka nje ya nchi yetu, kuja kufanya uharifu ndani ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, anaomba tuwe karibu zaidi na wadau wakuu wa Katiba hizi, yaani Wabunge na Wawakilishi, ambao ndio watunga Sheria. Sisi tunasema maoni ya Wabunge na Wawakilishi, tutayazingatia kupitia

semina hizo nilizozizungumza ili hatimaye tuweze kuyafikisha kwenye vikao vinavyohusika, kwa ajili ya kuboresha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, ametaka mpasuko wa kisiasa Pemba na Unguja ushughulikiwe na elimu itolewe kwa wananchi kuhusu masuala ya Muungano. Serikali imepokea hoja hizo na itazifanyia kazi na nataka nimhakikishie kwamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, anayeshughulikia masuala ya Siasa, analishughulikia suala hili na atatoa taarifa yake.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shoka Hamis Juma, amesema wale wanaofikiria kuwa *CUF* haiependi Muungano na kwamba wanataka kuuvunja, wanajidanganya. Sisi, tunashukuru kwa maneno haya, kama kwa kweli hawataki kuuvunja, basi tushirikiane katika kutatua kero ili tuuimarishe zaidi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Hemed Mohammed Hemed, amesema kuondolewa kwa hati za kusafiria, yaani *Passport*, kumechangia majambazi Zanzibar. Jambo ambalo nimeshalijibu. Vile vile amesema kero za Muungano zipo na ni vyema Serikali zetu, zisidharau hili. Tumeshatoa maelezo kwamba, hakuna anayedharau na vikao vinaendelea kutatua matatizo hayo.

Mheshimiwa Spika, vile vile amesema kuna ukiukwaji wa haki za binadamu katika Muungano. Hapa tunasema kwamba, haki za binadamu zinapokiukwa, kuna vyombo vilivyowekwa kisheria. Unaweza ukapeleka hoja Mahakamani au unaweza ukapeleka kwenye Tume ya Haki za Binadamu. Kwa hiyo, kama kuna jambo lolote ambalo yeye ameona limekiukwa, si tatizo la Muungano, vipo vyombo, apeleke litaweza kushughulikiwa.

Mheshimiwa Spika, sidhani kama ninao muda wa kutosha wa kuendelea kuwajibu Wabunge wote, lakini ninachosema ni kwamba, tutajitahidi kutoa maelezo haya kwa maandishi ili kila Mbunge aliyeuliza maswali yake, aweze kupata majibu ili tusaidiane katika kuujenga na kuudumissha Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimebakiwa na dakika chache, naomba nijibu hii hoja ya mwisho ya Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, anasema kwa nini Serikali inasita kuonyesha *Articles of Union* kwa wananchi ili kuondoa maneno yasiyokwisha. Serikali inapoteza nini ikiwa wazi?

Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi kwamba, suala hili liko Mahakamani, nadhani na yeye anafahamu, kwa hiyo, tusubiri hatma ya kesi hiyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba nimalizie kwa kusema nami naunga mkono hoja hii mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Rais, kwa kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mwenye Dhamana

ya Mazingira. Ninasema hivyo kwa dhati kabisa, nadhani kwa sababu zinazoeleweka. Namhakikishia Mheshimiwa Rais kwamba, nitafanya kazi kwa uadilifu na kwa uaminifu, kwa nguvu, akili na moyo wote, kwa manufaa ya nchi yetu ili kurudisha imani ambayo amenipa. Namshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kazi zetu wanasiasa ni ngumu, zinakuwa rahisi pale ambapo mizigo tunayobeba, tunashirikiana na familia zetu.

Mheshimiwa Spika, kwako hili ni dhahiri, kwani wewe ni Spika wa Kasi na Viwango, lakini mimi naamini Viwango na Kasi hiyo, mmeviweka pamoja na Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta. Hakika Wabunge tunawaonea wivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini leo wivu umepungua kidogo kwa upande wangu, kwani kwenye sehemu ya wageni pale na mimi yupo mke wangu Lucy, ambaye namshukuru sana yeye, watoto na sasa na mjukuu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, michango ya Waheshimiwa Wabunge, ilikuwa mizuri sana, kwa kweli ni somo. Kila wakati ninaposikiliza Wabunge, ninarudi shuleni, pamoja na Uprofesa. Maoni yao, yatatusaidia sana na naahidi kwamba, tutayazingatia.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida, naomba niwatambue waliochangia hasa sehemu ya Mazingira leo hii, kwa kusema Bungeni. Wao ni pamoja na Mheshimiwa Hassan Rajab Khatibu, Naibu Mwenyekiti wa Kamati ya Maliasili na Utalii na Mheshimiwa Said Amour Arfi, aliyesema kwa niaba ya Msemaji wa Upinzani, ambaye ni Waziri Kivuli wa Mazingira.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli namwombea kila la kheri, huyo Waziri Kivuli aendelee kukaa kwenye Kivuli kwa muda mrefu sana. Sisi tuko juani, tuko kazini. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Wilson M. Masilingi, Mheshimiwa Riziki Said Lulida, Mheshimiwa Ezekiel M. Maige, Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, Mheshimiwa Pindi H. Chana, Mheshimiwa Sameer I. Lotto na mwisho si kwa umuhimu ni Mheshimiwa Dr. Hussein Ali Mwinyi, ambaye vile vile ni mtoa hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa 42 wamechangia kwa maandishi. Wao ni pamoja na Mheshimiwa Hassan Rajab Khatib, Mheshimiwa Lucy T. Mayenga, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Azzan M. Zungu, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa Jacob D. Shibiliti, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, Mheshimiwa Sevelina S. Mwijage, Mheshimiwa Benedict K. Losurutia, Mheshimiwa Prof. Feethan F. Banyikwa, Mheshimiwa Mwantumu B. Mahiza, Mheshimiwa Mizengo P. K. Pinda, Mheshimiwa Fatma Mussa Maghimbi, Mheshimiwa Hasssan C. Kigwalilo, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Dr. Omari M. Nibuka, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Juma H.

Killimbah, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Hamis, Mheshimiwa Peter J. Serukamba, Mheshimiwa Daniel N. Nsanzugwanko, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa Mgana I. Msindai na Mheshimiwa Ahmed M. Shabiby.

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Dr. Luka J. Siyame, Mheshimiwa Monica N. Mbega, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa Christopher K. Chiza, Mheshimiwa Bujiku P. Sakila, Mheshimiwa Benito W. Malangalila, Mheshimiwa Bahati Ali Abeid, Mheshimiwa Estherina J. Kilasi, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mheshimiwa Dr. James M. Wanyancha, Mheshimiwa Masolwa C. Masolwa, Mheshimiwa Omar S. Kwaangw', Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya na Mheshimiwa Castor R. Ligallama.

Mheshimiwa Spika, hakika utakubaliana na mimi kwamba, Waheshimiwa Wabunge ni Wanamazingira. Mbali na kuchangia, wametutetea hasa kuhusu ufinyu wa fedha zilizotengwa kwa ajili ya Mazingira. Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapa, nadhani amewasikia. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, wengi vile vile walichangia kwenye hotuba ya Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango, Uchumi na Uwezeshaji na vile vile hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, wamechangia kwenye hotuba ya Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika na Waziri wa Maji. Hakika Mazingira ni suala mtambuka.

Mheshimiwa Spika, si rahisi kwa nusu saa kujibu kwa kutosheleza hoja zote za Waheshimiwa Wabunge. Naahidi kama ilivyo kawaida yetu kwamba, tutazijibu kwa maandishi na tutawapatia Waheshimiwa Wabunge wote.

Mheshimiwa Spika, ushauri na maoni ya Kamati ya Maliasili na Mazingira, naahidi pia tutavizingatia ipasavyo. Kuna moja katika maoni na ushauri, ambalo ningependa kulizungumzia, nalo lilikuwa ni ombi au ushauri wa Kamati kupitia ripoti za tathmini ya athari ya mazingira ili watoe ushauri. Kwa hilo, ninachoweza kusema ni kwamba, sisi tutazifanyia kazi, ndiyo kazi yetu. Tutazichambua, wataalam watazichambua na mimi nitawapatia Kamati, taarifa ya utekelezaji mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Upinzani, alizungumzia kuhusu kemikali ya hatari inayoitwa *Sodium Cyanide,* ambayo inatumika Duniani kote hasa katika shughuli za madini, hususan shughuli za kusafisha dhahabu. Ni kweli ni hatari, lakini huwa wanatumia kwa uangalifu mkubwa sana. Hamna kemikali mbadala katika hilo na taarifa tulizonazo ni kwamba, si kweli kwamba imepigwa marufuku huko Canada.

Mheshimiwa Spika, hoja za Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema ni nyingi, naomba nizijibu kwa pamoja katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, eneo la kwanza ni lile lililozungumziwa kwa uchungu na hakika kwa haki kabisa, nalo linahusu tunafanya nini kuhusu wafugaji ambao wameondolewa kutoka kwenye vyanzo vya maji hususan Ihefu.

Mheshimiwa Spika, sitaweza kuzungumza kwa umahiri zaidi ya yale aliyoyazungumza Mheshimiwa Waziri Mkuu, hakika ametoa maelekezo, nini cha kufanya. Mambo mawili aliyazungumzia; moja ilikuwa ni kuwa kueleza kwamba, nchi nzima haiwezi kuwa ni malisho ya mifugo, lakini vile vile alisema kwamba, wafugaji na mifugo yao ni muhimu kwa nchi yetu na wafugaji hawawezi kuwa wakimbizi katika nchi yao. Kwa maana hiyo, ametuwekea mipaka ya nini la kufanya sisi watendaji, kuanzia ngazi za Mawaziri, Wakuu wa Mikoa mpaka Wakuu wa Wilaya. Kwa hiyo, hatuwezi kuzungumza hili zaidi ya hapo, sasa, kazi ni kwetu.

Mheshimiwa Spika, lakini, naomba nitoe taarifa fupi tu kuhusu Ihefu. Kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, Ihefu iko Usangu, ni maarufu sana sasa, ina mita za Mraba 4,148. Ilitangazwa kuwa Pori la Akiba mwaka 1998 mwezi wa Saba, kupitia *GN No. 436,* kwa ajili ya kulinda na kutunza Bayoanuwai na maji ya eneo tengefu la wanyamapori la Utengule. Kwa nini nazungumza hivyo, tunapotumia neno uvamizi, tuna maana yake. Hatuna maana kwamba, kila mfugaji nchini ni mvamizi, hapana. Kwa maana ya eneo hili ambalo limetengwa kisheria, kuwepo kwake pale ni uvamizi. Basi, kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wabunge, tukitumia neno uvamizi, mtuwie radhi, hatuna maana kabisa kwamba, mfugaji yeyote nchi hii ni mvamizi, hata kidogo. Mara nyingi tumelitumia kwa maana ya Ihefu na kwa maana ya vyanzo vya maji. Sasa, hili la vyanzo vya maji na Ihefu, mtuwie radhi, halina mjadala kwa uhai wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Serikali tulichukua hatua za kuwaondoa wavamizi katika vyanzo vya maji, hususan Ihefu baada ya Tamko la Tarehe 1 Aprili, 2006. Kama nilivyosisitiza si kila mfugaji ni mvamizi. Operesheni ya Ihefu tulianzisha Tarehe 18 Mei, 2006. Mpaka sasa zaidi ya mifugo takriban 16,000 imeshaondolewa kutoka Ikoga, Nyota na Ulanga katika Vituo hivyo. Wavuvi 37 tumewaondoa na mkitumbwi yao 31. Wafugaji hao wamehamia maeneo ya Chunya. Taarifa tulizonazo, wengine walienda Ruvuma, wengine wako Iringa na wengine wamehamia katika Bonde la Rufiji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo, imetoa Tamko kuhusu namna ya kupitisha hiyo mifugo, namna ya kukubaliwa hiyo mifugo katika maeneo ambako wanakwenda kupitia Waraka wa Rais Namba 1 wa mwaka 2002. Baadhi ya Wilaya, zimeonyesha nia ya kuwapokea. Kwa hiyo, naomba tusiwakatishe tamaa hao ambao wangependa kuipokea hiyo mifugo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kufuatia Agizo la Waziri Mkuu, Wakuu wa Mikoa na Wilaya, kwa kweli tunawategemea kwamba, watatoa ushirikiano mkubwa kadri inavyowezekana ili kuwaelekeza wafugaji katika maeneo yanayohusika katika maeneo yao ili kuwapunguzia wafugaji adha, kuwapunguzia usumbufu wakati tukiandaa na kutekeleza taratibu za kudumu.

Mheshimiwa Spika, narudia kusema, wafugaji si waharibifu wa mazingira, wafugaji ni wana mazingira. Riziki yao inatokana na mazingira, isipokuwa mazingira yanaharibiwa na wafugaji, pale mifugo inapozidi uwezo wa malisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viumbe adimu, hususan chura wa Kihansi. Viumbe ni tunu ya Mwenyezi Mungu, kwa binadamu, vilivyo adimu ni zawadi kubwa zaidi. Tuvitunze, kwa sababu tusipovitunza, vitatoweka na kuna sababu nyingi sana, kwa nini vina faida kwetu. Kwa mfano, Tanzania ina mimea ya asili, nimewahi kusema kuna aina kama 10,000 na zaidi ya robo ya mimea hii, haipatikani popote Duniani isipokuwa Tanzania. Mmojawapo unaitwa *African Violet,* ambao kuna aina 18 za mmea huo Tanzania na Duniani kuna aina 20 tu. Kuna aina 13 za kahawa pori, nimewahi kusema, kati ya aina 40 Duniani, zinapatikana Tanzania tu.

Mheshimiwa Spika, katika Maziwa na Mito yetu, kuna aina 700 za Samaki. Ziwa Victoria kulikuwa na aina 300 za Samaki, kabla hatujaiweka Sangara, ambapo pamoja na chakula, kimazingira imekuwa ni balaa. Bahari yetu ina aina 600 za Samaki, miti kama vile Misambu, Mfimbo, Mikore na mingine, haipatikani popote Duniani isipokuwa Tanzania. Miti mingine imeanza kupotea na nimewahi kuitaja wakati fulani kama vile *Saint Paulia Magansus* imepotea huko Korogwe, *Saint Paulia Usambaroncis* imepotea katika Milima ya Usambara na karibu tutapoteza mmea mmoja wa aina yake, ambao Duniani unapatikana Amani, nao utapotea kama hatutachukua tahadhari za kuulinda.

Mheshimiwa Spika, kuna Nyani adimu Mahale, Kilombero, Udzungwa. Naomba kutoa taarifa vile vile kwamba, kwa mara ya kwanza katika miaka ya 83 duniani, Wataalam wamegundua aina Mpya ya Nyani Tanzania. Amegunduliwa si mahali pengine isipokuwa katika Milima ya Rungwe na amepewa jina la kisayansi na Wanasayansi Duniani, la *Rungwecebus Kipunji. (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sasa niende kwaenye chura wa Kihansi, hiyo ilikuwa ni utangulizi. Chura anayezaa, anayepatikana Tanzania tu huko Kihansi, mazalio yake ya asili yaliharibiwa na Mradi wa Umeme wa Kihansi. Tunajaribu kurudisha hali ya asili kama walivyokuwa wanaishi hao vyura, lakini ni ngumu sana kwa sababu wanaishi kwenye mvuke unaotokana na maporomoko. Kwa hiyo, imebidi sasa tuweke mvuke wa bandia ili ufanane fanane na hali yao ya zamani.

Lakini, wengi wamekufa, tumeweza kuokoa wachache. Tuliwaokoa tuliwapeleka Marekani mwaka 2000 ili wasife wote. Tuliwapeleka *Bron Zoo*, *Toledo Zoo* na *Detroit Zoo,* bila gharama zozote. Lakini Mkataba ulipokwisha, mwaka 2005, tuliingia Mkataba mpya, ambao sasa asilimia 39 za gharama za kuwatunza ni za nchi yetu na asilimia 61 ni za Marekani. Kwa hiyo, tunatumia Dola 75,000 kuwatunza hao vyura kwa mwaka. Lakini, kwa sababu tunafanya hii kazi kwa niaba ya Ulimwengu, tumepata msaada, tutawarejesha.

Mheshimiwa Spika, tumepanga kuwarejesha na tunaandaa Warsha Maalum ya Kimataifa, ambayo kwa kitaalam itaitwa *Population and Habitat Variability Assessment Workshop,* mwezi Oktoba, ambayo Wataalam Duniani kote watakuja Tanzania ili kutoa

ushauri wa Kitaalam kuhusu kutekeleza azma hii ya kuwarudisha, namna ya kuwarudisha na namna ya kuwatunza ili wasife.

Mheshimiwa Spika, tarehe 2 Machi, 2006, nilifanya ziara huko Kihansi, ilinibidi nipande mlima kwa zaidi ya saa tano nifike kwenye eneo la mazulio. Hao vyura mimi sikuwaona, lakini niliambiwa wapo na wana aibu, watalaam wamewaona wanasema wamejifungia chini. Siku nyingine nitarudi tena ili niwaone. Marekani mpaka sasa wako vyura 400, hii ndio taarifa niliyotaka kuitoa mbele ya Bunge lako, kuhusu wanyama na mimea adimu, ambayo ni tunu ya Mwenyezi Mungu kwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie haraka haraka kuhusu mambo ya kijumla, yanayohusu vinyungu. Nakiri kwamba, hili ni neno jipya nililolipata mimi baada ya kuingia Mazingira. Kwa hiyo, kila siku unajifunza istilahi mpya. Vinyungu ni maeneo ya maji ambako hasa Iringa ndiko neno linakotoka, wananchi wanalima katika maeneo ya mabonde hayo. Hatuna tatizo na kilimo cha Vinyungu, isipokuwa kama kilimo hicho ni kwenye chanzo cha maji, basi haiwezekani.

Lakini kama ni kwenye maeneo nje ya chanzo cha maji au chini *(down stream),* basi taratibu za kawaida ambazo inabidi ziwekwe na Halmashauri, zifuatwe kwa sababu wao wanaelewa maeneo hayo wanaweza wakapima, ni mita ngapi kilimo kinaweza kufanyika kutoka kwenye kingo za maji yanakotiririka. Sheria ya mazingira, Sheria Mama inazungumzia kuhusu mita 60 kutoka kingo. Lakini vile vile sheria hiyo hiyo, inazipa Halmashauri, mamlaka ya kuamua ni mita ngapi. Kwa hiyo, tunaamini kwa sababu jiografia inapishana, ndio maana sheria imeweka utaratibu huo ambao Halmashauri zimepewa mamlaka ya kuamua wafanye nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye miradi midogo midogo ya mazingira. Tumepata maombi mbalimbali kuhusu vikundi vidogo vidogo vingi vya mazingira, kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge, lakini pia kutoka kwenye vikundi vyenyewe nchi nzima. Nieleze tu maeneo manne ambayo sisi tunayasimamia ili yaeleweke, tunaweza tukavipatia vikundi vya namna hiyo fedha za kuendesha miradi hiyo. Tunao mpango unaitwa *Small Grant Program* wa *GEF* na *UNDP,* tumetengewa dola milioni 1.3, tumetumia dola 100,000 tu kwa mwaka huu. Kila mwaka tunatoa kipaumbele kwa eneo, kwa mwaka huu tumetoa kipaumbele kwa milima ya Tao la Mashariki. Kwa hiyo, miradi ya namna hiyo kwa mwaka huu, tunaweza kuipendekeza ili ipate fedha na mradi mmoja usizidi dola 50,000.

Tunao vile vile Mradi wa *Nile Basin Initiative,* nao unafadhiliwa na *GEF*. Tuna kiasi cha *USD* 300,000, tumetumia Dola 250,000 lakini kipaumbele ni kando ya Ziwa Victoria tu na miradi isizidi dola 30,000. Tunao Mradi mwingine wa *Conservation of Protected Areas Through Community Conservation Initiatives,* kiasi cha fedha zilizotengwa ni *USD* 200,000 zilizotumika ni dola 100,000. Kipaumbele ni Mlima wa Kilimanjaro na miradi isizidi dola 50,000. Mradi mwingine unaitwa *Capacity Building to Alleviate Poverty Through Multilateral Environment Agreements.* Tuna fedha kiasi cha dola 150,000, kilichotumika ni shilingi milioni 29,000 tu, kipaumbele ni nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, naahidi kwamba, tutaweka wazi zaidi, namna ya kutayarisha hiyo Miradi na namna ya kupata fedha kwa ajili ya hiyo Miradi. Kwa hiyo, nadhani nimewajibu Waheshimiwa Wabunge wengi, nini kinachowezekana kutokana na maombi ambayo tumeyapata.

Niende kwenye Mradi wa Ziwa Tanganyika, huu Mradi mkubwa kama nilivyosema kwenye hotuba, unahusu Hifadhi ya Bonde la Ziwa, ambao utahusisha Kigoma Mjini, Kigoma Vijijini na Kasulu na vile vile mwambao wa Ziwa Tanganyika katika Mkoa wa Rukwa, dola milioni 2.2. Kuna Mradi wa Uvuvi Endelevu. Wengi wamezungumzia kuhusu umaskini na mazingira, vinavyokwenda pamoja au umaskini na uharibifu wa mazingira, lazima uteke umaskini vile vile.

Kwa hiyo, uvuvi endelevu dola milioni 7.4, utafadhariwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika. Kuna Mradi wa Maji Taka kwa ajili ya Kigoma Ujiji, ambao ni mkubwa, huo tumepata *Euro* milioni sita, utafadhiriwa na *Nordic Bank* na vile vile *GEF* watatoa dola 300,000.

Nimeombwa nizungumzie kwa kifupi, kuhusu maeneo ya wakimbizi. Maeneo ya wakimbizi, inabidi yaainishwe katika Mipango ya Wilaya zinazohusika, kwa sababu kama nilivyosema, suala la mazingira ni suala mtambuka na inabidi liwe *main-streamed* katika Mipango ya Wilaya. Kwa maana hiyo, mipango yote ya kuondoa umaskini, lazima izingatie vile vile mpango wa kuongoa mazingira yaliyoharibika katika maeneo ya wakimbizi.

Lakini hata hivyo, nawaomba tutumie Miradi hii ambayo nimeitamka, pamoja na Mradi mkubwa kwa mfano, Ziwa Tanganyika, ili tuweze kufanya kazi kwa pamoja ili tuweze tukaongoa maeneo ambayo yameharibika. Tutaendelea kuzungumza na wafadhili ili tuweze kushughulikia hilo suala. Mimi naahidi, Mwenyezi Mungu atupe afya tu, ili niende Kigoma hivi karibuni, nikaone mwenyewe, maeneo haya ambayo yameathirika kutokana na shughuli za wakimbizi. Bila shaka, nitakuwa na picha nzuri ya kushirikiana na wenzangu, Waheshimiwa Wabunge wa Mikoa hiyo, ili tuweze kuongoa hayo maeneo, kwa faida ya sasa na vizazi vinavyokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, muda ni mfupi, hoja ni nyingi lakini kama nilivyosema, tutawajibu kila mmoja kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia kwa kuwashukuru tena kwa dhati kabisa, wananchi wa Rungwe Mashariki, nawashukuru wananchi wa Rungwe, nawashukuru wananchi wa Mbeya na nawashukuru wanamazingira wote wa Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mazingira ni uhai, tunza mazingira yakutunze. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Waziri. Kabla hatujaendelea na hatua inayofuata, nina furaha na kwa heshima napenda nimtambulishe mgeni mashuhuri, ambaye ana ujumbe kutoka nchi rafiki ya Angola. Yeye ni Waziri wa masuala ya migodi

kule Angola, Mheshimiwa Emmanuel Anthony Africano*; can you stand up your Excellency? Thank you.*

Yeye amekuja kumwona Mheshimiwa Rais, nadhani ni katika masuala ya kubadilishana uzoefu katika namna ya kushughulika mambo haya mazito ya madini na mwenyeji wake kwa hapa ni Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Karibuni. *We feel very privileged to have your Excellency and your delegation with us in the Assembly here, you are warmly welcome. Angola is our sister country, we are together in SADC and we shall always be together in future struggles. Thank you very much. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, napenda kutoa taarifa kwamba, suala la baridi linashughulikiwa. Leo sijui kuna nini, hata mimi ambaye nimevaa Joho zito na mimi kidogo nasikia kuna shida, nadhani ni halali kabisa, mafundi wameitwa wanalishughulikia hivi sasa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hapo, sasa kabla hatujaingia katika hatua ya Kamati ya Matumizi, kama kawaida yetu kwa hatua hiyo, ambayo hoja imetolewa na imeungwa mkono, nitawahoji ili tuingie katika hatua hiyo. Kwa hiyo, sasa muiamue hoja hiyo.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 - *Administration and General* … … …. Sh. 4,538,359,000/=
Kif. 1002 - *Finance and Accounts* …. … … …. Sh. 4,714,806,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2001 – *Union Secretariat* … … … … …. … Sh. 22,344,213,000/=

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nichangie. Naomba ufafanuzi, kifungu 2001 - *Union Secretariat, item* 280600 - *Transfers and Subsidy - Other Levels of Government,* shilingi 21,196,080,000/=. Ningependa kujua katika Hotuba ya Waziri, imeelezwa kwamba, hii fedha imetengwa kwa ajili ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; je, ni kwa ajili ya shughuli zipi na *criteria* ipi ilitumika katika ku-*allocate* fedha hizi? Je, hii ndiyo ile asilimia 4.5 na kwa nini imepungua kutoka ile *allocation* ya mwaka 2005? Naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali ya Mheshimiwa Dr. Limbu kama

ifuatavyo: Ni kweli kwamba, fedha hizo zinazozungumziwa ni fedha zinazokwenda kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hizo ni fedha za misaada na mikopo kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na *criteria* ndiyo hiyo ya asilimia 4.5 ya misaada na mikopo yote huwa ni mgao wa Zanzibar.

Kuhusu swali la kwamba, kwa nini imepungua, kwa kweli hiyo inatokana na upatikanaji wa hiyo misaada tunayoizungumzia mwaka hadi mwaka. Kwa hiyo, ukiangalia pale nyuma, utakuta vile vile mwaka kabla ya ule wa 2005, fedha hizo zilikuwa ndogo vile vile. Kwa hiyo, inategemea na upatikanaji, hata hivyo, endapo itatokea kupata msaada mwingine katikati, fedha hizi pia zitaongezeka. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. – 5001 - *Environment* .. … … … … … … … Sh. 5,675,971,000/=

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Najua Mheshimiwa Waziri, hakupata muda wa kuweza kunipa ufafanuzi wa jinsi ambavyo Wizara yake na hasa *NEMC,* walivyojipanga ili kusimamia masuala ya mazingira.

**MWENYEKITI:** Unazungumzia chini ya kasma gani?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Kifungu kidogo 250100, kwenye *subvote* 5001 - *Environment*.

**MWENYEKITI:** Nadhani mshahara?

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** Nilizungumzia kwenye hoja yangu wakati nachangia kwamba, ningependa kujua jinsi Wizara ilivyojipanga kusimamia masuala ya mazingira kwenye miradi yote, ambayo tumeizungumzia kwenye kilimo hasa umwagiliaji na miradi ya maji ili kuhakikisha kwamba, miradi hiyo inakuwa endelevu na hasa katika kusimamia suala zima la tathmini ya athari za mazingira. Nilitaka kujua watafanyaje kazi ili kuhakikisha kwamba, mazingira yanahifadhiwa katika utekelezaji wa Miradi yote katika nchi hii, ambayo fedha tumezitolea katika Miradi iliyotajwa ya Kilimo, Umwagiliaji na Miradi ya Maji? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Labda Mheshimiwa Waziri, urudie tu maelezo kwa sababu mlikwishaeleza Sera yote ya jinsi ya kuhifadhi mazingira, lakini si vibaya ukarudia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa ufafanuzi wa ziada wa hoja ya Mheshimiwa Prof. Raphael B. Mwalyosi, kama ifuatavyo: Sheria Mpya Na. 20 ya mwaka 2004, imetoa majukumu makubwa kwa Baraza, yaani *NEMC* katika suala zima la usimamizi na uratibu wa tathmini ya athari za mazingira. Kwa maana hiyo, Baraza limejipanga kwa kuwa na Kurugenzi Maalum, ambayo inasimamia suala hilo. Katika mtiririko wa kutoa hizo taarifa, inashirikiana na Kamati ya Kitaifa ya Kutathimini Miradi Mikubwa, ambayo

inaweza kuwa na athari kwa mazingira, inavyotakiwa na sheria. Lakini baada ya hapo vile vile, moja ya Idara ndogo za Idara ya Mazingira, inashughulika na suala zima la tathmini la athari kwa mazingira.

Kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu, hata katika Mikoa sasa kutakuwa na wanamazingira, kwa maana ya Maafisa Wasimamizi wa Mazingira na katika Wilaya watakuwepo Maafisa Wasimamizi wa Mazingira ndani ya Halmashauri. Kwa hiyo, tumejipanga. Labda nijibu tu hapa kwamba, hata katika mafunzo katika vyuo vyetu vya Sokoine na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wameingiza katika mitaala yao, suala zima la tathmini la athari kwa mazingira. (*Makofi*)

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko katika kifungu hicho hicho ni kwamba, labda tu kwa mwongozo wako, labda *heading* ndiyo inatutatanisha, kwa sababu kuna *environmental protection*. Sasa katika hili, tuna suala la hifadhi ya mazingira na kutunza. Wilayani kwangu Kiteto, nimeandika kwa maandishi, kuna matatizo makubwa ya uvamizi wa mazingira na *delegation* imekuja Kiteto, ikafika mpaka hapa. Tume imekwenda imeangalia, imerudi. Mazingira yanazidi kuharibika na kuvamiwa kwa kufyekwa. Serikali ina habari na ina taarifa ya Tume kwamba, mazingira ya Kiteto yanaharibiwa?

Sasa naomba tujibiwe kwamba ni lini, watatekeleza kikamilifu Taarifa ya Tume iliyothibitisha kwamba, ufyekaji wa misitu kwa kutumia *diesel,* utasimamishwa katika Wilaya ya Kiteto na wavamizi? Naomba nijibiwe kwamba, Serikali itashughulikia lini tatizo hili ambalo mpaka dakika hii, misitu inateketekea na wana habari? Naomba nijibiwe.

**SPIKA:** Nataka nikuelewe kidogo kama Mwenyekiti, unasema misitu inateketezwa kwa kutumia *diesel*?

**MHE. BENEDICT LOSURUTIA:** Ndiyo, kwa sababu wanapofyeka, ili iungue vizuri zaidi ibaki majivu, wananyunyizia *diesel,* ndiyo maana yangu. Nasema wanatumia *diesel* baada ya kufyeka, ukishafyeka ekari 400, 500, 600 ili isibaki hata na chembe, wanachukua gramu kama sita, saba, wanazungusha kwenye ile misitu halafu inalipuka kama bomu, ndiyo inawaka moto. Ndiyo maana hiyo kwamba, tuna bomu Kiteto. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Haya Mheshimiwa Waziri, naona kuna vita huko.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipokuwa nafanya majumuisho ya hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais, nilisema kwamba, wafugaji si waharibifu wa mazingira. Mfano mmoja wa hayo niliyonena ni Wilaya ya Kiteto na mmoja wa wanamazingira wakubwa ni Mheshimiwa Benedict Losurutia.

Ni kweli ujumbe ulikuja wa jamii ya wanavijiji, waliomo na wanaozunguka Hifadhi ya Suledo. Waliniona mimi, pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya

Waziri Mkuu - TAMISEMI, tuliwasikiliza. Baada ya kushauriana ndani ya Serikali tulimwomba Mkuu wa Mkoa wa Manyara, apeleke Tume huko ili ikafanye uchunguzi wa kina kuhusu uharibifu wa mazingira na uvamizi wa kile kilichosemekana, uvamizi wa wakulima katika maeneo ya wafugaji. Sasa imekuwa ni tofauti kabisa na Usangu, kule ni wafugaji kuingilia wakulima na maji, upande huu ni wakulima kuingilia maeneo ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti hii tumeipata si muda mrefu uliopita, katika wiki chache zilizopita, Serikali inaifanyia kazi na kwa sababu ilikuwa ni Tume ya Serikali, hata ingekuwa Tume nyingine, tungeifanyia kazi. Wametoa mapendekezo, naomba Mheshimiwa Benedict Losurutia, pamoja na wananchi wa Kiteto, wawe na subira, wataona matokeo yake baada ya muda si mrefu. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* 50 - *environmental protection, sub vote* 5001 - *environment* na fungu 250100. Kule Mbozi Mashariki, Jimboni kwangu, kuna kijiji kinaitwa Namlonga, kijiji hicho kwa sehemu kubwa kina msitu mkubwa sana. Lakini kwa muda mrefu, ukataji wa miti kule kwa ajili ya mkaa ni mkubwa sana. Hili suala nimelichangia kwa maandishi, nimempa Mheshimiwa Waziri, lakini namshukuru Mheshimiwa Waziri, alipokuja Mbozi, nadhani niliwahi kuzungumza naye, akasema kwamba, libaki kuwa suala la Wilaya na suala la Mkoa. Lakini naomba niseme kwamba, suala lile ni gumu, kwa sababu mkaa ule inasemekana unahitajika sana Wilaya ya Mbeya Vijijini, maeneo ya Mbalizi. Pia inasemekana Maaskari wa Jeshi la Wananchi, Kikosi cha Mbalizi, ndio wanaowatuma watu kwenda kukata miti, kwa ajili ya kuchoma mkaa katika eneo lile.

Kulishawahi kutokea vita kati ya wale wanaochoma mkaa, pamoja na uongozi wa kijiji chenyewe. Katika wakati mmoja iliwahi kutokea Mtendaji wa Kijiji, alitekwa alitaka azuie wale waache kuchoma mkaa, kwa maelekezo ya Kamati ya Ulinzi ya Wilaya. Lakini haikuwezekana na madhara makubwa yalipatikana, mpaka kijiji kikasema hakitaendelea tena kuwazuia hawa watu kukata miti kwa ajili ya mkaa.

Mimi nilikwenda pale kwenye mkutano, wale wananchi ambao walikuwa wanajihusisha na ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa katika kijiji kile, wao walisema wameacha lakini bado watu kutoka Wilaya ya Mbeya Vijijini, wanakata miti sana, wanachoma mkaa kwa kiwango kikubwa sana. Inasemekana zaidi ya magunia 50 mpaka 80 ya mkaa husafirishwa kila siku na mimi ni shahidi kwa sababu ninapopita kutoka Mbeya kwenda Mbozi huwa ninakutana na watu wale na bila aibu mchana wote wanasomba mkaa kwa baiskeli. Sasa kwa sababu inaonekana jitihada za Wilaya na Mkoa zimeshindikana, kwa sababu wameshakaa kwenye Vikao vya Kamati ya Ulinzi na Usalama, naiomba Serikali ichukue hatua za dhati ili kuokoa msitu wa Namlonga, vinginevyo utakwisha na ni msitu muhimu sana katika Wilaya yetu ya Mbozi. Kwa hiyo, naomba pengine Waziri sasa, awaeleze wananchi wa kule kwamba, Serikali inachukua hatua gani madhubuti kabisa ili kuzuia hali ambayo inaendelea ya uharibifu wa mazingira. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza, nimshukuru Mheshimiwa Godfrey W.

Zambi, hii ni mara yake ya pili, kunieleza hili suala. Nasema tumelipokea, hivi vyombo anavyovizungumzia ni vyombo vya Serikali na sisi vile vile ni Serikali, tutalishughulikia ipasavyo. Tutaomba msaada mkubwa sana, kutoka Halmashauri, tupate taarifa za uhakika ambazo zitatupelekea katika kupata ufumbuzi wa kudumu. Kwa kuwa umezitaja taasisi za Serikali, naomba niseme kwa upande wa Serikali kwamba, sisi tumefurahi kwamba, taasisi zilizotajwa Kitaifa, Jeshi la Wananchi la Tanzania, Polisi na Magereza, wamelichukulia vizuri na vilivyo, tamko la Serikali kuhusu uharibifu wa mazingira, kwa maana hiyo hatuoni kwamba, kutakuwa matatizo katika utekelezaji wake.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais**

Kif. 1001 – *Administration And General* ... ..... ... Sh. 462,700,000/=

**MHE. CHACHA Z. WANGWE:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Naomba kuuliza katika hicho kifungu cha 31, *Sub-Vote 1001*. Nilikuwa nahitaji tu ufafanuzi kutoka kwa Waziri, kwa masuala ya Muungano, katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Alipokuwa anajibu hoja ya Kambi ya Upinzani amesema ya kwamba, watu wanaohitaji Serikali tatu, ni kikundi kidogo cha Watanzania fulani, ambao ni wachache na akasema ya kwamba...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, unachoulizia ni suala la Sera, tuko katika Kitabu cha Maendeleo na hapa ni Jengo la Makamu wa Rais, haiwezekani kuzungumzia Sera. *(Makofi)*

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Nakushukuru Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi niweze kuomba ufafanuzi kwenye Fungu 31, Kifungu cha *1001, item 6309* - Ujenzi wa Nyumba na Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar.

Ukijumlisha idadi ya fedha ambazo zimetumika, tuki-*approve* makadirio haya toka mwaka 2004/2005 na 2006/2007 jumla inakuja shilingi bilioni 1.391. Nilikuwa naomba kuuliza kwamba, hii tunayo-*approve* leo ndiyo ya mwisho au na mwaka kesho zitaombwa? Haya majengo yanayojengwa yamefikia hatua gani, maana yake sasa imefikia shilingi 1.39 bilioni, naomba ufafanuzi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe maelezo kwa suala la Mheshimiwa Dr. Festus B. Limbu, kama ifuatavyo: Kwanza, nimweleze tu kwamba, ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar, bado haujaanza. Mwaka huu wa kwanza 2004/2005, fedha hizi zilizotengwa, hazikuweza kuanza ujenzi kutokana na tatizo la kiwanja. Niliwahi kujibu swali hapa Bungeni kwamba, kuna uzio ulijengwa sehemu, lakini baadaye Idara ya Usalama ikasema hapafai kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, ujenzi huo haukuendelea.

Kwa hiyo, fedha zilizobaki zilitumika katika kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam.

Mwaka uliofuata hivyo hivyo, pamoja na kwamba, fedha hizo zilikuwa *approved,* fedha hizo hazikutoka zote, zilizotoka baadhi tu na kwa kuwa kiwanja bado kilikuwa hakijapatikana hati yake, ziliendelea kukamilisha ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam. Sasa hivi ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Dar es Salaam umekamilika, fedha hizi ambazo ziko kwa mwaka huu wa fedha 2006/2007, ndiyo tutahakikisha sasa zinaanza maandalizi ya ujenzi wa Ofisi ya Makamu wa Rais Zanzibar na sasa tumeshapata hati miliki ya kiwanja hicho rasmi.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 5001 – *Environment* ..... ..... ..... .... .... .... .... Sh. 8,094,094,000/=

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nazungumzia *Sub-Vote 5001, Item 6569 – Lake Tanganyika Environment Management Project.* Katika maelezo ya jumla ya Waziri, amezungumzia kwamba, kwa Mkoa wa Kigoma, Mradi huu utafika mpaka Kasulu, Mkoa wa Rukwa, kama nimemsikia vizuri, amezungumzia mwambao wa Ziwa Tanganyika. Je, nilikuwa napenda tu kupata ufafanuzi kwamba, kama umeweza kufika Kasulu; kwa nini kwa Mkoa wa Rukwa usipande zaidi ya mwambao peke yake?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, katika hatua hii, tunatafuta maelezo kuhusiana na kilichokwisha tengwa, hatudai kwamba sasa hivi ipatikane ziada, ifanye hatua nyingine ya Mradi. Kwa hiyo, swali hilo mimi nitalisitisha, pale panaposema fedha hizi zitafanya kitu gani sehemu zote mbili Kigoma na Rukwa. Tupate tu hayo maelezo yanatosha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, bonde lina maana yake kijiografia na kiikolojia. Kwa maana hiyo mradi huu utahusu bonde la Ziwa Tanganyika kama linavyojulikana kijiografia. Maana yangu ni kwamba, hatuwezi kwenda nje ya eneo ambalo liko katika bonde hata kama liko katika mikoa hii ya Kigoma na Rukwa. Kwa hiyo, kama nilisema mwambao, kwa maana ya labda mita chache kutoka pwani au kutoka Ziwa lenyewe, sikuwa na maana hiyo, nilikuwa na maana ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Lakini siwezi kumhakikishia kwamba, Mpanda Mjini itakuwa nayo ndani ya bonde.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31, kifungu kidogo 5001, kifungu kidogo zaidi 6569. Nilipenda kufahamu, kwa kuwa Ziwa Tanganyika ni refu na pia linahusisha na nchi za jirani na kwa maana ya mazingira maeneo yote yanafanya uharibifu kwa viumbe hai vilivyopo katika eneo hilo. Nilitaka kufahamu kama Serikali pia, imeweza kushirikisha zile nchi jirani ambazo zinaharibu mazingira zaidi na mazingira hayo yanaathiri zaidi upande wa Tanzania, upande wa ziwa hilo kwamba, kwa kutumia pesa hizi, kuna juhudi gani za kushirikisha zile nchi nyingine ili Ziwa Tanganyika liweze kutunzwa vizuri zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naomba tu maelezo ya pesa hizi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumshukuru Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mbunge wa Nkasi, ambayo ipo ndani ya Bonde la Ziwa Tanganyika. Wilaya yake itahusika katika utekelezaji wa Mradi huu. Naomba kuthibitisha.

Mradi huu ni wa Kanda. Kwa maana ya kujumuisha nchi za Rwanda, Burundi, Congo, Zambia na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mradi ni mkubwa na gharama zake ni dola milioni 80 nao kama ilivyo sisi wana Miradi ya Kitaifa katika Bonde la Ziwa Tanganyika na wao vile vile itabidi waanzishe Makao Makuu kwa nchi zao au Ofisi kwa nchi zao, itakayosimamia na kuratibu utekelezaji wa Miradi hiyo.

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Ahsante Mheshimiwa Mwenyekiti. Nami naomba nielekee kwenye *Sub-Vote 5001,* Kifungu 6509 - *Tanzania Coastal Management Project.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo, naomba nirejee kwanza hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ukurasa wa 61, ambapo anazungumzia, naomba ninukuu: "*Tanzania Coastal Management Partinership,* iliendelea kutekeleza Mkakati wa Uwiano wa Kuhifadhi na Kusimamia Maeneo ya Pwani na Bahari pamoja na wa Kupambana na Umaskini. Utekelezaji huu ulianza na Wilaya za Bagamoyo, Pangani na Mkuranga, kwa mwaka 2005. Anasema baadaye kwamba, katika kipindi cha 206/2007, utekelezaji wa Mkakati utaendelea kwa kushirikiana na wananchi wa Wilaya za Kilwa, Lindi, Mtwara na Tanga katika kuandaa na kutekeleza Mipango ya Uwiano ya Kuhifadhi Maeneo ya Pwani katika Wilaya hizo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichotaka kupata ufafanuzi ni kwamba, mwaka 2005 kulikuwa na shilingi milioni 380, zilizotengwa kwa ajili ya Mradi, ambazo zilikuwa ni kwa Bagamoyo, Pangani na Mkuranga. Mwaka huu wa 2006, kuna shilingi milioni 458, ambazo ni kwa Kilwa, Lindi, Mtwara na Tanga, Pwani hatumo. Pwani maana yake ni Mafia, Mkuranga na Rufiji.

**MWENYEKITI:** Zungumza na Mwenyekiti. *(Kicheko)*

**MHE. ADAM K. A. MALIMA:** Ahsante Mwenyekiti. Sasa nataka kujua tu kwamba, mwaka 2005 tulikuwa na *allocation* hii, ningependa kupata ufafanuzi wa utekelezaji wa mwaka 2005 na kama kulingana na utekelezaji huo, basi mwaka huu Pwani, yaani Bagamoyo, Rufiji, Mkuranga na Mafia, kama tumo mwaka huu au hatumo katika *allocation* hii ya shilingi milioni 458? Nakushukuru Mwenyekiti.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuranga hatujawaruka, kwa sababu wamo katika utekelezaji

wa Mpango huu. Baada ya kuanzisha Mradi, matarajio yetu ni kwamba, ili uwe endelevu, maana yake ni kwamba, zile kazi zilizofanyika mwaka 2005, zitaendelea kwa njia moja au nyingine kupitia wananchi wenyewe, pamoja na Halmashauri yao.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, naomba niwataje tuliosahau kuwataja, ambao wamechangia katika hoja hii, nao ni Mheshimiwa Janeth M. Massaburi na Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa. Nakushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako Tukufu, limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu, Makadirio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2006/2007, kwa Ofisi ya Makamu wa Rais na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Spika, hivyo, naomba kutoa hoja kwamba, Makadirio hayo sasa yakubaliwe. Kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2006/2007 yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja iliyoko mbele yetu ni Bunge kuyapitisha Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ipo mbele yetu na imeungwa mkono. Kwa hiyo, Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, sasa yamepitishwa rasmi na Bunge. Kabla sijaingia hatua nyingine, naomba kutoa matangazo haya machache. Kwanza, Waheshimiwa Wabunge, mmeomba ratiba mpya ya mpangilio wa jinsi ambavyo Mawaziri watasilisha hoja zao hapa. Hilo tutalitekeleza kesho asubuhi na kila itakapotokea mabadiliko ingawa tunaisihi sana Serikali, nadhani haya mabadiliko pengine hayaepukiki. Lakini pengine itapendeza kama vile tutakapoitoa kesho, pengine itakuwa haina usumbufu tena wa kila mara kubadi ili Waheshimiwa Wabunge wajiandae. Wengine wanaahirisha safari ili wachangie hoja fulani, wanakuta tena haipo, basi inaleta usumbufu kidogo. Lakini nadhani kwa yale ambayo hayaepukiki, basi tutaelewa. Lakini tunaomba mtiririko ufuatwe kadri itakavyokuwa imetangazwa.

Tangazo la pili, kutoka kwa Mratibu wa Waheshimiwa Wabunge, ambao wanataka kujaribu kinachoitwa hapa ni kupiga shabaha, naona haya ni mambo ya jeshi. Anasema, wale wote watakaopenda kushiriki zoezi la upigaji shabaha JKT Makutopora, siku ya Jumapili, tarehe 16 Julai, 2006, wanaombwa wajiorodheshe hapa kwenye Mlango Mkuu wa Ukumbi mpya, pale tunapopatia *Order Papers.* Mwisho wa kujiorodhesha ili uingie katika zoezi hilo la kupiga shabaha ni kesho saa 7.00 mchana. Usipojiorodhesha basi hautakuwemo katika zoezi hilo. Kwa hiyo, Mheshimiwa William Shellukindo, ambaye ndiyo Mratibu wa shughuli hii, anasisitiza tukajiorodheshe ili wale wanaopenda waingie katika zoezi la kupiga shabaha JKT Makutopora Jumapili ya tarehe 16 Julai, 2006. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya hayo, kwa sababu muda wa kuahirisha Bunge kwa Mujibu wa Kanuni haujafika, ningemwomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia masuala ya Bunge, atoe hoja ya kuahirisha Bunge ili tuweze kuondoka kwa utaratibu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU – MHE. JUMA J. AKUKWETI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 21(3) na kwa sababu sasa muda haujatimia wa kumaliza shughuli zetu, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako liahirishwe sasa mpaka kesho saa tatu asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 01.18 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi Tarehe 13 Julai, 2006 Saa Tatu Asubuhi)*